# UDUMISHAJI WA LUGHA YA KIMARAGOLI KATIKA ENEOBUNGE LA URIRI, KENYA

**NA**

**SANGILI NABETA NIXON KENYANI**

**PKIS/9305/2014**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA LUGHA, ISIMU NA FASIHI KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII CHUO KIKUU CHA RONGO KWA MINAJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

**2019**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shughuli yoyote ile wala kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote kile. Ni hatia kutolesha au kurudufu nakala au sehemu ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Rongo.

-------------------------------- ----------------------------------

Nabeta K.N. Sangili Tarehe.

PKIS/9305/2014

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tulioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Rongo kama wasimamizi.

----------------------------------- ------------------------------

Prof. Mohochi E. Sangai Tarehe

Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Kibabii

----------------------------------- -----------------------------

Dr. Nyandiba N. Carren Tarehe

Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Rongo

**TABARUKU**

Kwa familia yangu, ya mwendazake baba Ainea Egehiza Sangili na Wamaragoli wanaodumisha lugha hii ulimwenguni kote.

## IKISIRI

Tafiti nyingi zimefanywa katika lugha mbalimbali hapa nchini Kenya na ulimwengu mzima kuhusu kutoweka kwa lugha kwa sababu ya kutodumishwa. Tatizo hili limetambuliwa na madola ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na Muungano wa Afrika mbali na mataifa binafsi mbalimbali. Baadhi ya lugha zilizotafitiwa awali, kupitia kwa wasemaji wake, zilihama maaeneo yake asilia na kuhamia kwingineko. Kimaragoli kinachozungumzwa katika eneobunge la Uriri ni mojawapo ya lugha zilizohamia maeneo tofauti na maeneo yake. Suala ni kwamba, japo tafiti zimefanywa kwingineko, panahitaji tafiti zaidi kuhusiana na hali ya Kimaragoli katika eneobunge la Uriri. Utafiti huu ulitambua pengo hili na kudhamiria kutafitia udumishaji wa Kimaragoli katika eneo Uriri. Ili kutimiza lengo hili, utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo : kuchunguza mikakati inayotumika kudumisha lugha ya Kimaragoli katika eneobunge la Uriri ; kutathmini umilisi wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake katika eneobunge la Uriri ; kubainisha athari ya lugha ya Kiluo katika Kimaragoli na kujadili mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli katika eneobunge la Uriri. Nadharia za Mtagusano Lugha iliyoasisiwa na Weinreich (1953) na kuboreshwa na Thomason na Kauffman (1988) na Uzalishaji Kijamii iliyoasisiwa na Bourdieu (1977) na Uhuishaji Kiethnoisimu ya Giles, Bourhis na Taylor (1977) zilikuwa kiunzi cha utafiti huu. Utafiti huu ulitumia miundo ya Uauzi na Uchanganuzi Linganishi. Idadi jumla ya watafitiwa ilikuwa Wamaragoli 20,000 katika Wadi 5 za eneobunge la Uriri. Fomula ya Yamane (1967) ilitumika kupata sampuli wakilishi ya watafitiwa 390 walioteuliwa kimaksudi. Mbinu ya kupata sampuli ya kimaksudi pia ilitumika kupata watafitiwa 5 na wanakundi 10 kwa ajili ya mahojiano na mijadala. Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji, mahojiano, mjadala wa kundi lengwa na ratiba ya uchunzaji. Uaminikaji na Udhabiti wa vifaa vya utafiti ulifanyiwa Idarani baada ya Utafiti awali kufanyika. Data ya kiwingiidadi ilichanganuliwa kwa kutumia idadi za kiumaratokezi, asilimia na kuwasilishwa kwa kutumia chati duara, majedwali, grafumihimili na maelezo. Data ya kithamano ilinukuliwa, kutafsiriwa na kusarifiwa kwa kuzingatia maudhui mbalimbali na unukulishi wa data iliyorekodiwa ulifanywa kimaandishi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba mikakati inayopendelewa sana ni matumizi ya idhaa za Kimaragoli wastani (75.8%), watoto kufundishwa Kimaragoli na wazazi wastani (73.2%) na kuongoea Kimaragoli nyumbani wastani (72.7%). Aidha, utafiti ulibaini kwamba wazee na makamo wana kiwango cha juu cha umilisi wa kimsingi wa Kimaragoli (93.4%), ikifuatiwa na watoto (93.3%) na vijana (89%). Umilisi huu kwa vijana na watoto unaathiriwa na utangamano na Kiluo. Utafiti ulitambua kwamba Kimaragoli kimeathiriwa pakubwa na Kiluo katika maeneotumizi, kileksimu na pia kwa wasemaji wa Kimaragoli. Uchanganyaji na uhamishaji ndimi kati ya Kimaragoli na Kiluo unashuhudiwa sana miongoni mwa vijana na watoto. Pia, utafiti huu ulitambua kwamba Wamaragoli wana mielekeo chanya kuhusu lugha yao ijapokuwa inatofautiana kiumri. Hata hivyo, mwelekeo ulikuwa wastani wa 83.4%. Matokeo haya yanaashiria kwamba Kimaragoli kinadumishwa kutokana na mikakati imara, umilisi wa kiwango cha juu, kutoathiriwa pakubwa kileksimu na kuwepo kwa mwelekeo chanya miongoni mwa Wamaragoli na Waluo. Matokeo haya yatakuwa amilifu kwa wataalamu wa kupanga lugha katika jamii, taaluma ya Kiswahili katika kujenga dafina ya mtagusano isimu, Wizara ya Elimu na dola za Kimataifa hasa AU na UNESCO wanaohusika katika utafiti wa kuhatarishwa kwa Lugha na Mikakati ya Uhuishaji wa Lugha ulimwenguni kote.

**ABSTRACT**

Numerous research projects on language death and attrition due to failure of maintenance have been done in different languages in Kenya and across the globe. Currently, this problem is well documented by international bodies like the United Nations and the African Union as well as their member states. Some of the languages researched had initially migrated from their ancestral land. Maragoli language spoken in Uriri constituency is one of these languages that migrated from their ancestral land. Whereas some of these languages have been researched and well documented, little had been done on Maragoli in Uriri Constituency. It is worth noting that without empirical evidence on the present situation of Maragoli, we could not establish if it was being maintained or not. It is from this aforementioned problem that this research was conceived. This research aimed at investigating maintenance of Maragoli language in Uriri Constituency. In order to fulfil this aim, the following objectives were used: to establish the language maintenance strategies used by the Maragoli speakers in Uriri Constituency; to evaluate the language competencies and performance of Maragoli speakers; to discuss linguistic impact of Maragoli and Dholuo contact and to discuss the role of attitudes of Maragoli and Dholuo speakers in maintenance of Maragoli language. The research was guided by an eclectic theories of Language Contact theory as propounded by Weinreich (1953) and improved by Thomason and Kauffman (1988), Social Reproductive Theory espoused by Bourdieu (1977) and Ethnolinguistic Revitalization theory as propounded by Giles, Bourhis and Taylor (1977). The research adopted descriptive survey and comparative research designs. The target population was 20,000 Maragoli speakers spread in 5 Wards of Uriri Constituency. Yamane's Formula (1967) was used to derive a representatuive sample of 390 respondents selected purposively. Data was collected using questionannaires, interviews and focus group discussion. Purposive sampling was also used to select 5 interviewees and 10 discussants. Quantitative data was analysed using frequency counts, percentages and means and presented using tables, graphs and pie charts. Qualitative data was transcribed, translated, organised into thematic areas and verbatim reports written. Findings revealed that Maragoli speakers have employed strategies of maintaining their language. The most preferred strategies included listening to Maragoli radio stations (75.8%), parents teaching children at home (73.2%) and speaking Maragoli at home (72.7%). However, variations in strategies were witnessed from one group to another. It was also discovered that the middle age and elderly group displayed highest competence level of Maragoli (93.4%), followed by children (93.3%) and youth (89%). It was discovered that competence among the youth and children is majorly affected by Dholuo interference in various domains. Dholuo interferes with Maragoli in domain use, lexicalization and individual Maragoli speaker's speech patterns. Code mixing and code switching is experienced among the youth and children. This has led to intergenerational changes of Maragoli language in Uriri. Maragoli speakers have displayed positive attitude towards their language despite slight variations in age groups. The average positive attitude was reported at 83.4%. These findings indicate that Maragoli is being maintained due to effective strategies, good competence levels, negligible lexical interference by Dholuo and positive attitude by Maragoli and Dholuo speakers towards the language. These findings will be pertinent and insightful to speakers of endangered ethnic languages on how they can revive their languages, building of scholary work on contact linguistics in Kiswahili, language planning technocrats, Ministry of Education and International bodies like AU and UNESCO who are involved in Research and Documentation of Language Endangerment and Language Revitalization Strategies across the globe.

**YALIYOMO**

UNGAMO……………………………………………………………………………...…ii

TABARUKU……………………………………….…………………………iii

IKISIRI……………..………………………………………...…………………...iv

ABSTRACT.........................................................................................................v

YALIYOMO…………………………………..………………………..………..vi

ORODHA YA MAJEDWALI.................................................................................vii

ORODHA YA VIELELEZO…………………………………………………..….xiv

ORODHAYA VIAMBATISHO...……………....………….……………...……......xvi

UFAFANUZI WA ISTILAHI…………………………………………….…...........xvii

AKRONIMU NA VIFUPISHO………………………………………………...…..xviii

SHUKRANI……………………………………………..……………...……xix

**SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI**

1.1 Utangulizi……………………………………………………………….….1

1.2 Usuli wa Mada.……………………………………………………………..…1

1.2.1 Kimaragoli na Wasemaji wake………………………………………………...4

1.2.2 Historia ya Wamaragoli katika eneobunge la Uriri………………………………6

1.3 Suala la Utafiti……………………………………………………….……..…9

1.4 Madhumuni ya Utafiti……………………………………………………..…...….9

1.5 Maswali ya Utafiti……………………………………………………….......….9

1.6 Sababu za uteuzi wa Mada ……………………..…………………………...10

1.7 Umuhimu wa Utafiti…………………………………………………………10

1.8 Upeo wa Utafiti...............................................................................................11

1.9 Nadharia za Utafiti……………………………………………………..….12

1.9.1 Nadharia ya Mtagusano Lugha.......................................................................12

1.9.2 Nadharia ya Uzalishaji Kijamii......................................................................17

1.9.3 Nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu…………………………………….……...19

1.9.4 Mwingiliano wa Nadharia..........................................................................22

1.10 Hitimisho..........................................................................................................23

**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI**

2.1 Utangulizi………………………………………….………………...……24

2.2 Dhana ya Udumishaji Lugha………………………………………….……..24

2.3 Mikakati ya Udumishaji lugha…………………………………………..…..26

2.3.1 Mkakati wa Elimu…………………………………………….…...…26

2.3.2 Uzungumzaji Lugha Nyumbani………………….…………………………...29

2.3.3 Dini ……………………………….……………………………………......31

2.3.4 Utumiaji wa wazee kudumisha lugha………..…………………………......33

2.3.5 Matumizi ya Tehama katika Udumishaji lugha……………………………....35

2.3 6 Kutembeleana miongoni mwa Wamaragoli ……………………....………...37

2.3.7 Mikutano ya Kijamii……………...……………………………………..…....39

2.4 Viwango vya Umilisi na Utendaji Lugha katika Jamii………………………………40

2.4.1 Umilisi na Utendaji wa Lugha Miongoni mwa Watoto…………...…………....41

2.4.2 Umilisi na Utendaji wa Lugha Miongoni mwa Vijana……………………..…..45

2.4.3 Umilisi na Utendaji wa Lugha Miongoni mwa makamo na wazee………...…...50

2.5 Athari za Mtagusano Lugha……………………………………………..…..54

2.5.1 Athari ya Kifonolojia……………………………………………………….55

2.5.2 Athari ya Kileksimu………………………………………………………...59

2.5.3 Athari ya Kimofolojia………………………..…………..………………...62

2.5.4 Uhamishaji Msimbo…………………………………...………………...65

2.5.5 Uchanganyaji msimbo…………………………………………………….....68

2.6 Mielekeo katika Udumishaji Lugha…………..……………………………………71

2.7 Hitimisho…………………………………………………………………….....78

**SURA YA TATU: MBINU NA NJIA ZA UTAFITI**

3.1 Utangulizi………………………………………………………………..…..80

3.2 Muundo wa Utafiti……………………………………………………..….80

3.3 Eneo la Utafiti……………………………………………………..………81

3.4 Idadi Lengwa…...……………………………………………………..…....82

3.5 Idadi ya Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli……………………..……......83

3.6 Mbinu na Vifaa vya Utafiti…………………………………………….……....85

3.6.1 Mwongozo wa Mahojiano……………………………………..…....86

3.6.2 Mwongozo wa Mjadala wa kundi lengwa……………………………....87

3.6.3 Mwongozo wa Uchunzaji…………………………………………….…87

3.6.4 Hojaji…………………………………………………………………...…87

3.7 Uaminikaji na Udhabiti wa Vifaa vya Utafiti……………………..……..……......90

3.7.1 Uaminikaji wa Vifaa vya Utafiti…………………………………..…90

3.7.2 Udhabiti wa Vifaa vya Utafiti……………………………………......90

3.8 Ukusanya Data ya Utafiti……………………………………………........…91

3.8.1 Ukusanyaji wa Data kwa Hojaji…………………………………….....91

3.8.2 Ukusanyaji Data kwa Uchunzaji………………………………………...92

3.8.3 Ukusanyaji Data kwa Mahojiano…………………………………….....96

3.8.4 Ukusanyaji Data kwa Mjadala wa Kundi lengwa…………………………......97

3.9 Maadili katika Utafiti……………………………………………..…..……98

3.9.1 Ulinzi wa Saikolojia ya Watafitiwa………………………...……………..…98

3.9.2 Ridhaa ya Utafiti………………………………………………..…......…98

3.9.3 Haki kwa Usiri wa Watafitiwa……………………………………….....99

3.9.4 Ulinzi wa Data…………………………………………………………………100

3.10 Uchanganuzi wa Data……………………………………………………..100

3.10.1 Uchanganuzi wa Data Kithamano……………………...………………101

3.10.2 Uchanganuzi wa Data Kiwingiidadi……………………………………………102

3.11 Hitimisho………………………..……………………………………….........103

**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO**

4.1 Utangulizi…………………………………………………………………………..104

4.2 Takwimu za Habari za Kimsingi za Watafitiwa…….……………………………...104

4.2.1 Msambao wa Kiwango cha mwitiko wa Watafitiwa……………………….……..104

4.2.2 Nduni za Kidemografia za Watafitiwa……………………………………………105

4.2.2.1 Jinsia……………………………………………………………...……..105

4.2.2.2 Umri wa Watafitiwa………………...………………………………………...106

4.2.2.3 Lugha ya Mtafitiwa……………………………………………………………...106

4.2.2.4 Ndoa Miongoni mwa Watafitiwa…………………………..……………106

4.3 Mikakati ya Udumishaji wa Kimaragoli Uriri……………………………………...106

4.3.1 Kusikiza Idhaa za Redio Zinazotangaza kwa Kimaragoli ……………………107

4.3.2 Kufundish(w)a kusiko rasmi na Kuamilia Kimaragoli Nyumbani…………….108

4.3.3 Kuongea Kimaragoli Nyumbani…………………………………………….…....111

4.3.4 Kutumia Kimaragoli katika ibada……………………………….…………….……114

4.3.5 Mikutano……………………………………………………………………………116

4.3.6 Kutembeleana miongoni mwa Wamaragoli …………………...……………...121

4.3.7 Sherehe za kitamaduni……………….……………………………………...124

4.3.8 Watoto kufundishwa Kimaragoli shuleni………………...……………….....126

4.3.9 Siasa na Utawala…………………………………………..……………...…128

4.3.10 Ndoa baina ya Wamaragoli na Waluo ………………...……………………..130

4.4 Umilisi na Utendaji miongoni mwa makundi ya Wamaragoli……………………..130

4.4.1 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Watoto wa miaka 12-17…….…………...131

4.4.2 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Vijana wa miaka 18-35…………………133

4.4.3 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Makamo na Wazee……………………....136
4.5 Athari ya Kiluo kwa Kimaragoli katika Uriri…………………………...………138
4.5.1 Maoni kuhusu athari ya Kiluo kwa Kimaragoli……..……..………………....139
4.5.2 Athari ya Kijumla kwa Umri wa Miaka 12-17…………...……………………143
4.5.2.1 Maoni ya watoto kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli……………………………………………………………..144
4.5.2.2 Maoni ya vijana kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli……………………………………………………………..145
4.5.2.3 Maoni ya makamo na wazee kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli…………………..………………………………………….....145
4.5.3 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo…………………………...………148
4.5.3.1 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Watoto………..…..149
4.5.3.2 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Vijana………......153
4.5.3.3 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Makamo na Wazee..159
4.6 Mielekeo ya lugha Katika Udumishaji wa Kimaragoli…………………………….163
4.6.1 Mielekeo ya Wamaragoli kuhusu Kimaragoli…………………………………164
4.6.1.1 Fahari Miongoni mwa Wamaragoli…………..…………………………..164
4.6.1.2 Thamani Miongoni mwa watoto wa Kimaragoli…………………………...176
4.6.1.3 Kupendelea Matumizi ya Kimaragoli……………………………….......185
4.6.1.4 Uamiliaji na Ujifunzaji usio rasmi wa Kimaragoli…………………………193
4.6.1.5 Heshima ya lugha miongoni mwa Wamaragoli……………………...…203
4.6.1.6 Utambulisho kama mzungumzaji wa Kimaragoli……………………...…..212
4.6.2 Mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli…………………………………….214
4.6.2.1 Kujifunza Kimaragoli tangu Utotoni……………………...……….......215
4.6.2.2 Ndoa kati ya Waluo na Wamaragoli…………………………...……..216
4.6.2.3 Mwelekeo chanya kuhusu Wamaragoli…………………………...…..217

4.6.2.4 Kuzungumza Kimaragoli mara kwa mara……………………………….218

4.7 Hitimisho……………………………………………………………………..….220

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi…………………………………………………………………..221

5.2 Muhtasari wa tasnifu…………………………………………………………….221

5.3 Muhtasari wa Matokeo……………………………………………...……221

5.3.1 Mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli Uriri……...…………………….…..221

5.3.2 Umilisi na Utendaji wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake Uriri……………………………………………………………………………….222

5.3.3 Athari ya lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli inayozungumzwa Uriri……………………………………………………………………………….223

5.3.4 Mielekeo ya Wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo kuhusu Uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri…………...……………………….……………...........224

5.4 Mahitimisho…………………………………………………………..…….225

5.4.1 Mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli Uriri…………………...…………..….225

5.4.2 Umilisi na Utendaji wa lugha ya Kimaragoli Miongoni mwa Wasemaji wake Uriri………………………………………………………………………………226

5.4.3 Athari ya lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli inayozungumzwa Uriri……………………………………………………………………………….226

5.4.4 Mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Waluo kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri…………………………………………….……………....227

5.5 Mapendekezo……………………………………………………….……...228

5.5.1 Mapendekezo ya Kisera na Kiutekelezi………………………….………….228

5.5.2 Mapendekezo ya Utafiti waBaadaye………………………………..……....228

MAREJELEO…………………………………………………………………..230

VIAMBATISHO…………………………………………………………….243

## ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI** **UKURASA**

2.1 Nomino zilizokopwa kutoka Kinorisi Azali hadi Kiingereza Azali...........................60

2.2 Maneno Mkopo kutoka kwa Kiarabu……………………………………………..61

3.1 Kiunzi cha Uteuzi wa Sampuli wa Kata Ndogo katika Wadi………………………..84

3.2 Majukumu ya Vifaa vya Utafiti……………………………………………...86

4.1 Msambao wa mwitiko……………….…………………………………………..105

4.2 Jinsia ya Watafitiwa…………………………………………………………...106

4.3 Athari jumla za Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli………………………...141

4.4 Maneno ya Kiluo katika Kimaragoli…………………………………………….143

4.5 Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa watoto…..…………………..144

4.6 Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa vijana………………..……...145

4.7 Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa makamo na wazee……..…...146

4.8 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo miongoni mwa watoto…..………………….150

4.9 Ruwaza za Uchanganyaji na Uhamishaji msimbo nyumbani miongoni mwa watoto..............................................................................................................................151

4.10 Uingizaji wa maneno ya Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa vijana....…..…153

4.11 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo miongoni mwa vijana…………………..…154

4.12 Ruwaza za Uchanganyaji na Uhamishaji msimbo nyumbani miongoni mwa vijana…………………………………………………………………………...156

4.13 Uingizaji wa maneno ya Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa makamo na wazee…………………………………………………………………………...159

4.14 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo miongoni mwa makamo na wazee ……….160

4.15 Ruwaza za Uchanganyaji na Uhamishaji msimbo nyumbani miongoni mwa makamo na wazee……………………………………………………………………..…161

4.16 Aibu ya kutoongea Kimaragoli miongoni mwa watoto…………………………...165

4.17 Mimi huona aibu kuona watoto wa Kiluo wanaongea lugha yao na wetu hawajui Kimaragoli…………………………….……………………………….…………….174

4.18 Nitahisi vibaya sana ikiwa sisi tutawacha kuongea Kimaragoli na kuongea Kiluo……………………………………………………………………………………175

4.19 Hakuna haja ya mimi mtoto kuongea Kimaragoli hapa Uriri……..……………...176

4.20 Tunaongea Kiluo kwa sababu ya uchumi Uriri….……………………………..175

4.21 Hakuna haja ya mimi Kijana kuongea Kimaragoli hapa Uriri……………………179

4.22 Hakuna haja ya mimi Makamo au Mzee kuongea Kimaragoli hapa kwa Waluo...180

4.23 Tunapenda kusikiliza idhaa za Kimaragoli………….…………………………...190

4.24 Mimi hufundisha watoto wetu na marafiki Waluo Kimaragoli…………………...196

4.25 Mimi kama kijana sina muda wa kujifunza Kimaragoli…………………………..199

4.26 Mimi hufundisha watoto wangu na marafiki wangu wa Kiluo Kimaragoli………201

4.27 Kiluo kinanipa heshima kubwa kuliko Kimaragoli……………………………….203

4.28 Wamaragoli tunaheshimu lugha zingine hapa Uriri………………………………209

4.29 Mimi kijana hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli…………………………..213

4.30 Mimi Mzee hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli…………………………...214

## ORODHA YA VIELELEZO

**KIELELEZO ……UKURASA**

Kielelezo 4.1 Umilisi na Utendaji wa Kimaragoli miongoni mwa watoto…………….131

Kielelezo 4.2 Umilisi na Utendaji wa Kimaragoli miongoni mwa vijana……………...134

Kielelezo 4.3 Umilisi na Utendaji wa Kimaragoli miongoni mwa makamo na wazee...136

Kielelezo 4.4 Uingizaji wa maneno ya Kiluo katika Kimaragol miongoni mwa watoto..........................................................................................................................149

Kielelezo 4.5 Najivunia kama Mtoto kuongea Kimaragoli…………..………………..165

Kielelezo 4.6 Hisia kuhusu Kimaragoli kukoma kuzungumzwa Uriri…………………167

Kielelezo 4.7 Najivunia kama Kijana kuongea Kimaragoli ……..…………………….169

Kielelezo 4.8 Mimi huona aibu kuona vijana wa Kiluo wanajua kuongea lugha yao na mimi sijui Kimaragoli…………………………….………………………………….171

Kielelezo 4.9 Najivunia kama Makamo na Mzeee kuongea Kimaragoli…….………...173

Kielelezo 4.10 Tunaongea Kimaragoli ili kukidumisha………………………….…181

Kielelezo 4.11 Tunafahamu Kiluo kwa sababu ya Uchumi hapa Uriri……………..…183

Kielelezo 4.12 Tunaongea Kimaragoli na watu wa ukoo………………………………186

Kielelezo 4.13 Tunaongea Kimaragoli zaidi kuliko Kiluo…………………………..187

Kielelezo 4.14 Tunaongea Kimaragoli na Ukoo wetu….……………………………...189

Kielelezo 4.15 Tunapenda kusikiliza idhaa za Kimaragoli………………………….....191

Kielelezo 4.16 Sina Muda wa kujifunza Kimaragoli…………………………………..194

Kielelezo 4.17 Kimaragoli kiendelee kufundishwa na kurithishwa……………………195

Kielelezo 4.18 Nikioa au kuolewa haitakuwa lazima watoto wangu kujua Kimaragoli……………………………………………………………………………...198

Kielelezo 4.19 Maoni ya Vijana kuhusu Kimaragoli kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee………………………………..……………………………………..…...200

Kielelezo 4.20 Maoni ya makamo na wazee kuhusu Kimaragoli kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee…………………………………………………………………...202

Kielelezo 4.21 Heshima ya Wamaragoli kwa lugha zingine…………………………...206

Kielelezo 4.22 Maoni ya Makamo na Wazee kuhusu Kimaragoli kuheshimiwa na kabila zingine hapa Uriri…………………..........................................................................208

Kielelezo 4.23 Tunaheshimu lugha zingine……………………………………………211

Kielelezo 4.24 Lugha yetu inaheshimiwa na wengine hapa Uriri……………………...212

## ORODHA YA VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO** **UKURASA**

Kiambatisho A: Mwongozo wa mahojiano na viongozi wa kijiji ……………………..243

Kiambatisho B: Matokeo ya mahojiano na viongozi wa kijiji…….…………………...244

Kiambatisho C: Mwongozo wa mahojiano na watu wa kwanza kuwasili Uriri.............248

Kiambatisho D: Matokeo Mahojiano ya mtafiti na wazee wa kwanza kuwasili Uriri…249

Kiambatisho E: Matokeo ya mahojiano ya mtafiti na mzee wa kwanza kuwasili Uriri……………………………………………………………………………….252

Kiambatisho F: Mwongozo wa mahojiano na vijana wanaozungumza Kimaragoli……………………………………………………………………...255

Kiambatisho G: Matokeo ya mahojiano kati ya mtafiti msaidizi na vijana wanaozungumza Kimaragoli…………………………...………………………....256

Kiambatisho H: Mwongozo wa Mjadala wa Kundi lengwa la wazawa wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli……………………...…………………………………259

Kiambatisho I: Matokeo ya mjadala wa Kundi Lengwa la wazawa wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli……………………………………………...……....260

Kiambatisho J: Mwongozo wa uchunzaji……………………………………...…265

Kiambatisho K: Hojaji ya watoto wa miaka kati ya 12-17…………………………..266

Kiambatisho L: Hojaji ya vijana kati ya miaka 18-35………………………………….269

Kiambatisho M: Hojaji ya makamo na wazee……………………………………….272

Kiambatisho N: Idhini ya Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Rongo………..…………...275

Kiambatisho O: Barua ya NACOSTI……………………………………..…………276

Kiambatisho P: Kibali cha NACOSTI ……………………………………………….277

Kiambatisho Q: Barua ya Wizara ya Elimu, Kaunti ya Migori……………………...278

Kiambatisho R: Barua ya Kamishna wa Kaunti ya Migori……………………...…..279

Kiambatisho S: Ramani ya Wadi katika eneobunge la Uriri…………………………...380

# UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Kimaragoli: | Ni lahaja inayozungumzwa na Wamaragoli. Pia huitwa Kimaragoli, Luragoli au Llogoli. Utafiti huu umetumia Kimaragoli. |
| Mkakati: | Mpangilio wa king'amuzi au usio wa king'amuzi, uliowekwa na Wamaragoli kwa ajili ya kudumisha lugha ya Kimaragoli. |
| Mwelekeo: | Hali ya kiakili iliyo na utaratibu au mpangilio wa kitajriba na inayoshinikiza mwitiko wa Mmaragoli au Mluo kuhusiana na Kimaragoli na Mmaragoli. |
| Uamiliaji lugha | Mchakato wa kupata lugha katika mazingira asilia. |
| Udumishaji lugha: | Hali ya lugha kuendeleza uhai wake licha ya kukumbwa na shinikizo kutoka kwa lugha nyinginezo. |
| Wamaragoli: | Ni watu ambao wamezaliwa katika utamaduni wa Mulogoli na wanasema lugha ya Kimaragoli eneo la Uriri na Migori kwa ujumla. |

# VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| HMU: | Haina Mwaka wa Uchapishaji |
| AU | :*African Union* |
| ACALAN | : *Academy for African Languages* |
| L1 | : Lugha ya Kwanza |
| L2 | :Lugha ya Pili |
| UNESCO | : *United Nations Educational, Social and Cultural Organization* |
| UN | : *United Nations* |
| NACOSTI | :*National Council for Science, Technology and Innovations* |
| K.M | : Kwa mfano |
| VLC | :*Visible Light Communication* |
| P.A.G | : *Pentecostal Assemblies of God* |
| KBC | *Kenya Broadcasting Corporation* |
| TY | Tafsiri Yangu |
| TYMS | Tafsiri ya Mtafiti Msaidizi |
| CBC | : *Competence Based Curriculum* |

# SHUKRANI

Shukrani zangu za awali ni kwa Mungu wangu; uhai amenitunuku kutenda yote haya. Pia faridhi kuwashukuru wahadhiri na wasimamizi wangu ninaowadhamini tangu kuanza safari za uzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo: Prof. Mohochi, S., Dkt. Nyandiba, C., Dkt. Kisurulia, S., Dkt. Ontieri, O., Dkt. Mwita, C., Dkt. Odero, O. na Dkt. Nyakoe, D.. Hatimaye, uhuru umepatikana baada ya safari ya kumbakumba kutamatikia kinoa miguu. Vilevile, nawashukuru wenzangu Bw. Kavoi, J., Bw. Barisecha, B., Bi. Burudi, J. na Bw. Nyonje, J. Kutakadamu si kazi nyepesi, hasa katika mazingira tulimoanzia. Nawashukuru wenzangu wa Uzamifu waliokuja baadaye Bw. Odawo, M., Bi. Sabula, A., Bi. Nyandwaro, L., Bw. Matara, P., na Bi. Owala, J. Namshukuru sana Bi. Mercy, K. kwa kuwa mtafiti msaidizi mwema na familia yake iliyojitolea kunisaidia kukusanya data na kutembea vijijini. Wema wenu Mungu awatuze. Nawashukuru wote waliojitolea kushiriki utafiti huu katika Kata mbalimbali za Uriri. Namshukuru bibi yangu, Caren Nekoye kwa kunivumilia kipindi kirefu ambacho nilikuwa Migori na hata kunichangia kifedha nilipokwama nyakati zingine. Mwisho sitamsahau Mwalimu, Mlezi, Mwelekezi, Mshauri na Marehemu Baba Ainea Sangili, maji ya Uzamifu nisingeyaogelea mapema hii kama si kwa msingi wako. Sijashuhudia hasara kubwa ulimwenguni kama kuondokewa nawe. Nimeyumba sana kihisia na kisaikolojia. Ulitamani siku zote unione nimevaa chepeo cha Uzamifu, lakini yote ya Mungu. Nampa kongole mamangu, Maria, kwa kunitia shime baada ya kundoka kwa baba. Ulianza kuuliza ninahafali lini kila nilipokuja nyumbani. Mungu akubariki siku zako zote ulimwenguni. Nawashukuru dada zangu wapendwa wangu, Serah, Anita, Hellen, Jackie, Afriah, Enid na Mago na kaka zangu Eric, Japheth na Fabian na familia zao kwa kunihimiza pia. Mwisho, Njambe, mwanangu, nimechora ramani. Ifuate kwa uwezo wa Mungu.

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imetanguliza tasnifu kwa kujadili vipengele mbalimbali vya utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni: usuli wa mada; suala la utafiti; madhumuni ya utafiti; maswali ya utafiti; sababu na umuhimu wa mada; eneo la utafiti; upeo na nadharia za utafiti.

## 1.2 Usuli wa Mada

Lugha ni kipengele muhimu sana katika maisha ya kila binadamu. Bila lugha, haiyamkiniki kuwa maisha ya binadamu yatakuwa na maana yoyote. Lugha ndiyo kani inayonatisha mahusiano ya kijamii pamoja na kuchapuza michakato mingine inayohusiana na binadamu. Kwa kuwa kila jamii ina lugha yake au lugha zake, hutokea kwamba lugha hizi zinajikuta katika mahusiano athirishi ya kiisimu kiasi cha lugha moja kuathiri nyingine kwa njia hasi au chanya (Blythe na Croft, 2012). Namna lugha zinavyojikuta katika mazingira haya ya wingilugha athirishi hutegemea sababu mbalimbali: uhamaji wa kila mara; sababu za kiuchumi, elimu na sera za ufundishaji miongoni mwa sababu nyinginezo. Sababu hizi ni za kijamii kwa mujibu wa Hudson (1996). Matokeo yake ni kwamba, lugha hizi zinajiongezea au kupunguza jumla ya msamiati. Wazawa wa lugha hizi hujikuta wanaimarisha au kudhoofisha lugha zao kutegemea athari hizi. Wanapoimarisha lugha zao, wazawa wake hujikuta katika mazingira ambayo lugha yao imetawala na kusambaa zaidi kuliko lugha nyingine yoyote katika mazingira ya wingilugha. Aidha, hutokea uwezekano mkubwa wa lugha iliyofaidika kujidumisha katika vizazi vingi baadaye. Kwa upande mwingine, lugha iliyodhoofika hujikuta katika hali ya hatari kwani wasemaji wake huanza kupunguza matumizi yake kimawasiliano, huanza kupoteza misamiati yake na hatima yake ni kupunguka kitakwimu kwa wasemaji wake. Lugha hizi zinapofika kiwango hiki cha

kukosa au kuwa na wasemaji wachache sana, basi huishia kufa kwani hazina wadumishaji wake (Crystal, 2000).

Suala la kudumisha lugha limekuwa tatizo katika vizazi mbalimbali ulimwenguni. Kama ilivyo sheria ya maisha, kisichoweza kujipigania uhai wake hufa, basi inalazimu lugha zote duniani kupigania udumishwaji wake. Ikiwa lugha haina satua ya kujidumisha, basi inaishia kuwa miongoni mwa lugha zaidi ya 2600 zilizopotea (au kufa) (Crystal, 2000; Croft, hmu). Udumishaji wa lugha za binadamu ni mchakato unaohitaji kwamba kila mzawa na msemaji lugha ahusike moja kwa moja katika matumizi yake ya kila mara licha ya kuzungukwa na lugha nyingine zenye uwezo mkubwa au uwezo sawa kiuamilifu. Wakati mwingine, wazawa wa lugha hujihusisha kwa kujua au bila kujua kwamba wanadumisha lugha zao. Hata hivyo, udumishaji huu si suala la mtu binafsi tu; hata vyombo vya dola chini ya wizara na tamaduni mbalimbali huhusika. Miaka ya hivi karibuni, tumeshuhudia shirika la UNESCO likitoa mapendekezo yanayotokana na ushahidi jarabati wa tafiti za wanalugha mbalimbali duniani. Mojawapo ya pendekezo ni kwamba wanajamii-lugha wote, kwa satua ya serikali au taasisi mbalimbali, wadumishe lugha zao, hasa zile zilizo katika hatari ya kupotea. Aidha, Umoja wa Afrika umefuata mkondo huu huu kwa kuunda taasisi ya ACALAN iliyo na jukumu la kusaidia kudumisha lugha za Kiafrika katika mataifa yote barani (AU, 1995). Satua hizi za uongozi husaidia kudumisha lugha maalumu, huhimiza na kuchapuza udumishaji wa lugha zilizo katika hatari ya kumezwa na lugha nyingine zilizo na hadhi au nguvu kubwa kiuamilifu katika maeneo mbalimbali ya kiisimu.

Katika tafiti mbalimbali zilizokwisha fanyika humu nchini (Obiero, 2013; Ngure, 2012; Odero, 2013), barani na kwingineko, jamii lugha kadhaa zimekuwa na tatizo la kudumisha lugha. Kwa mfano, nchini Afrika Kusini, watafiti wa lugha za Kihindi

(Mesthrie, 2007) walitambua kwamba katika muda wa miaka zaidi ya 147, lugha hizi zilipitia mabadiliko makubwa kiasi cha baadhi ya vizazi vya baadaye kukoma kusema lugha hizi na badala yake kujifunza na kutumia Kiafrikaana na Kiingereza. Kiafrikaana ndiyo lugha tawala iliyosemwa na watu wote bila kujali taifa ama lugha ya kwanza katika mji wa Western Cape ilhali Kiingereza kilitawala Kwa-Zulu Natal. Utambuzi huu ulichangia Wahindi kuanza juhudi za kufufua na kudumisha lugha zao katika uamilifu wa jamii (Mesthrie, 2007). Utafiti huu aidha unaonyesha namna ambavyo Wagiriki walipigania haki ya kudumisha Kigiriki nchini Afrika Kusini licha ya kwamba Kiingereza na lugha nyinginezo ndizo zilitawala. Wagiriki wenyewe walifanya juhudi za kuendeleza lugha hii kwa kuanzisha shule za Kigiriki, ambako walikifundisha, na hata waliandaa programu na kuzipendekeza kufundishwa katika baadhi ya vyuo vikuu. Palipokuwa na tatizo la walimu, waliwaleta kutoka taifa la Ugiriki. Tafiti hizi mbili zinaonyesha namna ambavyo tatizo la kudumisha lugha maalumu katika mazingira hatari ya kiisimu linachukuliwa kwa uzito mkubwa na wasemaji wenyewe. Haja ya kudumisha lugha hizi ni suala linalowashughulisha sio tu wazawa lugha bali pia vyombo vya dola na mifumo rasmi na isiyo rasmi ya shule (Mesthrie, 2007). Kinyume na ilivyo Ulaya na Marekani na baadhi ya mataifa ya Afrika kama vile Afrika Kusini na Nigeria, nchini Kenya, kuna uhaba wa tafiti zinazochunguza udumishaji wa lugha. Zilizoko kwa mfano Odero (2013) na Ngure (2012) zinazungumzia masuala ya uhamiaji lugha. Kwa mfano, Odero (2013) anadai mtagusano wa Kielmolo na Kisamburu umesababisha kudhoofika kwa Kielmolo kiasi cha lugha hii kuwa katika hatari ya kutoweka. Ngure (2012) anadai kwamba Kirendille kimo hatarini kupotea. Tafiti zao zinaonyesha kwamba wasemaji wa lugha maalumu wasipoweka juhudi kabambe katika udumishaji wa lugha yao, ipo hatari ya wao kuhamia lugha nyingine iliyo na satua na msambao mkubwa. Kisuba kwa upande mwingine, kilikuwa katika hatari ya kutoweka ila juhudi zilifanywa na serikali na wadau

mbalimbali kuhakikisha kwamba kilihuishwa na sasa wazunguzaji wake wanazidi kuongezeka. Lugha hii inadumishwa (Obiero, 2013).

### 1.2.1 Kimaragoli na wasemaji wake

Kimaragoli ni mojawapo ya lahaja za Kiluhya, ambazo ni za Kibantu cha Mashariki, na inasemwa nchini Kenya. Wasemaji wake wanapatikana katika kaunti ya Vihiga, eneo la Magharibi ambalo kiisimu, ndiyo asili ya lugha hii pamoja na lahaja nyingine za Kiluhya kama vile Kibukusu, Kimarama, Kisamia, Kiidakho, Kiisukha, Kitiriki, Kinyore, Kitsotso, Kiwanga, Kitachoni na kadhalika (Wangia, 2014). Kwa mujibu wa Ethnologue (2015) Kimaragoli pia hutamkwa Luragoli, Llogole, Logoli, Ragoli, Llugule, Maragoli au pia Uluragooli. Ina wasemaji wasiopungua 600, 000 kwa mujibu wa sensa ya 2009. Hata hivyo, idadi hii ni ile ya wasemaji walioko Kenya pekee. Kulingana na Guthrie (1971) katika Mahu (2009) Kimaragoli kinaainishwa katika kundi la JE41 huku kikiwa karibu na Ekegusii (JE42) na Kikuria (JE43). Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali (Ethnologue, 2015) Kimaragoli ni mojawapo ya lahaja za Kibantu cha Ziwa Kuu au cha Afrika Mashariki kilicho na asili yake katika lugha azali ya Naija-Kodofani. Kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu cha Afrika Mashariki, Kimaragoli ni lugha ambishi-bainishi.

Tafiti zinaonyesha kwamba Wamaragoli walihamia maeneo ya Vihiga kutoka Kameruni, wakiwa na wabantu wengine, na kwamba ni mojawapo ya lugha za Kikodofani-Naija (Nurse na Philippson, 2003; Sangili, 2017). Hata hivyo, katika fasihi simulizi yao, Wamaragoli wenyewe wanaamini kwamba asili yao ni Misri. Kulingana na Sangili (2014), inaaminika kwamba Wamaragoli walitokea maeneo ya *(Eluhya)* Kaskazini, yaani Misri. Baadaye, walihama kuelekea Kusini mwa Misri na wakaishi sehemu inayoitwa Lok Kitang, ambayo sasa ni Turkana, Kaskazini mwa Kenya. Uhamaji huu uliongozwa

na mzee aliyeitwa Andimi aliyeaminika kuwa na wake watatu. Mke wa kwanza ndiye aliyezaa Mulogoli. Mulogoli baadaye alioa na kupata watoto watano : wavulana wanne na msichana mmoja. Wavulana nao katika uzazi wao walipata watoto wengi ambao sasa ndio mbari ndogo za Mulogoli. Kuwepo kwa watoto wengi ndiko kulisababisha Wamaragoli kusambaa katika eneo zima la Vihiga na ujirani wake (Sangili, 2014) .

Hata hivyo, ilivyo hali ya mwanadamu, suala la watu kuhamia maeneo mengine kutoka maeneo yao asili ni la kawaida ; Wamaragoli hawakusazwa. Kutokana na mahojiano na wazee katika utafiti huu, Wamaragoli walianza kuhamia maeneo mbalimbali kama Kitale, Nandi na Migori kuanzia kipindi cha 1920 na hadi leo hii wanazidi kuhama. Sababu za kuhama ni changamani, ila inayotawala zaidi ni ya kutafuta rasilimali, hasa mashamba. Waliohamia maeneo ya Migori walijikuta katika hali ambapo wametoka kwa ujirani na lahaja nyingine za Kiluhya na kujikuta wamezingirwa na watu wanaozungumza Kiluo. Kimsingi, Kiluo ndicho chenye nguvu na kimesambaa katika gatuzi la Migori kuliko Kimaragoli, ambacho katika mazingira haya ya kiisimu, kina wasemaji wachache.

Wamaragoli wengi kwa mujibu wa utamaduni wao ni wakulima. Sababu moja kubwa ya wao kuhamia eneo la Migori ni kwa sababu waliona msitu mkubwa ambao ungefyekwa na kulimwa kwa ajili ya kuzalisha mazao. Aidha, wao ni wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Mbali, na kilimo, wengi wao ni Wakristo wa dhehebu la Marafiki (*Friends Church*). Hii ni kwa sababu Wamishenari (wa dhehebu la Quakers) walipokuja katika mkoa wa Magharibi kwa mara ya kwanza kutoka Marekani, waliweka makao yao maeneo ya Kaimosi mwaka wa 1902 na kusambaza kwa mara ya kwanza Injili ya Kristo miongoni mwa Wamaragoli. Kwa hiyo, wengi waliobatizwa katika Ukristo, walijiunga

na Kanisa la Marafiki. Hata hivyo, yapo madhehebu mengine kama vile Jeshi la Wokovu, P.A.G, Katoliki, African Holy Spirit na makanisa ya Kipentekote.

### 1.2.2 Historia ya Wamaragoli katika Kaunti ya Migori

Wamaragoli wana historia ndefu katika Kaunti ya Migori na hasa eneo la Uriri. Kutokana na mahojiano na wazee mbalimbali, mtafiti alitambua kwamba kundi la kwanza la Wamaragoli liliingia maeneo haya miongo ya 1930/1940. Kutokuwa na uhakika wa tarehe hizi kunatokana na sababu kwamba wengi wa waliohamia maeneo haya hawakuwa na elimu ya kutosha ya kujua kuhesabu miaka. Kundi hili la kwanza lilijumuisha familia 15 zilizotoka maeneo ya Bukuga, Vihiga, Madira, Muhanda, Ilinya na maeneo mengine ya Wilaya ya Kakamega Mashariki, ambayo sasa ni Wilaya ya Vihiga katika kaunti ya Vihiga. Familia hizi zilijumuisha mbari mbalimbali za Maragoli zikiwemo Vasaniaga, Vamavi, Vamuku, Vavulugi miongoni mwa mbari nyinginezo.

Baada ya kuhama kutoka wilaya ya Kakamega Mashariki, familia hizi zilisafiri kupitia ziwa Victoria hadi Homa Bay. Kutoka Homa Bay, walisafiri hadi Kisii katika eneo linaloitwa Nyaribari. Baadaye, walitawanyika katika maeneo mengine kama vile Nyakome, Gianchere, Boitang'are, Kiamokoma na Getembe. Mwishoni mwa miaka ya 1930, maeneo haya yalikuwa na Wamaragoli wengi mno na hii haikuwafurahisha wenyeji. Chifu wa wakati huo, bwana Nyandusi alihofia kwamba watu wake wangekosa mashamba na rasilimali hivyo aliongea na Chifu wa Migori, bwana Orema kuhusu kuhamishwa kwa baadhi ya Wamaragoli. Chifu Orema alikubali na hii ikawa ndio safari ya pili ya kuhamia eneo jipya baada ya kufunga safari yao kutoka Kakamega Mashariki. Hata kabla ya kuwasili katika maeneo ya Migori, mzee mmoja katika mahojiano alisimulia kwamba kiongozi mmoja, Bwana Otieno alikuwa ameota ujio wa watu wageni katika nchi yao ya Ujaluo. Aliota kwamba ameona watu wengi wakiwa kwenye maboti,

ziwani Victoria na wanaongea lugha ambayo wao (Waluo) hawaelewi. Watu hawa aliwaita 'Vayovoyi'. Neno hili lilitumiwa kurejelea lugha ya Kimaragoli ambayo ilionekana kuwa ngeni na ya kuyongoya. Kwa mujibu wa ndoto hiyo, watu hawa (Wamaragoli) walionekana wa amani, na mikononi walibeba majembe na shoka.

Walipowasili eneo la Migori, Wamaragoli walilakiwa na baadaye kukaribishwa kuhudhuria mkutano wa baraza ili waeleze usuli wao. Kwa kuwa Waluo walikuwa hawaelewi Kimaragoli, na wala Wamaragoli kufahamu Kiluo, mzee mmoja, bwana Okango, aliyeandamana na Wamaragoli wenzake, alijitokeza kukalimani semi zote zilizotamkwa kwenye mkutano huo. Mzee huyu ndiye aliyefahamu lugha hizi mbili na ndiye alijenga muamana kati ya jamii hizi mbili. Hatimaye, Wamaragoli walikaribishwa na kupewa eneo ambalo wangeishi. Chifu Orema alimtwika bwana Okello jukumu la kuhakikisha kwamba Wamaragoli hawa walikuwa wamepata eneo walilokuwa wametengewa. Hivyo, aliwaonyesha mipaka ya msitu ambao ulijaa wanyama wakali kama vile simba, chui, nyati, nyoka, swara na kadhalika. Hii ndiyo ingekuwa ardhi yao na hakuna mtu yeyote aliyestahili kuja kuwahamisha kwa namna yoyote. Wamaragoli hawa baadaye walienda kwenye mlima, wakaomba, wakaimba na kurai Mungu awape amani na ufanisi katika nchi mpya ambayo walikuwa wamehamia. Ni kwenye mlima huu ndipo walijenga kanisa la Marafiki la kwanza. Eneo hili baadaye waliliita Bware (*Vwari*). *Vwari* katika Kimaragoli ina fasili ya madhabahu. Kutokana na mahojiano ya wazee mbalimbali, aliyeongoza shughuli hizi aliitwa Mzee Igunza.

Baada ya kufyeka msitu na kuanza maisha mapya, Wamaragoli wengine walikuja kutoka Kisii na pia Kakamega ya Mashariki. Kwa kuwa walianza kuwa wengi, baadhi yao walihamia maeneo ya Kuria na hatimaye kuingia Tanzania. Utafiti wa Shirika la Ethnologue (2015) unaonyesha kwamba Wamaragoli wengi wangali Tanzania, mkoa wa

Mara. Hata hivyo, kwa kuwa walikuwa wageni, uhasama wa kijamii katika maeneo ya Kuria na Tanzania ulisababisha baadhi yao kurudi Migori na kuishi pamoja na wenzao. Waliomba nafasi zaidi ya mahali pa kuishi na huu ukawa mwanzo wa wao kusambaa maeneo mengine ambayo sasa ndiyo Kanyamkago Magharibi, Kanyamkago Kaskazini, Kanyamkago ya Kati, Kanyamkago Kusini na Kanyamkago Mashariki katika eneobunge la Uriri. Aidha, wapo wengine wanaoishi maeneobunge ya Suna Mashariki, Suna Magharibi, Rongo, Awendo, Migori, Kuria Magharibi na Kuria Mashariki katika Kaunti ya Migori. Wamaragoli wengine wamesambaa hadi katika Kaunti jirani kama vile Homa Bay na Kisii.

Kama zinavyodai tafiti mbalimbali (Crystal, 2000 ; UN, 2008; Eckert, 2008; Haynes, 2010) kuhusu mifanyiko ya kiisimujamii wakati ambapo lugha mbili (moja maarufu na yenye nguvu, na nyingine dhaifu na isiyo maarufu) zinakutana, huishia kwamba iliyo dhaifu aghalabu humezwa na iliyo na nguvu zaidi. Kumezwa huku ndiko wataalamu wengi hukuita kufa kwa lugha. Mchakato wa kumezwa kwa lugha si wa siku moja tu bali ni wa muda mrefu. Wasemaji wake huacha kusema lugha yao na kujifunza iliyo na nguvu, na kadiri inavyozidi kukosa wasemaji wa kila mara, ndivyo inazidi kutoweka katika ulimwengu wa lugha. Hata hivyo, siyo lugha zote duniani zinazojikuta katika mazingira haya ya kiisimu hufa au kutoweka, zipo lugha ambazo hujidumisha. Lugha ya Kimaragoli ni mojawapo ya lugha zinazojidumisha katika mazingira haya ya wingilugha. Sababu zinazochangia lugha hii kujidumisha zilihitaji utafiti wa kina ili kuzifahamu. Pamoja na kufahamu sababu hizi, palitokea haja ya kufanya utafiti wa nyanjani kutambua ikiwa lugha hii imeathiriwa au kuathiri lugha jirani katika kipindi hiki tangu miaka ya 1930/1940 ambapo inakisiwa ni miaka ambayo Wamaragoli wa kwanza walihamia maeneo ya Migori.

### 1.3 Suala la Utafiti

Kimaragoli kinachozungumzwa katika gatuzi la Migori na hasa Uriri ni mojawapo ya lugha zilizohamia maeneo mengine mbali na asili yake. Kinyume na Kisuba kilichomezwa na Kiluo, Kimaragoli kinaonyesha udumishwaji wake. Tokeo hili la kiisimu lilihitaji ufumbuzi kwa lengo la kuweka wazi sababu za lugha moja kujidumisha na nyingine kushindwa katika mazingira yaleyale ya kiisimu. Utafiti huu ulitambua pengo hili na kulenga kuchunguza udumishaji wa Kimaragoli Uriri. Kulikuweko na haja ya kufanya utafiti kipindi hiki ili kutambua hali halisi ya udumishaji wake kuwa ni zaidi ya miaka 78 tangu Wamaragoli wa kwanza kuhamia eneo hili la Uriri ambako Kiluo kinazungumzwa kwa wingi. Aidha, kwa kuwa mazingira ya mtagusano lugha huwa ya kipekee kwa kila lugha, ilikuwa muhimu kufanyia Kimaragoli utafiti ili kuthibitisha ikiwa kinajidumisha Uriri. Tafiti zinadai kwamba udumishaji lugha ni dhana changamani inayotofautiana kimkakati na kimielekeo na huhitaji kutafitiwa katika upekee wake.

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza udumishaji lugha ya Kimaragoli eneobunge la Uriri.  Ili kutimiza lengo hili, utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo :

i. Kuchunguza mikakati inayotumika kudumisha lugha ya Kimaragoli Uriri.
ii. Kutathmini umilisi wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake Uriri.
iii. Kuchunguza athari ya lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli kinachozungumzwa Uriri.
iv. Kujadili mielekeo ya wasemaji wa Kiluo na Kimaragoli kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulitarajiwa kujibu maswali yafuatayo :

i. Ni mikakati gani inayotumika kudumisha lugha ya Kimaragoli Uriri ?
ii. Je, viwango vya umilisi ni vipi miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli Uriri?
iii. Lugha ya Kiluo imeathiri vipi Kimaragoli kinachozungumzwa Uriri ?
iv. Je, wasemaji lugha za Kiluo na Kimaragoli wana mielekeo ipi kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri?

## 1.6 Sababu za Uteuzi wa Mada

Mada hii iliteuliwa kwa sababu kuna uhaba wa tafiti katika Kiswahili kuhusu suala la udumishaji wa lugha, hasa katika muktadha wa lugha za Kiafrika. Vilevile, utafiti huu ulifanyika kwa lengo la kutimiza mwito wa UNESCO na Azimio la Asmara chini ya Muungano wa Afrika kuhusu haja ya kutafitia na kudumisha lugha asili (UNESCO, 2003 ; AU, 1995 ; Constitution of Kenya, 2010). Pamoja na hizo sababu, kutodumisha lugha yoyote kuna hasara zake kama vile kupotea kwa vipopo vya tamaduni na falsafa za lugha, kupoteza uwezo wa kipekee wa kiisimu wa jamii kujieleza, kupoteza uwezo wa kipekee wa jinsi ya kutangamana kijamii (Constitution of Kenya, 2010) na hivyo palikuwa na haja ya kufanya utafiti katika lugha za Kiafrika na nyinginezo ulimwenguni kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa jinsi ya kuzidumisha lugha hizi (Thorold, 2005). Aidha, Kiluo kiliteuliwa kwa sababu ndicho kinatagusana na Kimaragoli kwa upana zaidi ya lugha zingine zilizo eneobunge la Uriri na Migori kwa ujumla. Mwisho, lugha ya Kiswahili haijapewa kipaumbele katika utafiti wa lugha za Kiafrika; mada hii imeteuliwa kutafitiwa katika Kiswahili kama chagizo na chachawizo la kuendeleza lugha za Kiafrika kwa kutumia lugha za Kiafrika.

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa taaluma ya Isimu Mtagusano kwani utachangia data ya kipekee ya mtagusano lugha baina ya Kimaragoli na Kiluo. Aidha, utafiti huu

utakuwa na umuhimu katika taaluma ya Kiswahili kwani utachochea ari ya kutumia Kiswahili kutafitia lugha za Kiafrika badala ya kutumia Kiingereza, Kifaransa au lugha kuu za Kimagharibi. Itakuwa ishara tosha kwamba Kiswahili kimekomaa kutekeleza wajibu muhimu kama zifanyavyo lugha za mataifa yaliyoendelea. Tatu, utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa wadau wa kuunda sera za lugha asili katika mfumo wa elimu nchini Kenya kwa sababu elimu na udumishaji lugha za kiasili ni masuala yanayoandamana. Nne, matokeo ya utafiti huu yatawafaidi Wamaragoli kwa sababu yatawapa shime ya kudumisha lugha yao. Hii ni kwa sababu, katika Kaunti ya Vihiga, mwaka wa 2019, wazee wa Kimaragoli walilalamika katika vyombo vya habari kwamba vijana na watoto wameanza kuacha kuzungumza lugha yao na kuhamia Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia kwa kuwapa maarifa ya jinsi vipengele kama vile mielekeo, teknolojia, mikutano na kadhalika vinaweza kutumika katika kudumisha lugha katika umri huu wa vijana.

**1.8 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika eneobunge la Uriri, Kaunti ya Migori. Wadi zilizoteuliwa ni Kanyamkago Kusini, Kanyamkago Mashariki, Kanyamkago Magharibi, Kanyamkago Kaskazini na Kanyamkago ya Kati. Sehemu hizi ziliteuliwa kwa sababu hapa ndipo Wamaragoli wengi wanaishi ingawa kunao wengine waliosambaa, japo kwa idadi ya chini, katika maeneo ya Awendo, Rongo mjini na Kuria. Utafiti huu umeteua eneo la Uriri ingawa kunao Wamaragoli wengine katika maeneo ya Kisii, Kitale, Nandi, Eldoret na Mlima Elgon. Hata hivyo, Wamaragoli wa Uriri ndio wengi zaidi kuliko haya maeneo mengine. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza udumishaji lugha miongoni mwa Wamaragoli kwa kujifunga kwa lugha inayozungumzwa kuliko andishi. Hii ni kwa sababu lugha andishi inatenda kazi ya kuhifadhi lugha huku udumishaji lugha ukilenga zaidi dhana ya uzungumzaji na utumiaji wake katika miktadha mbalimbali. Aidha, lugha

nyingi zimejidumisha kwa miaka mingi bila ya kuandikwa mahali popote ila zinarithishwa kwa njia ya mdomo. Utafiti huu pia ulijifunga katika makanisa, nyumbani na sehemu ambazo watoto na vijana hufanyia michezo yao, barabarani, mashambani na madukani/sokoni. Haya ndiyo maeneo ambayo tuliamini Kimaragoli kinatumika bila mipaka ya kuingiliwa na lugha nyinginezo kwa kiwango kikubwa. Walioshirikishwa katika utafiti huu walikuwa watoto (umri wa 12-17), vijana (18-35) na makamo na wazee (36 na zaidi) kwa lengo la kupata picha halisi ya udumishaji lugha katika vizazi mbalimbali. Pia, baadhi ya Waluo walitafitiwa ili kupata data kuhusu mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli. Utafiti huu ulijikita katika mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli, umilisi wa Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake, athari za Kiluo kwa Kimaragoli kinachozungumzwa Uriri na mielekeo ya Waluo na Wamaragoli kuhusu udumishaji wa Kimaragoli.

### 1.9 Nadharia za Utafiti

Utafiti huu uliteua nadharia tatu zilizojaribu kuvyaza uchanganuzi timilifu wa data. Nadharia zilizotumika ni Mtagusano Lugha, Uzalishaji Kijamii na Uhuishaji Kiethnoisimu.

#### 1.9.1 Nadharia ya Mtagusano Lugha

Nadharia ya mtagusano lugha iliasisiwa na Weinreich (1953) na Haugen (1952) katika Khan (2016) na kuboreshwa na Thomason na Kauffman (1988). Taaluma ya mtagusano lugha kulingana na Weinreich inahusisha kuchunguza athari za mtagusano lugha miongoni mwa wasemaji wa L1 na L2. Weinrich na Thomason na Kauffman walidai kwamba lugha mbili au zaidi zinapokutana na kutagusana, hutokea athari mbalimbali zikiwepo kudumisha lugha, kuhamia lugha nyingine, kufa kwa lugha au hata kubadilika kwa lugha kimfumo. Mfumo wa lugha unapobadilika, unasababisha lugha iliyoathiriwa

kuonekana kuwa ngeni hata kwa wasemaji wenyewe. Haugen (1952) katika Khan (2016) kwa upande wake alidai kwamba uchunguzi wa mtagusano lugha unastahili kuhusisha mtazamo wa kiisimu na kiisimujamii. Baadaye, Winford (2003) alipinga mawazo haya ya Weinrich na Thomason na Kauffman kwa kudai kwamba vipengele vya kimfumo (fonetiki, fonolojia, mofolojia na kadhalika) vya lugha haviwezi kukopeka kwa urahisi licha ya kuwepo kwa mtagusano mzito wa lugha au tamaduni mbili tofauti. Anatoa mifano ya tafiti alizofanya nchini Marekani katika miktadha ya Kiingereza/Kihispania na Kifaransa/Kiingereza katika kisiwa cha Prince Edward.

Nadharia hii inachunguza mtagusano lugha kwa ngazi mbili: kiwango cha mtu binafsi na kiwango cha jamii. Kiwango cha mtu binafsi kinahusisha kuangalia sababu zinazochangia msemaji kuteua maneno maalumu katika mazingira fulani ya wingilugha au umojalugha ilhali kiwango cha jamii kinachunguza mahusiano yaliyopo katika jamii yanayochapuza au kutinga athari fulani za mtagusano lugha. Mihimili ya nadharia inavyazwa na viwango hivi. Mihimili ya mtagusano lugha ni:

i. Muundo wa lugha;
ii. Isimunafsia ;
iii. Vipengele vya kijamii.

Mihimili hii imejadiliwa katika aya zinazofuata.

Katika mhimili huu wa kwanza, wanamuundo wanadai kwamba lugha ni mfumo dhabiti ambao hauwezi kubadilika kwa urahisi, hasa ikitokea kwamba mifumo inayotagusana hailandani. Hata hivyo, wanakiri kwamba kuna vipengele ambavyo vinaweza kuhamishwa kwa urahisi kutoka L2 hadi L1 au L1 hadi L2 ilhali vingine haviwezi. Masharti yanayowezesha uhamishaji wa vipengele kutoka lugha moja hadi nyingine ni:

i. Mfanano wa kitipolojia-yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia inayofanana.

Ikiwa L1 na L2 zinafanana katika vipengele hivi, basi ni rahisi kuhamisha vijenzi baina ya lugha hizi. Kwa mfano, lugha za Kibantu kwa kuwa zina tipolojia inayoelekea kufanana, ni rahisi, kwa mfano, Kimaragoli kuathiriana na Ekegusii au Kikuria kuliko kuathiriana na Kiluo au Kinandi. Licha ya kwamba Kimaragoli na Kiluo zina tipolojia tofauti, ilikuwa vyema kuchunguza hali iliyopo Uriri kwa sababu utafiti wa Lotta (2014) ulionyesha kwamba kuna uwezekano wa kutokea mwathiriano wa kifonolojia na kimofolojia ikiwa lugha zinazotagusana ni za mnasaba unaotofautiana.

ii. Mfanano wa kipengele maalumu kinachohamishwa.

Ikiwa neno au sauti zinahamishwa kutoka L1 na L2 zina mfanano wa sifa fulani, pengine kidoko, ni rahisi lugha L1 kukubali sauti kidoko zaidi kutoka L2. Aidha, ikiwa maana ya neno katika L1 inalandana na ya L2, ni rahisi maneno haya kupishana kimatumizi katika lugha zinazotagusana. Kwa mfano, katika lugha ya Kiluo na Kimaragoli, neno Nyasaye lina matumizi na maana moja na hivyo, ikiwa kuna maneno mengine yaliyo na sifa kama hizi, ni rahisi mwathiriano kutokea.

Tofauti za kitipolojia baina ya lugha zinazotagusana ndizo husababisha lugha kuwa na mabadiliko machache sana. Mabadiliko makubwa yanayoweza kutokea ni ya kimsamiati zaidi kuliko ya kimofolojia (Meillet, 1948 katika Stapert, 2013). Kwa kuwa neno pweke hutumika kila mara na linaweza kutumika kama mbadala katika mfumo, ni rahisi kupata misamiati pwekepweke katika L2 au L1 kuliko upya wa kimofolojia. Hata hivyo, Meillet anakiri kwamba mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia yanaweza kutokea katika mtagusano. Utafiti huu ulitumia mhimili huu kuchanganua madhumuni ya tatu. Tulifanya hivi tukifahamu kwamba hizi ni lugha zilizo za mnasaba tofauti: moja ni Kibantu na nyingine ni Kinailoti. Tulichunguza maneno ya Kiluo na ikiwa maneno haya

yamesababisha kuingia kwa maumbosauti mapya katika Kimaragoli. Kwa mfano, Meillet (1948) anaonyesha kwamba mfumo wa lugha ya Kigallo-Kirumi uliingiza sauti */w/* kutoka lugha za Kijerumani katika *werra* (vita), lakini kwa kuwa mabadiliko ya kifonolojia huwa dhaifu kutokana na mifumo tofauti, sauti hii ilidondoshwa baadaye na kuwa */g/* katika *guerre* (vita); sauti */g/* inapatikana katika lugha za Kirumi. Mabadiliko haya aidha yalitokea katika mtagusano wa Kiswahili na Kiarabu wakati ambapo sauti */q/* iliingizwa katika maneno kama vile *qasida, qauli, qawafu* na kadhalika (kwa mfano katika tenzi za Kiswahili) na baada ya muda, /q/ ilibadishwa kwa ajili ya /k/ iliyokuwepo katika lahaja za Kiswahili na lugha za mnasaba wa Kibantu maeneo ya Pwani.

Mhimili wa isimunafsia unadai kwamba akili ina nafasi kubwa sana katika udumishaji lugha. Uwililugha au wingilugha katika maisha ya mtu binafsi au jamii maalumu unaweza kuelezwa vyema kupitia mhimili huu. Umilisi lugha wa mtu binafsi katika jamii unategemea uwezo wa akili kubwia misamiati na vipengele vingine vya kiisimu na uwezo huu unaathiriwa na umri. Umri na akili ya binadamu vimetambuliwa kama vipengele muhimu wakati wa kueleza kwa nini watoto wadogo hujifunza lugha haraka kuliko wazee na kwamba vijana waliobaleghe ndio mawakala wa kusambaza mabadiliko katika L1 yao. Kupitia kwa mhimili huu, mtafiti aliweza kuchunguza kwa nini umri mchanga unajikuta katika hali ambapo umilisi wao wa L1 uko chini ilhali wa L2 uko juu. Na kwa kuwa wangependa kuzungumza L1 wasiyoijua vyema, huishia kuingiza misamiati ya L2 ili kukamilisha mawasiliano yanayotendeka kupitia L1 (Thomason, 2001; Robinson na Ellis, 2008). Mhimili huu ulikuwa muhimu wakati wa kupima umilisi kutegemea umri miongoni mwa Wamaragoli. Data iliyokusanywa kuhusu madhumuni ya pili (umilisi wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa makundi mbalimbali) ulichanganuliwa kwa mujibu wa mhimili huu. Aidha, ulisaidia kueleza tofauti zilizomo katika makundi mbalimbali kiumri. Mhimili huu pia ulisaidia kuelezea hali za

uchanganyaji msimbo, ubadilishaji msimbo kutegemea miktadha na uteuzi wa lugha kutegemea kikundi mahsusi na pia sababu zinazochochea msemaji wa L1 kusawazisha matamshi yake anapokutana na msemaji wa umri fulani wa L1 au L2 (Grosjean, 1982; Treffers-Daller, 1998).

Vipengele vya kijamii vimetambuliwa kama mhimili amilifu wakati wa utafiti wa mtagusano lugha. Vipengele hivi hujumuisha muda wa mtagusano na hadhi inayowekewa lugha inayoonekana kuwa kuu katika mazingira ya mtagusano, mielekeo ya mtu binafsi na ya jamii, umri na mitandao ya kijamii na siasa. Thomason na Kauffman (1988) wanaeleza kwamba historia ya isimujamii ndiyo huamua matokeo ya kiisimu na wala siyo mfumo wa lugha zao. Hii ina maana kwamba, dai la wanamuundo kuwa ni vipengele vichache vinavyoweza kuhamishwa linatiliwa shaka. Mhimili huu unadai kwamba katika jamii ambazo zimeishi kwa muda mrefu katika hali ya mtagusano lugha, chochote kinaweza kuhamishwa bila kujali tipolojia au mnasaba wa lugha (Thomason, na Kauffman, 1988). Tukirejelea mifano mbalimbali ya tafiti ambazo tayari zimefanyika Tanzania, ni bayana kwamba lugha za Kibantu zimeathiriwa kimaumbosauti na lugha za Kinailoti (Thomason, 2001; Lotta, 2014) kwa sababu ya kutagusana kwa muda mrefu. Kadiri mtagusano unavyozidi kuwa mzito na wa muda mrefu, ndivyo vipengele mbalimbali vinavyozidi kuingizwa katika lugha mahsusi. Mbinu ambayo wataalamu wengi (k.m., Thomason, 2001; Ralli, 2001) wanakiri inatumika kuhamisha vipengele vya kiisimu ni ukopaji. Wasemaji wa L1 wakiipa L2 hadhi ya juu, basi wataishia kujifunza lugha hii na kisha kuhamisha vijenzi mbalimbali katika L1 yao. Mwelekeo huu utasababisha wasemaji wa L1 kuhamia L2 na ndio utakuwa mwanzo wa kuathiri L1 yao. Lugha ya Kiluo imesifika kwa wepesi wake wa kimsamiati na ujifunzaji wake unachapuzwa kwa kuwa mfumo wake si ambishi sana kama wa lugha za Kibantu. Mhimili huu ulisaidia kueleza sababu za baadhi ya wasemaji wa Kimaragoli kudhihirisha

viwango tofautitofauti vya umilisi wa Kiluo na pia kuchunguza au kuelezea nafasi ya mielekeo ya wasemaji kuhusu udumishaji wa Kimaragoli.

Umri unadaiwa kuwa muhimu wakati wa kuchanganua umilisi wa wasemaji wa L1 wanapotagusana na L2. Kerswill (1996) anadai kwamba kila mtu anaweza kujifunza chochote katika lugha lakini kiwango cha ujifunzaji kitatofautiana na umri. Msemaji hujifunza vipengele changamani vya kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia akiwa mchanga, pengine baina ya miaka 3-13. Na kati ya umri wa 12-15, msemaji wa L1 huzungumza L2 kama wanavyosema wenyeji wa L2. Kwa hiyo, watoto wachanga wanaweza kujifunza haraka L2 kuliko wakubwa wao, ambao watajifunza tu msamiati mwepesi. Hata hivyo, Kerswill (1996) anadai kwamba watoto wadogo (miaka 6-12) hujifunza zaidi kutoka kwa wazazi wao na hukoma kujifunza kutoka kwa mama au baba yake anapokuwa na uwezo wa kutangamana na wenzao katika mazingira tofauti na ya nyumbani. Katika kipindi hiki, mtoto hujifunza lugha kutoka kwa wenzake zaidi kwani huwa ameumba mitandao ya kirafiki nje ya familia yake. Mtoto anapobaleghe, huwa chombo cha kusambaza kile alichojifunza kutoka kwa marafiki zake wa L2; anaweza kuwafundisha ndugu zake, familia yake, au wasemaji wenzake wa L1 na hivyo kuanzisha athari za L2 katika L1. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuchanganua madhumuni ya pili kuhusu umilisi lugha katika vikundi mbalimbali vya umri na kutambua tofauti zilizopo na vile vile kuelezea namna msambao wa Kiluo na Kimaragoli unavyoendelezwa miongoni mwa Wamaragoli. Aidha, mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuelewa ni kundi lipi linaloekea kudhoofisha uwezo wake wa kudumisha lugha ya Kimaragoli.

### 1.9.2 Nadharia ya Uzalishaji Kijamii

Kwa mujibu wa O’Riagain (1994) mwitifaki wa nadharia ya uzalishaji kijamii ni Bourdieu ambaye aliiasisi mwaka wa 1977 kwa lengo la kueleza namna ambavyo kizazi

kimoja hurithisha maarifa ya kiutamaduni kwa kizazi kinachofuata. Nadharia hii ina chanzo katika uwanja wa Sosholojia. Mihimili yake ni:

i. Kila kizazi huunda na kuweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata tija zake.

Kwa mfano, mikakati hii inaweza kuwa ya kufanikiwa katika elimu, ajira, lugha, mazingira na kadhalika. Mikakati hii, kama anavyodai O' Riagain (1994) huchangia katika udumishaji au uhamaji lugha. Mikakati hii inaweza kuwekwa na mtu binafsi au jamii nzima kwa makubaliano baada ya kuona tija zake. Wakati mwingine, mikakati hii inaweza kuendelezwa na wanajamii bila wao kuwa na ufahamu wa moja kwa moja kwamba wanadumisha amana fulani; hufanya hivi king'amuzibwete.

ii. Athari za mtagusano wa lugha moja na nyingine.

O'Riagain (1994) anatambua kwamba ili kufanikisha uchunguzi wa matokeo au athari za kiisimu zinazotokana na mikakati ya uzalishaji kijamii, inamlazimu mtafiti kuchunguza muundo wa jamii maalumu na uhusiano wake katika eneo pana. Eneo pana kwa maoni yake ni kitaifa na kimataifa. Anapozungumza kuhusu muundo wa kijamii, anasema kwamba hii huhusisha ruwaza za kila siku za mahusiano yao ya kijamii. Mahusiano haya hudhihirika nyumbani, sehemu za kazi, shuleni, sokoni miongoni mwa sehemu nyinginezo katika jamii. Vilevile, muundo wa kijamii huhusisha watu na bidhaa kutoka eneo moja hadi eneo jingine kama ilivyo katika uhamaji wowote na utalii. Ruwaza hii aghalabu hubadilika kila wakati jamii mahsusi inapotagusana na shinikizo za mazingira ya nje. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchanganua data ya madhumuni ya kwanza kwa kuwa ilimwelekeza jinsi ya kuchanganua na kujadili mikakati ambayo Wamaragoli wamekuwa wakitumia kudumisha lugha yao katika eneo la Uriri. Aidha, mhimili wa pili unaojadili athari za mtagusano lugha ulitumiwa pamoja na nadharia ya mtagusano lugha ulioweka bayana jinsi lugha huathiriana na vigezo vinavyoamua kiwango cha

mwathiriano kati ya lugha moja na nyingine. Kwa hivyo nadharia hii ilitumika kuchanganua na kujadili madhumuni ya kwanza na ya nne katika tasnifu hii.

### 1.9.3 Nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu

Giles, Bourhis na Taylor (1977) wanafasili Uhuishaji Kiethnoisimu kama nduni za kimfumo za vipengele vya hali ya lugha, uwasilish(w)aji kidemografia, kiisimu na usaidizi wa kitaasisi katika kuendeleza lugha. Katika kiunzi chao, wanapendekeza mihimili mitatu inayoathiri udumishaji wa lugha:

i. Uchumi,

ii. Jamii na

iii. Isimu .

Wanadai kwamba uhai wa kikundi cha kiethnoisimu ndio unakifanya kikundi hicho kuwa na umoja licha ya kuwepo katika makundi mengine ya kiisimu. Hii ina maana kwamba kadiri kundi moja linavyozidi kuwa hai, ndivyo linavyoimarisha satua yake ya kujidumisha kama kundi katika muktadha wa makundi mengi ya lugha (Yagmur na Kroon, 2003).

Katika kuunda nadharia hii, Giles na wenzake wanadai kikundi cha kiethnoisimu kinaweza kuathirika kihadhi kutokana na vipengele vifuatavyo: uchumi, jamii (historia ya jamii) na isimu. Muysken na Appel (1987) wanadai kwamba mabadiliko katika uchumi kama vile usasishaji na umijiishaji wa jamii ni muhimu katika kueleza udumishaji na uhamaji wa lugha. Ikiwa kikundi cha lugha kina hadhi ndogo kiuchumi, kuna uwezekano mkubwa wa kuhamia lugha ya wengi. Wanazidi kudai kwamba mabadiliko ya kiuchumi yanaweza kuathiri kichanya udumishaji wa lugha. Fahari ya kikundi cha lugha huathiriwa pakubwa na kiwango chao cha kiuchumi. Ikiwa kikundi cha lugha kina maskini wengi, wengi wa wasemaji wataanza kuhamia lugha ya walio

wengi na wanaoonekana kuwa wakwasi. Katika kutomelea hoja hii, utafiti wa Odero (2013) unaonyesha kwamba wasemaji wa Elmolo, kutokana na kiwango chao duni cha kiuchumi, walianza kuhamia lugha ya Kisamburu, iliyodhaniwa kuwa ya hadhi ya juu. Hii ni kutokana na mitazamo hasi ambayo iliwekewa lugha ya Kielmolo na wasemaji wa Kisamburu.

Hali ya historia ya kijamii inatokana na historia ya kiethnoisimu ya kikundi maalumu. Kwa mujibu wa Muandike (2011) makundi mengi katika muktadha wa mtagusano lugha yanaweza kudhihirisha kipindi cha kihistoria ambapo walitetea lugha yao ama walitaka kuwa huru kuendeleza lugha na utamaduni wao. Kadhia hizi za kihistoria zinaweza kuonekana au kufasirika kama mbinu za kuleta watu wa lugha moja pamoja ili watetee uhai wao na wa lugha yao. Mhimili huu wa historia ya kijamii una vipengele vidogo vidogo kama vile hadhi ya lugha na wasemaji wake, demografia (msambao wa kijamii) na msaada wa kitaasisi.

Hadhi ya lugha aghalabu huwa ni kigezo muhimu katika jamii za wingilugha. Ni rahisi kudumisha lugha iliyo na hadhi ya juu kuliko ile iliyo na hadhi ya chini. Ikiwa wasemaji wa lugha watajionea fahari kama kundi na pia kufurahia lugha yao, kutakuwepo na uwezekano mkubwa wa kuhifadhi lugha yao kuliko wasemaji wa lugha ya wachache wanaojidhalilisha na kukosa kuonea fahari lugha yao.

Kipengele cha kidemografia kinarejelea idadi ya wasemaji wa lugha maalumu na msambao wao kijiografia katika himaya nzima. Ikiwa idadi jumla ya wasemaji itapungua na kuwa ndogo, itaashiria ukosefu wa umuhimu na uamilifu wa lugha hiyo maalumu. Hii itasababisha uhamaji wa lugha (Muysken na Appel, 1987). Wataalamu hawa pia wanatambua kwamba kuwepo kwa ndoa za kati ya makabila kunaweza kuathiri pakubwa

asilimia ya wasemaji wa lugha ya wachache wanaojizatiti kudumisha lugha yao. Katika ndoa kama hizi, lugha ya hadhi ya juu ndiyo hupata fursa ya kudumishwa kwa kuwa hutumika kama lugha ya nyumbani. Lugha hii ndiyo hurithishwa watoto na wajukuu kwa kuwa wao huiamili kama lugha yao ya kwanza.

Msambao wa kijiografia wa wasemaji walio wachache huathiri sana udumishaji na uhamaji wa lugha. Wasemaji wachache wana satua kubwa ya kudumisha lugha yao ikiwa watasalia kama kundi na kuishi pamoja katika eneo moja. Katika miktadha ya wingilugha, idadi ya maeneo kunakotumika lugha ya wachache huwa muhimu katika kudumisha au kupoteza lugha. Fishman (1972) anafasili eneotumizi lugha kama kijenzi cha kijamii na kitamaduni kinachotokana na mada za mawasiliano, mahusiano kati ya wawasilianaji, na sehemu ya mawasiliano katika mipaka ya jamii-lugha. Wasemaji huamua lugha ya kutumia kila mara wanapokutana na kutagusana katika eneo maalumu kama vile nyumbani, hafla za kijamii (harusi, matanga, mikutano ya kitamaduni, kanisani na kadhalika). Na hata wanapokuwa nyumbani wasemaji hawa hujikuta wanatumia lugha fulani maalumu katika miktadha midogo midogo kama vile katika ukulima, kuadhibu, kufundisha dini, maombi au hata kuwatuma wanafamilia wenzao.

Msaada wa kitaasisi hurejelea uwezo wa kutumia lugha katika miktadha iliyo rasmi au isiyo rasmi katika kujadili, kufafanua, kutetea jamii-lugha katika vyombo vya habari, dini, serikali na hata katika elimu. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kuathiri udumishaji au uhamaji wa lugha. Ikiwa lugha ya hadhi ya chini inachapishiwa vitabu, ina idhaa za redio, televisheni, magazeti, majarida, na kadhalika basi uwezo wake wa kudumishwa unaimarika pakubwa. Vilevile, lugha ya wachache inapotumika katika maeneo ya ibada, huchapuza udumishaji (Ehala, 2010).

Vigezo geu hivi mintarafu Giles na wenzake (1977) huchangiana na huathiriana ili kufanya lugha ya wachache kuwa hai. Kundi linapokuwa na umoja, linapojivunia lugha na utamaduni wake na linapowakilishwa katika serikali, vyombo vya habari na mawasiliano, basi hujidumisha licha ya kwamba limezungukwa au linaishi katika muktadha wa wingi lugha au katika muktadha wa lugha moja iliyo na nguvu kuishinda.

Nadharia hii ilitumika kuchanganua kwa utondoti madhumuni ya kwanza, tatu na nne. Hii ni kwa sababu ilihusisha vipengele vingi vya kimsingi katika udumishaji wa lugha kama vile mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo, athari za mtagusano wa Kimaragoli na Kiluo, na mikakati iliyotumika kudumisha Kimaragoli. Aidha, nadharia hii iliteuliwa pamoja na nadharia nyinginezo kwa sababu ya uwezo wake kuangazia vijipengele vidogo zaidi katika mchakato mzima wa udumishaji wa lugha. Kwa mfano, uwezo wake wa kuangazia vijipengele kama vile mahusiano ya wasemaji wa lugha, fahari ya wasemaji wa lugha na hata uwakilishwaji katika siasa ilimpa mtafiti msingi wa kujadili na kuchangua vipengele vidogo vidogo ambavyo vilikuwa vinajitokeza katika data iliyokusanywa mintarafu madhumuni mahsusi ya utafiti huu.

### 1.9.4 Mwingiliano wa nadharia

Waitifaki wa nadharia ya Mtagusano lugha (k.v. Giles na wengine, 1977) wanadai kwamba hakuna nadharia inayojitosheleza kuelezea vipengele changamano ambavyo hujadiliwa katika taaluma ya mtagusano lugha. Nadharia tulizoorodhesha awali zinajadili na kuchanganua kipengele kimoja, viwili au vitatu. Kwa mfano, katika nadharia tulizoteua, yaani Mtagusano Lugha, Uzalishaji kijamii na Uhai wa Kiethnoisimu, hakuna nadharia iliyoweza kufafanua madhumuni yote ya utafiti. Nadharia ya kwanza ilishughulikia madhumuni ya pili, tatu na nne ilhali nadharia ya pili ilichanganua madhumuni ya kwanza. Hata hivyo, nadharia hizi ziliingiliana kwa kuwa zilichangia

kikamilifu katika kueleza dhana ya udumishaji lugha ya Kimaragoli. Wakati ambapo nadharia ya mtagusano lugha ilichunguza umri, jinsia na mahusiano ndani ya jamiilugha moja na kuonyesha jinsi mabadiliko yanajitokeza, nadharia ya uzalishaji kijamii ilijadili masuala haya ingawa kwa mtazamo tofauti. Inajadili jinsi dhana ya udumishaji lugha inaendeshwa katika jamii licha ya kuwepo kwa changamoto za mwingiliano na mwathiriano na jamiilugha jirani. Nadharia ya Uhai Kiethnoisimu kwa upande wake ilijaribu kufafanua vijipengele vidogo vidogo kama vile siasa, maeneo ya kimatumizi lugha, na habari na mawasiliano na kadhalika katika udumishaji wa lugha. Kwa hiyo ziliungana kutufafanulia mifanyiko ndani na nje ya jamiilugha zinazohusika.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imeangazia msingi wa utafiti huu kwa kushughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo wa utafiti, eneo la utafiti, sababu na umuhimu wa utafiti huu kwa wadau mbalimbali na pia nadharia zilizotumika kufanikisha uchanganuzi wa data. Mtafiti ameonyesha jinsi nadharia teule za utafiti zinavyoingiliana na kutagusana ili kuunda kiunzi bora cha nadharia za utafiti. Vipengele hivi ni muhimu kwa sababu ndivyo vilitoa mwelekeo wa utafiti.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imelenga kutalii maandishi ya tafiti za awali zinazojadili udumishaji lugha katika maeneo mbalimbali duniani na kuonyesha namna ambavyo yanaingiliana na mada yetu ya utafiti. Sura hii imegawika katika mada nne kuu: mikakati inayotumika kudumisha lugha; kiwango cha umilisi wa lugha miongoni mwa wasemaji lugha; athari za mtagusano lugha; na mielekeo ya wanajamii katika udumishaji lugha. Uhakiki umeonyesha pengo, mchango na umuhimu wa marejeleo haya katika tasnifu hii.

## 2.2 Dhana ya udumishaji lugha

Udumishaji lugha ni mchakato ambao kwao, wasemaji lugha maalumu hupitishia lugha zao kwa ajili ya kuziendeleza katika mawasiliano ya kila mara. Ni hali ambapo jamiilugha moja huhifadhi lugha yao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Batibo (2005) anafafanua udumishaji lugha kama hali ambapo lugha huendeleza uhai wake licha ya kukumbwa na shinikizo kutoka kwa lugha nyinginezo. Hii ina maana kwamba lugha inayojidumisha ina kani kubwa sana ya kujikinga kutokana na shinikizo la lugha iliyo na nguvu. Pauwels (2004) anafasili udumishaji kama hali ambapo msemaji, kundi la wasemaji, ama jamiilugha huendelea kutumia lugha yao katika baadhi au miktadha yote ya kimatumizi licha ya kuwepo kwa shinikizo kutoka lugha kuu. Udumishaji lugha pia unaweza kufasiliwa kama kiwango ambacho mtu binafsi au kundi linazidi kutumia lugha yake, hasa katika mazingira ya uwililugha au wingilugha au hata miongoni mwa wahamiaji (Richards na Schmidt, 2002). Kwa mujibu wa Baker (1992) udumishaji lugha ni hali ya kulinda na kuimarisha lugha ya kwanza au lugha asili katika jamii au kwa mtu binafsi, na hasa hulenga lugha za wachache. Istilahi hii pia hurejelea sera za kulinda na kuimarisha lugha za wachache.  Hivyo basi katika tasnifu hii, tulifasili udumishaji lugha

kama hali ambayo msemaji au wasemaji wa lugha maalumu huendeleza uhai wa lugha yake/yao licha ya kukumbwa na shinikizo kutoka kwa lugha nyinginezo zenye satua kubwa.

Kutokana na fasili hizi, ni muhimu kutambua kwamba mtu binafsi katika kundi zima la wasemaji lugha anaweza kuamua kudumisha lugha yake huku wengine wakihamia lugha nyingine au kundi zima linaweza kudumisha lugha yake huku mzungumzaji binafsi akihamia lugha nyingine. Hii ina maana kwamba udumishaji lugha unaweza kuwa mchakato na juhudi za mtu binafsi au kundi zima. Ingawa Baker (1992) anasisitiza udumishaji hutokea kwa lugha asili, hali halisi ni kwamba hata lugha kuu za kigeni zinadumishwa vilevile kwokwote ambako zinasemwa. Katika hali ya kujidumisha, lugha hubadilika kwa kiwango kidogo au kikubwa kutokana na kuingiliana na kuathiriana na lugha nyingine jirani. Mfumondani wa lugha, yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki huathirika kwa kiwango kidogo au kikubwa (Winford, 2003).

Katika hali ya kujidumisha, maeneo ya uzungumzaji wa lugha inayojidumisha hubaki vilevile, na kwamba kizazi kimoja hurithisha kizazi kinachofuata dafina zote za lugha mahsusi bila tatizo lolote. Idadi ya wasemaji wake aidha huwa kubwa kutokana na mielekeo chanya kuihusu. Batibo (2005) anaongezea kwa kusema udumishaji lugha unaweza kutokea katika mazingira ya lugha moja, mazingira ya uwililugha au wingilugha. Katika mchakato wa udumishaji lugha, wanajamii huhitaji mikakati ambayo hukubaliwa na kupangwa king’amuzi au wakati mwingine hutokea bila kutarajia/kupangwa. Mikakati ya kupangwa hukubaliwa na wazee katika jamii nzima kwa sababu wao ndio wamiliki na waendelezaji wa mila na desturi zote za jamii. Kwa hivyo, wao hukubaliana kwamba katika kuendeleza na kudumisha ndaro za jamii zao, mambo kadhaa yatakuwa yanatumika kama mikakati. Mikakati ya kushtukiza ni ile

ambayo hawakuiwazia wala kupangia ila jamii inajikuta katika mchakato wa kudumisha mila na desturi zao, ikiwemo lugha. Kwa mfano, mawasiliano kwa wenzo wa kiteknolojia ni mojawapo ya mkakati wa kushtukiza. Mikakati hii imejadiliwa kwa kina katika sehemu ya 2.3. Mijadala katika sehemu hii imejaribu kurejelea wataalamu mbalimbali na kuonyesha umuhimu wa mijadala hii katika utafiti huu. Mijadala hii imehusishwa kwa lengo la kufidia pengo la utafiti, kuonyesha mfanano uliopo kinadharia, kimbinu na kidhamira na utafiti wetu na pia kudhihirisha umuhimu wa tafiti hizi katika kazi yetu.

## 2.3 Mikakati ya Udumishaji Lugha

Mkakati ni mpango uliowekwa kwa ajili ya kutenda jambo fulani. Hivyo basi, mkakati wa udumishaji lugha ni mpango au utaratibu uliowekwa na wasemaji wa lugha mahsusi kwa lengo la kuendeleza uhai wa lugha yao kizazi baada ya kingine. Udumishaji lugha kwa kuwa ni mchakato wa king'amuzi na usio wa king'amuzi, wasemaji wake hufaridhika kuwa na mikakati ambayo hutumika kusaidia udumishaji wa lugha. Ili kuweza kukabiliana na changamaoto za kuhatarishwa na kufa kwa lugha, panahitajika kuwepo na mikakati ya kukinga lugha dhaifu dhidi ya udidimishwaji wao na hivyo kuzisaidia kudumishwa. Baadhi ya mikakati hii ni kama vile matumizi ya mfumo wa elimu, kutumia wazee kufundisha kizazi kichanga, matumizi ya teknolojia, uzungumzaji wa lugha asilia nyumbani na kadhalika. Mikakati hii tumeijadili kwa kina katika sehemu zinazofuata.

### 2.3.1 Mkakati wa Elimu

Ufundishaji lugha kama njia ya udumishaji ni mojawapo ya mkakati unaopendelewa sana na wataalamu wa lugha zilizomo hatarini. Utafiti wa McIvor (2009) unaonyesha kwamba mkakati huu wa udumishaji lugha unastahili kutekelezwa na walimu wanaofundisha

lugha asili katika taasisi za elimu. Mkakati huu unapendelewa kwa sababu unaweza kuwafanya wanafunzi wenye umri mchanga kujua lugha yao na kuweza kuitumia baadaye. McIvor anapendekeza kwamba walimu wanaotarajiwa kufundisha lugha asili wapewe mafunzo kabambe kuhusu mbinu za ufundishaji lugha. Baada ya wao kufuzu, waruhusiwe kufundisha viwango mbalimbali vya elimu kama vile shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu. Hata hivyo, kwa mujibu wa wataalamu, katika ufundishaji, suala la ufadhili wa miradi ya elimu lizingatiwe.

Romaine (2002) kwa upande wake anadai kwamba serikali iwe katika mstari wa mbele kufadhili ufundishaji wa lugha za kiasili katika mataifa kwani ndizo ziko katika hatari ya kufa. Hii ni kutokana na baadhi yazo kuwa na wasemaji wachache mno au kukosa mashiko miongoni mwa wasemaji wake. Hata hivyo, ingawa ufundishaji shuleni wa lugha asili ni mojawapo ya mikakati, satua yake katika kudumisha lugha, Romaine anadai kuwa si ya tija sana. Iwapo mkakati huu utatumiwa na wasemaji lugha, basi wasiutumie kama mkakati mkuu na wa pekee;uwe ni mkakati changizi tu. Hii ni kwa sababu, mara nyingi serikali hukoma kufadhili miradi hii ya elimu ya lugha asilia. Aidha, katika baadhi ya mataifa, hasa yanayostawi, malengo na matamanio ya jamii mara nyingi hayadahiliwi katika mfumo wa elimu ambao unaundwa na asasi za kiserikali. Lugha hizi ni sehemu ya tamaduni na zinastahili kuwa amana inayotawaliwa na kuongozwa na wanajamii mahsusi (Walsh, 2001).

Utafiti wa Arka (2013) unaonyesha kwamba nchini Indonesia, lugha asili zimepewa kipaumbele katika juhudi za udumishwaji kupitia mfumo wa elimu. Hata hivyo, kwa kuwa ni lugha nyingi, kuna tatizo la kiutawala ambapo hakuna rasilimali inayoweza kutosheleza lugha hizi zote (Kijava, Kisundani, Kibalini, Kilampung na Kiasenyesi). Hivyo, ufadhili wake katika elimu huyumba kipindi baada ya kipindi. Arka anatoa

mapendekezo kwamba serikali ijitahidi kuandaa walimu zaidi kisha kuwaajiri kwa lengo la kufundisha na kuzidumisha lugha hizi badala ya kuzitupilia mbali na kusahaulika. Utafiti wake unaonyesha kwamba wapo wasemaji wanaohamia lugha nyinginezo kwa sababu hawana watu wa kuwafundisha lugha zao asili katika miktadha ya shule. Utafiti wetu hivyo ulilenga kuthibitisha ikiwa wasemaji wa Kimaragoli walikuwa wanahamia Kiluo kutokana na kukosa watu wa kufundisha Kimaragoli.

Fang (2017) anadai kwamba kutumia elimu kudumisha lugha ni suala linalotegemea mtazamo wa serikali kuhusu sera ya lugha katika taifa maalumu. Anadai kuwa sera ya lugha inagawika katika aina tatu: sera ya elimu ya kutajirisha uwililugha; sera ya selimu ya mpito wa uwililugha na sera ya elimu ya kudumisha uwililugha. Anadai iwapo serikali itakuwa na aina ya tatu ya sera, basi itaweka udumishaji lugha kama msingi mkubwa katika mfumo wa elimu. Anatoa mfano wa Uchina ambapo kumekuwepo na udumishaji lugha ingawa si kwa kiwango cha kuridhisha. Mahitimisho yake ni sawa na ya Romaine kwamba japo mkakati huu una tija, haufai kuwa wa kimsingi.

Fishman (1980) anadai msingi wa elimu katika taifa la Marekani si mzuri wa kudumisha lugha za wachache. Anaamini kwamba mfumo wa shule kwa kuwa ni kama jamii kivyake, una wanafunzi ambao wengi wao ni wachanga, wanafuata wanachoambiwa na ni rahisi wao kuathirika hata kiisimu. Walimu wanapozitoa sheria za kuongoza matumizi ya lugha maalumu, huwepo adhabu kwa wanaokaidi na zawadi kwa wanaotii. Hivyo, mfumo wa elimu unapokataa matumizi ya lugha fulani, wasemaji wake wachanga wanajikuta katika mtanzuko wa aina fulani kwa sababu hawaruhusiwi kuzungumza lugha zao. Baada ya kipindi, wanajikuta wanahamia lugha waliyofundishwa shuleni huku wakitelekeza lugha yao. Maoni ya Fishman yanaonyesha kwamba katika baadhi ya miktadha, mfumo wa elimu unaweza kukwaza uamiliaji na udumishaji wa baadhi ya

lugha kutokana na sera zake za kimapendeleo. Wazo hili ni tofauti mno na walivyopendekeza Romaine (2002) na Fang (2017) kwamba mfumo wa elimu unaweza kuwa mkakati mojawapo wa kudumisha lugha za wachache.

Tafiti za wataalamu hawa zinatofautiana na utafiti huu kwa sababu, kwanza, walizingatia lugha nje ya bara la Afrika na pili, walizingatia tu mkakati wa ufundishaji. Hii ndiyo sababu kuu ya Romaine (2002) kutaja kuwa ufundishaji haufai kuwa ndio mkakati mkuu na wa pekee kwa kuwa mchango wake huenda usiwe mkubwa katika udumishaji lugha. Tatu, wataalamu hawa hawakutaja moja kwa moja mbinu walizotumia kukusanya data au kuchunguza mkakati huu wa elimu. Kutokana na uhaba wa marejeleo kuhusu elimu kama mkakati wa kudumisha lugha, ilikuwa muhimu kufanya utafiti huu, hasa katika muktadha wa lugha za Kiafrika kwa lengo la kufidia mianya iliyokuwepo.

### 2.3.2 Uzungumzaji Lugha Nyumbani

Uzungumzaji wa lugha nyumbani ni mkakati ambao watafiti wengi wanapendekeza (Mcarty & Watahomigie, 1998; Nettle & Romaine, 2000; Strubell, 2001; Romaine, 2002 ; Arka, 2013) kwa sababu ndiyo njia thabiti ya kudumisha lugha. Romaine (2002) anadai kwamba kutaifisha lugha asili au kuiweka katika mifumo ya elimu ni rahisi ila haitakuwa na manufaa kwa udumishaji lugha. Ikiwa wasemaji wa lugha asili hawazisemi nyumbani, basi vizazi vinavyokuja, hata vikifundishwa shuleni, havitazidumisha. Upashaji wa lugha kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika mazingira ya nyumbani ndio bora kuliko sheria na miundombinu ya kiserikali na imethibitishwa kuwa bora zaidi ya mikakati yoyote. Hii ndio sababu nadharia ya uzalishaji kijamii inashadidia kwamba urithishaji wa vipopo vya tamaduni ni suala linalotegemea mkakati na pia kizazi cha wazee.

Strubell (2001) ana maoni kwamba namna familia zinavyokuzwa na lugha wanazotumia katika makuzi haiambatani na juhudi za kiserikali-ni jukumu la kila mzazi au mlezi. Mcarty na Watahomigie (1998) wanasema kwamba kuzipa lugha haki zake hakumaanishi kuzidumisha. Udumishaji wake utategemea juhudi za kifamilia; kwamba ni lugha gani watatumia kuwasiliana. Aidha, kuipa lugha asilia mamlaka (kama vile urasimishwaji au utaifishwaji) ilhali kundi hilo halina nguvu katika jamii, hakutaamanisha kwamba mamlaka hayo yatadumisha lugha; lazima pawepo na mikakati mingine ya kusambaza lugha kutoka kizazi hadi kizazi (Nettle & Romaine, 2000).

Arka (2013) akitafitia udumishaji wa lugha za kiasili nchini Indonesia, alitambua kwamba ipo haja ya kutumia mkakati wa uzungumzaji lugha asili nyumbani ili vizazi vya baadaye viweze kuzirithi bila tatizo. Miongoni mwa mapendekezo aliyotoa kuhusu udumishaji lugha, moja lilidai kwamba wanajamiilugha wanastahili kuhimizwa kushiriki katika michakato ya kudumisha lugha zao asili kwa kuzitumia katika maeneo ya nyumbani ingawa hataji makundi ya kiumri. Arka alitumia mbinu ya mahojiano katika mikoa mbalimbali kukusanya data ya utafiti. Aidha, alitumia mbinu linganishi kuweza kuonyesha hali ilivyo nchini Indonesia na taifa la Papua New Guinea kuhusu udumishaji lugha kwa kuwa haya ndiyo mataifa mawili duniani yaliyo na lugha nyingi.

Makala ya wataalamu hawa yalionyesha mapengo kadha yaliyofidiwa na utafiti huu. Kwanza, watafiti walizungumzia sana suala la haki, kuzipa lugha asili mamlaka kimatumizi na utaifishaji wa lugha asilia. Pili, wao wamezungumzia sana lugha za Kizungu na za Kiasia. Tatu, wataalamu hawa hawakuonyesha mbinu na sampuli ya utafiti wakati wa kukusanya data yao.

### 2.3.3 Dini

Baadhi ya wataalamu wametambua kwamba dini ina uamilifu mkubwa katika udumishaji wa lugha (Thomason, 2001 ; Hamde, 2005 ; Darquennes na Vandenbussche, 2011 ; Park, 2012 ; Vedernikova, 2014). Kwa mfano, Hamde (2005) akitafitia udumishaji lugha ya Kiblin/Kibilini miongoni mwa Waeritrea wanaoishi Eritrea na waliohamia Uswidi, alitambua kwamba kumekuweko na juhudi kubwa za kidini kufufua na kudumisha lugha hii. Utafiti wake ulihitimisha kwamba matumizi ya lugha ya Kibilini katika michakato mbalimbali ya kidini ilikuwa na tija kubwa katika ufufuo na maendeleo yake. Akitumia mbinu za ukusanyaji data kama vile uhakiki wa maandishi, uchunzaji shiriki na mahojiano, alidai kwamba Kibilini kilipigwa marufuku katika shughuli za ukatekisti na badala yake lugha ya Kitigrinya kupewa kipaumbele. Wanafunzi wa upadre na utawa waliojaribu kutumia Kibilini waliadhibiwa na hivyo wengi wakaogopa kukizungumza. Hata hivyo, maendeleo ya baadaye (hasa 1990) yanaonyesha kwamba baada ya Vatican kuingilia kati na kutatua shida hii, lugha hii ilipewa hadhi ya kutumika katika dini. Bibilia ilitafsiriwa kwa Kibilini na shughuli za Kikanisa kuendeshwa kwa lugha hii. Utafiti wa Hamde ulihoji watu watatu, wawili moja kwa moja na mmoja kupitia kwa simu ilhali utafiti huu ulihoji watu wengi wakiwemo wazee, vijana na watoto. Aidha, utafiti huu ulitumia mbinu ya hojaji kukusanya data zaidi kama vile mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo na kiwango cha umilisi, masuala ambayo Hamde hakushughulikia. Pamoja na hayo, utafiti wa Hamde haukukita uchanganuzi wa data kwa misingi ya kinadharia. Mwisho, utafiti wa Hamde uliegemea data ya kithamano ilhali utafiti huu ulitumia data za kithamano na za kitakwimu kuchora taswira kamili ya udumishaji lugha ya Kimaragoli katika eneobunge la Uriri, nchini Kenya. Hivyo, kutokana na tafiti za wataalamu hawa, utafiti huu ulitendeka kwa lengo la kutaka kujua ikiwa kwa vyovyote vile, dini ilichangia udumishaji wa Kimaragoli katika eneo la Uriri.

Thomason (2001) anadai kuwa katika taifa la Australia, dini ilibainishwa kama njia mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza lugha za wahamiaji. Aidha, utafiti wake katika makundi mawili ya wasemaji wa uwililugha (wasemaji wa Kiitaliano-Kiingereza na Kigiriki-Kiingereza) unaonyesha kwamba kundi moja liligura lugha yao ilhali lingine lilidumisha. Kundi la kwanza la wasemaji wa Kiitaliano-Kiingereza lilihama kutoka Kiitaliano hadi Kiingereza baada ya mpito wa vizazi vitatu huku kundi la Wagiriki-Wamarekani likidumisha lugha yao ya Kigiriki kwa vizazi vinne. Sababu kubwa iliyosaidia kudumisha Kigiriki ilikuwa ni kuabudu kwa pamoja katika kanisa moja la Kiothodoksi huku waliopoteza lugha ya Kiitaliano walitumia Kiingereza peke yake na waliabudu katika makanisa tofautofauti.

Mbali na mahubiri kanisani, Thomason anazidi kusema kwamba Kigiriki kilianza kufundishwa kanisani, na Bibilia iliyotumika ilikuwa ya Kigiriki. Kwa njia hii basi Kigiriki kikadumishwa ikilinganishwa na Kiitaliano ambapo waumini wake walihudhuria makanisa yaliyohubiri kwa Kiingereza na baada ya muda, wakahamia Kiingereza. Mahubiri, nyimbo, mikutano na mahimizano katika lugha ya Kigiriki yalifanikishwa pakubwa kwa lugha ya Kigiriki.

Ingawa utafiti wa Thomason (2001) ni muhimu, ulilenga sana lugha kuu za Kimagharibi (Kiingereza, Kigiriki na Kiitaliano). Aidha, hakutaja mbinu zilizotumika kukusanya data yake na pia idadi ya watafitiwa. Utafiti huu kwa upande mwingine ulilenga lugha za Kiafrika, hasa Kimaragoli. Vilevile, wakati ambapo utafiti wa Thomason ulizingatia wahamiaji wa kimataifa, utafiti wetu ulichunguza wahamiaji wa ndani kwa ndani. Kutokana na utafiti huu, ilikuwa bayana kwamba wahamiaji wa ndani kwa ndani wana uwezo wa kushiriki katika kanisa moja na hata kuwakaribisha wenzao walioko katika maeneo mengine ya Eneobunge la Uriri. Kuwepo kwa makanisa mengi yaliyoanzishwa

na kuendelezwa na Wamaragoli kumesaidia kudumisha lugha ya Kimaragoli. Utafiti huu kwa hivyo uliona vyema kuzipa kipaumbele lugha ndogondogo na za kimaeneo kama vile Kimaragoli kwani ndizo zimo katika hatari kubwa ya kutodumishwa na hivyo kutoweka bila juhudi zozote za kuzifufua (Robins na Eugenius, 1992 ; Grenoble na Lindsay, 1998 ; Wade, 1999 ; Nettle na Romaine, 2000). Utafiti huu ulitambua kwamba mkakati wa kutumia dini katika kudumisha Kimaragoli umekuwa ukitumika kuanzia miaka ya 1930 Wamaragoli wa kwanza walipohamia maeneo haya ya Uriri.

Putrayasa (2016) akijadili mikakati ya udumishaji wa lugha ya Kibali nchini Indonesia, anaeleza kwamba kuna mikakati mitatu, mojawapo ukiwa ni matumizi ya lugha katika dini. Ingawa haelezi kwa kina jinsi lugha hizi zinaweza kutumika katika dini na hivyo kuendelezwa, utafiti wake unaonyesha kwamba mkakati huu unaweza kuwa na tija kubwa. Hata hivyo, licha ya yeye kusisitiza mkakati huu, makala yake yalikuwa ya kijumla mno na hayakuonyesha idadi ya watafitiwa, eneo la utafiti, misingi ya kinadharia au mbinu na njia za utafiti. Utafiti huu uliweka wazi vipengele hivi vyote ili kuweza kuzalisha data, matokeo na mijadala ambayo ingeweza kuwa na msingi wa kisayansi kiutafiti.

**2.3.4 Utumiaji wa wazee kudumisha lugha**

Mkakati huu umekuwa ukitumika katika jamii mbalimbali duniani kwa lengo la kudumisha au kufufua lugha zilizo katika hatari ya kumezwa na lugha zenye nguvu zaidi. Nchini Kenya, utafiti wa Obiero (2013) unaonyesha kwamba wazee wa Kisuba walitumiwa kufufua na kudumisha Kisuba kilichokuwa katika hatari ya kumezwa na Kiluo. Kwa mujibu wa utafiti wake, wazee walisaidia sana katika kufufua lugha hii kwa sababu walipewa nafasi katika redio ya Kisuba iliyoanzishwa kufundisha Wasuba lugha yao. Aidha, walikuwa katika mstari wa mbele kuhakikisha kwamba serikali na wadau

wengine wamefanikisha juhudi za ufufuaji wa lugha yao. Utafiti wa Obiero (2013), uliotumia mbinu ya mahojiano, ulihusisha watafitiwa 48 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Nyanza Kusini. Maswali yake mengi (8/17) yaliegemea ufufuaji lugha huku mengine yakizungumzia vipengele vya kiisimujamii kama vile lahaja ya Kisuba inayozungumzwa sana na umilisi miongoni mwa wasemaji. Ingawa utafiti huu ni muhimu katika udumishaji lugha, uliegemea sana suala la ufufuaji lugha.

Utafiti huu ulitumia pengo hili kwa kujikita katika udumishaji lugha kwa kuchunguza vipengele vinne : mikakati ya udumishaji lugha, umilisi lugha, athari za Kiluo kwa Kimaragoli na mielekeo katika udumishaji wa Kimaragoli.

Iseke (2013) alichunguza majukumu ya wazee nchini Canada katika udumishaji wa lugha yao ya Kimichifu. Utafiti wake ulitambua kwamba wazee walihimiza matumizi ya lugha yao katika kusimulia hadithi kwa vizazi vichanga. Walieleza kwamba mkakati huu wa kuhadithiana visa unasaidia kuimarisha utambulisho, historia, utamaduni, na mwonoulimwengu miongoni mwa wasemaji wa Kimichifu. Utafiti wa Iseke ulitumia mbinu ya mijadala ambapo wazee 7 walioteuliwa waliketi katika duara na kuwa na mijadala kuhusu masuala maalumu. Vilevile, baada ya kukusanya data ya kimsingi, alifanya utafiti wa baadaye kwa kutumia mahojiano ya simu, mawasiliano ya barua pepe, na uchunzaji wa hafla za kijamii na mikutano ya Wamichifu ili kuthibitisha habari zilizokuwa zimetolewa na wazee hawa.

Utafiti wa Iseke ulitofautiana na utafiti huu kwa njia kadhaa: kwanza, Iseke alitumia mbinu moja ya kukusanya data (mijadala na wazee). Utafiti huu ulitumia hojaji, mahojiano, mijadala ya kimakundi, na uchunzaji kukusanya data kwa wakati mmoja. Kwa hakika, hojaji ndicho kifaa kikuu kilichotumika kukusanya data ya kimsingi huku

njia nyinginezo kama vile mahojiano, uchunzaji na vikundi lingani zikiwa za kuthibitisha data ya hojaji. Pili, utafiti huu ulilenga makundi mbalimbali ya Wamaragoli (wazee, vijana na watoto) ilhali Iseke alitumia wazee peke yake kuchunguza udumishaji wa Kimichifu.

Kwa mujibu wa *Department of Culture, Language, Elders and Youth* (2014) katika taifa la Canada, wazee wanatambuliwa kama hazina na dafina ya kina katika uendelezaji wa tamaduni, mila, lugha na maarifa. Licha ya kukumbana na mabadiliko ya kijamii katika maisha yao, wamejizatiti kudumisha lugha zao. Kwa hivyo, wanaweza kutumia maarifa waliyo nayo kufundisha vizazi vichanga jinsi ya kudumisha lugha zao katika mazingira yanayozidi kubadilika na kuathiri matumizi ya lugha. Ingawa ripoti hii haikueleza kwa kina masuala mbalimbali ya udumishaji lugha, ilimpa mtafiti fursa ya kujikita katika udumishaji lugha kwa lengo la kutambua ikiwa wazee walikuwa wanatekeleza jukumu la kupasha maarifa ya Kimaragoli kwa vizazi vichanga.

### 2.3.5 Matumizi ya Tehama katika Udumishaji lugha

Utafiti wa Obiero (2013) unaonyesha kwamba redio ilikuwa ni mojawapo ya mkakati wa kufufua Kisuba. Obiero alifanya mahojiano na wasemaji wa Kisuba na kutambua kwamba watu wazima na wazee ndio walikuwa wanasikiliza na kutumia redio ya KBC (Matangazo ya Kisuba) kutunga na kutuma masimulizi, kutunga na kuimba nyimbo, kutuma matangazo kama vile ya vifo, salamu, na mazungumzo ya kiutamaduni kwa lugha ya Kisuba. Katika utafiti wake, anadai kwamba nusu ya watafitiwa (16) hawakuwahi kushiriki katika vipindi hivi isipokuwa kusikiliza tu. Aidha, matangazo ya Kisuba yalikuwa yanaendeshwa kwa saa moja na dakika kumi na tano pekee kila siku. Alihitimisha kwamba kutokana na hali hizi, ingechukua muda mrefu kufufua Kisuba kwa sababu ya kuwepo muda mfupi wa matangazo ya redio. Jambo la muhimu katika utafiti

huu ni kuwa redio, kama kifaa cha Tehama, ina nafasi kubwa katika ufufuaji na udumishaji wa lugha. Hata hivyo, tofauti na utafiti wake, utafiti huu ulilenga kuchunguza makundi yote ya kiumri kwa lengo la kutambua ikiwa wasemaji husikiliza na kufaidika kupitia kwa redio za Kimaragoli.

Utafiti wa Marti-Bucknall (2007) unaonyesha kwamba teknolojia ni zana muhimu katika udumishaji wa lugha mbalimbali ulimwenguni. Kadiri jamii zinavyozidi kutandawazishwa ndivyo uwezekano wa lugha kutoweka unavyozidi. Kwa kuwa jamiilugha zinahamia maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, teknolojia inajitokeza kama kifaa cha kitalifa kinachosaidia kudumisha lugha za wahamiaji. Teknolojia kwa kuwa ni pana na inahusisha vipengele mbalimbali, watafiti huteua kipengele kimoja na kukichunguza. Kwa mfano, Marti-Bucknall alichunguza matumizi ya televisheni za kisatalaiti na mtandao miongoni mwa wanafunzi wahamiaji wanaoishi Basel, Uswizi. Matokeo yalionyesha kwamba walimu wengi hawatumii teknolojia katika ufundishaji na hivyo kuathiri ufundishaji wa lugha za watoto wahamiaji. Kwa kuwa watoto hawa hawafundishwi lugha zao, wao hujifundisha lugha kuu peke yake. Wanapokua, hawawezi kujieleza kwa lugha zao asilia.

Tofauti kati ya utafiti huu na wa Marti-Bucknall ni kwamba aliegemea sana TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ilhali utafiti huu ulichukua mwelekeo wa udumishaji lugha kwa ujumla. Pili, utafiti wake ulizingatia matumizi ya televisheni na mtandao.Utafiti wetu ulichunguza matumizi ya redio. Tatu, utafiti wake ulifanyika Uswisi, taifa lililoendelea, ilhali Kenya ni taifa linaloendelea. Uwezo wa kiteknolojia baina ya nchi hizi mbili unatofautiana pakubwa. Familia nyingi tulizochunguza hazina televisheni za Kisatalaiti isipokuwa redio na simu tamba. Vifaa hivi vilikuwa amilifu katika udumishaji lugha ya Kimaragoli.

Mbali na matumizi ya redio na televisheni, wataalamu wengine wamedai kwamba lugha zinaweza kufufuliwa na kudumishwa kupitia kwa tovuti na jukwaa la *Youtube* (McIvor, 2009 ; Iseke, 2013 ; Hermes na King, 2013). Kwa mfano, Iseke (2013) anadai kwamba lugha ya Kimichifu imefufuliwa na kudumishwa kupitia kwa matumizi ya tovuti (www.Learnmichif.com na www.michifspeaker.com) na pia kuwepo kwa video za kujifunza Kimichifu kwenye jukwaa la *Youtube*. Msemaji wa Kimichifu anaweza kusoma/kusikiliza matamshi, msamiati na vipengele vinginevyo katika lugha hii. Watafiti McIvor (2009) na Hermes na King (2013 waliegemea sana suala la teknolojia katika uhifadhi wa lugha asilia kuliko kudumisha. Utafiti huu ilichunguza udumishaji lugha.

**2.3.6 Kutembeleana miongoni mwa Wamaragoli**

Wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya wamethibitisha kwamba kutembeleana ni mkakati wa kudumisha lugha zao za kiasili (Michieka, 2012). Utafiti wa Michieka ulilenga wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya na aliuliza sababu zilizofanya wanafunzi kuendeleza au kudidimiza lugha zao asilia. Wanafunzi walidai kwamba sababu moja iliyowasaidia kuzidi kuzungumza lugha yao ni kuzuru nyumbani wakati wa likizo. Utafiti wake ulithibitisha kwamba baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu wanapoenda nyumbani, wao huzungumza lugha yao ya kiasili badala ya Kiswahili, Kiingereza au msimbo wa Sheng' waliozoea vyuoni kwa ajili ya kuwasiliana na wazazi. Utafiti wa Michieka ulitathmini wanafunzi 240 na ulitumia mbinu ya hojaji kukusanya data. Madhumuni yake yalitalii matumizi ya lugha, aina ya lugha inayotumiwa sana katika miktadha maalumu na pia kiwango cha umilisi. Utafiti wa Michieka ulikuwa na tofauti kadhaa : kwanza, utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha moja maalumu (Kimaragoli) ikilinganishwa na Michieka aliyechunguza lugha kadhaa; pili, utafiti huu ulitafitia wasemaji wa makundi yote ya kiumri (watoto, vijana na wazee) huku Michieka akisaili wanafunzi wa vyuo vikuu peke yake; na tatu, mbali na hojaji katika utafiti wa

Michieka, utafiti huu ulitumia mbinu kadhaa kukusanya data-mahojiano, uchunzaji, na mijadala ya makundi lingani.

Barnes na McDuling (hmu) walitafitia wahamiaji wa Kigiriki nchini Afrika Kusini na kutambua kwamba mojawapo ya mkakati wa kudumisha lugha ulikuwa ni kutembeleana. Wanadai kwamba wanamuziki kutoka Ugiriki walikuwa wanaalikwa kila wakati kutoka Ugiriki kwa ajili ya kuwatumbuiza wahamiaji. Utafiti wa wataalamu hawa ulisaili watoto 40 kutoka shule ya Kigiriki ya Saheti na watu wazima 49 kutoka familia mbalimbali za Kigiriki nchini Afrika Kusini. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa sababu moja kuu : ulikuwa unathibitisha kwamba udumishaji lugha ni tendo linalotegemea mkakati huu wa kutembeleana. Hata hivyo, utafiti wa Barnes na McDuling ulitofautiana na huu kwa misingi kwamba wahamiaji walioshughulikiwa katika utafiti huu walikuwa wa ndani kwa ndani na hivyo ilikuwa muhimu kutambua ikiwa kutembeleana ni kwa kila mara ama nadra. Hii ni kwa sababu inahitaji gharama kubwa kutembeleana kutoka nchi moja hadi nyingine ikilinganishwa na kutembeleana ndani ya nchi.

Kwa mujibu wa Hildebrandt (2004), Nonaka (2009), Ehala (2010) na Sallabank (2010) kadiri wasemaji wanavyozidi kuwa pamoja katika mtandao wa kijamii, ndivyo wanazidi kudumisha lugha yao. Hii ina maana kwamba kutembeleana miongoni mwa wasemaji lugha ni tendo la kufanya mtandao wao kuwa dhabiti na hivyo kuifanya lugha izidi kutumika katika miktadha mbalimbali. Licha ya kwamba Ehala alitumia nadharia ya Udumishaji lugha Kimakundi, matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kwamba matumizi ya mkakati huu wa kutembeleana yana manufaa kwa lugha. Tofauti na utafiti wa Ehala kinadharia, utafiti huu ulitumia nadharia mseto : mtagusano lugha, uhuishaji kiethnoisimu na uzalishaji kijamii. Aidha, utafiti huu ulikuwa na vipengele vingi vilivyochunguzwa vikiwemo athari za Kiluo kwa Kimaragoli.

### 2.3.7 Mikutano ya Kijamii

Aswegen (2008) akitafitia udumishaji na uhamiaji lugha miongoni mwa Wamaale nchini Ethiopia, alitambua kwamba mojawapo ya mkakati uliotumika ni mikutano ya kijamii. Utafiti wake ulitambua kwamba Wamaale walikuwa wanafanya kazi kikoa, walikuwa na mashirika ya wakulima na pia walikuwa na michezo ya kijamii miongoni mwao. Mikutano hii ya kijamii iliwaleta pamoja Wamaale na hivyo kusaidia kudumisha lugha yao. Utafiti wa Aswegen ulichukua miaka 6 na ulikuwa na Watafitiwa wakuu 8. Aidha, alitumia mbinu za uchunguzi wa nyaraka za kihistoria, uchunzaji na uchunzaji-shirikishi kukusanya data yake. Utafiti wake ulikuwa wa kithamano. Utafiti wa Aswegen (2008) unatofautiana na utafiti huu kwa sababu mbili: kwanza, utafiti huu haukutumia nyaraka za kihistoria kwa sababu mtafiti hakupata maandishi yoyote yaliyozungumzia Wamaragoli Uriri. Maandishi yaliyopo kuhusu Wamaragoli ni ya kijumla na hasa yanalenga historia yao walipohamia kutoka maeneo ya Misri hadi Mkoa wa Magharibi. Pili, utafiti huu ulihulutisha data ya kithamano na ya kiwingiidadi ilhali Aswegen alitumia data ya kithamano pekee.

Utafiti wa Barnes na McDuling (hmu) ulitambua kwamba Wagiriki walikuwa na sherehe mbalimbali kama njia ya kukutana na kuzungumza lugha yao nchini Afrika Kusini. Anataja sherehe kama vile harusi na densi vilabuni kama njia ambazo Wagiriki hukutana ili kuendeleza lugha yao. Miongoni mwa wanafunzi waliohojiwa, wengi walidai kwamba walijihusisha na hafla mbalimbali chuoni kama vile kuigiza michezo ya Kigiriki kwa Kigiriki, mavazi na vyakula vya Kigiriki, kuabudu kwa Kigiriki, mikutano ya jinsia ya kike na michezo. Utafiti wa Barnes na McDuling ulithibitisha kwamba udumishaji lugha ulitumia mikutano mbalimbali kama mkakati. Ingawa utafiti wake ulisaili wanafunzi wa vyuo vikuu, utafiti huu ulilenga wasemaji wote wa Kimaragoli ili kutambua mikutano mbalimbali inayowaleta pamoja na kuwasababisha kuzungumza lugha yao.

## 2.4 Viwango vya Umilisi na Utendaji lugha katika jamii

Umilisi na utendaji lugha ni uwezo wa mtu kufahamu na kutumia lugha yake, iwe ya kwanza au ya pili kwa kiwango fulani bila utata. Newby (2011) na Lehmann (2006) wanafafanua umilisi lugha kama uwezo wa kijumla wa maarifa, stadi, na nduni zinazomsaidia msemaji lugha kutekeleza majukumu yake. McNeil (1996) na Robins (1980) nao wanafasili umilisi kama maarifa kuhusu sheria, kategoria na kadhalika, yanayoweza kueleza zaidi kuhusu msemaji na lugha yake, na kwamba maarifa haya yanapotumika katika uzungumzaji na usikilizaji basi umilisi unakuwa utendaji. Kwa mujibu wa Bortolato (2012), umilisi lugha huathiriwa na sababu mbalimbali kama vile kutoamilia lugha kikamilifu na uchakaishaji wa lugha kwa mtu binafsi. Katika udumishaji wa lugha asilia, pana haja ya kufanya tathmini ya viwango mbalimbali vya umilisi na utendaji lugha kwa kutegemea baadhi ya vipengele kama vile umri na kiwango cha mahusiano baina ya kizazi kichanga na kizazi komavu (hasa wazee). Sababu kubwa ya kutathmini kwa kutumia kigezo cha umri ni kwamba kupitia kwacho, tunaweza kutambua namna vizazi tofautitofauti vinatumia lugha na pia kukisia ikiwa vizazi vichanga vitadumisha lugha yao au kuigura.

Udumishaji lugha ni mchakato ambao huathiriwa na vizazi : kizazi cha kwanza, ambacho aghalabu huwa ni wazee, huonyesha umilisi na utendaji mkubwa wa lugha asilia. Kizazi cha pili, ambacho ni watoto wao, huonyesha dalili za mabadiliko katika viwango vya kiisimu na hata matumizi ya lugha asilia katika miktadha anuwai. Kizazi cha wajukuu hudhihirisha umilisi na utendaji duni kiasi kwamba wasiporithishwa lugha asilia vyema, wanaweza kuhamia lugha nyingine iliyo na satua kubwa kiuamilifu  na iliyosambaa katika eneo lao. Tafiti hizi zinaweka vipengele vya umri, jinsia na wakati pamoja kama vigezogeu ambavyo huathiri umilisi lugha wa msemaji. Kwa hiyo, kwa mujibu wa

udumishaji lugha, vipengele vya kiumri na mahusiano baina ya makundi mbalimbali ya kiumri hutumika katika upimaji wa umilisi na utendaji.

### 2.4.1 Umilisi na Utendaji lugha Miongoni mwa Watoto

Zipo tafiti zinazodadavua suala la umilisi, utendaji na udumishaji lugha asilia miongoni mwa watoto (Park na Sarkar, 2007; Kipp, 2009; Verdon, McLeod na Winsler, 2013). Kipp (2009) anadai kwamba njia nzuri ya kuimarisha umilisi miongoni mwa watoto wadogo ni kupitia kwa ufundishaji wa shuleni. Katika mbinu anayoiita "programu ya uzamishaji", anasema kwamba hii ndiyo mbinu bora kuendeleza lugha miongoni mwa watoto wadogo. Ingawa utafiti wa Kipp (2009) uliegemea uimarishaji wa umilisi miongoni mwa watoto wa Hawaii kwa kuwafundisha darasani kisha kutathmini kupitia kwa mazungumzo na maandishi, utafiti huu ulilenga kupima moja kwa moja kiwango cha umilisi miongoni mwa watoto Wamaragoli kupitia kwa majibu na maswali simulizi/ya mdomo. Vilevile, haikujulikana ikiwa Wamaragoli walikuwa na mbinu yoyote inayotumika kuimarisha umilisi wa lugha hii miongoni mwa wasemaji wake. Ni hali iliyohitaji kutafitiwa kwa kina katika utafiti huu.

Shirika la Umoja wa Mataifa (UN, 2008) limetambua kwamba miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na tatizo la kizazi kichanga kupata lugha asilia kutoka kwa wazazi wao. Hakika, kizazi kichanga hakina umilisi wa lugha zao asilia kwa sababu hakuna utangamano kati yao na wazee walio na umilisi mkubwa wa lugha hizo. Hata pale ambapo wazee wanazungumza lugha asilia, kizazi kichanga hujikuta hakifahamu lugha hiyo kwa sababu mbalimbali. Sababu kubwa ni ya kutorithishwa kutoka kwa wazee wao (UN, 2008). Kwa mujibu wa Ang'iela (2002) watoto wasiporithishwa lugha huishia kujifunza lugha ya watoto wenzao katika mazingira yaleyale ya wingilugha. Mawazo ya Kipp (2009), UN (2008) na Ang'iela (2002) yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu.

Kwanza, yalionyesha matatizo ya udumishaji lugha yaliyopo katika kizazi cha leo. Ilikuwa muhimu kuchunguza umilisi wa wasemaji wachanga wa Kimaragoli kubainisha ikiwa matokeo ya UN na Ang'iela yaliwafiki hali halisi ya Uriri. Pili, mtafiti aliangalia mchango wa wazee Wamaragoli katika kudumisha au kudhoofisha lugha ya Kimaragoli kwa lengo la kukisia udumishaji wake siku zinazokuja. Mtafiti alichunguza watoto katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutambua umilisi wao.

Utafiti wa Verdon, McLeod na Winsler (2013) kuhusu umilisi wa lugha miongoni mwa watoto na udumishaji wake katika jamii unaonyesha kadiri watoto wanavyofundishwa lugha nyumbani, ndivyo wanavyofahamu zaidi na kuweza ku(z)idumisha miaka ya baadaye. Pia, utafiti wao unaonyesha kwamba lugha ambazo wazazi wanawafundisha watoto wao ndizo zitakazothaminiwa na kupewa mielekeo chanya na watoto hawa siku za baadaye. Kwa mfano, ikiwa mtoto atafundishwa lugha ya Kiingereza, Kivietinamu, Kiarabu, na Kiitaliano kwa kipindi kimoja akiwa utotoni, lugha hizo zitadumishwa ingawa kwa viwango mbalimbali vya umilisi na utendaji. Hata hivyo, lugha hizi huanza kutoweka katika ung'amuzi wa watoto baada ya miaka mitano kwa kuwa Kiingereza hutumiwa mno. Kwa hivyo, walihitimisha kwamba, umilisi na utendaji wa lugha miongoni mwa watoto unaweza kujitokeza na kudumishwa hadi miaka 5 ila baada ya hapo, mtoto anaishia kuhamia lugha nyingine (Kiingereza) na kusahau yake ya kwanza. Utafiti wa Verdon, McLeod na Winsler (2013) ulitafitia watoto wa wahamiaji nchini Australia na walilenga umri wa kati ya miaka 0-5. Jumla ya sampuli wakilishi 4252 iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya unasibu. Utafiti wao ulitumia muundo wa Utafiti radidi miongoni mwa Watoto wa Australia (LSAC) ambao ulianzishwa na unaendelezwa na serikali ya Australia. Muundo huu unahakikisha kwamba kila baada ya miaka miwili, data ya watoto wote walio hai inakusanywa na kusakinishwa mtandaoni na hivyo ni

rahisi watafiti kuweza kukusanya data kuhusu lugha inayotumiwa na wazazi wao kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa tano.

Ingawa utafiti wa Verdon, McLeod na Winsler (2013) ulikuwa muhimu katika kuelezea mabadiliko ya lugha na sababu zake miongoni mwa watoto, ulitofautiana na utafiti huu. Kwanza, utafiti wao ulikuwa wa muda mrefu na hivyo walikuwa na muda wa kuchunguza watoto hadi wanapofikia mwaka wa tano. Utafiti huu kwa kuwa ni wa muda mfupi, ulichunguza watoto kuanzia kwa umri wa miaka 12-17. Tuliteua umri huu kwa sababu unaakisi lugha ambazo zinaweza kutumiwa na watoto hawa hadi utu uzima. Tuliamini kwamba ikiwa mtoto wa miaka 18 anafahamu Kimaragoli, basi anaweza kukizungumza na kuitumia hata akiwa mtu mzima. Katika taaluma ya udumishaji lugha, hii ina maana kwamba mtoto huyu atadumisha lugha yake na kuweza kuirithisha kwa vizazi vya baadaye. Pili, wataalamu hawa hawakutathmini watoto moja kwa moja ila walitegemea maelezo ya wazazi wao. Katika utafiti huu, umilisi na utendaji lugha miongoni mwa watoto wa miaka 12-17 ulitathminiwa kwa kuuliza watoto wenyewe na pia kuwachunguza jinsi walivyotumia lugha katika maeneo na miktadha mbalimbali.

Utafiti wa Magga, Nicolaisen, Trask, Skutnabb-Kangas na Dunbar (hmu) unadai kwamba njia ya kipekee ya kuhakikisha lugha za+ wachache ulimwenguni zinadumishwa na kurithishwa ni kupitia kwa ufundishaji na uamiliaji, hasa kwa kizazi kichanga. Wanadai kwamba wingilugha unastahili kuwa tokeo mojawapo miongoni mwa watoto kadiri wanavyozidi kupitia mfumo wa elimu. Hata hivyo, mabadiliko katika sera na mifumo ya elimu inayodondosha lugha asili kwa ajili ya lugha kuu kama vile Kiingereza yanaathiri wingilugha miongoni mwa watoto hawa na hii inasababisha watoto kushindwa kuendeleza lugha zao za kiasili. Ufundishwaji lugha asili ni mojawapo ya mkakati

ambao, badala ya kuondolewa shuleni, unastahili kupewa kipaumbele na sera pamoja na serikali maalumu duniani kwa ajili ya kuendeleza wingilugha (UNESCO, 2010a: 2010b).

Utafiti wa wataalamu hawa ambao uliegemea zaidi umuhimu wa ufundishaji lugha shuleni pamoja na sera ya lugha katika mataifa mbalimbali, ulitofautiana na utafiti huukwa njia kadhaa. Kwanza, kwa kuwa mawazo yao yalikuwa ya kijumla kwa ajili ya kongamano la Umoja wa Mataifa, hayakulenga mataifa maalumu wala lugha maalumu. Utafiti huu ulilenga Kimaragoli na jinsi kinavyodumishwa na wenyeji wa eneo bunge la Uriri, Kenya. Pili, utafiti wao uliazimia kurai viongozi wa kilimwengu kuzingatia ufundishaji wa lugha asilia na wala sio kuziondoa katika mitaala ya shule.

Norbury, Gooch, Baird, Charman, Simonoff na Pickles (2016) walitafitia umilisi na utendaji miongoni mwa watoto wa miaka 4-5 waliokuwa wanaanza shule ya chekechea na kutambua kwamba baadhi yao walikuwa na shida za lugha (kujieleza). Sababu kubwa iliyochochea tatizo hili ni kutokomaa kwa kiwango chao cha kiakili ikilinganishwa na wanafunzi wa umri mkubwa. Wazazi wa watoto hawa kwa kuwa hawakuwa na ufahamu tosha wa hali hii, walikuwa wakiwapeleka watoto wao hospitalini kuchunguzwa na wataalamu. Matokeo ya watafiti hawa yalipendekeza kwamba walimu watumie mbinu mbadala za kufundisha watoto hawa ili wazazi wapunguze gharama za hospitali. Utafiti huu hata hivyo ulilenga kuchunguza umilisi na utendaji miongoni mwa watoto wa kuanzia miaka ya 12-17 kwa lengo la kutambua ikiwa wanadumisha Kimaragoli au la.

Utafiti wa Norbury na wenzake (2016) japo ulishughulikia watoto katika nchi ya Uingereza, ulikuwa na mchango kwa utafiti huu. Ulionyesha kwamba katika kiwango hiki, kitengo cha lugha cha kiakili miongoni mwa watoto kingali kichanga na hivyo hawawezi kutafitiwa kuhusu umilisi na utendaji. Kiwango hiki ni cha uamiliaji lugha

zaidi ya udumishaji lugha. Licha ya mchango wa utafiti huu, palikuweko na tofauti kadhaa: kwanza, utafiti huu ulikuwa wa kimatibabu na ulilenga kuthibitisha kuwa watoto wadogo wana umilisi na utendaji finyu wa lugha hivyo wazazi wao hawastahili kuwapeleka hospitalini kuchunguzwa. Pili, haukulenga udumishaji lugha katika umri huu. Utafiti huu uliazimia kutambua ikiwa kizazi kichanga (miaka 12-17) kilikuwa kinajua na kuongea Kimaragoli, na hivyo kuthibitisha kwamba kinaidumisha.

Kwa mujibu wa O'Riagain, Williams na Moreno (2008) umri wa kubaleghe (11-18) ndio nyeti kabisa katika udumishaji au uhamaji lugha. Katika kipindi hiki, mielekeo huumbwa na kudumishwa na mwishowe huathiri lugha maalumu. Utafiti wao katika nchi ya Ireland unaonyesha kwamba wengi wa wanafunzi wasiosema Kigaeltak wanapomaliza shule, hukoma kuongea Kiairishi. Hii ni kwa sababu ya mielekeo wanayoumba baada ya kutagusana na wasemaji wa Kiingereza, hasa wanapojiunga na vyuo vikuu au makundi mengine ya wasemaji wa Kiingereza. Utafiti huu unaelekea kutilia mkazo wazo kwamba ikiwa kizazi hiki hakitajua na kudumisha lugha yao, basi siku za baadaye huenda lugha maalumu ikawa mashakani. Utafiti huu ulinufaika na utafiti wa wataalamu hawa kwa sababu ulimfanya mtafiti kutilia maanani kundi hili la watoto miongoni mwa Wamaragoli.

### 2.4.2 Umilisi na Utendaji lugha miongoni mwa Vijana

Yoshiro (1992) alipotafitia udumishaji lugha ya pili miongoni mwa wanafunzi wa Sekondari wa Kijapani waliosomea mataifa ya nje, alitambua kwamba walitamani kudumisha lugha walizozipata wakiwa katika mataifa nje kama vile Uingereza na Marekani. Aidha, wazazi wao waliwashinikiza kuzidumisha lugha hizi kwa kutumia mikakati mbalimbali kama vile kuhudhuria madarasa, kuzungumza nyumbani, kuwasiliana na wenzao na hata kujihusisha katika hafla zinazotumia lugha za kigeni.

Sababu kubwa iliyowasukuma wanafunzi hawa kudumisha lugha hizi ilikuwa ni ajira. Yoshiro (1992) anaweka wazi kwamba wanafunzi hawa walizidi kuzungumza lugha walizojifunza katika mataifa mengine kwa sababu ya kutafuta kazi na pia kupewa motisha na wazazi wao. Muhimu katika utafiti huu wa Yoshiro (1992) ni vichocheo vya wasemaji kuweza kuimarisha umilisi wa lugha. Utafiti wake ulitumia mbinu ya mahojiano peke yake kukusanya data. Utafiti huu, katika harakati ya kukusanya data kuhusu umilisi lugha miongoni mwa vijana, uliangalia vipengele mbalimbali zaidi ya utafiti wa Yoshida. Baadhi ya vipengele hivi ni kiwango cha umilisi wa Kimaragoli na sababu zinazowafanya kuwa na umilisi mkubwa katika Kiluo. Uchunguzi wa umilisi wa Kiluo miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli ulikuwa muhimu kwa sababu ungetupatia taswira kamili kuhusu athari ya Kiluo kwa Kimaragoli katika ngazi ya umilisi.

Katika utafiti wa Grosjean (1982) ilitambulika kwamba kuliibuka ruwaza maalumu ya udumishaji lugha miongoni mwa vizazi vitatu tofauti: kizazi cha kwanza kilionyesha kudumisha lugha yao ya Kihispania; kizazi cha pili kilidumisha Kihispania na pia Kiingereza na kizazi cha tatu kikaonyesha kutumia Kiingereza na kusahau Kihispania. Kizazi hiki cha tatu kilijumuisha  vijana waliokuwa wanasoma katika shule za upili. Hii ina maana kwamba katika harakati za kudumisha lugha, juhudi huanza kufifia katika kizazi cha tatu au vijana waliozaliwa baada ya babu zao. Kwa kuwa kila jamii ina vijana, ikiwemo jamii ya Wamaragoli wa Uriri, ni vyema kufanya utafiti ili kubainisha hali halisi. Tafiti hizi kwa kuwa zinaonyesha kwamba vijana wanaelekea kupoteza lugha zao asili, basi ni wazi kwamba kuna haja ya kufahamu umilisi wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji vijana.

Kwa mujibu wa O’Riagain (2008) tafiti tatu zilifanywa kuhusiana na vijana na udumishaji lugha katika nchi ya Ireland. Utafiti wa kwanza wa 1973 ulionyesha kwamba

vijana wengi walikuwa wameanza kuhamia lugha ya Kiingereza na kupuuza Kiairishi. Matokeo ya mahojiano ya kina miongoni mwa vijana kati ya miaka 16-23 yalionyesha kwamba viwango vya uzungumzaji wa Kiairishi ulipunguka. Sababu kubwa ni kwamba vijana katika kundi hili la umri walikuwa wanajiunga na vyuo au kuanza kufanya kazi na hivyo Kiingereza kilipewa kipaumbele.

Utafiti wa mwaka wa 1997 ulitathmini vijana 21 walio kati ya umri wa 18-36 mjini Galway na ulitambua kwamba vijana wengi waliodumisha Kiairishi walikuwa na marafiki au jamaa ambao waliwachagiza kutumia lugha hiyo. Wasemaji hawa wangetumia Kiairishi kazini ikiwa wafanyikazi wenza walikuwa wanakiongea. Hata hivyo, matumizi yake yalipungua kadiri makundi ya kijamii yanayosema lugha hii yalizidi kuwa machache. Utafiti wa tatu wa 1999 uliwalenga wazazi wa watoto waliokuwa wanahudhuria shule za msingi hivyo basi haukuwa na mchango wa moja kwa moja katika sehemu hii.

Kutokana na tafiti za vipindi hivi, O'Riagain alihitimisha kwamba: kwanza, kiwango cha mahusiano kijamii ndicho kinachangia matumizi lugha ya Kiairishi, na hivyo kukidumisha miongoni mwa vijana; pili, kuweko kwa taasisi na asasi maalumu kama vile shule, na sehemu za kazi kunarahisisha mtagusano miongoni mwa vijana wanaosema lugha moja (Kiairishi) na hivyo kukidumisha miongoni mwa vijana na tatu, tabaka linachangia udumishaji wa lugha ya Kiairishi hivi kwamba tabaka la juu lilipendelea Kiingereza ilhali la chini, kwa kuwa makazi yake yalikuwa ya vitongojini, walitumia Kiairishi kuwasiliana zaidi. Kuishi vitongojini kuliwafanya wao kuishi pamoja kama kikundi-lugha.

Utafiti wa O'Riagain unaonyesha kwamba udumishaji wa lugha miongoni mwa vijana ni suala la kijamii kuliko la mtu mmoja. Kadiri vijana wanavyozidi kuwa pamoja na kufanya kazi, ndivyo wanavyozidi kudumisha lugha yao. Hata hivyo, wanapobadilisha tabaka, matumizi yake yanapungua, na badala ya Kiairishi, Kiingereza ndicho kinapewa hadhi, heshima na kukwezwa kimatumizi. Utafiti huu ulichukua mawazo haya na kutaka kubainisha ikiwa vijana katika umri wa 18-35 walikuwa na umilisi na utendaji wa kudumisha Kimaragoli.

Moreno (2008) akitafitia Kikatalunya alitambua kwamba vijana japo walikuwa wanajifundisha lugha shuleni, haikuwa inawapa mawanda mapana ya kutumia lugha hiyo. Wengi wao hawangeweza kuhamisha urasmi wa lugha ya Kikatalunya cha shule kwa matumizi ya kawaida au ya kimtaa. Utafiti wake ulipendekeza kwamba, ili vijana waweze kuimarisha umilisi na utendaji wa lugha hii miongoni mwao, ilikuwa lazima watumie mikakati kama vile kufundisha vijana kutunga nyimbo na mashairi kwa Kikatalunya, kuandaa mikutano ya kijamii, kuzuru masoko na vijiji ambako lugha hii inasemwa, kutazama filamu na programu za Kikatalunya, kuhimiza matumizi ya misimu ya Kikatalunya na hata pia kuwatafutia wanafunzi kazi katika mashirika au mazingira ambayo yanahimiza matumizi ya lugha hii. Mbinu hizi zingewasaidia vijana kuimarisha umilisi wa Kikatalunya katika miktadha yote badala ya muktadha wa urasmi peke yake.

Utafiti wa Moreno ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa sababu ulidhihirisha mikakati inayoweza kutumiwa kuimarisha na pia kupima umilisi wa vijana. Kwa hivyo, mtafiti alikopa mawazo haya na kuyahusisha katika utafiti wake, hasa kuhusiana na kutathmini umilisi na utendaji wa Kimaragoli katika miktadha mbalimbali ikiwemo nyumbani, michezoni, sokoni/madukani, shambani, kanisani na maeneo mengine yaliyoteuliwa kuchunguzwa katika eneobunge la Uriri. Licha ya faida zake,

utafiti wa Moreno (2008) ulifungua mianya ambayo utafiti huu ulilenga kufidia: kwanza, Moreno hakuonyesha mbinu za utafiti wala nadharia ya kuchanganua data; pili, eneo la utafiti wake lilikuwa ni Uhispania; na tatu, lengo lake halikuwa hasa kuchunguza udumishaji lugha bali matumizi ya lugha miongoni mwa vijana wa Kikatalunya. Utafiti huu uliteua mbinu za ukusanyaji data pamoja na nadharia ya utafiti. Tuliteua eneo la Uriri nchini Kenya kwa sababu ndilo liliakisi mtagusano lugha halisi baina ya wasemaji wa Kimaragoli na Waluo (na pia lugha nyinginezo kama vile Kikuria ingawa si sehemu ya utafiti huu), na lengo kuu lilikuwa kutathmini umilisi na utendaji miongoni mwa vijana ili kutambua ikiwa Kimaragoli kinadumishwa au la.

Grixti (2006) alitafitia vijana wa Kimalta kuhusiana na umilisi na utendaji wao wa kiisimu wa lugha ya Kimalta. Kwa kutumia mbinu ya mahojiano ya kina, Grixti alitambua kwamba vijana wengi wa tabaka la juu hawakujua Kimalta kwa sababu walikuwa wametagusana na Kiingereza katika miktadha mbalimbali kama vile shuleni, kutazama sinema na filamu, kutazama vipindi vya Kiingereza, na kwenda katika sehemu za burudani zilizotumia Kiingereza. Vijana hawa walionyesha mwelekeo hasi kabisa kuhusu Kimalta kwani walisema kwamba ni lugha isiyo na uwezo wowote wa kuwatambulisha ikilinganishwa na Kiingereza. Hata hivyo, vijana katika tabaka la chini hawakuonyesha mwelekeo huu hasi bali walidai kwamba walipenda lugha yao. Kinyume na vijana wa tabaka la juu, wa chini walipenda kusikiliza vipindi vya Kimalta kwenye runinga na redio, walisoma vitabu na magazeti ya Kimalta pamoja na kuzungumza Kimalta kila wakati hata wakiwa nyumbani. Kwa mujibu wa Grixti (2006) kiwango chao cha umilisi na utendaji katika Kimalta kilikuwa juu sana ikilinganishwa na vijana wa tabaka la chini.

Utafiti wa Grixti ulikuwa na mchango katika utafiti huu kwa sababu moja kuu: kwamba tabaka linaweza kuathiri umilisi na utendaji wa lugha miongoni mwa vijana. Tabaka la chini linaonyesha kiwango cha juu cha umilisi na utendaji kuliko tabaka la juu. Utafiti huu ulitumia mawazo haya kuweka msingi wa kuainisha vijana katika matabaka kwa lengo la kutambua ruwaza za umilisi.

Lee (hmu) alifanya utafiti wake miongoni mwa wasemaji wa Krioli ya Kireno cha Malacca (pia kinaitwa Papia Kristang) na kutambua kwamba wazazi walilalamikia hali ya lugha hii miongoni mwa watoto wao. Kwa kutumia mbinu ya mahojiano, watafitiwa wengi walilalamika kwamba watoto wao, ambao walikuwa vijana, walikuwa wameanza kusahau lugha yao na badala yake kujifunza lugha nyinginezo. Mmoja wa watafitiwa alidai kwamba watoto wake hata wanapoulizwa swali kwa Krioli cha Kireno cha Malacca, wanauliza tafsiri yake kwa lugha wanayoelewa kama vile Kireno au Kichina. Mtafitiwa mwingine alidai kwamba ikiwa watoto wao hawaelewi wala kuzungumza Krioli hii, basi ina maana wajukuu wao hawatazungumza Krioli ya Kireno cha Malacca kabisa kwa sababu watoto wao watakosa kitu cha kuwarithisha.

Utafiti wa Lee japo ulidadisi viwango vya umilisi katika umri mbalimbali, ulitegemea tu mbinu moja ya ukusanyaji data: mahojiano. Aidha, ulitegemea mno data ya wazazi katika kuelezea umilisi lugha wa watoto wao. Utafiti huu, katika kutathmini umilisi miongoni mwa Wamaragoli, ulitumia mbinu mseto za hojaji, mahojino na pia uchunzaji. Mbinu mseto zilikuwa bora kwa sababu zilizalisha data kamilifu, ya kithamano na kitakwimu.

### 2.4.3 Umilisi na Utendaji lugha miongoni mwa Makamo na Wazee

Tafiti nyingi katika taaluma ya mtagusano lugha zinakubaliana kwamba wazee ni kipengele muhimu katika uendelezaji na urithishaji wa tajriba na dafina zote za lugha (Milroy na Muysken, 1995; Thomason, 2001; Zhang, 2004; Obiero, 2008; Sallabank, 2010; Bartolato, 2012; Odero, 2013 ). Kwa kuwa wazee wameishi miaka mingi bila kupoteza vipengele vya lugha na utamaduni wao, hujukumika kuvipasha kwa vizazi vya baadaye ili viweze kuiendeleza (Tsitsipis, 1989 ; Hinton, Steele na Vera, 2002; Kipp, 2009). Sehemu hii imejadili kwa kina tafiti maalumu kutoka Kenya, Afrika na sehemu nyinginezo ulimwenguni kuhusu mchango wa wazee katika udumishaji wa lugha.

Obiero (2008) alipotafitia uhuishaji wa Kisuba, alitambua kwamba wazee walikuwa na jukumu kubwa la kuchangia ufufuzi na maendeleo yake katika jamii. Ulinganisho wake baina ya makamo na wazee ulionyesha kwamba wazee walitumia lugha katika maeneo mapana kama vile mazishini, kanisani, sokoni, nyumbani na katika mikutano ya hadhara. Aidha, wazee walishirikishwa katika uundaji wa vipindi vya redio vilivyopeperushwa kwa wasemaji wa Kisuba. Hata hivyo, Obiero hakutathmini moja kwa moja kiwango cha umilisi miongoni mwa wazee hawa. Alielekea kutathmini utendaji zaidi katika miktadha mbalimbali ya matumizi lugha. Utafiti huu kwa hiyo ulilenga kuchunguza moja kwa moja, kwa kutumia hojaji na mahojiano, kiwango cha umilisi na utendaji miongoni mwa wazee wanaosema Kimaragoli.

Utafiti wa Odero (2013) unaonyesha kwamba wazee wa Elmolo ndio wana umilisi na utendaji mkubwa wa kuwasiliana kwa lugha ya Elmolo, huku watu wachache wa makamo wakionyesha umilisi na utendaji huu katika miktadha mbalimbali kimatumizi. Katika utafiti wake, ruwaza za kimatumizi zinaonyesha kwamba mawasiliano katika lugha hii yalitokea sana baina ya wazee kwa wazee na wazee kwa makamo. Mawasiliano

baina ya wazee-vijana yalitumia lugha ya Kisamburu zaidi. Sababu kubwa aliyotambua nyanjani kuelezea ruwaza hii ni kwamba wazee ndio hazina ya maarifa ya lugha na utamaduni wa Kielmolo. Umri wa makamo hautumii lugha hii sana kwa sababu wameshajua Kisamburu na wanakionea fahari licha ya kwamba wana ufahamu haba wa Kielmolo. Matokeo miongioni mwa vijana (miaka 16-25) yalionyesha kwamba vijana hawakujua lugha hii kwa sababu hawakutaka kufundishwa na wazee wao. Hii ndiyo sababu Odero alihitimisha kwamba, Kielmolo huenda kikafa ikiwa hakutakuwa na juhudi za kuirithisha kwa vijana. Utafiti wa Odero (2013) japo ulishughulikia umilisi na utendaji, haukujifunga kwa makundi ya wazee. Makundi aliyochunguza kwa kutumia hojaji ni watu wazima (miaka 26-55), vijana (miaka 16-25) na watoto walio chini ya miaka 15. Kwa hiyo, utafiti wake haukulenga wazee waliozidi miaka 55. Utafiti huu ulihakikisha kwamba kundi hili limetathminiwa kwa lengo la kupata data iliyoakisi taswira kamili ya makundi yote ya kiumri na kuonyesha mchango wake katika udumishaji wa lugha hii kwa vizazi vya makamo, vijana na watoto.

Birman na Poff (2011) katika utafiti wao walitambua tofauti za kiumilisi zilizokuwepo kati ya vizazi viwili vya wahamiaji nchini Marekani: wazazi walikuwa na umilisi wa hali ya juu ilhali watoto wao walikuwa na wa kiwango duni. Baada ya miaka kadhaa ya uhamiaji, watoto waliishia kuhamia Kiingereza huku wazazi wakidumisha lugha zao za kiasili (lugha za Kiturathi) kwa sababu hawakuwa na hazina tosha ya msamiati kujieleza kama wazee wao. Wanadai kwamba, watoto hawa huchukua kati ya mwaka 1-2 kujifunza lugha ya wenyeji na miaka 5-7 kufikia kiwango cha umilisi wa wenyeji. Kwa kuwa wazazi wao hawana kasi na ari ya kujua lugha kama watoto wao, huamua kudumisha lugha yao. Tatizo hutokea baadaye kimawasiliano kwa sababu vizazi hivi viwili hushindwa kuwasiliana kutokana na ukosefu wa umilisi katika lugha maalum

(wazee hawana umilisi wa lugha ya wenyeji ilhali watoto hawana umilisi wa lugha yao asili).

Utafiti wa Birman na Poff (2011) japo ulishughulikia lugha za wahamiaji Marekani, ulikuwa na mchango katika utafiti huu. Ulimpa mtafiti umakini wa kuzingatia tofauti za kiumilisi kati ya makundi haya mawili. Aidha, ulimpa mtafiti fursa ya kuchunguza ikiwa kunazo juhudi zozote za kurithisha umilisi wa kiisimu kutoka kwa wazee hadi kwa watoto na vijana.

Inaaminika kwamba wazee ndio hazina na dafina ya lugha asilia. Kwa kuwa wameizungumza tangu wakiwa watoto wadogo, inadhaniwa kwamba kiwango chao cha umilisi ni cha juu sana ikilinganishwa na vizazi vinavyowafuata. Utafiti wa Kipp (2009) unathibitisha kwamba wazee ndio walitumiwa kudumisha lugha ya *Blackfoot* wakati hapakuwepo na vijana walimu. Walifundisha watoto sauti, silabi na namna ya kuzitamka. Aidha, walifundisha methali, mafumbo, misemo, viziada lugha, upole na adabu inayopatikana katika *Blackfoot*. Ni kupitia kwa wazee hawa basi lugha hii ilipata wazungumzaji wachanga. Utafiti miongoni mwa jamii asilia za Michigan unaonyesha kwamba wazee wa *Anishinaabemowin* walikusanyika kwa lengo la kuweka nadhiri ya kuwafundisha vijana wao lugha baada ya kutambua kwamba walikuwa wanaelekea kuzungumza Kiingereza na kusahau *Kianishinaabemowin*. Walitambua uwezo wao wa kuhodhi maarifa ya kiasili yaliyostahili kurithishwa kwa kizazi hiki cha vijana (Noori, 2009). Nchini Ugiriki, utafiti wa Tsitsipis (1989) katika Thomason (2001) unaonyesha kwamba ni wazee tu waliweza kuongea na kudumisha lugha ya Kiarvanitika. Mzee mmoja alidai kwamba hawezi kuongea na vijana kwa sababu hawajui; hawana umilisi wa Kiarvanitika isipokuwa wazee wenzake tu.

Katika jimbo la Carlifornia, kulitokea mradi wa kuunganisha wazee na vijana kwa lengo la kurithisha lugha asili. Vijana waliwekwa katika makundi au seti iliyojumuisha kijana na mzee na kuwa na mazungumzo ya kawaida tu katika lugha asilia. Hali hii ilikuwa ikifanyika kila mara hadi wazee waliporidhika kwamba wamepasha kizazi kipya lugha yao ya Kiarvanitika (Maracle na Richards, 2002; Hinton, Steele na Vera, 2002). Juhudi hizi zote zinaonyesha namna ambavyo wazee wanamiliki uwezo mkubwa, sio tu wa msamiati, bali pia maarifa ya kitamaduni ambayo huandamana na lugha hizi asilia.

Tafiti hizi zinaonyesha kwamba kwanza, wazee ni kipengele muhimu sana katika udumishaji lugha. Pili, wazee wanapowekwa na vijana pamoja kwa ajili ya kurithisha lugha na utamaduni, huu unageuka kuwa mkakati wa kudumisha lugha. Hata hivyo, mbinu hii ya kurithisha ilikuwa juhudi ya king'amuzi na ndiyo ilizalisha matokeo mazuri ya udumushaji lugha. Hali halisi ya mtagusano wa wazee na vijana Uriri ilistahili kuchunguzwa. Ilikuwa muhimu katika utafiti huu kutambua kwamba kuchunguza umilisi wa wazee wanaosema Kimaragoli pamoja na juhudi wanazofanya katika kudumisha lugha hii kungechangia kupata data faafu. Hii inatokana na pengo lililopo katika tafiti za Kipp (2009), Noori (2009) na Tsitsipis (1989) kuwa waliangazia lugha asilia za mataifa mbalimbali isipokuwa bara la Afrika. Pia, mikakati ya kuunganisha wazee na vijana katika mikutano maalumu huenda haitumiki katika jamii ya Wamaragoli na hivyo kulikuwa na haja ya kuchunguza jinsi urithishwaji wa Kimaragoli unafanyika.

## 2.5 Athari za Mtagusano Lugha

Mtagusano lugha ni mchakato ambapo lugha mbili au tatu zinajikuta katika utangamano athirishi, yaani, lugha moja inaathiri nyingine kwa vipengele kama vile msamiati na muundo wa lugha (Sankoff, 2001 na Thomason, 2001). Wataalamu wengi (Ralli, 2001; Sankoff, 2001; Dawson, 2003; Heine na Kuteva, 2008 na Hoffer, 2002) wanaelekea

kukubaliana kwamba kuna athari au matokeo manne ya mtagusano lugha: Athari ya kifonetiki/kifonolojia; Athari ya kileksimu; Athari ya kisarufi/kisintaksia na kidiskosi/kiuamali; Athari ya kimofolojia. Thomason (2001) anaongezea athari mbili ambazo zinatokea katika mtagusano lugha: ubadilishaji msimbo; uchanganyaji msimbo. Athari hizi zimejadiliwa katika sehemu zinazofuata.

### 2.5.1 Athari ya kifonolojia

Lugha mbili zinapotagusana kwa muda mrefu, huishia kuathiriana kwa kiwango cha kimsingi kabisa (Ralli, 2001); kiwango cha kifonolojia. Kwa kuwa kila lugha ina sauti zake, namna ya kuzitamka, mahala pa kuzitamkia na kadhalika, lugha hizi zinapotagusana, baadhi ya nduni hizi za kimsingi huhawilishwa kutoka L1 hadi L2 (Poplack na Sankoff, 1984). Ikiwa nduni hizi za kimsingi kama vile toni, mkazo na hata ukopaji wa foni utakubalika na kuwa sehemu ya lugha moja, basi wataalamu hawa wanadai kwamba hayo ni mabadiliko yanayotokana na athari za mtagusano lugha.

Kwa mfano, tafiti kadha zinaonyesha kwamba Kiswahili kilipata sauti [θ], [ð], [kh] na [gh] baada ya kutagusana na kuathiriwa na Kiarabu kwa zaidi ya karne 5 (Baldi, 2012 na Thomason, 2001). Katika kipindi cha urasimi mkongwe wa ushairi, lugha ya Kiswahili ilijiongezea sauti [q] ila baada ya muda mfupi sauti ya [k] ya Kiswahili ilionekana kutamalaki kiuamilifu sauti hii ngeni ya Kiarabu na hivyo kuififisha. Hata hivyo, sauti [θ, ð] zilisalia kwa kuwa hapakuwepo na vibadala vyake katika fonolojia ya Kiswahili. Utafiti wa Baldi unaonyesha kwamba fonolojia ya lugha moja iliyo kuu inaweza kuathiri nyingine kupitia kwa ukopaji wa maneno. Hata hivyo, utafiti huu uliegemea mbinu ya nyaraka kukusanya data. Mtafiti alitumia kamusi na maandishi mengine (ambayo hakutaja) kukusanya maneno yaliyokopwa kutoka Kiarabu hadi lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulitumia mbinu ya makundi ya mijadala lingani, mahojiano na hojaji kukusanya data kuhusu jinsi Kiluo kimeathiri Kimaragoli.

Watera (2014) alipotafitia athari za mtagusano lugha kati ya Lubukusu na Kiingereza alitambua kwamba Kibukusu kilikopa maneno kutoka kwa Kiingereza na hivyo kuchukua baadhi ya nduni za kisauti kama vile uimarishaji, udondoshaji, ubadilishwaji, unazalishaji na ubadilishaji wa konsonanti na irabu. Alitambua kwamba japo lugha hizi mbili hazina tipolojia au mnasaba mmoja, lugha ya Lubukusu inapochukua maneno ya Kiingereza, inayabadilisha ili yaendane na mfumo wa fonolojia ya Lubukusu. Utafiti wa Watera ulitumia mbinu ya mahojiano na kinasa sauti kukusanya data ya utafiti miongoni mwa watafitiwa 85. Alitumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ya Hooper. Utafiti wa Watera (2014), ambao ulikuwa wa kithamano, ulitambua kwamba Kibukusu hakikuathiriwa kwa mujibu wa kifonolojia kwa sababu kilifuata taratibu zote wakati wa kuhamisha neno kutoka kwa Kiingereza hadi Kibukusu. Tofauti na utafiti wa Watera, utafiti huu ulitumia mbinu mseto kukusanya data ya utafiti hasa kwa kuangalia kwa ujumla jinsi Kimaragoli kiliathiriwa na Kiluo.

Utafiti wa Ontieri (2013) unaonyesha kwamba Kiswahili kimeathiriwa na lugha za kwanza miongoni mwa wanafunzi wa Kibantu wanaojifunza Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yanathibitisha kwamba namna mwanafunzi anaandika maneno ya Kiswahili inategemea kiwango cha athari ya lugha yake ya kwanza. Alibainisha kwamba wanafunzi walikuwa wanachopeka, wanadondosha au wanabadilisha fonimu kwa baadhi ya maneno katika insha zao. Utafiti wa Ontieri japo uliegemea athari za kifonolojia katika uamiliaji wa lugha ya pili iliyo na mnasaba mmoja na lugha asilia ya mwamiliaji, ulikuwa na mchango katika utafiti huu. Ulionyesha jinsi mwathiriano huu wa kifonolojia unaweza

kutokea na kwa kiwango gani. Aidha, alidhihirisha kwamba lugha ndogo (asilia) inaweza kuathiri lugha kuu (Kiswahili).

Hata hivyo, utafiti wa Ontieri ulitofautiana na utafiti huu kwa misingi kadhaa: kwanza, Ontieri aliegemeza utafiti wake kwa uchanganuzi wa makosa miongoni mwa wanafunzi wanaoamilia lugha ya pili. Pili, alichunguza fonolojia ilhali utafiti huu ulichunguza vipengele vingine kama vile mofolojia, uchanganyaji na ubadilishaji msimbo. Utafiti huu ulilenga kubainisha athari hizi na pia sababu zake. Hii ndiyo sababu mtafiti alitumia mbinu za mahojiano, makundi lengwa ya mijadala, uchunzaji na ushiriki ili kukusanya data inayoweza kujieleza kikamilifu. Tatu, utafiti wake ulitumia nadharia ya uchanganuzi wa makosa kwa sababu lengo kuu lilikuwa ni kuainisha na kuchanganua makosa ya wanafunzi. Utafiti huu kwa kuwa haukulenga kutafuta makosa, ulitumia nadharia ya Mtagusano lugha kujaribu kueleza matokeo ya mtagusano lugha kati ya Kimaragoli na Kiluo.

Utafiti wa Lotta (2014) unaonyesha kwamba lugha ya Ikoma iliathiriwa na Datooga katika namna ya utamkaji. Utafiti huu ulitambua kwamba Ikoma (lugha ya Kibantu) inayosemwa Mkoani Mara Tanzania, imeathiriwa na Datooga (lugha ya Kinailoti) katika mfumo wa toni katika fonolojia. Utafiti huu ulianzishwa na Nurse na Rottland (1991) waliotoa nadharia tete kwamba, lugha za Kibantu (JE40) katika maeneo ya Mara ziliathiriwa na lugha za Kinailoti katika (jinsi ya) utamkaji wa irabu. Winford (2003) anakiri kwamba wakati mwingine, ukopaji wa fonolojia kutoka lugha ya wengi hadi lugha ya wachache ni tukio nadra sana, ila si kwamba haliwezi kutokea. Hivyo, utafiti huu ulitaka kuthibitisha dai hili la Nurse na Winford ikizingatiwa kwamba tulikuwa tunatafitia Kimaragoli (Bantu) na Kiluo (Nailoti) kwa lengo la kupinga au kuunga mkono.

Utafiti wa Marina (2014) unaonyesha kwamba athari za lugha ya wengi kwa lugha ya wachache inawezekana. Anakita utafiti wake katika lugha za Kiingereza na Kiairishi ambazo zimetagusana tangu mwisho wa Karne ya 12. Anabainisha kwamba Kiairishi kimeathiriwa na lugha ya Kiingereza hasa katika baadhi ya maumbosauti kwani nduni kama vile ukaakaaishaji imeingizwa ndani yake. Mbali na ukaakaaishaji, baadhi ya sauti kama vile irabu zinaweza kufupishwa ikiwa lugha zinazotagusana zina sifa za urefushaji wa mkazo wa irabu ilhali nyingine ina ufupishaji wa mkazo wa irabu. Kwa mfano, lugha za Kale za Italia kama vile Kietruskani, Kilatini na lugha za Kisabeli zilikuwa na mkazo wa irabu, hata hivyo, baada ya mtagusano na lugha nyinginezo kama vile Kiitaliano, lugha hizi zimeishia kuwa na irabu iliyofupishwa (Nicholas, 2014). Thomason (2001) anadai kwamba lugha ya Kizulu ilikopa fonimu kidoko kutoka lugha za Kikhoisani na hivyo kuathiri mfumo wa fonolojia wa Kizulu. Tafiti za wataalamu hawa zinaonyesha kwamba fonolojia inaweza kuathiriwa kwa kiwango cha toni, mkazo au hata kubadilisha sauti fulani maalumu. Mtagusano lugha ni suala ambalo hutofautiana kutegemea eneo la kijiografia na hivyo utafiti huu ulitegemea kwamba matokeo ya mtagusano lugha kati ya Kimaragoli na Kiluo yangekuwa tofauti. Hii ni kwa sababu mtagusano kati ya lugha za Kiingereza, Kiairishi, Kilatini, Kietruskani na Kisabeli unatendeka ndani ya mnasaba mmoja hivyo ni rahisi kutokea ikilinganishwa na minasaba tofauti kama vile Kimaragoli na Kiluo.

Tafiti za wataalamu hawa, hasa Marina (2014), na Thomason (2001) zinaonyesha kwamba uwezekano wa athari hizi upo. Hata hivyo, tafiti za Marina na Thomason zilizingatia lugha zilizo katika mnasaba mmoja wa Kihindi-Kiulaya na Kibantu cha Kusini wakati ambapo Kimaragoli na Kiluo ni za familia mbili tofauti: Kibantu na Kinailoti. Utafiti wa Rotland na Nurse (1991) ulichunguza lugha zilizotagusana kwa

zaidi ya miaka mia moja nchini Tanzania. Ni muhimu kutambua kwamba Kimaragoli na Kiluo hazijazidi miaka mia moja na hivyo hali inaweza kuwa tofauti.

### 2.5.2 Athari ya kileksimu

Kwa mujibu wa Prihantoro (2009) na Khrisat na Mohamad (2014), lugha zote duniani zimekuwa zikikopa maneno kutoka kwa lugha nyinginezo na sababu kubwa ni ukosefu wa msamiati mwafaka wa kueleza dhana fulani. Hata hivyo, baada ya kila lugha kukopa ma(neno), huhakikisha kwamba (ma)neno hayo yamefuata mifanyiko yote ya kifonetiki na kifonolojia ili kuhakikisha kwamba sifa za lugha pokezi zimejitokeza katika neno mkopo. Mbali na mabadiliko ya kifonetiki na kimofolojia, maneno hayo pia huweza kupata maana mpya (Khrisat na Mohamad, 2014).

Nagy (1996; 2010) anadai kwamba leksimu katika lugha yoyote ndicho kipengele kikubwa ambacho huathirika katika mtagusano lugha. Hiki ndicho kipengele cha kwanza katika kuathirika kwa lugha ya wachache kisha baada ya muda mrefu, ngazi zingine kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia huathirika. Mbinu ambayo hutamalaki uingizwaji wa leksimu mpya katika lugha ya wachache ni ukopaji. Ukopaji wa leksimu ni mchakato wa kimsingi wa mtagusano lugha, ambao ukiruhusiwa kuendelea kwa muda mrefu, husababisha wingilugha, uhamaji lugha au hata uhamaji utamaduni (T’sou, 2001). Athari ya kileksimu aghalabu huzuka kutokana na mbinu ya ukopaji wa maneno maalumu kutoka L2 hadi L1 (Sankoff, 2001) ambapo katika utafiti wake, L2 ni lugha Kuu au yenye satua kubwa (hadhi ya juu) na L1 ni lugha ndogo (hadhi ya chini). Kwa mujibu wa utafiti huu, L1 itakuwa ni Kimaragoli huku L2 ikiwa Kiluo. Hivyo, utafiti ulitaka kuthibitisha ikiwa kweli Kiluo (L2) kimeathiri Kimaragoli (L1).

Katika hali ya mtagusano lugha, ukopaji hujitokeza bayana katika lugha ya wachache, ambayo ndiyo inakuwa L2 huku lugha ya wengi ikiwa ni L1. Tafiti za Poplack na wenzake (1998) na van Hout na Muysken (1994) zinaonyesha kwamba aina za maneno ambayo hukopwa sana na lugha ya wachache huwa ni nomino, vitenzi na vivumishi. Wanatoa sababu ya ukopaji wa aina hizi za maneno kuwa ndizo za kimsingi katika lugha na wakati wa mawasiliano baina ya wasemaji wa L1 na L2, umaratokezi wake kitakwimu si mdogo. Baadhi ya nomino ambazo hukopwa kutoka lugha ya wengi ni majina ya vyakula (T'sou, 2001). Utafiti wa Dawson (2003) unaonyesha baadhi ya nomino zilizokopwa kutoka lugha ya Kinorisi Azali na kuingizwa katika Kiingereza Azali miaka ya 800-100BK.

Ingawa misamiati hii ilikopwa kutoka lugha ya Kinorisi Azali, palitokea mabadiliko katika kiwango cha kifonolojia ya Kiingereza Azali. Hata hivyo, kuna maneno ambayo yalichukuliwa kama yalivyokuwa kutoka Kinorisi Azali hadi Kiingereza Azali bila kubadilisha hata umbosauti moja. Kwa mfano, jedwali 2.1 linadhihirisha mchakato huu:

**Jedwali 2.1: Nomino mkopo kutoka Kinorisi Azali hadi Kiingereza Azali**

| **Kiingereza Azali** | **Kinorisi Azali** | **Tafsiri (Kiswahili)** |
|---|---|---|
| **Eyethurl** | Eye hole | Kitasa |
| **Vindauga** | Window | Dirisha |
| **Taka** | Take | Chukua |

(Hisani ya Dawson, 2003)

Maneno haya yalichukuliwa na kuwa sehemu ya Kiingereza sanifu ambacho kinasemwa hadi leo. Maneno ya Kiingereza Azali "Eyethurl", "Vindauga" na "taka" yalidondoshwa kabisa na kuchukuliwa mahali pake na maneno ya Kinorisi Azali (Dawson, 2003). Hii ina maana kwamba maneno hayo ya Kiingereza Azali yalipotea kabisa. Kiingereza cha sasa kina maneno "eye hole", "window" na "take" yaliyokopwa kutoka Kinorisi Azali.

Katika mchakato wa ukopaji leksimu kutoka lugha ya wengi hadi lugha ya wachache, kuna vibadala ambavyo hutawala mchakato huu. Vibadala hivi ni jinsia, umri, tabaka la kijamii, mtandao wa kijamii na mielekeo ya kiisimu (Chambers, 1992; Nagy, 2010). Kibadala cha jinsia kimeibuka kuwa kichapuzi kikubwa katika ukopaji wa misamiati mipya. Kwa kuwa wanawake huolewa kwa wanaume wanaosema lugha ya wengi, huishia kujifunza misamiati ya lugha yao na hatimaye kuiingiza katika lugha zao ambazo huwa za wachache (Nagy, 2010; Thompson, 2001; Obiero, 2008; Paulston, 1994; Ang'iela, 2002). Utafiti wa Chambers (1992) unaonyesha kwamba wasemaji wachanga wa lugha ya wachache hujifunza leksimu za lugha ya wengi na hatimaye kuidahili katika lugha yao ikilinganishwa na wasemaji wazee. Anahitimisha kuwa ikiwa patatokea mabadiliko makubwa katika matamshi na leksimu ya lugha ya wachache, basi wachangizi wakubwa watakuwa wasemaji wachanga.

Wataalamu mbalimbali waliochunguza mwingiliano wa lugha ya Kiswahili na Kiarabu wametambua uhusiano mkubwa uliopo kimsamiati (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Baldi, 2012; Babusa, 2012;Adung'o, 2016). Walitambua kwamba Kiswahili kimekopa maneno mengi kutoka kwa Kiarabu baada ya kutagusana kwa muda mrefu. Jedwali 2.2 linaonyesha aina za maneno yaliyokopwa kutoka kwa Kiarabu:

**Jed. 2.2 Maneno mkopo kutoka kwa Kiarabu**

| Nomino | Vielezi | Vivumishi | Vihisishi |
|---|---|---|---|
| Majinuni | Alhamisi | Wastani | Alhamdulillahi! |
| Hujaji | Alfajiri | Saba | Afanalek! |
| Maharaji | Alasiri | Tisa | Kefle! |
| Kitabu | Zamani | Wahedi | Salaale! |
| Mahari | Kadhaa | | Akh! |

(Mifano kutoka kwa Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Babusa, 2012; Baldi, 2012 na Adung'o, 2016).

Ni muhimu kutambua kwamba Kiswahili kilikopa mno (30%) kutoka kwa Kiarabu lakini hali hii imebadilika tangu kitagusane na Kiingereza. Kiswahili kinakopa kutoka kwa Kiingereza kwa sababu kwa sasa, Kiingereza ndiyo lugha ya hadhi ya juu na inayoathiri

pakubwa watumiaji wa Kiswahili. Kwa kuwa wasemaji wa Kiswahili wanazungumza Kiingereza kwa wingi kuliko Kiarabu au lugha nyingine yoyote ile ya Kimagharibi, ni rahisi wao kuhamisha maneno kutoka Kiingereza hadi kwa Kiswahili. Kwa jinsi hii basi, Kiswahili kinaathiriwa na Kiingereza.

Kwa mujibu wa Babusa (2012) Kiswahili kimekuwa kikikopa maneno haya kutoka kwa Kiarabu ila kwa kuhakikisha kwamba mfumo sauti wa fonolojia ya Kiswahili umezingatiwa. Mawazo haya ya utohozi pia yanasisitizwa na watalaamu waliotafitia mitagusano ya lugha nyinginezo kama vile Kiingereza-Kiarabu (al-Badri, 1986; Khrisat naMohamad,2014),Kijapani/Kiingereza(Hoffer,2002),Kiingereza/Kiitaliano/Kilatini/Kifaransa/Kijerumani/Kihebrania/Kichina (Hoffer, 2002) na Kikorea-Kiingereza (Prinhantoro, 2009). Kwa ujumla, wanakubaliana kwamba lugha moja inapokopa lugha nyingine katika mazingira ya mtagusano, maneno mkopo huishia kuwa sehemu ya lugha hiyo, na hata kwa kiasi fulani, kusanifishwa na kutumiwa na wasemaji wa lugha hiyo. Utafiti huu ulichunguza hali hii ya ukopaji wa leksimu baina ya Kimaragoli na Kiluo katika eneobunge la Uriri, nchini Kenya. Mtafiti alitaka kujua iwapo baadhi ya maneno yamekuwa sehemu ya Kimaragoli au ni ya kutumika kama misimu na kutoweka baada ya kipindi au katika kundi fulani la kiumri.

### 2.5.3 Tokeo la kimofolojia

Lugha mbili zinapotagusana, aghalabu hutokea shani ya kukopana vipengele anuwai vya kiisimu. Mojawapo ya vipengele hivi ni mofolojia. Mofolojia kama kiwango cha isimu hushughulikia uundaji wa maneno na mnyambuliko (Karanja na Habwe, 2004; Matinde, 2012). Mtagusano lugha huathiri kiwango hiki kwa njia kadhaa: kwanza, lugha moja inaweza kuchukua mofu maalumu na kuchopeka katika maneno yake maalum; pili, lugha inaweza kuchukua neno zima (mofu huru) na kulifanyia mabadiliko ili lilingane na

muundo wa mofu za lugha hiyo. Tafiti kadhaa zimefanywa na wataalamu kuhusu jinsi ambavyo mtagusano wa lugha umesababisha mabadiliko katika mofolojia ya lugha pokezi.

Utafiti wa Mufwene (2014) unaonyesha kwamba Kiswahili kiliposambaa na kuingia nchini Kongo, hakikuchukua muundo wa Kiswahili cha Pwani ya Afrika Mashariki. Kiswahili hiki cha Pwani kilifanyiwa marekebisho kutegemea lugha za Kikongo kama vile Kilingala na Kishaba. Mufwene anadai kwamba viambishi vya lugha hizi za Kongo vya kuonyesha hali vilichukuliwa na kupachikwa mwishoni mwa neno la Kiswahili, hasa vitenzi. Kwa mfano, mofu ya hali ya kawaida au kitenzi kuendelea {-nga} ilichukuliwa na kuambishwa mwishoni mwa vitenzi hivi vya Kiswahili kama vile "balikujanga" na "alikwendanga" (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Utafiti wa Mufwene (2014) unaonyesha kwamba ukopaji na utohozi wa vipengele vya kimofolojia ni suala linalowezekana katika mtagusano lugha. Hata hivyo, ingawa utafiti wake ulikuwa na umuhimu, ulikuwa na udhaifu: haukuonyesha data isipokuwa mjadala wa kijumla kuhusu lugha ya Kiswahili ilivyotagusana na kuathiriwa na lugha zisemwazo Kongo. Utafiti huu ulionyesha moja kwa moja njia na mbinu za utafiti pamoja na nadharia ya utafiti.

Anyona (2016) alitafitia lugha ya Ekegusii na jinsi inavyoathiri maneno mkopo ya Kiingereza. Alihitimisha kwamba mofolojia ya Ekegusii hailingani wala kuingiliana na ya Kiingereza na hivyo maneno yaliyokopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza hayakuzingatia mfumo wa kimofolojia wa Kiingereza. Alipendekeza kwamba tafiti zaidi zifanywe kati ya Ekegusii na lugha nyinginezo (za Kiafrika) katika ngeli mbalimbali. Pia utafiti huu ulijitokeza kufidia pengo hili la kiakademia ila kwa kuchunguza lugha ya Kimaragoli na Kiluo. Hata hivyo, Anyona alitafitia wasemaji 17 wa Ekegusii huku utafiti

huu ukitumia wasemaji 244. Hii ina maana kwamba utafiti huu ulikuwa na uwezo wa kupata data nyingi na ya kina.

Gibson (2013) aliyetafitia visaidizi katika lugha ya Kirangi inayosemwa katika Bonde la Ufa la Kati na Kaskazini mwa Tanzania alitambua kwamba visaidizi vinavyozungumzia nafsi si asili ya Kirangi bali huenda vilikopwa kutoka kwa Kialagwa au Kiburunge. Matokeo yake yanadai kwamba vikanushi katika Kirangi havitokei mwishoni mwa sentensi bali kikanushi {si} kinatokea ndani ya sentensi. Hata hivyo, Kirangi kina kikanushi {tuku} ambacho kinatokea baada ya kitenzi; upya huu wa kimofosintaksia anavyodai Gibson (2013) huenda ulikopwa baada ya Kirangi kutagusana na Kialagwa na au Kiburunge. Katika utafiti wake, Gibson anadai kwamba matokeo ya aina hii hayawezi kutokea kwa muda mfupi, na pia, lazima mtagusano wa lugha hizi mbili uwe wa hali ya juu. Utafiti huu ulikuwa na mchango kwa utafiti huu kwa sababu ulimwongoza mtafiti kuchunguza viambajengo vya kimofosintaksia ambavyo huenda chanzo chake ni lugha ya Kiluo.

Ralli (2001) alipotafitia lugha za Kituruki na Kiaivialoti (Kigiriki cha Asia Ndogo) alitambua kwamba baadhi ya vitenzi vya Kiaivialoti vilikuwa vimesheheni mofu kutoka kwa lugha ya Kituruki. Anadai kwamba lugha hizi zimetagusana kwa zaidi ya karne 3, na muda huu mrefu ndio umesababisha athari hii ya Kituruki katika Kigiriki cha Asia Ndogo licha ya kwamba Kituruki ni lugha ambishi na Kiaivialoti ni lugha ambishi tenganishi. Lugha zinaweza kukopa vitenzi au elementi za vitenzi kwa kufuata kanuni zifuatazo: kuchopeka mzizi wa kitenzi katika mofolojia ya lugha pokezi; kukopa kitenzi kisaidizi kutoka kwa L1 hadi L2 (ambacho lengo lake ni kusimilisha kitenzi mkopo); kukopa kitenzi kizima kama kinavyotumika katika L1 (Wichmann na Wohlnemuth, 2008). Utafiti wa Ralli unaonyesha kwamba ruwaza ya ukopaji ilizingatia mbinu ya

unominishaji na mbinu ya kukopa vitenzi mahsusi. Hata hivyo, katika mchakato wa ukopaji, kanuni za kisarufi za Kigiriki ndizo zilitawala muundo wa kitenzi mkopo. Ingawa utafiti huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu, uliegemea lugha za Kiulaya zilizotagusana kwa muda mrefu.

Tafiti kadhaa zinaonyesha namna ambavyo Kiingereza kimeanza kuathiri mofolojia ya maneno ya Kijapani (Hoffer, 2002). Kwa mfano, neno kama vile *demo (ru)* lina mofu inayotokana na neno la Kiingereza *demo (nstrate).* Mofu ya Kiingereza *{demo}* imeingizwa katika Kijapani na kisha kuongeza kiishio cha kitenzi *{ru}.* Aidha, mofu *{now}* ya Kiingereza imeingizwa katika Kijapani na kuchukua umbo lililotoholewa *{nau};* umbo hili kisha linaongezewa kiishio cha kitenzi cha Kijapani *{i}* na kuunda neno *{naui}* kwa maana ya sasa. Neno jingine ambalo limetokana na mofu *{nau}* ni *{naukatta}* kwa maana ya 'haijasasishwa'. Utafiti wa Hoffer unazingatia sana kipengele cha mwathiriano kwa mujibu wa teknolojia na vijana. Upya uliomo katika Kijapani unachapuzwa na vigezogeu hivi viwili. Hata hivyo, lugha ya Kimaragoli haimo katika teknolojia kama vile ya simu, tarakilishi na tovuti.

### 2.5.4 Uhamishaji Msimbo

Uhamishaji msimbo unaweza kuelezwa kama, "matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo au tendo la uzungumzi"(Grosjean, 1982; Malik, 1994). Myers-Scotton (2006) anaeleza dhana hii kama matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo bila kuathiri sarufi ya lugha pokezi. Winford (2003) anaona kuwa uhamishaji msimbo ni shughuli inayohusu uhamishaji wa maneno kati ya lugha mbili zinazotumika na mzungumzaji mmoja. Romaine (2002) anasema kuwa, "uhamishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo au maandishi". Kulingana na maelezo haya yote, kile kinabainika wazi ni kuwa dhana ya uhamishaji msimbo hujitokeza pale

mzungumzaji mmoja au kundi jamii lake wana umilisi wa lugha mbili tofauti au zaidi wanazoishia kuzitumia kwa wakati mmoja katika mazungumzo yao au maandishi. Lugha hizi ni pamoja na lugha yake ya mama na pia lugha nyinginezo ambazo amejifunza shuleni au katika mazingira asilia pale jamii yake au yeye binafsi (w)anapokutana na kutagusana na lugha hizo maalumu (Gumperz, 1982a; 1982b). Kuna tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini Kenya na ulimwenguni kuhusu dhana ya uhamishaji lugha.

Uhamishaji msimbo miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu unaendelezwa kwa sababu mbalimbali, ikiwemo ya kiteknolojia (Barasa, 2016). Mtafiti huyu alichunguza wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya na kutambua kwamba wao kufahamu lugha zaidi ya moja, Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama, na kuwepo kwa teknolojia kunawasababisha kuhamisha misimbo kila wanapowasiliana. Utafiti wa Barasa ulichunguza majukwaa ya kiteknolojia ya barua pepe, *Facebook, Youtube*, arafa za simu tamba, na jumbe za papo kwa papo. Utafiti wa Barasa ulihitimisha kwamba kuwepo kwa zaidi ya lugha moja kunachochea michakato ya uhamishaji lugha. Hata hivyo, utafiti wake ulitofautiana na huu kwa sababu ulilenga jamii ya wanafunzi wa vyuo vikuu peke yake katika mtazamo wa kiisimujamii ilhali utafiti huu uliangazia wasemaji wa Kimaragoli kwa mtazamo wa udumishaji lugha. Kwa hivyo, malengo ya tafiti hizi yalitofautiana licha ya kwamba tafiti zote ziliangazia dhana ya uhamishaji msimbo.

Bosire (2006) alitafitia uhamishaji msimbo miongoni mwa Wakenya wanaoishi mjini Albay Creek, New York, Marekani. Alitambua kwamba Wakenya wengi waliochunguzwa walikuwa na lugha tatu walizotumia katika mazungumzo: Kiingereza, Kiswahili na lugha asili (hasa Ekegusii). Lugha hizi zilitumiwa kwa mpishano kutegemea washiriki wa mazungumzo. Ikiwa washiriki wa mazungumzo wote ni Wakisii, walitumia Ekegusii na Kiingereza kuwasiliana. Aidha, katika utafiti wake, Bosire alitambua

kwamba kuna baadhi ya washiriki ambao hawakutaka wenzao wahamishe msimbo au hata kuchanganya kwa sababu hii ilipunguza hadhi ya Kiingereza. Ingawa utafiti huu ulikuwa na umuhimu kwa utafiti huu (hasa mbinu za kukusanya data ya uhamishaji msimbo) ulitofautiana na utafiti huu. Tofauti ya kwanza ilikuwa eneo la utafiti: Bosire alichunguza washiriki waliohamia Marekani ilhali utafiti huu ulichunguza wahamiaji wa ndani ya nchi ya Kenya. Kwa kuwa tofauti za kieneo huathiri matokeo ya utafiti wa kiisimujamii, utafiti huu ulitambua kwamba matokeo ya tafiti hizi mbili hayangelingana. Pili, utafiti wa Bosire ulichukua mwelekeo wa kiisimujamii kwa hivyo alitaka kufahamu hali halisi ya uhamishaji lugha miongoni mwa Wakenya waliohamia Marekani ilhali utafiti huu ulitaka kujua ikiwa kuwepo kwa Kiluo kunaathiri udumishaji wa Kimaragoli.

Utafiti wa Ogechi (2002) ulichunguza uhamishaji msimbo miongoni mwa wasemaji wa lugha tatu: Kiingereza, Kiswahili, Ekegusii na msimbo wa Sheng' miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu, wanafunzi waliohitimu vyuo vikuu, wafanyikazi kama vile wahadhiri, mawakili na wahasibu. Utafiti wake ulitambua kwamba uhamishaji msimbo ni suala la kawaida miongoni mwa makundi haya. Utafiti wa Ogechi hata hivyo ulitofautiana na huu kwa misingi kadhaa: kwanza, madhumuni ya utafiti wake yalikuwa kuchunguza aina za uhamishaji, na sababu za uhamishaji na hivyo kuonyesha kwamba utafiti wake haukuchukua mwelekeo wa uhamishaji lugha kama athari mojawapo ya mtagusano lugha. Pili, utafiti wa Ogechi ulilenga wasemaji wa Ekegusii huku utafiti huu ukilenga wasemaji wa Kimaragoli. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba utafiti huu ulikopa masuala kadhaa kutoka kwa utafiti wa Ogechi: jinsi ya kukusanya data ya uhamishaji msimbo na pili, kutambua aina ya uhamishaji msimbo.

Mbali na Ogechi (2002) utafiti mwingine uliotafitia uhamishaji msimbo kwa kuzingatia Sheng' ni wa Mazrui (1995). Mtafiti huyu alitambua kwamba Sheng' ni msimbo wa

mawasiliano ulioibuka kwa sababu ya mtagusano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo zilizokuwa zinasemwa Nairobi. Ingawa Mazrui anatatizika kuhusu tofauti ya uchanganyaji na uhamishaji msimbo, utafiti wake unadhihirisha wazo kuu kwamba ili pawepo na uhamishaji msimbo, lugha mbili lazima zitagusane na kuathiriana. Utafiti wa Mazrui ulikuwa wa kuwekea msingi tafiti za baadaye kuhusu Sheng' na hivyo haukujikita kwenye mbinu za utafiti, nadharia au uchanganuzi wa data. Kazi yake ilikuwa andiko la kuchochea ufikiriaji kuhusu msimbo wa Sheng'. Kutokana na upungufu katika kazi yake, utafiti huu ulielewa haja ya kuhakikisha kwamba mbinu na nadharia za utafiti zilikuwa bayana kama zilivyofafanuliwa kiangavu katika Sura ya 3. Aidha, utafiti huu ulichukua mkondo wa kithamano na kitakwimu ili kuchora taswira kamili ya kisayansi kuhusu udumishaji lugha ya Kimaragoli.

### 2.5.5 Uchanganyaji msimbo

Kulingana na Bokamba (1989) uchanganyaji msimbo ni hali ya kuchopeka vizio au vipengele mbalimbali vya kiisimu kama vile viambishi, maneno, na vishazi vinavyotumiwa na washiriki mazungumzo kuelezea mawazo ambayo washiriki wenza wanafahamu au wanaweza kufahamu. Naye Ouma (2014) anadai kwamba uchanganyaji msimbo ni uhamishaji wa vipengele vya kiisimu kutoka lugha moja hadi nyingine; ni mchakato wa kuchopeka neno ama kishazi katika sintaksia ya lugha nyingine inayohusishwa katika mawasiliano. Kwa mujibu wa Wardhaugh (1992; 2002), uchanganyaji msimbo si tendo la kishelabela bali huhitaji washiriki mazungumzo kuwa na umilisi tosha wa lugha zote zinazohusika katika mawasiliano. Katika miktadha ya uchanganyaji msimbo, ni muhimu kufahamu kwamba hali ya kiisimu lazima iwe ya wingilugha dhabiti na kwamba mazungumzo yanapoendelea, yasikumbane na vikwazo vya kiuamali. Hii ina maana kwamba washiriki lugha faradhi wafahamu lugha zote kwa undani kiasi cha kufahamu viambishi, maneno, na vishazi vinavyotumika. Uchanganyaji

msimbo, kama ilivyo uhamishaji msimbo, ni tukio maalumu la mtagusano lugha. Katika kujaribu kujenga msingi wa dhana hii kwenye utafiti huu, tulirejelea wataalamu kadhaa walioshughulikia uchanganyaji msimbo nchini Kenya na kwingineko.

Utafiti wa Lee (2006) ulishughulikia uchanganyaji msimbo katika taifa la Korea. Malengo ya utafiti wake yalikuwa hasa kutambua mbinu zinazotumika katika uchanganyaji msimbo (uchopekaji, ubadilishaji na leskimu sambamba) na pia sababu za uchanganyaji msimbo baina au miongioni mwa washiriki mazungumzo. Miongoni mwa sababu zilizobainishwa ni kama vile sababu za kimuktadha, jukumu la washiriki, vipengele mahsusi vya kiujumbe, mielekeo ya washiriki mazungumzo, ubabe wa kiisimu na kutaka kujihisi salama kimawasiliano. Ingawa Lee hakuonyesha mbinu za sampuli wala nadharia za utafiti, mawazo yake yalinufaisha utafiti huu kwa sababu ulibainisha mbinu za uchanganyaji msimbo zilizostahili kuchunguzwa ikiwa zilikuwa zinajitokeza au la miongini mwa wasemaji wa Kimaragoli eneobunge la Uriri. Kwa kuwa Lee hakushughulikia uchanganyaji msimbo kwa mkabala wa udumishaji lugha, utafiti huu uliona pengo lililostahili kufidiwa kiutafiti: kwamba uchanganyaji msimbo unaweza kuathiri udumishaji lugha?

Kalmanlehto (2014) alitafitia uchanganyaji na uhamishaji msimbo miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu cha St. Augustine, Mwanza, Tanzania. Utafiti wake ulitambua kwamba wanafunzi wengi walikuwa wanachanganya msimbo wa Kiswahili-Kiingereza hata wanapoulizwa swali kwa lugha ya Kiingereza. Sababu kubwa ya hali hii ni umilisi finyu wa lugha ya Kiingereza. Utafiti wa Kalmanlehto ulitumia mbinu za mahojiano, uchunzaji na hojaji kukusanya data ya kimsingi pamoja na uhakiki mbalimbali ya maandishi kuhusu lugha nchini Tanzania. Kwa ujumla, alihoji wanafunzi 8 wa michepuo wa anthropolojia na elimu na pia kugawa hojaji 51 (zilizorudi ni 33). Kiini cha utafiti wa

Kalmanlehto kilikuwa kuchunguza matumizi lugha katika mazingira ya wingilugha miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu. Hii ina maana kwamba utafiti wake ulitofautiana na utafiti huu kwa sababu zifuatazo: kwanza, wakati ambapo Kalmanlehto alilenga kuchunguza tabia za lugha katika wingilugha, utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi uchanganyaji msimbo ni sehemu ya mtagusano lugha, na hasa unavyoathiri udumishaji wa Kimaragoli. Pili, utafiti wa Kalmanlehto ulichunguza wanafunzi wa vyuo vikuu ilhali utafiti huu ulilenga wasemaji wa Kimaragoli. Tatu, utafiti wake ulikuwa wa kithamano ilhali utafiti huu ulikuwa mseto: kithamano na kiwingiidadi.

Ouma (2014) aliyetafitia uchanganyaji msimbo wa Kiluo-Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi Uriri alitambua kwamba mchakato huu ni wa kawaida na wa kila siku miongoni mwao. Aidha, alitambua kwamba wanafunzi walishiriki aina tatu za uchanganyaji msimbo: wa ndani ya neno, ndani ya sentensi na uambishaji. Wanafunzi hawa ingawa hawakujua kwamba wanashiriki uchanganyaji msimbo (kwa kuwa ni tendo la king'amuzibwete), walifurahia kila wakati. Ouma (2014) anatoa mifano kama vile, ***Ka oola betie, adwaro ni***we go home (nimechoka kukaa hapa nataka kuenda nyumbani) na ***Piny osiko to ok sikie,*** indeed death is inevitable (ulimwengu ni wa milele lakini kifo hakiepukiki). Ouma alihitimisha kwamba kadiri wanafunzi hawa wanavyozidi kuchanganya msimbo ndivyo wanavyozidi kuathirika katika kukumbuka baadhi ya maneno ya lugha maalumu. Hitimisho lake lilikuwa na mchango katika uumbaji wa tasnifu hii kwa sababu tokeo la uchanganyaji msimbo linaathiri uwezo wa akili kukumbuka kwa haraka maneno ya lugha asilia. Hali hii inaporuhusiwa kuendelea kwa muda mrefu, huathiri wasemaji wa lugha asili kwani hupunguza idadi ya msamiati na hata kusababisha uchakaishaji wa lugha asilia.

Mawazo haya ya Ouma (2014) yanakwenda sambamba na ya Odero (2013) aliyetambua kwamba vijana na makamo wa Kielmolo walikuwa na mazoea ya kuchanganya msimbo kwa sababu hawakuwa na ujuzi wa Kielmolo. Hivyo, ili kufidia udhaifu wao, waliishia kuchanganya maneno ili wajiwasilishe. Utafiti wa Ouma (2014) na Odero (2013) licha ya kwamba zilikuwa na mchango katika utafiti huu, zilikuwa na malengo tofauti. Lengo kuu la Ouma lilikuwa ni kubainisha hali halisi ya uchanganyaji msimbo ilhali Odero aliazimia kutambua mabadiliko ya kiisimujamii katika lugha ya Kielmolo. Lengo kuu la utafiti huu ni kuweka wazi hali halisi ya udumishaji lugha ya Kimaragoli. Kwa hivyo, mtazamo tuliochukua kuhusiana na uchanganyaji msimbo uliegemea udumishaji wa Kimaragoli.

## 2.6 Mielekeo katika Udumishaji Lugha

Mielekeo imekuwa na fafanuzi mbalimbali kutegemea mtazamo wa mtaalamu. Kwa mujibu wa Allport (1935) mielekeo ni hali ya kiakili na kineva, iliyo na mpangilio wa kitajriba, na inayoshinikiza mwelekeo na kuathiri mwitiko wa mtu fulani kuhusiana na kitu fulani. Ianos (2014) anadai mielekeo aghalabu hujifunga kwa kitu, mtu au jambo fulani katika jamii na huvyazwa na watu wengine kadiri mtu anavyozidi kukumbana na kitu au jambo hilo katika jamii au mazingira yake. Tunavyotazama ulimwengu kunategemea jinsi akili na mawazo yetu yanavyoumba taswira kuhusu mambo tunayoyapenda au kuyachukia. Kupenda au kuchukia huku ndiko kunaibua mielekeo chanya na hasi.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa wawili, tunaweza kufasili mielekeo ya lugha kama dhana kuhusu lugha maalumu, iliyoko ndani ya akili na inayojieleza, moja kwa moja au kimafumbo, kupitia kwa michakato ya kisaguzi, imani, matamshi/vitamkwa, mawazo na maoni, kumbukumbu teule, hasira, ridhiko, ama mihemko mingineyo na pia

kupitia kwa vipengele vingine vya kitabia. Mielekeo lugha husababishwa na mambo mbalimbali kama anavyodai Mohochi (2005): wazazi, shule, mahusiano na watu wengine, vyombo vya habari, kuiga na kushawishiwa na kinga.

Katika mazingira ya wingilugha, mielekeo ni dhana muhimu sana (Onadipe-Shalom, 2014) kwani huamua ikiwa lugha itadumishwa, itakufa au wasemaji wake watahamia lugha nyingine katika mazingira ya wingilugha (Myers-Scotton, 2006). Bradely (2002) ana maoni sawa anaposema kwamba hakika, kigeu kikubwa katika udumishaji lugha ni mielekeo ya wasemaji wake. Wakati mwingine, wasemaji hawa wanaweza kuunda lugha mpya ikiwa wanakumbana na jamii nyingine inayosema lugha tofauti na yao na kuna haja ya kuwasiliana (Winford, 2003). Hata hivyo, kanuni tawala katika uundaji wa lugha ya kati ni kwamba, kila msemaji lazima ashikilie lugha yake kiuamilifu. Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusiana na suala la mielekeo katika ufundishaji na uamiliaji lugha, udumishaji, uhamaji, kufa na kupotea kwa lugha za binadamu (Mohochi, 2005; Kuncha na Bathula, 2004; Fink, 2005; Dyers, 2008; Aswegen, 2008; Perlin, 2009; Ianos, 2014; Onadipe-Shalom, 2014).

Utafiti wa Mohochi (2005) ulionyesha kwamba mielekeo ya lugha huathiri matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya kitaifa. Utafiti wake uliolenga kutambua ikiwa kulikuweko na tofauti ya kimielekeo baina ya wanafunzi wa Mkoa wa Nyanza na wa Pwani, na pia ikiwa mielekeo iliathiri matokeo ya Kiswahili, ulitambua kwamba mielekeo ya wanafunzi wote waliotafitiwa ilikuwa sawa kinyume na imani ya wengi kwamba Mkoani Nyanza, mielekeo kuhusu Kiswahili ni hasi. Aidha, Mohochi alihitimisha kwamba mielekeo haiathiri matokeo ya wanafunzi kwa sababu wapo wanafunzi walioanguka mtihani wa Kiswahili licha ya kuwa na mielekeo chanya. Utafiti wake ulitumia hojaji (iliyoboreshwa kutoka kwa Kitanga cha Likert) na mahojiano kukusanya data ya

kimsingi kutoka kwa watafitiwa 278 (walimu na wanafunzi). Licha ya umuhimu wa utafiti huu wa Mohochi (2005), kulikuweko na tofauti kubwa na utafiti huu: upimaji wa mielekeo ulilenga kibadala cha matokeo ya mitihani. Utafiti huu hata hivyo, ulilenga kuchunguza dhima ya mielekeo katika udumishaji wa lugha ya Kimaragoli. Hii ina maana kwamba maswali ya kimsingi katika hojaji ya Mohochi na ya utafiti huu yalitofautiana pakubwa. Kuwepo kwa maswali tofauti basi kulimaanisha kwamba tafiti hizi mbili zingekuwa na matokeo na mahitimisho tofauti.

Fink (2005) alichunguza mielekeo ya Wakenya kuhusiana na lugha mbalimbali zinazosemwa katika taifa la Kenya. Utafiti wake, uliojifunga katika jiji la Nairobi ulitambua kwamba vijana wa Kikenya wanaoishi Nairobi wanadhihirisha mielekeo hasi kuhusu lugha zao za kiasili huku wakipendelea msimbo wa Sheng'. Fink alilinganisha vijana na wazee na kutambua kuwa wazee walipendelea lugha asili na kujionea fahari kuliko vijana. Alihitimisha kwamba siku za baadaye, huenda lugha za kiasili zikawa katika hatari ya kutoweka kwa sababu ya miekeleo hasi inayokinza juhudi za udumishaji wake. Ingawa utafiti wa Fink ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu, hasa katika upimaji wa mielekeo, palikuwepo na tofauti kadhaa: kwanza, Fink aliegemea lugha zinazosemwa jijini Nairobi kwa ujumla na jinsi mielekeo inavyoziathiri huku utafiti huu ukitathmini Kimaragoli na namna kinavyoathiriwa na Kiluo. Pili, utafiti wake haukutathmini watoto chini ya miaka 18 na hivyo hauonyeshi taswira kamili ya lugha kijamii jijini Nairobi. Utafiti huu ulizingatia makundi matatu: watoto, vijana na wazee. Tatu, utafiti wake ulichunguza mielekeo peke yake ilhali utafiti huu ulishughulikia athari za mtagusano, mikakati ya udumishaji, na pia viwango vya umilisi miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli.

Utafiti wa Karanja (2012) ulioshughulikia mielekeo ya wasemaji wa lahaja za Kiamu na Kimvita ulionyesha kwamba lahaja hizi zimo katika hatari ya kumezwa na Kiswahili sanifu, Kiingereza na msimbo wa Sheng'. Kwa kutumia mbinu mseto kukusanya data ya kimielekeo, alitambua kwamba kizazi kichanga kilikuwa kinapendelea matumizi ya lugha hizi tatu kuliko lahaja zao kwa sababu mbalimbali. Waliona kuwa lahaja za Kimvita na Kiamu hazikuwa na umuhimu wowote ikilinganishwa na kizazi cha wazee kilichoshikilia matumizi ya lahaja hizi. Utafiti wake ulitumia vigezogeu vya elimu, ajira, urafiki, utamaduni na matumizi ya kijumla kutathmini mielekeo ya wasemaji wa lahaja hizi. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Karanja (2012) na utafiti huu ni kwamba tuliegemea lugha mbili tofauti (Kimaragoli na Kiluo) na pia tuliongeza vigezogeu zaidi kama vile fahari, redio, na ibada. Pamoja na hayo, utafiti wa Karanja ulichukua mkondo wa kimielekeo na kuhatarishwa kwa lugha ilhali utafiti huu uliangazia mielekeo na udumishaji lugha.

Odero (2013) alichunguza hali ya kiisimujamii ya Kielmolo na kutambua kwamba mielekeo ya ndani na nje (yaani Waelmolo wanavyojifikiria na wanavyodhaniwa na makabila mengine) ya wasemaji wa Kielmolo ilikuwa na mchango mkubwa katika kudidimia na kufa kwa Kielmolo. Kwa kutumia mbinu ya mahojiano, alitambua kwamba Waelmolo hawakuthamini lugha yao na wala hawakuionea fahari kiuamilifu. Hii ndiyo sababu kubwa ya wao kujifunza na kuhamia Kisamburu. Aidha, Wasamburu wanawaona kama watu maskini na wasio na uwezo wowote wa kiuchumi. Hii ndiyo sababu mojawapo inachangia Kielmolo kutoweka kwa kuwa wanajibidiisha kujua Kisamburu kama nyenzo ya kujikwamua kutoka kwa umaskini. Hata hivyo, japo Odero alichunguza mielekeo ndani na nje ya jamii, hakuwadadisi Wasamburu ili kufahamu jinsi walivyohisi kuhusu Waelmolo na lugha yao. Utafiti huu ulichunguza wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo kwa lengo la kutaka kujua mielekeo yao kuhusu Kimaragoli. Katika kukusanya

mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli, mtafiti alikuwa na kikundi lingani kilichofanyika Uriri na kilichochukua dakika 30. Wakati utafiti wa Odero (2013) unadhihirisha mielekeo hasi na kutoweka kwa Kielmolo, utafiti huu ulitambua kwamba Wamaragoli na Waluo wana mielekeo chanya kuhusu Kimaragoli na ndiposa lugha hii inazidi kujidumisha tangu miaka ya 1930/40. Mielekeo chanya imesababisha hata Waluo kujifundisha na kuzungumza Kimaragoli.

Kuncha na Bathula (2004) walitafitia dhima ya mielekeo katika udumishaji na uhamaji wa lugha miongoni mwa wahamiaji nchini New Zealand. Maswali yao yalilenga lugha mbili: Kiingereza na Kitelugu. Utafiti wao ulitambua kwamba mielekeo ya wazazi na watoto ilitofautiana pakubwa katika lugha hizi tatu. Wazazi waliekea kupenda kudumisha lugha ya Kitelugu huku watoto wao wakipenda Kiingereza au kuchanganya lugha zote. Hata hivyo, walibainisha kwamba wazazi ndio sababu kubwa ya watoto kujifunza na kutumia Kiingereza zaidi kwa sababu waliwahimiza kila mara kujua Kiingereza ili kuweza kuishi vyema kama wahamiaji.

Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa sababu ulionyesha haja ya kuchunguza mielekeo kwa kikundi mahsusi cha kiumri na wala sio kujumuisha jamiilugha yote. Hii ndiyo sababu utafiti huu uligawa hojaji katika makundi matatu kukidhi hali hii. Hata hivyo, licha ya mchango wake, utafiti wa Kuncha na Bathula (2004) ulitofautiana na huu kwa njia kadhaa: kwanza, eneo la kiutafiti lilikuwa New Zealand na hivyo, kwa mujibu wa watalaamu wa mtagusano lugha (Thomason, 2001; Weinrich, 1958) kila eneo la mtagusano lugha huwa na upekee unaoweza kuzalisha matokeo tofauti katika udumishaji au uhamaji lugha. Hii ndiyo sababu utafiti wa wataalamu hawa unaonyesha kwamba katika miaka miwili ya uhamiaji nchini New Zealand, kuliweko na taashira za kuhamia lugha ya Kiingereza miongoni mwa kizazi

kichanga. Utafiti huu ulionyesha kwamba kwa zaidi ya miaka 80, wasemaji wa Kimaragoli wanazidi kudumisha lugha yao licha ya wao kujifunza Kiluo na kutagusana nacho kwa miaka hii yote. Kwa hiyo, eneo na hali ya mtagusano huzalisha matokeo tofauti tofauti baina ya lugha zinazotagusana.

Pili, Kuncha na Bathula walitumia mbinu za mahojiano na hojaji kukusanya data miongoni mwa watoto wa miaka 11 na zaidi na pia kina mama zao. Hii ina maana kwamba matokeo yao hayakuonyesha taswira kamili kuhusu lugha ya Kitelugu kwa kuwa wanaume (hasa kina baba) hawakuhusishwa. Huenda hii ndiyo sababu utafiti wao ulihitimisha kwamba ndani ya miaka miwili, wasemaji wa Telugu walikuwa wameanza kuhamia Kiingereza baada ya kuhamia New Zealand. Ili kupata matokeo wakilishi, utafiti huu uliangazia makundi yote ya kijamii: kijinsia na kiumri.

Katika utafiti uliofanyika nchini Afrika Kusini, Dyers (2008) alitambua kwamba wasemaji wa Kiafrikana walidhihirisha mielekeo miwili tofauti kuhusu lugha ya Kiafrikana na Kiingereza na pia lugha za wachache zinazosemwa Western Cape. Utafiti wake uliolenga wanafunzi wa darasa la nane (K8) na tisa (K9) ulitumia mbinu za maandishi kwa wanafunzi lengwa, mahojiano katika nyuga za michezo na matumizi ya makundi lingani ya mjadala baina ya mwaka wa 2004-2006 kukusanya data. Kutokana na utafiti wake, mambo matatu yaliibuka:

a. Mielekeo ya lugha inaweza kuathiri namna tunavyoorodhesha lugha zetu akilini na maishani.
b. Mielekeo inaweza kuathiri namna tunavyojihisi kuhusu lugha zetu.
c. Mielekeo inaathiri mitagusano na tabia za wasemaji wa lugha moja kuelekea wasemaji wa lugha nyingine na lugha zao katika mazingira mamoja ya lugha.

Matokeo yanaonyesha kwamba wanafunzi wa K8 walielekea kukubali kwamba Kiingereza kilikuwa muhimu kwa sababu kingechangia wao kupata kazi baada ya masomo lakini walipenda Kiafrikana kwa kuwa ni lugha yao; ni nzuri kuitamka; na pia ni rahisi kuielewa. Wanafunzi wa K9 walielekea kupenda Kiingereza kwa sababu ni lugha inayoweza kuwafungulia milango ya kazi siku za baadaye mbali na kuwatangamanisha na wasemaji wa lugha nyinginezo nje ya Western Cape. Wanafunzi hawa walikuwa na mengi ya kuzungumzia Kiingereza kuliko Kiafrikana. Utafiti huu unaonyesha kwamba mielekeo ya wasemaji haiwezi kuepukika wakati wa kutafiti dhana ya udumishaji lugha kwa kuwa ni kizio muhimu na cha kimsingi kwa kuwa kinachochea wasemaji kugura au kudumisha lugha zao.

Utafiti wa Dyers ulitofautiana na utafiti huu kwa njia kadhaa. Kwanza, licha ya kwamba utafiti huu ulifanyika barani Afrika, haukulenga lugha asilia barani. Pili, utafiti wa Diers (2008) uliwalenga tu wanafunzi wa shule za msingi na hivyo kupunguza mawanda ya watafitiwa. Tatu, utafiti huu wa Dyers (2008) ulichukua miaka miwili ambapo kulikuweko na muda wa kutosha kufuatilia na kurekodi maendeleo au mabadiliko ya mitazamo miongoni mwa wanafunzi. Nne, maoni ya wanafunzi yalihusu lugha na uchumi au ajira na hivyo huenda hawakutilia maanani wazo la kudumisha lugha kwa ajili ya utambulisho na fahari. Utafiti huu ulilenga kujaza mapengo haya kwa kuongeza makundi ya watafitiwa hivi kwamba yalijumuisha wazee, watoto na vijana. Pamoja na hayo, utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha asilia na jinsi ambavyo mielekeo ya wasemaji wake na Waluo ilivyochangia udumishaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri.

Perlin (2009) alipotafitia mielekeo lugha ya wasemaji wa T’rung (Durong) ya China Kusini alitambua kwamba wazee na vijana walikuwa na mielekeo iliyotofautiana. Kundi

moja (vijana) lilidhihirisha kwamba lugha hii ilikuwa na maarubu katika maisha ya Watirung wote ingawa msambao wake ulizidi kufifia kila uchao. Kundi la pili (wazee) liliomboleza namna ambavyo Kit'rung kilikuwa kinakufa na kupoteza uamilifu miongoni mwao. Waliona kwamba Kit'rung hakiwezi tena kutumika katika maisha yao ya kila siku kwa sababu Kichina kilikuwa na mvuto mkubwa mbali na tija za kiuchumi na kijamii. Utafiti wake unaonyesha kwamba wanawake na watafitiwa walio na umri wa zaidi ya miaka 50 walidhihirisha hisia mseto kuhusu Kit'rung huku wakitilia nguvu Kilisu, lingua franca ya maeneo ya Kusini mwa China.

Vijana kwa upande wao walidhihirisha mshawasha wa kutambulishwa na lugha hii licha ya hamaniko kuhusu mustakabali wake na pia maeneo ya matumizi yake. Perlin (2009) alihoji watafitiwa 48 kwa muda wa mwezi mmoja. Mtafiti alizingatia jinsia na umri- hasa vijana na waliozidi umri wa miaka 50. Hata hivyo, licha ya matokeo haya, utafiti wake ulitumia tu mbinu moja ya kukusanya data: mahojiano. Utafiti huu ulitumia hojaji, makundi lengwa, mahojiano na uchunzaji kama njia ya kukusanya data inayoweza kutegemewa. Mbinu hizi zilizalisha data nyingi kuliko ya Perlin (2009).

## 2.7 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, mambo yafuatayo ndiyo yalikuwa ya kimsingi katika sura hii. Kwanza, udumishaji wa lugha ni jambo linalohitaji mikakati maalumu kuweza kufanikiwa. Mikakati hii inabuniwa na wanajamii wenyewe na kupewa uamilifu kutegemea jinsi wanavyoionea fahari lugha yao. Ukosefu wa mikakati ndio hatari kubwa inayokumba lugha zenye satua ndogo ya kujidumisha na ndiyo sababu zinatoweka katika ramani ya lugha ulimwenguni. Inaonekana kwamba mikakati ya kuzungumza lugha nyumbani, kutumia wazee na kufundishana ndiyo yenye tija kubwa katika kudumisha lugha. Pili, umilisi na utendaji hutofautiana kutoka kundi moja la kiumri hadi kwa lingine. Wazee

wanaonekana kuwa na umilisi mkubwa wa lugha ikilinganishwa na vijana na watoto. Hivyo, iwapo lugha itajidumisha, lazima wazee hawa waweze kurithisha vijana na watoto maarifa ya lugha. Kadiri mtu anavyojifunza na kutumia lugha, ndivyo umilisi wake unavyoimarika.

Tatu, mtagusano lugha ni lazima uzue athari ya kiisimu na kiisimujamii. Watafiti wote waliorejelewa wanakubaliana kwamba lugha zinaweza kuathiriana kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia na kileksimu. Pia athari hizi zinaweza kuzalisha uhamishaji msimbo na uchanganyaji msimbo. Wengi wanakubaliana kwamba tokeo la kifonolojia japo ni nadra kutokea kwa lugha zilizo na mnasaba tofauti, uwezekano wa kutokea upo. Aidha, baadhi yao wanakubali kwamba lugha zinapotagusana kwa kipindi kirefu, ukopaji hutokea na hivyo kuathiri idadi ya leksimu ngeni katika lugha pokezi. Nne, mwelekeo ni kipengele muhimu katika udumishaji wa lugha. Wazee wanadhihirisha mwelekeo chanya ikilinganishwa na vijana ambao msukumo wa kiuchumi na kutozingatia utamaduni kunawafanya wao kuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha yao na ndio sababu umilisi wao ni wa kiwango cha chini.

# SURA YA TATU

## MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichanganua kihakiki maandishi mbalimbali kuhusu dhana ya udumishaji lugha, mikakati ya udumishaji lugha, umilisi lugha, athari za mtagusano lugha na mielekeo ya lugha. Sura hii inafafanua jinsi utafiti huu ulitendeka. Sura hii inajumuisha muundo wa utafiti, idadi lengwa na mikakati ya kupata sampuli, vifaa vya kukusanya data, udhabiti na uaminikaji wa vifaa, taratibu za kukusanya data, mazingatio ya maadili, na taratibu za kuchanganua data kama ilivyojadiliwa katika sehemu za 3.1 hadi 3.10.

### 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia Muundo Elezi Uauzi na Muundo wa Uchanganuzi Linganishi. Utafiti wa uauzi ulitumika kuchunguza na kutathmini maoni na mapendeleo katika muktadha maalumu wa utafiti. Muundo huu unaaminiwa kuwa mzuri zaidi wa kupima mielekeo, imani na masuala mbalimbali kuhusu mtu binafsi katika muktadha ulio halisi. Mtafiti anaweza kutumia mitihani, mizani ya mielekeo au dodosi (Leeds, 1993). Kulingana na Kothari (2004) muundo elezi wa Uauzi hutumika wakati ambapo mtafiti anachunguza idadi kubwa ya watafitiwa na angependa kupata sampuli sadifu inayoweza kuwakilisha jumuiya. Nwogu (2006) ana maoni kwamba muundo huu huzingatia tu watafitiwa wachache ambao wanaweza kuwa na sifa zinazoelekea kufanana na data inayozalishwa inakuwa wakilishi. Katika utafiti huu, muundo huu ulitumika kuteua watafitiwa 390 na kupata maoni yao kuhusu udumishaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri. Kwa upande mwingine, muundo wa Uchanganuzi Linganishi ulitumika kuchanganua kwa kulinganisha vigeu mbalimbali ambavyo vinaingiliana na kuathiriana

katika utafiti. Muundo huu ulimsaidia mtafiti kukusanya na kuelezea data ambayo inaweza kutumika kuelezea mlingano na tofauti zilizopo (Kothari, 2004 ; Kombo na Tromp, 2007). Hapa data iliyohusishwa ni ile ya mielekeo na umilisi wa makundi mbalimbali ya kiumri miongoni mwa watafitiwa.

Miundo hii iliteuliwa kwa sababu kadhaa. Kwanza, ilimsaidia mtafiti kupata ukweli kuhusu mielekeo na maoni ya wasemaji wa lugha za Kimaragoli na Kiluo kuhusu udumishaji lugha. Pili, ilimsaidia mtafiti kukusanya data iliyoweza kueleza hali halisi ya wakati huo bila kutoa makisio kuhusu hali ilivyo (Cohen, Manion na Morrizon, 2000). Tatu, uauzi huzalisha data ya haraka, inayotegemewa na kwa njia nyepesi kuhusu jumuiya tafitiwa (Oso na Onen, 2006). Uauzi huwa bora pale ambapo hakuna data iliyokusanywa hapo awali, na katika muktadha wa utafiti huu, hakuna data iliyokusanywa kuhusu mikakati ya udumishaji lugha ya Kimaragoli na pia athari za Kiluo katika lugha ya Kimaragoli. Vilevile, kabla ya utafiti huu, hakukuwepo na data yoyote kuhusu umilisi wa lugha ya Kimaragoli Uriri. Baada ya kukusanya data hii, kulikuwa na haja ya kuonyesha jinsi vigeu kadhaa vinaathiriana. Kwa mfano, tofauti za kiumilisi zilizopo baina ya wazee na vijana au watoto ambao mzazi wao mmoja ni Mmaragoli na mwingine Mjaluo na kadhalika. Ulinganisho ulimsaidia mtafiti kutoa picha halisi ya udumishaji lugha katika eneobunge la Uriri.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eneobunge la Uriri, Kaunti ya Migori, Kenya. Eneobunge la Uriri linapatikana Kusini mwa Nyanza na limezungukwa na maeneobunge ya Rongo, Awendo, Migori, Nyatike, Kuria Magharibi, Kuria Mashariki, Suna Magharibi na Suna Mashariki. Ukubwa wake ni takriban kilomita mraba 381 na lina watu wapatao 115, 751 katika jumla ya wadi 5 ambazo ni Kanyamkago Kusini, Kanyamkago Kaskazini,

Kanyamkago Mashariki, Kanyamkago Magharibi na Kanyamkago ya Kati (KBS, 2009; http://softkenya.com/constituency/uriri-constituency/). Eneobunge la Uriri na wadi zake mbalimbali zimewekwa kama Kiambatisho S uk. 280.

Eneobunge hili lina jamii mbili kuu : Waluo na Abaluhya. Wamaragoli ni mojawapo ya kabila la Waluhya. Hata hivyo, katika eneo hili la Uriri, Wamaragoli ndio wengi miongoni mwa Waluhya. Kadirio la chini linadhaniwa kuwa ni watu wasiopungua 30,000. Eneo hili liliteuliwa kwa sababu linadhihirisha mtagusano wa lugha hizi mbili : Kimaragoli na Kiluo- ambao umedumu kwa zaidi ya miongo minane na ulihitaji kufanyiwa utafiti kutambua namna lugha ya Kimaragoli imezidi kujidumisha licha ya kuzungukwa na Kiluo, lugha iliyo na msambao mpana na kani kubwa.

### 3.4 Idadi Lengwa

Bryman (2012) anafasili idadi lengwa ya utafiti kama watu wote, vitu vyote, au matukio yote ambayo mtafiti angependa kujumuisha katika matukio ya utafiti wake. Kombo na Tromp (2007) wanadai kwamba ni watu au vitu vyote vilivyo na nduni maalumu inayoweza kutafitika. Akuezuilo na Agu (2003) na Arubayi (2003) wanadai kwamba idadi lengwa katika utafiti wa kitakwimu hutumika kwa maana maalumu ambayo hailengi watu tu, bali pia taasisi, matukio, wanyama, idara na vitu vilivyo na nduni zinazolandana.

Katika utafiti huu, Idadi lengwa imegawika kuwili: Idadi ya watu na pia idadi ya maeneo. Eneobunge la Uriri lina watu 115, 751 (KBS, 2009). Wamaragoli ni takribani 10,000-30,000 (http://softkenya.com/constituency/uriri-constituency/). Kwa hivyo, katika utafiti huu, idadi lengwa ni watu wapatao 20,000. Idadi hii ni wastani ya watu 10,000-30,000. Katika Idadi ya maeneo, utafiti ulizingatia Kata ndogo 7 za eneobunge zima la Uriri.

Aidha, Waluo wachache (10) walihusishwa kwa lengo la kupata mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli.

### 3.5 Idadi ya Sampuli na Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya utafiti huu ilikuwa watafitiwa 390. Idadi hii ilisambazwa katika Kata ndogo za eneobunge la Uriri. Ilihusisha Wadi 5 na Kata Ndogo 10 kutoka kwa jumla ya Kata Ndogo 19. Wadi zote tano ziliteuliwa kwa ajili ya kupata msambao halisi wa wasemaji wa Kimaragoli. Kata ndogo 2 katika kila wadi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa sampuli kimfumo. Mbinu hii ilikuwa nzuri ya kupata data ambayo inawakilisha kila kizio ambacho kinatafitiwa (Kothari, 2004). Kothari anapendekeza kwamba mtafiti anaweza kuchagua nambari fulani maalumu ya kiwakilishi katika orodha ya idadi. Katika jedwali 3.1, mtafiti alichagua Kata ndogo ya kwanza na pili. Hii ilihakikisha kwamba hakuna mwegemeo wowote katika sampuli wakilishi. Mtafiti alichagua sampuli katika eneobunge zima na idadi hii ilichukuliwa na mtafiti kuwa ni wakilishi. Kata ndogo ya Kamsaki ndiyo ilitumika katika utafiti awali, hivyo si sehemu ya matokeo ya utafiti huu. Kiunzi cha usampulishaji kimeonyeshwa katika jedwali 3.1. Mpangilio katika jedwali hili umetokana na IEBC (2013) na wala si wa mtafiti.

**Jedwali 3.1: Kiunzi cha Usampulishaji wa Kata Ndogo katika Wadi Maalumu**

| WADI | KATA ndogo | KATA NDOGO TEULE |
|---|---|---|
| **KANYAMKAGO MAGHARIBI** | 1. Kajulu II<br>2. Kajulu I<br>3. Kajulu | 1. Kajulu II<br>2. Kajulu I |
| **KANYAMKAGO KASKAZINI** | 1. Komenya Masoge<br>2. Katieno II<br>3. Kamgudho I<br>4. Katieno I<br>5. Kamgudho II | 1. Komenya Masoge<br>2. Katieno II |
| **KANYAMKAGO YA KATI** | 1. Kawere II<br>2. Kawere Rateng Mashariki<br>3. Kawere Rateng ya Magharibi<br>4. Nyaobe<br>5. Kawere Rateng ya Kati | 1. Kawere II<br>2. Kawere Rateng Mashariki |
| **KANYAMKAGO KUSINI** | 1. Bware<br>2. Lwala<br>3. Kamsaki<br>4. Got Uriri | 1. Bware<br>2. Lwala |
| **KANYAMKAGO MASHARIKI** | 1. Thim Jope<br>2. Arambe | 1. Thim Jope<br>2. Arambe |

(**Chanzo: IEBC, 2013)**

Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni watu 390 ambayo ilipatikana kwa kutumia fomula ya ukokotozi ya Yamane (1967) ya kupata sampuli wakilishi. Fomula ya Yamane inadhania kwamba msambao wa kawaida wa uwakilishi huwa ni 95% na P=5%. Wasemaji wa Kimaragoli wanaaminika kuwa wamesambaa sawasawa kwa kuzingatia uzungumzaji wa Kimaragoli na pia vizingiti vinavyotinga au kuchapuza udumishaji wa lugha yao. Fomula hii kwa hiyo inaaminika kuzalisha sampuli sadifu na wakilishi (Yamane, 1967). Fomula hii ni kama ifuatavyo:

$$n = \frac{N}{1 + N \times (e)^2}$$

Ambapo:

n= sampuli wakilishi

N= idadi jumuiya

e= taksiri ya usampulishaji inayokubalika (taksiri ya 5% = 0.05)

Mchakato wa ukokotoaji sampuli teule umewasilishwa katika sehemu inayofuata:

$$(n) = \frac{20,000}{1 + 20,000 \times (0.05)^2}$$

$$n = \frac{20,000}{1 + 20,000 \text{ x } (0.0025)}$$

$$n = \frac{20,000}{1 + 50}$$

$$n = \frac{20,000}{51}$$

$$n = 392.2$$

Kwa kuwa mtafiti alilenga kuwasilisha idadi sawa ya hojaji kwa kila Kata ndogo, idadi ya 390 badala ya 392 ilichukuliwa na hivyo kila Kata ndogo ikawa na hojaji 39.

**3.6 Mbinu na Vifaa vya Utafiti**

Mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya data ni mahojiano, vikundi lengani vya mijadala, uchunzaji, na pia hojaji. Mbinu hizi zilifanikishwa kwa vifaa mbalimbali kama vile hojaji, ratiba ya uchunzaji, na mwongozo wa mahojiano na mwongozo wa makundi ya mijadala. Hojaji ndicho kilikuwa kifaa cha muhimu na cha kimsingi katika kupata data ya kiwingiidadi. Ratiba ya uchunzaji na miongozo ya mahojiano na mijadala zilitumika kukusanya data ya kithamano. Vilevile, kulikuweko na vifaa vingine kama vile vinasa sauti, shajara, kalamu, simu, na kamera ambavyo vilimsaidia mtafiti kukusanya data kwa kutumia mbinu tulizotaja. Majukumu ya vifaa hivi yameonyeshwa katika jedwali 3.2. Mbinu za utafiti zimeelezwa baada ya jedwali.

**Jedwali 3.2: Majukumu ya vifaa vya utafiti**

| Na. | Kifaa | Jukumu |
|---|---|---|
| **1.** | Kinasa sauti/simu | - Kunasa mijadala/majibu katika VLM na mahojiano |
| **2.** | Shajara | - Kuandika tarehe za mahojiano<br>- Kunakili majibu ya mijadala ya VLM |
| **3.** | Kalamu | - Kuandika katika shajara |
| **4.** | Kamera | - Kupiga picha za baadhi ya washiriki<br>- Kurekodi baadhi ya majibu ya washiriki wa mijadala na mahojiano. |

**(Chanzo: Mtafiti)**

### 3.6.1 Mwongozo wa Mahojiano

Kifaa hiki kilikuwa na maswali wazi na kilitumika kukusanya data ya kithamano katika mbinu ya mahojiano. Miongozo hii ilikuwa na vipengele mbalimbali vilivyolenga kupata data kuhusu mikakati ya udumishaji lugha ya Kimaragoli; hisia kuhusu uzungumzaji wa Kimaragoli. Waliohojiwa kwa kutumia kifaa hiki walikuwa wazee wanaozungumza Kimaragoli, kundi la mjadala la wazawa wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli. Katika pendekezo la utafiti, mtafiti alikuwa ameratibu kuhoji viongozi wa Kata na wakuu wa shule za msingi ila walengwa hawa wakaondolewa baada ya utafiti awali kufanywa. Utafiti wa awali ulionyesha kwamba makundi haya ya wahojiwa hayangechangia data mpya au ya kipekee kwa sababu mambo mengi ambayo mtafti alilenga yalikusanywa kwa hojaji, mahojiano, uchunzaji na kundi la mjadala. Aidha, mtafiti angekuwa na data nyingi ambayo ingemwia vigumu kuchanganua na kuzingatia katika uandishi wa tasnifu hii. Hivyo, viambatisho vyake viliondolewa. Maswali kwenye miongozo iliyotumiwa yalilenga kukusanya data kuhusu historia ya Wamaragoli, uhalisia wa umilisi na matumizi ya Kimaragoli maeneo ya Uriri miongoni mwa makundi matatu ya kiumri na mielekeo ya watafitiwa kuhusu lugha ya Kimaragoli katika maeneo teule ya Uriri. Miongozo hii ni Kiambatisho A, uk. 243, C, uk. 248 na F, uk.255.

### 3.6.2 Mwongozo wa Mjadala wa Kundi Lengwa

Kikundi cha Mjadala kilihusisha maswali wazi yaliyolenga kukusanya data kuhusu mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli. Kikundi hiki kwa mapendekezo ya Kruegger (1988) kilikuwa na watu saba. Mtafiti aliteua watu saba kwa sababu zifuatazo: kwanza, kwa kuwa mtafiti alitumia vijiji saba katika wadi nne, ilikuwa sadifu kuteua mwakilishi mmoja kutoka kwa kila kijiji. Pili, mpangilio huu ulimsaidia mtafiti kupunguza gharama na muda wa kuandaa makundi mengi ya washiriki na tatu, kwa kuwa habari zilizokuwa zinazalishwa ni zilezile, mtafiti aliepuka uradidi wa data nyingi ambayo ingezua tatizo la kiuchanganuzi. Idadi hii ilikuwa ya kutosha ili kumshirikisha kila mtu katika kikundi. Mwongozo huu umewekwa kama Kiambatisho H, uk.259.

### 3.6.3 Mwongozo wa Uchunzaji

Uchunzaji ni mbinu ambayo humfanya mtafiti kuwa sehemu ya watafitiwa na kushiriki katika baadhi ya shughuli zao. Kila anapopata habari maalumu za utafiti wake, ananakili kwa ajili ya uchanganuzi wa baadaye. Ingawa Patton (1990) anapendekeza aina mbalimbali za uchunzaji, utafiti huu ulipendelea mtafiti kuwa sehemu ya watafitiwa katika mikutano yao ya kitamaduni, kisiasa, makanisa na hata soko. Kutokana na utafiti wa awali, mtafiti aliongeza maeneo ya uchunzaji kutoka matatu ambayo yalikuwa ni kanisa, mikutano ya baraza na soko hadi maeneo sita ambayo ni kanisani, nyumbani, shambani, sokoni, sherehe/mazishi na michezoni. Mwongozo wa Uchunzaji umewekwa kama Kiambatisho J, uk. 265.

### 3.6.4 Hojaji

Hojaji ilitumiwa kukusanya data kuhusu mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli, ruwaza za matumizi lugha katika miktadha mbalimbali, mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo, na pia umilisi lugha wa Wamaragoli. Hojaji hii ilikuwa na sehemu tatu. Sehemu

ya kwanza ilikuwa na habari zinazoeleza lengo la utafiti, rai ya kujaza hojaji na ahadi ya usiri wa data. Sehemu ya pili ilikuwa na habari za kitawasifu (jinsia, umri na ndoa). Sehemu ya tatu ilikuwa na masuali kuhusu lugha inayotumika nyumbani, nje ya nyumbani, miktadha anuwai ya kijamii, na mieleko ya lugha. Hojaji ndicho kilikuwa kifaa cha kimsingi kabisa katika ukusanyaji wa data ya utafiti huu.

Kutokana na utafiti wa awali na mikutano na wasimamizi, marekebisho yalifanyiwa kifaa hiki. Kwanza, hojaji iliyowasilishwa katika utafiti awali ilizua matatizo ya ujazaji habari kwa sababu ilijumuisha habari zote zilizohusu wazee na makamo, vijana na watoto. Hii ilikuwa changamoto kwa sababu baadhi ya familia hazikuwa na watoto, au vijana, hivyo haikujazwa. Kwa ushauri wa wasimamizi, mtafiti aliengua habari za wazee, watoto na vijana na kuunda hojaji tatu zilizoweza kutathmini habari maalumu za wazee na makamo, vijana na watoto. Aidha, mtafiti aliongeza maswali ya kipekee ambayo yalilenga kutathmini habari maalumu kuhusu umilisi wa lugha kutegemea kundi la kiumri.

Katika hojaji ya wazee na makamo, mtafiti aliongeza habari kama vile lugha inayozungumzwa sana na wazee; athari ya Kiluo kwa Kimaragoli; matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali; ulinganisho wa matumizi ya Kimaragoli kati ya wazee na vijana; tathmini ya kiwango cha umilisi; na miktadha ya uchanganyaji na uhamishaji ndimi. Vipengele hivi viliongezwa ili kuleta msambao bora wa maswali mintarafu madhumuni na maswali ya utafiti. Katika sehemu iliyotathmini mielekeo ya Wamaragoli kuhusu lugha yao, mtafiti alidondosha kauli ambazo hazikuwa na umuhimu katika utafiti licha ya kwamba zilikuweko katika utafiti wa awali. Jumla ya kauli 6 ziliondolewa kwa sababu zifuatazo: kwanza, kuna baadhi ya kauli ambazo zingezua data iliyofanana na hivyo ili kupunguza uradidi wa data, kauli hizo ziliondolewa. Pili, baadhi ya kauli

zililenga vijana au watoto. Kwa kuwa mtafiti aliengua habari za watoto na vijana, haikuwepo haja yoyote ya kusalisha habari hizi kwenye hojaji ya wazee. Kwa hiyo habari zilizosalia kwenye hojaji hii zililenga wazee na makamo peke yake.

Katika hojaji ya vijana habari pia zilichujwa ili kukusanya data iliyolenga vijana waliokuwa kati ya umri wa miaka 18-35. Habari zilizoongezwa ni lugha inayozungumzwa sana na vijana; athari ya Kiluo kwa Kimaragoli miongoni mwa vijana; matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali; ulinganisho wa matumizi ya Kimaragoli kati ya vijana na wazee; tathmini ya kiwango cha umilisi; na miktadha ya uchanganyaji na uhamishaji ndimi. Kauli za kutathmini mielekeo ya vijana kuhusu Kimaragoli zilikuwa 22.

Hojaji ya watoto wa miaka 12-17 iliundwa upya kwa sababu haikuwepo katika utafiti wa awali ila kulikuweko na maswali saba peke yake yaliyotathmini Kimaragoli miongoni mwa watoto. Habari za kimsingi katika hojaji hii zililandana na za wazee na makamo na vijana. Hata hivyo, sehemu iliyolenga kukusanya data kuhusu mielekeo ilikuwa na kauli 18 peke yake. Hii ni kwa sababu haikuhusisha masuala ya ndoa, ufundishaji usorasmi wa Kimaragoli kwa vizazi vya baadaye na masuala ya ajira.

Kwa kuwa mtafiti alikuwa anatafitia suala la udumishaji wa Kimaragoli miongoni mwa Wamaragoli katika eneobunge la Uriri, ilikuwa muhimu kuhakikisha kwamba habari zilizokuwa katika Hojaji hizi tatu haikutofautiana mno. Hivyo, mtafiti alihakikisha kwamba habari nyingi zilifanana katika Hojaji hizi zote tatu. Hojaji hizi ni Viambatisho K (uk. 266), L (uk. 269) na M (uk.272).

### 3.7 Uaminikaji na Udhabiti wa Vifaa vya Utafiti

Sehemu hii inajadili kwa ufupi jinsi vifaa vya utafti viliundwa, kurekebishwa na kutumiwa katika upimaji awali kwa lengo la kuhakikisha kwamba vinazalisha matokeo ya kutegemewa.

#### 3.7.1 Uaminikaji wa Vifaa vya Utafiti

Uaminikaji ni uwezo wa matokeo ya vipimo vya mjarabu kutegemewa (Kombo na Tromp, 2007). Ili kubainisha uaminikaji wa vifaa, utafiti wa majaribio ulifanywa katika kata ya Kamsaki na jumla ya watafitiwa awali walikuwa watu 39. Watafitiwa hawa wa kimajaribio ni asilimia 10% ya idadi ambayo haikujumuishwa kama sehemu ya sampuli. Tulitumia maoni ya Nieswiadomy (2002) aliyependekeza upataji 10% ya watafitiwa ambao watatokana na idadi jumla ya utafiti. Watafitiwa awali ambao ni 39 walitokana na asilimia kumi ya 390. Watafitiwa hawa walipewa hojaji kwa lengo la kujaza na baada ya siku mbili, mtafiti alizikusanya na kuzichanganua. Mtafiti alilenga kuangalia namna watafitiwa walijibu maswali yote, utata uliotokea katika kujibu maswali hayo na namna majibu ya kila mtafitiwa yalifanana au kutofautiana. Kwa kuwa majibu mengi ya watafitiwa yalifanana katika hojaji zote 39, basi ilikuwa wazi kwamba iwapo watafitiwa wangepewa tena baadaye, wangezalisha majibu yale yale kwa maswali yote.

#### 3.7.2 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti

Uthabiti ni uwezo wa kipimo kuweza kupima kile kinachostahili kupimwa (Kombo na Tromp, 2007). Kifaa cha utafiti ni kubalifu ikiwa maudhui yake ni faafu na yanawafiki madhumuni ya utafiti. Upimaji wa uthabiti huu ulihakikisha kwamba muundo na maudhui ya vifaa hivi yanakubalika. Mapendekezo na ushauri uliotolewa na wasimamizi wa mtafiti Idarani kuhusu uimarishaji wa vifaa vya utafiti baada ya utafiti awali ulitumika kuimarisha maudhui na utendakazi wa vifaa hivi. Aidha, hii ilisaidia

kubainisha usahihi na utoshelevu wa vipengele vya utafiti. Kutokana na utafiti wa awali, ukokotoaji wa vipimo vya uaminikaji na uthabiti ulikuwa wa asilimia 80% na hii ilimaanisha kwamba vifaa hivi vilikuwa na uwezo wa kukusanya data inayotegemewa.

### 3.8 Ukusanyaji wa Data ya Utafiti

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa njia mbalimbali. Njia hizi zimejadiliwa katika vijisehemu vinavyofuata.

#### 3.8.1 Ukusanyaji data kwa hojaji

Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji 273 zilizowasilishwa kwa watafitiwa ambao walijumuisha wazee na makamo, vijana na watoto katika Kata ndogo 7 zilizoteuliwa kutafitiwa. Idadi ya watafitiwa ilipungua kwa sababu Kata ndogo tatu zilizoteuliwa na mtafiti hazikuwa na Wamaragoli. Kata ndogo hizi zilikuwa Komenya Masoge, Katieno II na Kajulu I. Hojaji hizi zilisambazwa kwa kutumia mbinu ya kimaksudi. Hii ina maana kwamba mtafiti na wasaidizi wake waliteua tu nyumba ambazo zilikuwa na wazee na makamo, vijana na watoto kati ya umri wa 12-17. Hivyo, ilikuwa lazima kuuliza kwa kila nyumba au boma ikiwa kulikuweko na wazee au makamo, vijana na watoto kabla ya kuacha hojaji. Hojaji hizi zilikuwa katika makundi matatu: 13 za wazee na makamo; 13 za vijana; na 13 za watoto. Watafiti wasaidizi walipewa hojaji 39 kila mmoja na kuzigawa kwa maeneo ambayo kila mmoja alikuwa amechagua kuwakilisha. Wasaidizi hawa walizigawa na kisha kuzichukua baada ya juma moja. Hata hivyo, kwa kuwa baadhi ya watafitiwa walikuwa hawajui jinsi ya kujaza hojaji, watafiti wasaidizi waliketi na kuwaongoza kujaza na kisha kuzichukua baada ya kukamilisha. Hii ni kwa sababu wasaidizi wote walikuwa wamepewa mafunzo kabla ya kuanza kukusanya data. Kila nyumba au boma lilipewa hojaji moja kwa kila kundi la kiumri. Jumla ya hojaji 273 zilisambazwa katika Kata ndogo saba teule za eneobunge la Uriri. Baada ya

kusambazwa, na kujazwa hojaji zote 273 zilichukuliwa kutoka kwa watafitiwa na kisha mtafiti akazichukua kutoka kwa watafiti wasaidizi aliokuwa ameteua kumsaidia.

### 3.8.2 Ukusanyaji Data kwa Uchunzaji

Mbinu hii ilihusisha uchunzaji shirikishi na uchunzaji usoshirikishi. Katika baadhi ya miktadha hasa ya mashambani, mtafiti na msaidizi wake hawakujihusisha katika kazi za shamba ila walisimama au kutembea katika njia ambazo walengwa walikuwa wakifanya kazi mashambani. Mtafiti na msaidizi wake walitumia mwongozo wa uchunzaji.

Mtafiti na msaidizi wake walichunguza matumizi ya Kimaragoli vijijini Bware na Lwala mashambani, sokoni na nyumbani. Kwa kutumia mwongozo wa uchunzaji, mtafiti na msaidizi wake walikuwa wanaweka alama ya sahihi kwenye kisanduku maalumu. Kwa mfano, iwapo Kimaragoli kilikuwa kinatumika sana, alama iliwekwa kwa kisanduku cha 'sana'. Iwapo uchanganyaji ndimi ulishuhudiwa, alama iliwekwa kwa kisanduku cha 'uchanganyaji ndimi'.

Baadaye, mtafiti na msaidizi wake waligawana maeneo ya uchunzaji. Mtafiti alichunguza maeneo ya Thim Jope na Arambe kwa kuwa yanapakana huku mtafiti msaidizi akichunguza maeneo ya Kajulu I na Kajulu II. Ripoti yake ilionyesha kwamba Wamaragoli walikuwepo katika Kajulu II peke yake. Katika eneo la Kajulu II, alichunguza Wamaragoli wakiwa mashambani, sokoni, nyumbani. Mtafiti msaidizi alisikiliza Wamaragoli wakizungumza nyumbani na kuweka alama kwa kisanduku maalumu. Kisha akatembea sehemu za mashambani, kusilikiza na kuweka alama ya sahihi kwenye visanduku mahsusi. Ukusanyaji wa data hii ulifanywa kwa njia ya uchunzaji usoshiriki ili watafitiwa wasijue walikuwa wanachunguzwa. Mtafiti kwa upande wake alitembea mashambani na kusikiliza matumizi ya Kimaragoli. Ikiwa

sehemu moja walizungumza Kimaragoli sana shambani, aliweka alama sahihi kwenye mwongozo wake. Iwapo walikuwa wanachanganya ndimi, vilevile aliweka alama kwenye kisanduku cha ‘uchanganyaji ndimi’. Masoko ambayo yalichunguzwa yalikuwa ni Stella, Bware na Nyasoko. Masoko haya yaliteuliwa kinasibu. Ukusanyaji wa data kwa njia hii ulitumia uchunzaji usoshiriki na mtafiti na msaidizi wake walikuwa wanasimama eneo maalumu ambalo wangeweza kukusanya data bila watafitiwa kufahamu wanachunguzwa.

Mtafiti msaidizi alihudhuria ubatizaji na utoaji wa majina kwa mtoto ambaye wazazi wake ni washiriki wa Kanisa la Jeshi la Wokovu ili kuchunguza matumizi ya Kimaragoli. Sherehe hii ilifanyika nyumbani na hivyo msaidizi huyu alitazama na kushiriki katika nyimbo na maombi. Hivyo, kwa kutumia mwongozo wa uchunzaji, aliweka alama ya sahihi kwa kila sehemu iliyotumia Kimaragoli ‘sana’, ‘kidogo’, ‘wanachanganya ndimi’ na ‘wanahamisha ndimi’.

Mtafiti alihudhuria na kushiriki ibada ya kanisa la Marafiki la Bware huku msaidizi wake akihudhuria ibada ya Jeshi la Wokovu la Emuhanda na kuchunguza matumizi ya Kimaragoli. Mtafiti alishiriki katika nyimbo na maombi ya kanisani. Kwa kutumia mwongozo wa uchunzaji, mtafiti aliweka alama ya sahihi kwenye sehemu ya kanisani. Hivyo, kila walipoimba nyimbo za Kimaragoli, kutoa matangazo kwa Kimaragoli, au kuhubiri kwa Kimaragoli, mtafiti aliweka alama ya sahihi kwa ‘sana’, ‘kidogo’, ‘wanachanganya ndimi’ au ‘wanahamisha ndimi’. Mtafiti msaidizi vilevile alijaza mwongozo wa uchunzaji kwa kuweka alama ya sahihi kwa kila sehemu ya ‘sana’, ‘kidogo’ ‘wanachanganya ndimi’ na wanahamisha ndimi’ jinsi alivyoshuhudia na kushiriki katika ibada.

Kwa kuwa makanisa haya yana ibada za watoto na watu wazima, mtafiti na msaidizi wake walihudhuria zote. Mtafiti na msaidizi wake walijitambulisha baada ya uchunzaji ili kuzuia uwezekano wa kubadilisha uhalisia wa matumizi ya Kimaragoli katika ibada. Aidha, hatukujitambulisha kwa waumini wote isipokuwa utawala wa makanisa tuliyozuru.

Maeneo yaliyokuwa yamesalia ya Kawere II na Kawere Rateng ya Mashariki yalichunguzwa kati ya tarehe 14-15, Oktoba, 2017 wakati mtafiti alikuwa anaandamana na mtafiti msaidizi katika uwasilishaji wa hojaji. Kwa kuwa ulikuwa wakati wa upanzi na pia wanafunzi wengi walikuwa nyumbani, mtafiti aliweza kuchunguza matumizi ya Kimaragoli shambani, nyumbani, katika michezo ya watoto na madukani. Aidha, kwa kuwa ulikuwa msimu wa kampeni za marudio ya kura za Urais, mtafiti alishiriki katika mazungumzo ya vijana na wazee barabarani na sokoni. Hata hivyo, mijadala ambayo mtafiti alishiriki ni ile iliyoendelezwa katika lugha ya Kimaragoli peke yake. Hii ilimpa mtafiti fursa ya kutathmini umilisi wa vijana na wazee katika kutumia Kimaragoli kujadili baadhi ya masuala ya kijamii. Wadi ndogo za Komenya Masoge na Katieno II ndiyo maeneo ya mwisho kuchunguzwa na mtafiti. Maeneo haya yalichunguzwa mwezi wa Novemba 26. Mtafiti baada ya kutembea maeneo haya, aliambiwa kwamba hapakuwepo na Wamaragoli. Hivyo haikuwezekana kuwasilisha hojaji au kukusanya data ya aina yoyote kuhusu Wamaragoli.

Uchunzaji wa matumizi ya Kimaragoli katika masuala ya kitamaduni na siasa yalifanyika awali mwezi wa Disemba 2016 kwa kuwa ni wakati huu ndio Wamaragoli hufanya sherehe kuu ya Kitamaduni. Kwa kuwa sherehe hii hufanyika mara moja baada ya miaka 10, mtafiti alilazimika kuenda na kurekodi video na kupiga picha za sherehe ya kitamaduni. Sherehe hii iliteuliwa kufanyika katika shule ya Msingi ya Makuyu. Mtafiti

kwa kutumia kamera ya Nikon CoolPix L100, alianza kurekodi video za watoto na makundi mbalimbali yaliyowasili uwanjani yakiimba nyimbo za tohara za Kimaragoli. Mtafiti alirekodi makundi 15 yaliyowasili kuanzia saa tatu hadi saa sita mchana. Kila kundi lilipokuwa njiani kuelekea uwanjani, mtafiti alitoka nje ya shule na kuanza kunasa hadi walipoingia shuleni na uwanjani maeneo ya sherehe. Hali ilikuwa hivi kwa kila kundi hadi makundi 15 yalipoingia uwanjani. Sherehe ilipoanza, mtafiti alienda mbele ya jukwaa kulikokuwa na kamera za wanahabari na kurekodi hotuba zilizokuwa na mchango katika utafiti huu. Vilevile, alizunguka uwanja mzima akirekodi mazungumzo ya mahudhura waliokuwa wanazungumza kwa Kimaragoli. Matukio yaliyorekodiwa kwa video yalijumuisha nyimbo za kitamaduni za Kimaragoli, maigizo, mafundisho ya Kimaragoli kuhusu utamaduni wao, hotuba za kisiasa pamoja na mavazi/shani za utamaduni wa Kimaragoli. Sherehe hii ilikuwa ya kisiasa pia kwa sababu ulikuwa ni msimu wa siasa na ilihusisha wajumbe wa ngazi mbalimbali katika serikali za Kaunti za Migori, Homabay na Vihiga.

Mtafiti msaidizi kwa upande wake, alitembea akisikiliza mazungumzo ya mahudhura. Kwa kuwa ilikuwa sherehe, aliweka alama ya sahihi katika kijisanduku cha ‘sana’, ‘kidogo’, ‘wanachanganya ndimi’ na ‘wanahamisha ndimi’. Vilevile, mtafiti msaidizi alitumia shajara kunukuu miktadha ambamo Kiluo, Kiingereza, Kiswahili kilitumika. Kwa mfano, katika hotuba za Gavana wa Migori, na wagombea wengine wenye asili ya Kiluo waliotumia Kiingereza, Kiswahili na Kimaragoli kidogo, mtafiti msaidizi alikuwa ananukuu kila mojawapo ya viongozi hawa. Ikiwa kiongozi alitanguliza salamu kwa Kimaragoli, mtafiti msaidizi alinukuu, na kisha kueleza kwamba baadaye alitumia mchanganyiko wa Kiingereza na Kiswahili katika hotuba yake.

### 3.8.3 Ukusanyaji Data kwa Mahojiano

Data iliyokusanywa kwa njia ya mahojiano ilikuwa ya kithamano na ilihusisha washiriki wazee na pia viongozi wa makanisa. Lengo la mahojiano haya lilikuwa ni kukusanya data ambayo ilisaidia kuthibitisha data iliyokusanywa na hojaji.

Mahojiano ya kwanza kabisa yalihusisha wazee watatu maeneo ya Emuhanda. Mahojiano haya yalifanyika nyumbani kwa wahojiwa. Mahiojiano ya kwanza yalihusisha bwana na bibiye, na bwana mzee mmoja wa kijiji hicho cha Emuhanda. Mtafiti na msaidizi wake waliwasili eneo la mahojiano saa sita mchana. Mahojiano yalichukua muda wa dakika arobaini na tano. Mtafiti alitumia mwongozo wa maswali ya mahojiano kukusanya habari zilizokuwa zinahitajika. Mtafiti aliuliza swali na watafitiwa kujibu kwa zamu. Mtafiti alitumia simu ya *Lenovo A1000* na *Neon Vodafone Smart Tab 3G* kunasa majibu yote yaliyotolewa na watafitiwa wote.

Mahojiano ya pili yalifanyika Bware, nyumbani kwa Mzee wa Kijiji baada ya wiki moja kuanzia saa tano hadi saa tano na nusu asubuhi. Mtafiti na mtafitiwa waliketi nje ya nyumba ya mtafitiwa. Mtafiti, aliuliza maswali kutegemea mwongozo wa mahojiano aliokuwa nao. Mtafiti alitumia simu ya *Neon Vodafone Smart Tab 3G* kunasa majibu ya mtafitiwa. Baada ya mahojiano, mtafiti alishukuru mtafitiwa na kuondoka. Mahojiano ya tatu yalifanyiwa Arambe, nje ya nyumba ya mtafitiwa (nyanya 2). Maswali yalitokana na mwongozo wa mahojiano. Tatizo lilitokea katika unasaji wa sauti kwa sababu ya upepo mkali uliokuwa unavuma pamoja na sauti hafifu ya mtafitiwa kutokana na uzee. Baada ya dakika thelathini, mahojiano yalikamilika mwendo wa saa sita na dakika thelathini na tano.

### 3.8.4 Ukusanyaji Data kwa Mjadala wa Kundi Lengwa

Mtafiti alitumia njia hii kukusanya data ya kithamano kwa kutumia kundi lengwa moja. Kundi hili lilijumuisha washiriki wa jinsia zote wanaozungumza Kiluo kama lugha yao ya kwanza lakini pia wanazungumza Kimaragoli kwa umilisi mkubwa. Mkutano ulifanyikia Uriri. Mjadala katika kundi hili ulichukua muda wa dakika 45 na ulihusisha washiriki 10 peke yake. Mkutano huu ulianza saa sita hadi saa sita na nusu mchana. Watafitiwa wote waliwasili mwendo wa saa tano na dakika arobaini, na baada ya maandalizi, mkutano ukaanza saa sita. Mtafiti alianza kwa kujitambulisha, na kueleza lengo la mkutano huo. Watafitiwa nao pia walijitambulisha pamoja na maeneo walikokuwa wanatoka. Baada ya hapo, mtafiti alianzisha mjadala kwa kutaka kujua watafitiwa walijifunzia wapi Kimaragoli. Kila mtu alipewa nafasi ya kutoa majibu yake. Kwa kutumia simu ya *Tecno Droipad 7C Pro*, mtafiti alirekodi usemi wa kila mshiriki. Kila mshiriki alipewa dakika moja au ikizidi sana, dakika mbili kujieleza. Iwapo mmoja au wawili walisema wenzao wameshataja hoja yao hivyo hawakuona haja ya kurudia, mtafiti hakuwalazimisha kuirudia. Mazungumzo yote yalirekodiwa kwa njia ya simu na hapakuwepo na matumizi ya shajara au kamera. Mtafiti aliongoza kundi hili kwa lengo la kuhakikisha kwamba habari zozote mpya zilirekodiwa na ufafanuzi muhimu kutolewa.

Mjadala wa pili ulihusisha vijana wenye asili ya Kimaragoli. Mkutano huu ulifanyika eneo la Nyasoko, siku ya Jumamosi. Ulihusisha jinsia zote. Mtafiti alianza mjadala saa nane na nusu hadi saa tisa mchana. Mahojiano haya yalifanyika katika kibanda cha kutazama mpira. Kwanza kabisa, mtafiti alijitambulisha na kueleza lengo lililosababisha mkutano huo. Baada ya kujitambulisha kwa mtafiti, kila mshiriki alipewa fursa ya kujitambulisha kwa kutaja jina na eneo analotoka. Aidha, kila mshiriki alieleza iwapo wazazi wake walikuwa wote Wamaragoli au Mluo na Mmaragoli. Baada ya utambulisho uliochukua dakika saba, mjadala ulianza moja kwa moja. Mtafiti aliongozwa na

mwongozo wa maswali ya mjadala. Mazungumzo yote yalirekodiwa kwa kutumia *Tecno Droipad 7C Pro.*

### 3.9 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika maadili ya taaluma ya utafiti. Hali hii ilisaidia kukwepa changamoto zozote za kimaadili ambazo zingetokea wakati wa ukusanyaji data. Frankael na Wallen (2006) wanaeleza kwamba neno maadili katika utafiti hurejelea kile ambacho ni sahihi au si sahihi katika mchakato wa utafiti. Mugenda na Mugenda (2003) wanadai kwamba mazingatio ya maadili ni kipengele muhimu katika utafiti. Maadili hugawika katika sehemu zifuatazo: ulinzi wa saikolojia ya watafitiwa; ridhaa ya kutafiti au kutafitiwa; haki kwa usiri wa watafitiwa; uwazi kwa wanataaluma (Leedy na Ormond, 2005 ; Halai, 2006). Utafiti huu uliweka mikakati ya kuzingatia haya maadili.

#### 3.9.1 Ulinzi wa Saikolojia ya Watafitiwa

Ulinzi wa saikolojia ya watafitiwa ulihusisha kuuliza maswali ambayo hayakukwaza watafitiwa kuhusu utamaduni wao, kuuliza maswali kwa namna ambayo haikuzua uchungu au majuto ya mambo yaliyotendeka na pia kuhakikisha kwamba hakuna utamaduni wa mtu yeyote unadhalilishwa. Ulinzi huu ulizingatiwa katika hojaji na mahojiano mbalimbali.

#### 3.9.2 Ridhaa ya utafiti

Kabla ya kuenda ughani, mtafiti alitafuta kibali kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI) kupitia Kitivo cha Elimu ya Juu ili kukusanya data kutoka kwa watafitiwa katika gatuzi dogo la Uriri. Kibali hiki kilipatikana kupitia kwa usajili wa kimtandao. Baada ya kupata kibali cha NACOSTI, mtafiti aliendа katika Afisi za Utafiti za Kaunti zilizoko Migori kwa ajili ya kupata vibali zaidi vya kutafitia eneo na

wakaazi wa Uriri. Baadaye alienda katika Afisi ya Kamishana wa Kaunti kwa kibali cha utafiti katika Kaunti ya Migori.

### 3.9.3 Haki kwa Usiri wa Watafitiwa

Usiri ni dhana inayorejelea haki ya watafitiwa kutaka kupata hakikisho kwamba habari wanazotoa hazitaanikwa hadharani kwa yeyote ambaye hakuhusika kenyekenye katika utafiti (Trochim, 2003). Ili kuhakikisha uzingatiaji wa usiri katika utafiti huu, mtafiti aliwakumbusha watafitiwa kwamba habari zote ambazo wangetoa zingekuwa za kufaulisha utafiti huu na wala si kwa lengo lingine. Pamoja na hayo, watafitiwa waliambiwa kwamba data na habari ambazo wangetoa zingehifadhiwa kwa siri kubwa. Hii pia ilihusisha picha ambapo baadhi ya watafitiwa waliomba wasipigwe picha ama wakipigwa, zisisambazwe kwa umma. Mtafiti aliwahakikishia kwamba maombi yao yangezingatiwa. Aidha, majina yao yangewekwa siri.

Vilevile ufichaji wa majina ni sehemu ya kutunza usiri. Ufichaji wa majina ni kanuni mojawapo muhimu katika maadili ya utafiti (Trochim, 2003). Kulingana na Abelson, Frey na Gregg (2004), sababu kubwa inayochangia majina ya watafitiwa kufichwa ni kwamba inawapa uhuru wa kuelezea wanachohisi na kufikiri bila kuwa na uoga wowote. Watafitiwa katika utafiti huu walihimizwa kujaza hojaji bila hofu yoyote kwa kuwa hawangetambuliwa. Aidha, mtafiti alidondoa kipengele cha majina ya watafitiwa katika sehemu ya kwanza ya hojaji baada ya kufanya utafiti awali. Ili kuzingatia usiri wa watafitiwa, mtafiti alitumia herufi kwa minajili ya kuficha majina yao. Katika muktadha huu, mtafiti alibana majina halisi kwa kutumia mtindo wa matumizi ya herufi au tarakimu. Kwa mfano, katika wazee, mtafiti alisimba kwa kutumia Nyanya au Babu kisha tarakimu (kama vile Nyanya 1 au Babu 1). Kwa watoto, mtafiti alisimba kwa kutumia Mtoto A, B, C na kadhalika na vijana, mtafiti alitumia K kisha tarakimu kama

vile K1 kwa maana ya kijana wa kwanza na kadhalika. Katika kundi la mjadala la wasemaji wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli, mtafiti alitumia Bwana/Bibi kisha herufi ya jina la kwanza (mfano, Bwana L au Bibi M). Katika soko, mtafiti alitumia Mnunuzi 1, Mnunuzi 2 na kadhalika na Muuzaji. Mazungumzo yaliyonaswa katika familia yalihitaji usimbaji. Hivyo, mtafiti alitumia Dada A, Dada B kwa ndugu wa familia moja, na pia Kaka, Binti na Mama. Haki hii ya ufichaji majina ilikuwa muhimu sana kwa kuwa iliwapa watafitiwa uhuru wa kushiriki katika utafiti huu bila uoga wowote. Hii iliimarisha uaminikaji wa majibu. Hata hivyo, endapo jina limetajwa katika utafiti huu, mtafitiwa au mshiriki aliomba atajwe.

### 3.9.4 Ulinzi wa Data

Ni jukumu la kila mtafiti kulinda data aliyopata kutoka kwa watafitiwa. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2007), ulinzi wa data ni muhimu katika utafiti wowote. Ulinzi wa data unahusisha kanuni za uchakataji habari za kibinafsi kama vile nyaraka zilizowekwa kama rekodi, na vilevile datatepe. Katika utafiti huu, data ghafi ya Hojaji ilihifadhiwa mahali salama huku data iliyochakatwa ikihifadhiwa katika kipakatalishi kilichokuwa na nywila iliyofahamika na mtafiti peke yake. Washiriki wote walipewa msimbo wa nambari uliotumika kujumuisha na kupanga data zote zilizofuatia. Data iliyokusanywa ilipangwa na kuwasilishwa kama tasnifu.

## 3.10 Uchanganuzi wa Data

Data ya utafiti iliwekwa katika misimbo, kupangwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kithamano na pia Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii (SPSS).

### 3.10.1 Uchanganuzi wa Data Kithamano

Kwa mujibu wa Grbich (2007), uchanganuzi wa kithamano ni mchakato wa ugawaji katika vipande, uainishaji na uhusishaji wa vipengele vya data ya ufasili wa mwisho. Katika kufasiri data kwa kutumia uchanganuzi wa dhamira, maneno au maelezo ya watafitiwa yanawekwa pamoja na ya watafitiwa wenzao ili kumsaidia mtafiti kufafanua data, kutafuta uhusiano baina ya sehemu mbalimbali za data na kuelezea mlingano katika mahusiano dhahiri (Mathews na Ross, 2010). Kulingana na Mathews na Ross (2010) maswali elekezi katika uchanganuzi wa dhamira ni kile kilichosemwa na watafitiwa, kwa nini huenda wakasema hayo na huenda wakamaanisha nini kwa kusema hayo ? Maswali haya huwa amilifu katika kutoa mwongozo wa kina kuhusu data ya takwimu.

Hatua ya kwanza katika uchanganuzi wa data ya kithamano ilikuwa kusikiliza semi zote za mahojiano na mjadala wa kundi lengwa zaidi ya mara moja kisha kunakili simulizi zote kwa kipakatalishi. Baada ya kunakili kwa kipakatalishi, mtafiti alipitia data hiyo na kisha kuichanganua kutegemea madhumuni ya utafiti. Pale palipohitaji unukuzi wa moja kwa moja wa maoni ya watafitiwa, dondoo zilichukuliwa kutoka kwa data iliyochapwa kwenye kipakatalishi. Maswali ambayo Mathews na Ross (2010) wanazua yalikuwa mwongozo muhimu katika kupanga data na kuichanganua ili kuhakikisha kwamba kauli za watafitiwa zimezingatiwa mintarafu muktadha wa utafiti.

Pili, video zote zilizorekodiwa kwenye kamera ya *Nikon CoolPix L100* zilihamishwa kwenye kipakatalishi na kutazamwa zaidi ya mara moja. Mawazo makuu yaliyohusu utafiti huu yalinukuliwa na palipohitajika idhibati ya picha tuli, mtafiti alichakata sehemu za video kwa kutumia programu ya *VLC Media Player* na kuzalisha picha tuli. Picha hizi ziliambatanishwa na maelezo ili kutomelea data.

Tatu, data kutoka kwa hojaji zilizokuwa na maswali wazi zilipangwa katika dhamira na kuwasilishwa kwa unukuzi wa semi mbalimbali. Hii data ilisaidia kueleza waziwazi majibu ya washiriki katika maswali funge. Katika utafiti huu, data kutoka maswali wazi ililinganishwa miongoni mwa watafitiwa, iliainishwa na mwishowe kufasiliwa. Maelezo yaliyohusiana na data ya kitakwimu yalikusanywa katika hojaji za maswali funge na kuripotiwa kidondoo na hivyo kuweka wazi matokeo.

### 3.10.2 Uchanganuzi wa Data ya kiwingiidadi

Pallant (2002) anadai kwamba takwimu elezi kama vile hesabu za umaratokezi, asilimia na wastani ni amilifu katika kuelezea nduni za sampuli. Katika utafiti huu, mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli, mielekeo ya wasemaji kuhusu udumishaji wa lugha ya Kimaragoli na pia umilisi wa wazungumzaji wa Kimaragoli ndiyo ilichanganuliwa kitakwimu kwa kutumia hesabu za umaratokezi, asilimia, wastani, majedwali, na chati duara. Mtafiti alitumia Kichanganuzi cha Data ya Kitakwimu ya Sayansi Jamii (SPSS) ili kuchakata na kuzalisha hesabu za umaratokezi, asilimia na wastani. Katika kufanya hivi, mtafiti alisimba data kutoka kwa hojaji, kisha kuipanga katika nduni maalum ambazo zilipewa misimbo ya kihisabati. Misimbo hii ilichapwa katika kichanganuzi ili kuzalisha asilimia kuhusu wasemaji wa Kimaragoli, umaratokezi wa vipengele vinavyoathiri umilisi wa lugha na pia kuzalisha chati na majedwali yanayofafanua zaidi data ya utafiti huu.

Vilevile, mtafiti alihusisha mihimili mbalimbali ya nadharia za Mtagusano lugha, Uzalishaji kijamii na nadharia ya Uhai wa Kiethnoisimu ili kuhakikisha kwamba kila madhumuni ya utafiti yamezingatiwa. Tafiti zilizofanywa kwingineko zilirejelewa ili kutilia uzito uchanganuzi wa data ya utafiti kwa kuonyesha mfanano na au msigano wa

matokeo yetu na ya tafiti hizo za awali, matokeo mapya yaliyopatikana baada ya uchanganuzi yaliripotiwa.

### 3.11 Hitimisho

Sura hii imeelezea jinsi ambavyo utafiti ulifanyika. Mtafiti amezungumzia kwa kina na kwa kutumia majedwali na vielelezo, vifaa, mbinu za utafiti na jinsi data ilikusanywa. Mtafiti pia ameelezea jinsi alichanganua data yake na kisha kuiwasilisha. Masuala ya kimaadili pia yameelezwa kikamilifu ili kulinda utaaluma wa mtafiti na utafiti wake. Hii ni muhimu kwani inaweka wazi jinsi ambavyo utafiti ulifanyika kuanzia mwanzo hadi wakati wa kuchanganua data na kuwasilisha matokeo.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

### 4.1 Utangulizi

Sura hii ni wasilisho la matokeo ya utafiti yaliyojadiliwa mintarafu madhumuni na maswali ya utafiti. Data ya utafiti imechanganuliwa kwa kutumia takwimu na kuwasilishwa kwa njia za majedwali, asilimia, chati duara na grafu. Vilevile, kauli mbalimbali za watafitiwa zimenukuliwa kwa ajili ya kuthibitisha majibu yaliyotolewa kwa maswali funge katika hojaji. Fauka ya hayo, ithibati kutoka kwa ratiba ya uchunzaji iliyotumika katika utafiti imetumiwa kuthibitisha majibu ya kitakwimu. Ithibati pia imetolewa kutoka kwa majibu ya maswali wazi watafitiwa ili kutomelea takwimu mbalimbali.

### 4.2 Takwimu za kimsingi za Watafitiwa

Utafiti huu ulidhamiria kukusanya data kutoka kwa hojaji 390 pamoja na njia zingine mbalimbali. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa Wamaragoli katika wadi ndogo tatu, hojaji 117 hazingeweza kusambazwa katika maeneo haya. Hivyo, zilizosambazwa na kurudishwa zilikuwa 273. Kati ya hizi, hojaji 29 hazikujazwa vyema na hivyo wakati wa kusafisha data, ziliondolewa. Zilizosalia 244 ndizo zimetumika katika uchanganuzi wa sura hii ya nne. Katika jumla ya hizi takwimu, 75 ni za kundi la miaka 12-17, 82 ni kundi la miaka 18-35 na 87 ni kundi la makamo na wazee (walio na miaka zaidi ya 36).

#### 4.2.1 Msambao wa Kiwango cha mwitiko wa Watafitiwa

Mtafiti alisambaza hojaji 273 kwa makundi matatu ya watafitiwa waliogawanywa kiumri. Makundi haya yalikuwa watoto (miaka 12-17), vijana (18-35) na makamo na wazee (zaidi ya miaka 36). Hojaji hizi zilisambazwa katika Kata saba zilizokuwa na Wamaragoli, kila Kata ikitengewa hojaji 39. Katika jumla ya hojaji 273 zilizosambazwa,

249 zilirudishwa. Baada ya uchanganuzi wa kimsingi, mtafiti alitambua kwamba hojaji 29 hazikujazwa ilivyostahili na hivyo zikaondolewa katika jumla ya zile zilizotumika katika uchanganuzi huu. Kata ya Kamsaki iliyotumika katika utafiti awali si sehemu ya matokeo haya. Mtafiti alisimba na kuchanganua hojaji zote baada ya utafiti wa ughani kukamilika. Kiwango cha mwitiko kilikuwa 89.4%. Jedwali 4.1 linaonyesha msambao wa watafitiwa katika kata zote saba na hojaji zilizorudishwa.

***Jedwali 4.1: Msambao wa mwitiko***

| | Umaratokezi | Asilimia | Kiwango cha mwitiko |
|---|---|---|---|
| Arambe | 30 | 12.2 | 76.9 |
| Bware | 31 | 12.7 | 79.5 |
| Kajulu II | 39 | 16 | 100 |
| Kawere II | 38 | 15.6 | 97.4 |
| Kawere Rateng | 37 | 15.2 | 94.9 |
| Lwala | 38 | 15.6 | 97.4 |
| Thim Jope | 31 | 12.7 | 79.5 |
| **Jumla** | **244** | **100.0** | |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

### 4.2.2 Nduni za Kidemografia za Watafitiwa

Mtafiti alitaka kujua habari za kimsingi za watafitiwa. Nduni za kidemografia zilijumuisha ndoa, jinsia, miaka na lugha zinazozungumzwa. Habari hizi zilikuwa za kimsingi katika kufasili na kujadili udumishaji wa Kimaragoli Uriri.

#### 4.2.2.1: Jinsia

Utafiti ulionyesha kwamba kutoka kwa hojaji 244 zilizokubalika, 117 (48%) zilikuwa za watafitiwa wa kiume ilhali 127 (52%) walikuwa wa kike. Msambao wa kijinsia umeonyeshwa katika Jedwali 4.2. Jedwali hili linaonyesha kwamba mtafiti alikusanya data kutoka kwa jinsia zote hivyo kuzuia uwezekano wa kuegemea upande mmoja wa jinsia katika kufafanua data ya watafitiwa.

**Jedwali 4.2. Jinsia ya Watafitiwa**

| | Jinsia ya Kiume | Jinsia ya Kike | Jumla |
|---|---|---|---|
| Arambe | 16 | 14 | 30 |
| Bware | 14 | 17 | 31 |
| Kajulu II | 17 | 22 | 39 |
| Kawere II | 18 | 20 | 38 |
| Kawere Rateng | 16 | 21 | 37 |
| Lwala | 16 | 22 | 38 |
| Thim Jope | 20 | 11 | 31 |
| Asilimia | 48 | 52 | 100 |
| **Jumla** | **244** | **100.0** | |

*(Chanzo: Data ya nyanjanii)*

#### 4.2.2.2 Umri wa Watafitiwa

Utafiti pia ulidhihirisha kwamba 87 (35.7%) ya watafitiwa ilikuwa ya watu waliozidi miaka 36, 82 (33.6%) wakiwa wa miaka 18-35 huku 72 (30.7%) wakiwa watoto kati ya miaka 12-17.

#### 4.2.2.3 Lugha ya Watafitiwa

Kama inavyoonyeshwa katika kielelezo 4.2, 146 (59.8%) wanaongea Kimaragoli, 90 (37%) wanaongea Kimaragoli na Kiluo (ingawa lugha yao ya mama ni Kimaragoli) huku 8 (3.2%) wakiongea Kiluo.

#### 4.2.2.4 Ndoa miongoni mwa Watafitiwa

Kutokana na majibu ya utafiti, 100% ya watafitiwa waliozidi miaka 36 walikuwa katika ndoa. Waliokuwa kati ya miaka 18-35, 61 (74.4%) walikuwa katika ndoa huku 21 (25.6%) wakiwa hawako katika ndoa.

### 4.3 Mikakati ya Udumishaji wa Kimaragoli Uriri

Sehemu hii imejadili madhumuni ya kwanza ambayo ni mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri. Ili kutathmini mikakati inayotumika kudumisha

lugha ya Kimaragoli Uriri, mtafiti aliuliza watafitiwa swali lifuatalo: Kitu gani ambacho kinafanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa mpaka leo hapa Uriri? Matokeo yamejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.3.1 Kutumia Idhaa za redio

Redio ni kipengele mojawapo kinachotumika kuendeleza na kudumisha lugha za binadamu katika kizazi cha leo. Miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli, idhaa mbili kuu zenye masafa yanayofika Uriri na Kenya nzima ni Redio *Mulembe* FM na *Vuka* FM za Royal Media House. Hapo awali, KBC ndiyo ilikuwa idhaa ya kipekee iliyopeperusha matangazo kwa Kimaragoli japo kwa muda mfupi. Redio hizi zimekuwa na mchango mkubwa katika kukumbusha wasemaji wake maneno ya Kimaragoli bila kujali maeneo waliyoko. Mkakati huu ndio ulipendelewa na watafitiwa wengi katika makundi yote ya kiumri. Mkakati wa kutumia idhaa ulikuwa na wastani wa 185 (75.8%). Sababu kubwa ya kupendelea mkakati huu ni kwamba kuwepo kwa kipengele cha redio katika simu kunafanya mtu yeyote kuisikiliza wakati wowote mahali popote. Aidha, miongoni mwa wazee wa Kimaragoli, usikilizaji wa redio ni suala la kawaida wakiwa nyumbani, shambani, au hata wanapolisha mifugo wao.

Matokeo haya yanawiana na ya utafiti wa Obiero (2008) uliodai kwamba lugha ya Kisuba ilihuishwa na inadumishwa hadi sasa kupitia kwa kuanzishwa kwa idhaa ya Kisuba. Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha, huu ni mkakati ambao wasemaji wa lugha maalumu hukubaliana na kuuanzisha kwa kushirikiana na dola mahususi. Aidha, Kulingana na nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu, huu ni mkakati unaohitaji juhudi za serikali kwa kuwa leseni ya kuanzisha redio hutolewa na wizara za Habari na Mawasiliano. Aya zifuatazo zimejadili kwa kina matokeo kwa kila kikundi.

Miongoni mwa watoto kati ya miaka 12-17, 50 (66.7%) walikubali kwamba hii ni njia mojawapo ya kudumisha Kimaragoli. Watafitiwa wengi 64 (78%) katika kundi la vijana pia walikubali kwamba kusikiliza idhaa zinazotangaza kwa Kimaragoli kulikuwa amilifu katika kudumisha Kimaragoli maeneo haya ya Uriri na Migori kwa ujumla. Miongoni mwa makamo na wazee, 72 (82.8%) ya watafitiwa katika kundi hili waliteua kuwa mkakati mkuu wa kuendeleza Kimaragoli. Kama tulivyoonyesha hapo awali, uchunzaji wetu ulionyesha kwamba katika nyumba zilizochunguzwa, ni 4 zilizokuwa na redio iliyokuwa inaimba au kuongea. Hata hivyo, miongoni mwa makamo na wazee, idhaa za *Mulembe* na *Vuka* zinakuwa sehemu ya maisha yao kwa kuwa zinawapa habari katika lugha yao ya Kimaragoli. Baadhi ya wazee katika kundi hili hawakuenda shuleni au kupata masomo ya kutosha kufahamu Kiswahili au Kiingereza, hivyo kuwepo kwa idhaa hizi kunawasaidia sio tu kupata habari za kitaifa na kimataifa bali pia kujikumbusha lugha ya Kimaragoli.

Kijumla, matokeo katika makundi haya matatu yanashabihiana na ya Marti-Bucknall (2007) aliyedai kwamba kadiri watu wanavyozidi kuhamia maeneo mbalimbali kitaifa na kimataifa, teknolojia ya masafa ya mbali imekuwa muhimu kuwasaidia watu hawa kuweza kuendeleza lugha zao .

### 4.3.2 Kufundish(w)a kusiko rasmi na Kuamilia Kimaragoli nyumbani

Ufundishaji usorasmi na uamiliaji wa lugha asili katika mazingira ya nyumbani ni mojawapo ya mkakati ambao umetumika kwa muda mrefu, hata kabla ya kuasisiwa kwa mbinu za maandishi au teknolojia. Mkakati huu unachukuliwa kuwa wa kimsingi kabisa kwa kuwa utukizi wake ni wa kiasilia. Hii ndiyo sababu watafitiwa wengi waliupendelea na ulikuwa na wastani wa 178 (73.2%).

Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na tafiti za Romaine (2002), Strubell (2001) na Arka (2013) kwamba ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kizazi kinachofuata kimerithishwa lugha ya kwanza, kupitia hasa uamiliaji na ufundishaji usio rasmi. Aidha, wanakubaliana kwamba huu ni mkakati mojawapo unaothaminiwa sana katika udumishaji wa lugha yoyote katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha, mkakati huu ni wa jamii nzima na wala si wa mtu au familia binafsi. Pamoja na hayo, nadharia ya Uzalishaji kijamii inashikilia kwamba mkakati huu unastahili kuchunguzwa kwa mujibu wa jamii pana ili kupata mwanga kamili wa udumishaji lugha. Vilevile, inashikilia kwamba mahusiano ya kijamii, yakiwemo maeneo ya matumizi lugha ni muhimu katika kuendeleza lugha, ambayo katika muktadha huu ni kufundishwa Kimaragoli nyumbani.

Ingawa mkakati huu ulikuwa wa pili katika wastani, matokeo miongoni mwa makundi halisi yalionyesha tofauti za hapa na pale. Watoto wengi 58 (77.3%) walikubali kwamba wao kufundishwa lugha ya Kimaragoli nyumbani na wazazi wao ni njia bora ambayo imekuwa ikisaidia kudumisha lugha yao. Ili kuhakikisha uhalali wa takwimu hizi, mtafiti pia aliuliza watafitiwa hawa ni wapi walijifunzia Kimaragoli. Watafitiwa 55 (73.3%) walikiri kuwa mazingira ya nyumbani yalisababisha wao kujua Kimaragoli. Mbali na wazazi, walidai kwamba watu wengine wa ukoo nyumbani kama vile babu, mjomba, majirani, nyanya na watoto wenzao walichangia wao kujua Kimaragoli. Takwimu hizi zinashadidiwa na kauli zilizotolewa na wazee katika mahojiano kwamba:

> **Babu A:** *Anze hee, murogori nu mundu agotitsa mima gigye dave. Hosi hakutsidza kumaa komoroma lulimwi lwitu. Kwigiza vaana vitu Llimi rwavo koveye hango.*
> *[Mmaragoli ni mtu ambaye hapotezi mila zake. Popote tunapoenda, tunaongea lugha yetu. Tunafundisha watoto wetu tukiwa nao nyumbani. TY]*
> **Nyanya B**: *Vaana vitu vatsiyi kukina wu Mmbo, waramoroma Rovo. Na vaana vu Mmbo nivatsi kukina hango hu Murogori, varamoroma Llogori. Sasa garondekana na Havana vatsiyi kukina. [Watoto wetu wakienda kucheza nyumbani kwa Mluo, watatumia Kiluo. Na watoto wa Mluo wakija kuchezea kwa*

*boma la Mmaragoli, watatumia Kimaragoli.Sasa inategemea mahali walikoenda kuchezea. TY] (Chanzo: Data ya nyanjani)*

Kauli ya Babu A na B zinaonyesha kwamba ufundishaji usorasmi na uamiliaji wa lugha ya Kimaragoli katika mazingira ya nyumbani kumekuwa muhimu katika kukidumisha.

Miongoni mwa kundi la vijana, 61 (74.4%) walipendelea mkakati huu kudumisha lugha ya Kimaragoli. Katika kundi hili, watafitiwa 57 (69.5%) walikuwa wameolewa huku 25 (30.4%) wakiwa hawajaolewa. Katika 57 walioolewa, 30 (52.6%) walikuwa wa kike huku 27 (47.4%) wakiwa wa kiume. Kutokana na takwimu hizi, ni bayana kwamba wengi wanaopendelea mkakati huu tayari ni wazazi na hasa wazazi wa kike. Kijumla, Kuncha na Bathula (2004) wanadai kwamba wanawake katika jamii zote, hasa kina mama, ndio wahafidhina na wana jukumu la kudumisha mila na lugha. Hii ina maana kwamba wao ndio wana jukumu kubwa la kuwafunza watoto lugha ya kwanza. Hii ndiyo sababu lugha asilia kwa kiasi kikubwa ikapewa jina la lugha mama. Kwa mujibu wa nadharia ya Uzalishaji Kijamii, kila mwanajamii anapewa jukumu analostahili kutimiza katika mkufu mzima wa udumishaji lugha, na jukumu analopewa mama ni kuhakikisha kwamba watoto wake wanaweza kuzungumza lugha yake asilia huku baba akihakikisha mila na desturi za jamii yake zinafuatwa.

Kwa upande mwingine, watafitiwa wa makamo na wazee 59 (67.8%) waliunga mkono mkakati huu. Ufundishwaji wa lugha nyumbani si sawa na hali ilivyo katika mfumo wa shule. Katika mfumo huu wa nyumbani, wazazi huzungumza na watoto wao na katika hali hiyo hiyo, watoto wakawa wanajifunza lugha. Hivyo basi, kutoka kwa mzazi, mtoto anajifunza namna ya kutamka maneno ya Kimaragoli, anafahamu jinsi ya kuyatumia katika miktadha maalumu miongoni mwa ndaro zingine zinazoambatana na uamiliaji lugha ya kwanza. Kwa mfano, katika mahojiano ya wazee watatu, mmoja wao alikuwa

anafunza vijana aina za nyasi katika Kimaragoli, historia ya kuanza kwa chai kwa kutumia nyimbo ambazo maneno yake ni nadra kusikika katika vizazi vya leo kwa kuwa hayatumiki sana. Aidha, alikuwa anafunza hata jinsi ya kutamka majina ya Kimaragoli. Mojawapo ya wimbo alioimba ni huu:

Vandu vanwetsanga ichayi, varakasune, yeye yeye
Vandu vanwetsanga ichayi, varakasune, yeye yeye
Umruvilli avugura kisanda, adaha anwaa
Avora nu vwuki.

Watu wanaokunywa chai, watashindwa kuzaa, yeye yeye
Watu wanaokunywa chai, watashindwa kuzaa, yeye yeye
Mchochezi anachukua kata, anachota na kuonja
Anadai ni asali (TY) (Chanzo: Data ya nyanjani)

Ingawa huu ni wimbo kuhusu chanzo cha chai miongoni mwa Wamaragoli, una maneno ambayo ni nadra sana kutumika siku hizi kwa mfano, “kusuna” (kuwa mgumba/tasa), na mruvilli (mchochezi), kisanda (kata). Hata hivyo, wazee wanapoketi na kusimulia watoto wao au wajukuu hadithi za kale zilizo na maneno haya, ni rahisi kuyaamilia, kuyabwia na kuyatumia katika maisha ya kila siku kwa kuwa yanakuwa sehemu ya ung’amuzi wa mtoto kuanzia umri mchanga hadi utu uzima.

### 4.3.3 Kuongea Kimaragoli nyumbani

Mkakati wa kuzungumza aghalabu huenda sambamba na mkakati wa kujifunza au kufundishwa lugha asilia nyumbani. Ni bayana kwamba mtoto, kijana au makamo na mzee anapofunzwa au kujifundisha lugha yake, litakalofuata kimantiki ni kujaribu kuizungumza katika mazingira hayo hayo. Hii ndiyo sababu matokeo ya mkakati huu yalionyesha mapendeleo ya kiwango cha wastani cha 177 (72.7%). Matokeo haya yanathibitisha ripoti ya Arka (2013) kwamba mkakati huu pia umewahi kutumika katika mataifa ya Indonesia na Papua New Guinea huku mafanikio yake yakiwa makubwa.

Kulingana na nadharia ya Uzalishaji Kijamii, huu ni mkakati ambao hutokea bila kupanga, yaani ni mkakati wa king'amubwete au kiasilia.

Katika kuzingatia makundi mahsusi, watoto 39 (52%) walikubali kwamba kuzungumza Kimaragoli nyumbani kumesaidia kuidumisha. Uchunzaji uliofanyika katika kata saba ulionyesha kwamba nyumba 14 (100%) zilikuwa zinatumia Kimaragoli mashambani, katika michezo ya watoto nje ya nyumba zao, katika kufanya kazi za nyumbani, katika malisho ya mifugo, au wakiogelea au wakiwinda.

Miongoni mwa vijana waliojaza hojaji hii, 72 (87.8%) walikubali kwamba kuongea Kimaragoli nyumbani ndio mkakati bora na maarufu zaidi katika kudumisha lugha yao. Hii ni idadi ya juu ikilinganishwa na idadi ya watoto 39 (52%) waliokubali mkakati huu kuwa maarufu katika kudumisha lugha. Hii ndiyo sababu pia watafitiwa 75 (91.5%) katika kundi hili walikiri kujifundisha Kimaragoli wakiwa nyumbani pamoja na nyanya/babu, mama/baba, wajomba, na ndugu zao. Sababu kubwa inayochangia vijana wa umri huu kutumia Kimaragoli zaidi ni kwa sababu wametambua thamani iliyomo katika kutumia lugha yao pamoja na kwamba wengine wao ni wazazi na wanajaribu kuwa mfano bora katika kuendeleza mila na utamaduni wa Kimaragoli, ikiwemo lugha yao. Nadharia ya Mtagusano lugha inadai kwamba kundi hili ndilo lenye satua kubwa ya kudumisha au kufifisha lugha yao. Nadharia hii pia inadai kwamba wanajamii wanaokaribia kubaleghe na waliobaleghe ndio mawakala wakuu wa mabadiliko na msambao wa lugha katika jamii. Hivyo, hili ni kundi ambalo umilisi wao umeimarika na linaweza kuuboresha zaidi au kuudamirisha na hivyo kudumisha au kuangamiza lugha yao. Katika uchunzaji uliofanywa, mtafiti alitambua kwamba vijana wengi walikuwa wanatumia Kimaragoli wakiwa mashambani, malishoni na wakiwa na jamaa zao nyumbani. Ni familia moja tu ambayo mtafiti alitambua walikuwa wanachanganya

Kimaragoli na Kiluo. Sababu kubwa ilikuwa ni kwamba mama alikuwa Mluo na baba Mmaragoli.

Miongoni mwa wazee na makamo, jumla ya watafitiwa 68 (78.2%) katika kundi hili walikubali kwamba kuzungumza Kimaragoli nyumbani kunasaidia kuidumisha. Kwa mujibu wa data ya uchunzaji, mazungumzo ya Kimaragoli katika nyumba mbalimbali yalijumuisha watoto/vijana kutumwa kutenda shughuli mbalimbali, salamu, siasa, dini miongoni mwa mambo mengine. Katika mijadala na baadhi ya watafitiwa, ilikuwa wazi kwamba rika la vijana, hasa wanaosomea nje ya maeneo lugha au wanaofanya kazi mbali na nyumbani au wanawake walioolewa mbali kwa Waluo walikuwa wanapata tatizo la kuzungumza lugha hii kwa ufasaha na mtiririko. Hii ndiyo sababu Mzee M na nyanya 2 alisema kwamba:

> **Mzee M:** *Orora vaana vitu vanyingi vamenyi ichova kigira masomo. Wa vaziza si vagaana na varogori vavo mba, kari niva varava mu schools ziveyemu na varogori kutura Evorogori, vatiza kuzya kuvoo kigira vamanyi Llogori vurah dave. Vivisaa. Kunarilla Ruswahili sana ruvarombaa vava nu vudinyu komoroma Llogori. Ku vaduka havundu vagadahara. Kuri vaana vamenyi mu town, rwavaza kumenya mmadara yinu, vaveza vamanyi Llogori dave, ku nave ni mihiga gyanga ndi, irwo rwahula Llogori kutanga.[Unaona watoto wetu wengi wanaishi nje kwa sababu ya masomo. Wanapoenda, hawakutani na wasemaji wa lugha yao au hata wanapokutana na wanafunzi kutoka maeneo ya Umaragolini, wanaogopa kuongea nao kwa sababu hawajui Kimaragoli vizuri. Wanajificha. Wengine wanaoishi mjini, wanapokuja huku vijijini, huwa hawajui Kimaragoli. Wanachukua muda ndio wajifunze. TY]*
> **Nyanya 2:** *Niimbeye na visukuru hango, komoromaza Llogori. Kari twana tudi yitu.[Nikiwa nyumbani na wajukuu, tunaongea tu Kimaragoli. Hata hawa wadogo. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hizi mbili zinaonyesha kwamba zipo juhudi za kuendeleza Kimaragoli nyumbani licha ya kuwepo kwa changamoto kwa baadhi ya vijana ambao hawaishi vijijini. Kadiri wazee wanapoendelea kuzungumza na watoto na wajukuu wao kwa Kimaragoli, ndivyo wanavyoidumisha na pia ndivyo wanavyopasha vizazi vichanga dafina na hazina ya Kimaragoli. Matokeo haya yanaoana na mawazo ya nadharia ya uzalishaji kijamii inayoshikilia kwamba matumizi ya lugha maalumu katika maeneo kama ya nyumbani

yanasaidia kudumisha lugha hiyo na kwamba njia nzuri ni kuhakikisha kizazi kinachofahamu lugha vyema kinastahili kuwa mstari wa mbele katika kurithisha dafina hizi kile kizazi kisichojua lugha hii.

Kulingana na Finocchiaro (2004), Kipsisey (2010) na Kheirkhah na Cekaite, (2015) kuzungumza lugha ya asili nyumbani ndio mkakati bora zaidi wa kudumisha lugha. Hii ni kwa sababu uzungumzaji lugha nyumbani unasaidia kujenga uzoefu wa kuitumia katika mazingira mbalimbali alimuradi Kimaragoli kinaweza kutumika.

### 4.3.4 Kutumia Kimaragoli katika Ibada

Nadharia ya uzalishaji kijamii inashikilia kwamba udumishaji lugha ni tendo linalostahili kuzingatia maeneo mbalimbali ya matumizi lugha, na katika muktadha huu, kanisani. Kanisa ni sehemu moja ambayo Thomason (2001) na Hamde (2005) wamekubaliana ni muhimu katika kuendeleza au kudumisha lugha yoyote ile, ikiwemo Kimaragoli. Ni kipengele mojawapo kinachoweza kutumika katika kushawishi waumini kuchukua mwelekeo fulani, ukiwemo wa kuabudu kwa kutumia lugha mahsusi. Utafiti wa Hamde (2005) katika sura ya pili ulionyesha jinsia ambavyo matumizi ya Kiblini kanisani kulisaidia kuhuisha na kudumisha lugha hii. Udumishaji wa Kimaragoli kwa kiasi kikubwa unategemea matumizi yake katika ibada za madhehebu mbalimbali. Hii ndiyo sababu matokeo wastani yalikuwa 143 (58.7 %). Matokeo ya mkakati huu yamejadiliwa kwa kina na kwa kila kikundi katika aya zinazofuata.

Matokeo ya kimakundi yanaonyesha watoto 52 (69.3%) walikiri kwamba kutumia Kimaragoli kanisani ni njia mojawapo ya kuidumisha. Matokeo haya yanatiliwa nguvu na mahojiano yaliyofanyika katika eneo la Bware kwamba:

**Mzee M:** *umanyi hee, ku vaana, rwu mwigizi yatsaza ma avavola ndi kurimba muLlogori,rwa avigiza rwimbu, vatangaza kwimba. Ndio vakonyeka kumanyal'limi rwavo.[Unajua, kwa watoto,mwalimu wa kanisa anapokuja na kuwaambia kwamba wataimba kwa Kimaragoli, akishawafunza wimbo, wao wanaanza kuimba tu. Hivyo wanasaidika kufahamu lugha yao.TY]*

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Data ya uchunzaji pia inaonyesha kwamba watoto katika kundi hili la umri lilitumia lugha ya Kimaragoli kufundishwa dini ya Kikristo. Mtafiti alichunguza kongamano la vijana wa Kanisa la Friends lililofanyika katika eneo la Thim Jope na kutambua kwamba hata michezo ya kukimbia, mashindano ya kuvuta kamba na kusakata dansi yaliyofanyika katika kongamano hili yalitumia Kimaragoli.

Miongoni mwa vijana, 29 (35.4%) walikiri kutumia ibada kudumisha Kimaragoli. Watafitiwa katika kundi la makamo na wazee 58 (66.7%) walikubali kwamba wamekuwa wakitumia mkakati huu kudumisha Kimaragoli. Ukweli wa hoja hii unathibitishwa na mahojiano na Mzee 2 na mchungaji wa Bware Friends waliodai kwamba:

**Mzee M:** *Hii, koveye muno na Friends, Salvation, na P.A.G na alafu kuvaa nu tuvugana tunditudii kuri Pentekoste, African Israel, Vadivai. Mavugana yagaa nigakitangaa gaari varoogori veree navutswa vavoo vatanga kwingira mu.[Naam, tuna makanisa ya Friends, Salvation, P.A.G, na mengine madogo madogo kama vile Pentekoste, African Israel, Divine. Makanisa haya yalipoanza yalikuwa ya Wamaragol ipekee lakini katika baadhi, Waluo walijiunga na kuanza kushiriki. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Katika mahojiano zaidi na Mzee huyu, ilikuwa wazi kwamba makanisa mengi yenye asili ya Kimaragoli yalikuwa yameanza kuathirika kutokana na wageni wanaojiunga nao. Kutokana na data ya uchunzaji, kanisa la Uriri Friends mjini Uriri, linatumia Kiswahili katika mahubiri, nyimbo na matangazo; Kanisa la Bware linatumia Kiswahili/Kiingereza/Kimaragoli katika mahubiri lakini matangazo ya kina mama yanafanyika katika Kimaragoli; kanisa la Mukuyu Friends linatumia Kimaragoli/Kiswahili, makanisa ya Jeshi la Wokovu ya Emuhanda na Bware yanatumia

Kimaragoli/Kiswahili. Vilevile, katika kongamano la vijana lililofanyika mwezi wa Disemba 2017 katika shule ya Thim Jope, washiriki walitumia Kiswahili/Kimaragoli/Kiingereza. Mhubiri mkuu alialikwa kutoka maeneo ya Magharibi na alihubiri kwa Kiidakho/Kiswahili. Mtafiti pia alichunguza ruwaza za matumizi ya lugha katika maeneo ya makanisa na kutambua kwamba watoto wadogo wanafundishwa kwa kutumia Kimaragoli/Kiswahili, washiriki wanapotawanyika baada ya ibada, wanatumia Kimaragoli tu au Kimaragoli-Kiswahili kutegemea wawasilianaji. Kama inavyodai nadharia ya Uhuishaji kiethnoisimu, kuendelea kutumia lugha katika muktadha maalumu kunasaidia kuidumisha lugha hiyo, ni muhimu Kimaragoli kiendelee kutumiwa kanisani iwapo kitaendelezwa siku za baadaye. Kujiunga kwa waumini wa Kiluo wasioelewa au kuzungumza Kimaragoli huenda kukawa na athari hasi katika juhudi za udumishaji wa lugha hii.

### 4.3.5 Mikutano

Mikutano ni tukio la kila siku miongoni mwa wanajamii. Ni njia inayotumiwa kuwaleta wasemaji wa lugha moja pamoja kwa ajili ya kujadili au kutafuta mwelekeo wa jamii katika masuala mbalimbali yakiwemo ya lugha na utamaduni. Watafiti mbalimbali tuliohakiki katika sura ya pili walionyesha kwamba mkakati huu hutumika kudumisha lugha. Katika utafiti huu, mtafiti alitambua aina za mikutano kama vile mikutano ya vyama vya kina mama na wazee, ya wakulima, mikutano ya kiutawala na ya kitamaduni (sherehe mbalimbali za kijamii). Kwa mujibu wa majibu yaliyotolewa na watafitiwa, kulikuweko na tofauti za kimakundi. Tofauti hizi zimejadiliwa kwa kina.

Matokeo ya mkakati huu yanaonyesha kwamba watoto 40 (53.3%) katika kiwango hiki cha kiumri walikubali kwamba lugha ya Kimaragoli inadumishwa kupitia mikutano, hasa ya wazee na kina mama. Mikutano hii inajumuisha ya vyama vya maendeleo (*masanga)*

ambapo kila mwezi, wao hukongamana katika nyumba ya mmoja wa wanachama na kumchangia pesa, sukari au mahindi. Watoto ambao wazazi wao ni wanachama walikubali kwamba wazazi wao wanapowakaribisha wanachama wenzao, wao hutumia lugha ya Kimaragoli. Aidha, wanapoulizwa kusaidia katika kuwalaki na kuwatumikia, hutumia Kimaragoli. Mtafiti alishuhudia mkutano wa "*One Acre Fund*" uliofanyika kando ya kanisa la Bware ambapo wakulima wa miaka ya makamo na wazee walikuwa wanapewa mbegu za mahindi kwa ajili ya upanzi. Katika mkutano huu, lugha ya Kimaragoli ilikuwa ikitumika kuhamasisha wakulima.

Watafitiwa 40 (48.8%) katika kundi la vijana wa miaka 18-35 walikubali kwamba mikutano mbalimbali ya kina mama na wazee ni amilifu katika kudumisha lugha yao. Mikutano hii ilihusisha vyama vya ukulima, uchangianaji pesa au rasilimali na muhimu zaidi mikutano ya Halmashauri ya Wazee wa Kiluhya Migori. Katika mahojiano na Mwenyekiti wa Halmashauri hii, alikubali kwamba wao hutumia Kimaragoli zaidi maana 90% ya wanahalmashauri ni Wamaragoli. Sababu kubwa aliyotoa ni kwamba kabila ndogondogo za Waluhya zilizomo Migori kama vike Wakhisa, Wabukusu, Wanyore na wengineo, hawajawalikilishwa ipasavyo kwa kuwa hakuna wazee waliojitokeza kujiunga na chama. Katika mjadala na washiriki wa Kiluo, mmoja wa kina mama Mluo aliyeolewa kwa Mmaragoli, alisema kwamba:

> **Mama M**: *Tuna kina mama karibu 20 wa Kiluo ambao tumeolewa kwa Wamaragoli. Tumesambaa katika maeneo mbalimbali na kwa muda mrefu tumekuwa na mikutano ya Merry-go-round ingawa imepungua kwa sababu ya kuzeeka. Tulikuwa na shida ya kujua Kimaragoli siku za awali lakini sasa tunafahamu. Mimi huwezi kujua ni Mluo kwa sababu naongea Kimaragoli vizuri. Mikutano hii ilitusaidia kujua mila na lugha ya Wamaragoli. Lakini si kina mama wote wanajua kuongea vizuri.* Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni haya yanaonyesha namna ambavyo hata wanawake wa Kiluo walivyofaidika na mikutano ya aina hii katika kujifunza na kuzungumza lugha ya mabwana zao. Hivyo,

mikutano ya aina hii japo ni ya kujengana kiuchumi, kijamii au kidini, ina nafasi kubwa sana katika kujenga umilisi na utendaji wa Kimaragoli miongoni mwa Wamaragoli wenyewe au wageni wanaojifunza Kimaragoli.

Watafitiwa 52 (59.8%) katika kundi la makamo na wazee walikubali kwamba lugha ya Kimaragoli imedumishwa katika eneo hili kutokana na mikutano mbalimbali. Mikutano hii inajumuisha vyama vya kina mama, vyama vya wakulima, mikutano ya kikanisa (*Vidieri*-ibada ya wiki za nyumbani), mikutano ya kupanga sherehe maalumu, mikutano ya kisiasa, mikutano ya Halmashauri ya Wazee na kadhalika. Kwa kuwa wazee hawa wamezoea Kimaragoli, ni rahisi wao kuizungumza na hivyo kuiendeleza. Uchunzaji wetu ulithibitisha takwimu hizi kwani wazee waliochunguzwa walikuwa wanaongea Kimaragoli. Uchunzaji ulizingatia mkutano wa wakulima wa *One Acre Fund* uliofanyika kando ya kanisa la Bware na mkutano wa Utamaduni wa Wamaragoli uliotendeka katika shule ya msingi ya Mukuyu. Aidha, katika kujibu swali lililotaka kujua mahali walikojifunzia Kimaragoli, 1% walikiri kujifunza katika mikutano. Hii inaonyesha kwamba watafitiwa wanapokutana katika shughuli mbalimbali za mikutano, wao hutumia Kimaragoli na pia ni njia ya kujifunza maneno kadhaa ya Kimaragoli. Katika mahojiano na vijana, mmoja wao alikiri kwamba anazungumza Kimaragoli na wakulima kila anapoenda nyanjani:

> **K3**: *Ah, ninyoye kagasi ku mu Acre Fund, kutumikira tsyosi kwagani na Vavoo, komoroma Rovo, kwagani nu Murogori, komoroma Llogori. [Ah, nikipata kazi katika Acre Fund, tunatumia zote; tukikutana na Waluo, tunazungumza Kiluo, tukiwa na Mmaragoli, tunazungunza Kimaragoli. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Mbali na mikutano hii, mtafiti pia alikusanya data kutoka kwa watafitiwa kuhusu matumizi ya Kimaragoli katika mikutano ya kiutawala, hasa mikutano ya machifu na manaibu wao. Hii ilikuwa muhimu kutokana na wazo kwamba utawala huwa na mchango muhimu katika kusaidia kushadidia ajenda ya kijamii, na katika muktadha huu,

kutunza amana ya lugha ya Kimaragoli. Matokeo yamewasilishwa kutegemea makundi mbalimbali.

Matumizi ya Kimaragoli katika mikutano ya machifu iliungwa mkono na watafitiwa 24 (32%) katika kundi la kiumri la miaka 12-17, 10 (12.2%) walio na miaka kati ya 18-35 na 20 (23%). Kuwepo kwa asilimia ya chini hivi kunamaanisha kwamba mikutano hii imekuwa nadra sana pamoja na kwamba machifu wa Kimaragoli wanatumia Kiswahili sana kutekeleza majukumu yao. Katika mahojiano na Mzee 1, alisema kwamba siku za awali katika ujio wao hapa Migori, walipewa ardhi waliyojitawala wenyewe. Hivyo, walikuwa na machifu wa Kimaragoli kama vile marehemu Jumba waliokuwa na nguvu nyingi sana nyakati zao za kale na walikuwa wanatumia Kimaragoli kuendesha mikutano ya baraza. Aidha, mahojiano ya Mtafiti Msaidizi na vijana ilikuwa wazi kwamba Kiswahili kimechukua nafasi ya Kimaragoli.

> K2: *Machifu madiku gano vatumirika Ruswahili sana. Ndatsya ku mu. Fwana madikugakavita yago. [Machifu siku hizi wanatumia Kiswahili sana. Nimewahi kuhudhuria. Pengine walitumia siku za kitambo. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hii inaonyesha kwamba Kiswahili kimechukua nafasi ya Kimaragoli katika muktadha wa mikutano ya machifu. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu, kundi linapopewa nafasi ya kujitawala hujivunia mno na huonyesha fahari kwa kutumia lugha asilia kuendesha shughuli zao. Panapotokea hali ya kuingiliwa na lugha nyingine, basi huanza kuyumba na mwishowe kupotea katika matumizi mahsusi. Hii ina maana kwamba Kimaragoli kutotumika katika mikutano ya kiutawala kama hii kunamaanisha upo uwezekano wa kukosa kupewa kipaumbele katika udumishwaji wake.

Hata hivyo, mikutano hii imepungua kutokana na watu kutoizingatia na pia kuwepo kwa mabadiliko katika mfumo wa kiutawala ambapo Mwakilishi Wadi anaonekana kuwa na

ushawishi zaidi kuliko Chifu na manaibu wake. Mikutano mingi ya machifu inapuuzwa na inapohudhuriwa na wachache, lugha amilifu ni Kiswahili. Hii ni kwa sababu baada ya kipindi kirefu cha Wamaragoli kuishi peke yao, walianza kuuza mashamba yao kwa jamii nyinginezo na kusababisha mseto wa jamii katika baadhi ya Kata ndogo. Kutokana na mahojiano na vijana, walikiri kwamba mikutano hii japo ingalipo, Kiswahili kinatumika zaidi.

Hii inathibitisha kwamba Kimaragoli kilikuwa na nafasi kubwa katika mikutano ya Chifu siku za kitambo. Kama tulivyoeleza awali, Wamaragoli walikuwa wanajitawala kiasi cha kuwa na viongozi wao hadi kiwango cha machifu. Hata hivyo, kuingiliwa na jamii ya Waluo katika mazingira yao kulibadilisha hali maana kulilazimu machifu hawa kutumia Kiswahili kuwasiliana na watu. Mbali na Waluo, Wakisii, Wakisa, Wasomali na makabila mengine pia yalikuwa yanahudhiria mikutano hii.

Kwa mujibu wa nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu, mfumo wa kijamii una nguvu kubwa katika kudumisha lugha au hata kuididimiza. Hivyo, kuwepo mabadiliko katika mfumo wa kiutawala kunaonekana kuathiri mno matumizi ya Kimaragoli katika mikutano ya machifu na hivyo kughafilisha mkakati huu kiasi kwamba unaonekana kupoteza nguvu kiuamilifu. Hata hivyo, kama alivyokiri mzee mmoja, Wamaragoli walipopewa uwezo wa kujisimamia miaka ya 1940, walianza kuwa na machifu wao kama vile marehemu Jumba na hao walisaidia mno kuvumisha na kuendeleza Kimaragoli kwa kuwa waliendeleza mikutano yao kwa lugha hiyo.

Matokeo katika makundi haya yote yanaonyesha jinsi ambavyo mikutano mbalimbali imekuwa amilifu katika kudumisha Kimaragoli tangu miaka ya kale. Matokeo ya utafiti huu yanalandana na utafiti walioufanya Okpanachi na Abuh (2017) kuwa kadiri

wasemaji wa Igala, Bassa-Nge na Bassa-Komo walivyotumia lugha hizi katika mikutano yao, ndivyo walivyozisaidia kudumishwa. Mikutano hii aghalabu huleta wasemaji wa lugha moja pamoja na hii huimarisha uwezo wa mtandao wa wasemaji wake kukaribiana na kudumisha lugha yao. Nadharia ya Mtagusano lugha inatilia mkazo wazo hili kwa kudai kwamba kadiri mfumo wa wasemaji lugha unavyokuwa na nguvu, ndivyo uwezo wao wa kutumia na kudumisha lugha yao unaimarika. Aidha, kulingana na nadharia ya Uzalishaji Kijamii, wasemaji lugha wanapokuja pamoja kwa ajili ya mahusiano kama haya, wao hujikuta wanafaridhika kutumia lugha yao na hivyo kuisaidia kudumishwa.

### 4.3.6 Kutembeleana miongoni mwa Wamaragoli

Huu ni mkakati ambao wataalamu mbalimbali walipendekeza kuwa na manufaa katika juhudi za kudumisha lugha. Mtafiti hivyo alitaka kujua ikiwa Wamaragoli wamekuwa wakitumia mkakati huu kuendeleza lugha yao. Mkakati huu ulikuwa na wastani wa 110 (44.2%). Matokeo katika kila kundi yamejadiliwa kwa kina.

Watoto 33 (44%) walikubali kwamba kutembeleana ni njia mojawapo ya kudumisha Kimaragoli. Kutembeleana huku hata hivyo hakukuwa tu kati ya Wamaragoli wa Kaunti ya Migori na Kaunti ya Vihiga bali kutembeleana ndani ya kaunti ya Migori pia. Sababu kubwa ya mkakati huu kuwa na watoto 33 pekee ni kwa sababu wengi walipoulizwa kama wana watu wanaojua katika Kaunti ya Vihiga, wengi walisema wanasikia tu maeneo ya “Umaragolini” lakini hawajui ni wapi. Wengi wa waliozaliwa katika kiwango hiki cha umri hawajafika katika Kaunti ya Vihiga ambako wasemaji wengi wa Kimaragoli wanaishi. Katika mahojiano na mama mmoja, alikiri kuwa:

> **Nyanya*1*:** *Kare kwadzitsa kogendela vandu vitu yengo. Navutswa vanyingi vakudza na vaana vivurwa inyima si vakumanyi mba. Kandi varora ndi, kutsiyi kuvagendela, kuhima mirimi gyavo. [Kitambo tulikuwa tunaenda kuwatembelea nyumbani.Lakini wengi wameshakufa na waliozaliwa baadaye hawatujui. Tena*

*wanasema kwamba tukienda kuwatembelea, tunalenga kuchukua mashamba waliyorithi. TY]* *(Chanzo: Data ya nyanjani)*

Majibu ya mahojiano haya yanaonyesha kwamba mkakati wa kutembeleana ulikuwa unatumika miaka ya kale ila baada ya vizazi vya kwanza kuaga katika pande zote, mkakati huu ulipungua sana. Hii ndiyo sababu watoto kati ya miaka 12-17 hawatembelei ukoo wao maeneo ya Vihiga.

Watafitiwa 33 (40.2%) miongoni mwa vijana kati ya miaka 18-35 walikubali kuwa mkakati wa kutembeleana ni muhimu katika kudumisha lugha yao. Sababu ya kuwa na asilimia ya chini ni kwa sababu wengi wa wazazi wao walishaaga au kuzeeka na hawajui watu wa ukoo wao waliosalia maeneo ya Vihiga. Hata hivyo, walikubali kwamba wao hutembeleana wao kwa wao katika Kaunti ya Migori kwa kuwa huku ndiko wasemaji wenzao wa Kimaragoli wanaishi au wamesoma pamoja.

Utafiti ulibaini kwamba ni watafitiwa 44 (50.6%) katika kundi la makamo na wazee walioushabikia mkakati huu. Mahojiano na wazee mbalimbali yalielekea kuhitimisha kwamba mkakati huu pia umeanza kupoteza nguvu kwa kutokana na vifo vya vizazi vya kwanza na vya pili vilivyohamia maeneo haya miaka ya 1940. Wazee walioshiriki katika utafiti huu walikiri kuhamia maeneo haya na wazazi wao wakiwa kati ya miaka 7-10. Wazee hawa walizidi kutembeleana na watu wao waliosalia Vihiga, Emuhanda, Ilinya na maeneo mengine, na kila walipoenda, waliandamana na baadhi ya watoto. Hata hivyo, wengi walianza kuaga na watoto wao walipokomaa na kuoa, safari hizi zilianza kupungua. Hii ndiyo sababu mama mmoja alipoulizwa ikiwa anaenda nyumbani kwao Vihiga alijibu:

***Nyanya 2**: Hii, kuzitsa kogendayo navutswa rigari mba. [Ndio, tunaenda kutembea huko lakini sio sana]* *(Chanzo: Data ya nyanjani)*

Alipoulizwa ikiwa amewahi kuwapeleka wajukuu wake maeneo ya Vihiga, alisema kwamba hajawahi. Ilikuwa ajabu baadhi ya watoto wake (walio na miaka zaidi ya 30) vilevile walikuwa hawajapelekwa kutembelea watu wao wa ukoo. Hii ina maana kizazi cha sasa cha watoto na vijana hakijui ukoo wao pamoja na kwamba wameanza kuathirika katika kiwango cha uzungumzaji wa Kimaragoli kama itakavyojadiliwa baadaye katika tasnifu hii. Hata hivyo, mmoja wa vijana alisema kwamba matembezi yake Mkoa wa Magharibi ambako ndiko wanaishi Wamaragoli kunatokana na shughuli za Kanisa la Friends.

> **K3:** *Mimi naweza kusema juzi mwezi wa nane nilienda Kakamega kwa kanisa. Kanisa la Friends lilibeba watu wote Wamaragoli. Hata mchungaji mkuu alizungumza Kimaragoli tu.*
>
> **K1**: *Hata nyanya yangu wa Jeshi la Wokovu walikuwa na wageni kutoka Mbale. Ingawa mimi sijawahi kuenda kule na sijui ni wapi lakini inasaidia kwa sababu watu wanaongea Kimaragoli kutoka maeneo mbalimbali.* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli za K1 wa K3 zinathibitisha kutembeleana kati ya Wamaragoli kunasaidia kudumisha Kimaragoli na pia kunasaidia kuinua kiwango cha uzungumzaji kwa wale wanaoishi Uriri na Migori kwa ujumla.

Matokeo haya yanalandana na ya Hildebrandt (2004), Nonaka (2009), Ehala (2010) na Sallabank (2010) waliodai kuwa kadiri wasemaji wanavyozidi kuwa pamoja katika mtandao wa kijamii, ndivyo wanazidi kudumisha lugha yao. Mawazo haya ya kutembeleana na kudumisha mitandao ya mahusiano yanatomelewa na nadharia ya Mtagusano lugha. Hii ina maana kwamba kutembeleana miongoni mwa wasemajilugha ni tendo la kufanya mtandao wao kuwa dhabiti na hivyo kuifanya lugha izidi kutumika katika miktadha mbalimbali. Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano Lugha, kadiri mtandao unavyokuwa dhabiti, ndivyo wasemaji wake wanajikinga dhidi ya kupoteza

lugha yao. Njia bora ya kufanya mitandao ya Wamaragoli kuwa dhabiti ni kupitia kwa kutembeleana wao kwa wao au watu wa ukoo walioko Kaunti ya Vihiga au Kaunti ya Migori

### 4.3.7 Sherehe za kitamaduni

Utafiti huu ulitaka kujua ikiwa sherehe za kitamaduni zilikuwa mkakati mojawapo wa kudumisha Kimaragoli. Matokeo ya kijumla yalionyesha kwamba watafitiwa 133 (54.7%) walikiri mkakati huu kuwa amilifu katika udumishaji wa lugha ya Kimaragoli. Matokeo mahsusi yamejadiliwa kwa kina.

Watoto 26 (34.7%) walikubaliana na kauli kwamba ni mkakati unaotumika kudumisha Kimaragoli. Hii ilijumuisha sherehe kama vile tohara, ndoa na ubatizo miongoni mwa mikutano mingine. Matokeo haya yanathibitishwa na data ya uchunzaji ambapo mtafiti alihudhuria sherehe ya tohara na utoaji wa jina kwa rika lililotahiriwa mwaka wa 2017. Kwa kuwa sherehe hii hufanyika mara moja baada ya miaka 8 au 10 katika maeneo yote palipo na wasemaji wa Kimaragoli, eneobunge la Uriri na Kaunti nzima ya Migori haikusazwa. Waliandaa sherehe hizi katika Shule ya Msingi ya Mukuyu.

Katika sherehe hii, mtafiti alishuhudia watoto hawa pamoja na jamii zao wakiimba nyimbo za Kimaragoli mbali na kuongea Kimaragoli. Katika sherehe hii vilevile, walifundishwa mila za Kimaragoli katika Kimaragoli. Hata hivyo, sababu za kuwa na asilimia ndogo ni kuwa sherehe hii ni tukio la nadra na la kipindi kifupi na pia katika umri huu mdogo, watoto hawajatambua turathi na thamani zilizomo katika sherehe za kitamaduni.

Kulingana na watafitiwa katika kundi la miaka 18-35, 40 (48.8%) walikubaliana na kauli kwamba utamaduni, sherehe za tohara na mila za Kimaragoli zimechangia udumishaji wa Kimaragoli tangu siku za kale hadi sasa. Baadhi ya watafitiwa wa kiume ambao walikuwa na watoto wa kiume waliotahiriwa mwaka wa 2017 walisisitiza kwamba watoto wao lazima wapashwe tohara na kufundishwa mila zinazostahili kwa mtoto Mmaragoli wa kiume. Hii ndiyo sababu, baadhi ya waliohudhuria tamasha za utoaji wa jina kwa rika lililotahiriwa mwaka wa 2017 walikuwa wazazi katika kundi hili la kiumri. Kama ilivyotajwa hapo awali, mkakati wa sherehe, mila na utamaduni ni muhimu sana katika kuendeleza lugha maana ni katika hafla kama hizi masuala ya kale hufundishwa na kukumbusha kizazi ambacho kimeingia katika rika la "ukomavu". Baadhi ya mila zilizotajwa kuwa muhimu pia zilikuwa makumbusho ya wafu, hasa yanayohusu Wamaragoli peke yake na ubatizaji wa watoto wachanga. Mtafiti na msaidizi walihudhuria mojawapo ya sherehe ya ujinaishaji na ubatizaji wa mtoto chini ya kanisa la Jeshi la Wokovu na kutambua kwamba licha ya kuwepo wageni waalikwa wa Kiluo, wenyeji walitumia Kimaragoli kuendeleza hafla hii japo kwa kuchanganya na Kiswahili. Kiluo hakikutumika. Sababu kubwa pia ilikuwa wageni hawa wa Kiluo wanaongea Kimaragoli au wanakielewa.

Jumla ya watafitiwa 70 (80.5%) katika kundi la makamo na wazee walikubali kwamba matumizi ya Kimaragoli katika sherehe za tohara na mila za Kimaragoli inasaidia kuidumisha. Takwimu hizi zinatomelewa na data ya uchunzaji ambayo mtafiti alikusanya nyanjani wakati wa sherehe kubwa ya Utamaduni wa Maragoli iliyofanyika katika shule ya msingi ya Mukuyu. Katika sherehe hii, mtafiti alitambua kwamba: kwanza, watoto na jamii nzima ya Wamaragoli walikongamana na kufundishwa mila za Kimaragoli kuanzia miaka ya 1700. Mtafiti alirekodi mzee mmoja ambaye ni mwanahalmashauri ya Baraza la Waluhya Migori akisoma historia ya Wamaragoli katika Kimaragoli. Pili, mtafiti

alishuhudia wazee wakipewa nafasi ya kufundisha waliohudhuria vifaa na zana za kale zilizotumika katika upanzi, ufugaji wa ngo'mbe, matibabu na kadhalika.

Kulingana na mahojiano na vijana, mmoja wao alikiri kwamba sherehe hizi za tohara zimekuwa na nafasi kubwa katika kudumisha Kimaragoli.

> **K3**: *Mikutano gya utamaduni kuri kekevo chakavita, mikutano gye ibaraza kandi. Ma kandi koveye ku nu mkutano gwa vasukuru vatsitsamu ingereka Bware. Wa Baba Cynthia matsitsa*. *[Mikutano ya utamaduni kama vile tohara hii ambayo imekwisha, mikutano ya baraza na pia mikutano ya wazee huko ng'ambo ya Bware ambako Baba Cynthia huhudhuria.]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Sherehe hii inatiliwa mkazo na nadharia za Mtagusano lugha na Uhuishaji Kiethnoisimu zinazodai kuwa kadiri wasemaji wa lugha wanavyokuja pamoja, ndivyo wanafundishana lugha yao na ndivyo wanaidumisha katika maeneo lugha mbalimbali. Vilevile, nadharia ya Uzalishaji Kijamii inatomelea mawazo ya nadharia hizi kwa kudai kwamba kila jamii ina mbinu zake za kurithisha vizazi vya baadaye mila na desturi zake.

### 4.3.8 Watoto kufundishwa Kimaragoli shuleni

Ufundishaji wa Kimaragoli shuleni ni mkakati ambao ulitumika kwa muda mrefu hadi mwishoni mwa miaka ya 1990. Na hata kabla ya hapo, serikali ya Kikoloni ilikuwa ikitumia Kimaragoli kama lugha ya kufundishia. Hata hivyo, miaka ya baada ya 1990, Wizara ya elimu iliamua kutotilia maanani ufundishaji wa lugha asilia katika mtaala wa shule za msingi. Hivyo, mtafiti alitaka kujua iwapo mkakati huu ulikuwa na umuhimu au nafasi katika kudumisha Kimaragoli kwa watoto, hasa wale waliosoma kipindi cha mwishoni mwa miaka ya 1990. Mkakati huu ulikuwa na wastani wa 3.1%.

Miongoni mwa watafitiwa kati ya miaka 12-17, hakuna aliyetaja mkakati huu. Hii ni kwa sababu hautumiki tena shuleni. Watafitiwa 3 (3.6%) wa miaka kati ya 18-35 walikubali

kwamba ufundishaji wa Kimaragoli shuleni ulikuwa ukisaidia kudumisha lugha ya Kimaragoli. Watafitiwa katika kundi hili (hasa walioolewa) walikubali kwamba walikuwa wanafundishwa Kimaragoli shuleni lakini hali si hiyo tena kwa kuwa mradi wa TUSOME umechukua nafasi yake. Kutilia mkazo takwimu hizi, mzee 2 alidai kwamba:

> **Mzee M***: Vakitangira hee... Umanyi hee, vakitangira venyaa ndio. Vandu venya vahiri vaana vavo mu tsisukuru zyavo. Vavoo vahira vaana mu tsyavo, na Varogoori valla ndi, kari kuyi kokore ndio. Kari administration na supervisors wa masomo, vatura evorogori. Ku mihigya gyene yigyo, vavoo vatanga kuzaa mu tsisukuru zya varogori, na vivuli na vigidzi valaa ndi kunyara kuvakunga dave. Ku rigyiza Llogori mu tsiskuru zindala zyatanga kureka kwigiza LLogori. Valaa ndi,Kulazimisha Vavoo kwiga Llogori,variruka vazyee mu tsiskull zindii. [Wakianza, walitaka hivyo. Watu walikuwa wanapeleka watoto wao kwa shule zao. Mluo alipeleka mtoto wake kwa shule ya Kiluo na Mmaragoli kwa shule ya Kimaragoli. Wasimamizi na wakaguzi wa shule za Kimaragoli walikuwa wanatoka Umaragolini. Lakini miaka ya baadaye, Waluo walianza kuleta watoto wao katika shule za Kimaragoli, na hivyo wazazi na walimu wakaona ni vyema ikiwa watawakumbatia. Hivyo kufundisha Kimaragoli katika baadhi ya shule hiz kulisitishwa. Waliona kwamba wakiwalazimishia Waluo kujifundisha Kimaragoli shuleni wangetoroka waende katika shule nyinginezo. TY]*
>
> (Chanzo:Dataya nyanjani)

Kauli hii inaonyesha kwamba lugha ya Kimaragoli ilikuwa ikifundishwa lakini baada ya wanafunzi wa jamii nyinginezo kupewa nafasi za kusoma, walilazimika kukomesha kukifunza. Miaka hii ya awali, wanafunzi walifundishwa kuimba, kucheza, kusimulia hadithi na kufanya mambo mengi kwa lugha ya Kimaragoli.

Kwa upande mwingine, watafitiwa 5 (5.7%) kati ya miaka 35 na zaidi walikiri kwamba mkakati huu japo hautumiki tena, ulikuwa muhimu sana nyakati zao walipohamia maeneo haya ya Migori wakiwa na wazazi wao. Kama tulivyonukuu Mzee M, walimu walikuwa wakitoka Mkoa wa Kakamega Mashariki kuja kufundisha katika shule za Wamaragoli maeneo haya. Pamoja na hayo, wakaguzi na wasimamizi wa elimu walitoka maeneo ya Kakamega pia. Aidha, misururu ya vitabu viliyotumika kufundisha Kimaragoli vilitoka maeneo ya Vihiga, kipindi hicho cha miaka ya 1950, kukiitwa Wilaya ya Kakamega.

Ingawa mkakati huu kama alivyodai Romaine (2002) huenda hauna faida kubwa, utafiti huu unathibitisha kwamba Kimaragoli kilidumishwa na hata kusambazwa kwa wasemaji wa Kiluo kupitia mfumo wa elimu. Huenda haukuwa ndani ya darasa bali kupitia michezo na nje ya mazingira ya darasa kama walivyokiri wazungumzaji wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli. Mazingira ya shule yalisaidia Waluo kujifunza Kimaragoli ila kwa watoto wa Kimaragoli wa wakati huo, walifaidika pakubwa maana walifundishwa kusoma, kuimba, kukariri hadithi, methali, vitendawili na kuandika kwa Kimaragoli. Kizazi cha sasa japo kinajua Kimaragoli kwa kiwango kidogo, wengi wao huenda wakawa na tatizo la kukisoma au kukiandika.

Ili mkakati huu uwe na tija, wataalamu kama vile McIvor (2009) na Romaine (2002) wanashikilia kwamba lazima serikali au taasisi za kielimu zitilie mkazo maandalizi ya walimu pamoja na matini za kufundishia ili uwe na ufanisi. Wanakubali kwamba mkakati huu ni bora katika kufundisha watoto wadogo kwa kuwa wanapozidi kukomaa, wana uwezo wa kuendeleza lugha yao. Wazo hili linaendana na mhimili wa nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu unaoshikilia kwamba lazima pawepo na uwekezaji wa kitaasisi ili lugha iweze kudumishwa. Ehala (2010) anapodadavua nadharia hii, anashikilia kwamba lugha ya wachache inapopewa kipaumbele katika uchapishaji wa vitabu na kuvitumia katika mfumo wa elimu, basi huchapuza udumishaji wake. Hivyo, huu ni mkakati ambao wizara ya elimu nchini Kenya inastahili kutilia mkazo na kuhakikisha ufundishaji wa lugha asili unarejeshwa tena nchini kwa kuwa utasaidia kuimarisha lugha za kiasilia.

### 4.3.9 Siasa na Utawala

Siasa na utawala ni vipengele viwili vidogo ambavyo vina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya lugha. Watafitiwa miongoni mwa makamo na wazee walipoulizwa wataje

mikakati mingine inayotumiwa kudumisha Kimaragoli, 58 (70.7%) walisema kwamba siasa ina mchango mkubwa. Wazee waliohojiwa walisema kwamba tangu enzi za marehemu Chifu Otieno, Wamaragoli walijiona wenye fanaka kubwa kwa sababu walikuwa na uhuru mkubwa wa kujitawala. Miaka mingi baada ya wao kusambaa katika maeneo ya Kanyamkago na maeneobunge mengine, walianza kupata machifu wa Kimaragoli ambao waliendeleza matakwa, mahitaji na utamaduni wa Kimaragoli. Aidha, wanasiasa wa Kimaragoli walianza kujitokeza kuwania ubunge ingawa hawakufanikiwa. Ugatuzi ulipozinduliwa nchini Kenya mwaka wa 2013, wasemaji wa Kimaragoli walikuwa miongoni mwa wale walioteuliwa kushikilia nyadhifa za utawala katika Kaunti ya Migori. Kwa kuwa Wamaragoli wameongezeka katika idadi ya wapiga kura kiasi cha wao kutambuliwa na wanasiasa wa makabila mengine, imekuwa wazi kwamba uwezo wao wa kuamua au kuchangia siasa za Kaunti ya Migori umeimarika. Na hii ndiyo sababu Gavana wa Migori ameteua baadhi yao katika utawala wa kaunti.

Kulingana na Muandike (2011) nadharia ya Uhuishaji wa Kiethnoisimu inashikilia kwamba katika kipindi fulani cha kihistoria, jamiilugha huja pamoja na kutafuta namna ya kuwa uhuru au kujitawala kwa lengo la kutunza maslahi yao kama vile utamaduni, hadhi na lugha. Hii ndiyo sababu kubwa ambayo Wamaragoli walipokuja Migori mara ya kwanza, walipewa eneo lao, wakawa na machifu wao na sasa wana viongozi katika utawala wa Kaunti ya Migori. Hii inainua hadhi ya lugha na hivyo kuifanya kudumishwa. Kutokana na mahojiano na baadhi ya watafitiwa, Wamaragoli walitaka eneobunge lao ili wawe na mbunge lakini walionywa kwamba ilikuwa mojawapo ya mbinu ya kuendeleza ukabila na kujitenga kikabila; ilikuwa kinyume na juhudi za kutangamanisha wanajamii.

### 4.3.10 Ndoa baina ya Wamaragoli na Waluo

Ndoa ni kijipengele muhimu ambacho kimezungumziwa na wataalamu kama vile Jagodic (2011), Sevinc (2016) na Wei (1994). Wanadai kina mchango mkubwa katika kudumisha lugha au kuhamia lugha nyingine katika mazingira ya wingilugha. Katika utafiti huu, ilibainika kwamba kuna kina mama wengi wenye asili ya Kiluo ambao wameolewa katika jamii ya Wamaragoli na wamelazimika kujifunza Kimaragoli. Mtafiti alipouliza wapi watafitiwa walijifunzia Kimaragoli, 2 (2.2%) walidai kujifunza Kimaragoli walipoolewa kwa Wamaragoli. Aidha, katika kundi la vijana, mtafitiwa mmoja wa kike mwenye umri wa miaka 34 alidai kuwa alijifunza lugha hii alipoolewa kwa Mmaragoli. Hoja hii inatomelewa na matokeo ya mahojiano kati ya mtafiti na mama 1 aliyedai kuwa:

> **Nyanya 2**: *Mkana natsiyi kodeka ku musatsa na sivamoroma L'limi l'lara dave, mukana amanya yiga L'limi rwu musatsa. Ku uma onyora yenya avugulwi kuri mundu wahango, anyara kukora vindu kuri vandu va hango hene yaho.[Msichana akienda kuolewa kwa mwanamume ambaye hawaongei lugha moja, msichana huyo hulazimika kujifunza lugha ya bwana. Hivyo yeye hutaka achukuliwe kama mwenyeji, na sehemu ya boma lao, anayeweza kufanya mambo kama watu waboma hilo. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na mahojiano haya, ni bayana ndoa kati ya Wamaragoli-Waluo zinachangia udumishaji lugha. Matokeo haya yanakinzana na ya Igboanusi na Wolf (2010) kuhusu ndoa kuchangia kuhamia kwa lugha nyingine.

## 4.4 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Makundi ya Wamaragoli


Utafiti huu pia ulitathmini umilisi wa Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake. Ili kutathmini kiwango cha umilisi, kwanza mtafiti aliuliza watafitiwa, kutegemea kiwango cha umri, waeleze kiwango chao cha uzungumzaji wa Kimaragoli; pili, aliuliza ikiwa kuna mambo ambayo wao hupata tatizo kueleza au kufanya katika Kimaragoli na tatu,

waliokuwa na shida ya kujieleza, wataje mambo yanayowashinda. Majibu yao yamejadiliwa kutegemea viwango vya umri.

### 4.4.1 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Watoto wa miaka 12-17

Watafitiwa wa miaka 12-17 walipoulizwa waeleze kiwango wanachozungumza Kimaragoli, 36.8% walisema kiwango chao ni kizuri sana, 54% wakasema kizuri, 6.6% walisema ni kizuri kidogo huku 2.6% wakisema ni kibaya. Kielelezo 4.1 kinawasilisha matokeo haya:

**Kielelezo 4.1: Umilisi na Utendaji miongoni mwa watoto**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na takwimu hizi, ni wazi kwamba watoto wanaozungumza Kimaragoli katika eneobunge la Uriri, wana viwango vizuri vya umilisi. Hii ni jumla ya watoto 70 (93.3%) ambao walikiri kwamba kiwango chao ni "kizuri sana" na "ni kizuri". Ili kuthibitisha takwimu hizi, mtafiti alihoji watafitiwa ikiwa kuna mambo ambayo yanawashinda kufanya katika lugha hii. Watafitiwa 45 (60%) walisema kwamba hawana tatizo la kujieleza katika Kimaragoli kuhusiana na masuala mbalimbali, 30 (40%) walisema wana matatizo katika baadhi ya masuala. Baadhi ya mambo waliyotaja kuwa magumu

kujieleza yalijumuisha: istilahi za ukoo; aina za pesa ambazo shule huhitaji kwa mfano majina ya pesa za matanga na pesa za karo; kusoma na kuomba kwa Kimaragoli; aina ya wadudu; vitu vya kiturathi; aina za vyungu; mila za jandoni; maombolezo; mapambo na fasihi. Sababu walizotoa kuelezea kutindikiwa huku zilikuwa ni kuzoea Sheng, uchanganyaji wa ndimi, Kimaragoli ni kigumu na wengine wakasema wao ni wazawa wa Kiluo japo mama mzazi ni Mmaragoli. Sababu hizi zinatomelewa na hoja zilizojitokeza katika mahojiano na mzee 1 na 2 kwamba:

> **Mzee M**: *Madiku gandi vana vang'ele vitu vavora ndi Llogoro nu rudinyu kuvita Rovoo. Icho kigira nonyora ndi vigaa Rovoo kutanga ma Llogori. Vavora ndi, Llogori roveza na mang'ana madinyu.[Siku zingine watoto wetu wanasema kwamba Kimaragoli ni kigumu kuliko Kiluo. Hii ndio sababu wanajifunza Kiluo kisha Kimaragoli. Wanasema kwamba katika Kimaragoli, kuna baadhi ya maneno ambayo ni magumu. TY]*
>
> **Mzee M:** *Kunarilla Ruswahili sana ruvarombaa vava nu vudinyu komoroma Llogori. Ku vaduka havundu vagadahara. Kuri vaana vamenyi mu town, rwavaza kumenya mmadara yinu,vaveza vamanyi Llogori dave, ku nave ni mihiga gyanga ndi, irwo rwahula Llogori kutanga. Ma naduki mihiga 10 kuzya imbiri, irwo rwatanga kwiga mang'ana gaviri gavage gu Llogori. [Kuzoea Kiswahili sana kunawafanya wao kuwa na tatizo la kumiliki Kimaragoli. Kwa hivyo,wanafika mahali wanazembea kujifunza zaidi. Kwa mfano, watoto wanaoishi mjini, wanapokuja kuishi huku vijijini, huwa hawajui Kimaragoli, na ndio wanasikia Kimaragoli kwa mara ya kwanza. Akifika miaka karibu 10 na zaidi, ndio anaanza kujifunza maneno mawili au matatu kwa Kimaragoli. TY]*
>
> (Chanzo: Data ya Mtafiti)

Kutokana na mahojiano haya, ni wazi kwamba watoto 7 (9.3%) waliokosa umilisi wa Kimaragoli wanakumbana na tatizo la mielekeo hasi kuhusu lugha yao au ya mmoja wa wazazi wao. Vilevile, ukosefu wa umilisi wao unatokana na sababu kwamba baadhi ya wazazi wao hawawafundishi Kimaragoli wanapokuwa wachanga.

Data ya uchunzaji vilevile ilionyesha kwamba watoto wa shule za msingi kila walipotoka shuleni, walikuwa wanaongea na kucheza barabarani huku wakiongea Kimaragoli. Aidha, katika kongamano la vijana wa kanisa la Friends la Thim Jope lililoleta watoto na vijana kutoka Kaunti nzima ya Migori, watoto walikuwa wanaongea Kimaragoli. Katika


sherehe za Utamaduni wa Wamaragoli zilizofanyika katika shule ya msingi ya Mukuyu, watoto waliokuwa wametahiriwa walikuwa wanazungumza na wenzao pamoja na watu wengine kwa Kimaragoli. Hii inaonyesha takwimu zilizotolewa za 93.3% za watoto wanaoongea vizuri sana na wanaoogea vizuri zinatetewa na matokeo ya uchunzaji. Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha asilimia kubwa ya watoto hawa ilithibitisha uwezo mkubwa wa kuamilia na kubwia maneno yanayotosha kiwango chao cha kiakili kiasi cha kuwawezesha kuwasiliana katika miktadha mbalimbali bila kuingiza au kuhamia Kiluo. Hii ina maana kwamba kiwango cha umilisi kinapokuwa cha juu, kinarahisisha uwezo wa wazungumzaji katika miktadha anuwai.

Kwa mujibu wa Verdon, McLeod na Winsler (2014) kwamba siri kubwa ya kudumisha lugha siku za baadaye ni kuhakikisha kwamba watoto wanafundishwa na wanatumia katika siku zao. Vilevile, maoni ya O'Riagain, Williams na Moreno (2008) kwamba umri wa kubaleghe (11-18) ndio nyeti kabisa katika udumishaji au uhamaji lugha yanaibuka kuwa muhimu katika kuhakikisha kwamba kundi hili limefundishwa na kurithishwa Kimaragoli. Katika kipindi hiki, mielekeo huumbwa na kudumishwa na mwishowe huathiri lugha maalumu. Utafiti huu japo utajadili mielekeo baadaye, ni wazi katika mahojiano kwamba kundi hili limeanza kuathirika japo kwa kiwango cha chini wanapozidi kutagusana na Kiluo.

### 4.4.2 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Vijana wa miaka 18-35

Vijana wa miaka 18-35 walipoulizwa kiwango chao cha kimaragoli, 36.6% walisema ni kizuri sana, 52.4% walisema ni kizuri, 7.3% walisema ni kizuri kidogo huku 3.7% wakisema ni kibaya. Takwimu hizi zimewasilishwa katika Kielelezo 4.2

**Kielelezo 4.2: Umilisi na Utendaji miongoni mwa vijana**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kulingana na kielelezo hiki, ni wazi kwamba vijana katika kiwango hiki wana umilisi mkubwa wa kimsingi wa 89%. Mbali na kujua kiwango cha umilisi wa kimazungumzo, mtafiti pia alitaka kujua ikiwa watafitiwa katika kundi hili wanaweza kuimba, kusimulia hadithi na kuongea kwa ufasaha kwa Kimaragoli. Watafitiwa 68 (82.9%) walisema wanaweza kufanya hivyo, 14 (17.1%) wakisema wana tatizo katika kuongea, kuimba au kusimulia hadithi kwa Kimaragoli.

Vilevile, mtafiti alitaka kujua ikiwa watafitiwa katika kundi hili walikuwa na masuala mbalimbali ambayo, licha ya kufahamu Kimaragoli kwa kiwango fulani, walikuwa wanashindwa kutenda kwa Kimaragoli. Watafitiwa 58 (70.7%) walisema hawana tatizo lolote kwa sababu wanaweza kufanya mambo yote kwa Kimaragoli bila tatizo huku 24 (29.3%) wakikiri kwamba wanakumbana na changamoto mbalimbali wanapozungumza Kimaragoli. Changamoto walizotoa zilijumuisha kutojua kusoma kwa Kimaragoli, kuimba, kuomba, kusimulia hadithi, majina ya vitu mbalimbali, dira za dunia, mila, vyakula, matunda na mbari za Wamaragoli. Mmoja wa vijana aliyehusika katika

mahojiano ya mtafiti msaidizi alisema Kimaragoli ni kigumu kwa sababu kina maneno magumu:

> **K3**: *Umanye shida Llogori roveye na mang'ana madinyu mala kari kumanyi mba (wakicheka) [Unajua Kimaragoli kina maneno magumu ambayo hata sisi hatuyajui…TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani*)*

Vilevile, mahojiano na Mchungaji yalionyesha kwamba vijana wana matatizo makubwa katika kujieleza kwa Kimaragoli:

> **Mchungaji**: *Hii vang'ele vaveye nu vudinyu vonene komoroma Llogori, sanasana vavoleywe vimbi marago. Vatitsa sana. [Naam, vijana wana tatizo la kutumia Kimaragoli, hasa wanapoambiwa waimbe nyimbo za Krisimasi. Wanaogopa sana.TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hizi za K3 na Mchungaji zinaonyesha kwamba japo wanakubali wanaweza kuzungumza Kimaragoli, yapo maneno ambayo yanawapa tatizo mno au matumizi katika baadhi ya miktadha inawapa tatizo. Matatizo haya yanatokana na wao kutumia Kiluo au Kiswahili wakati wanashindwa kupata neno mwafaka linalowafiki muktadha wa kueleza dhana fulani. Kwa kuwa hawana muda wa kutosha wa wazee wanaojua maneno mbalimbali katika miktadha mbalimbali, basi vijana wanaishia kudumaza umilisi wao wa Kimaragoli.

Matokeo haya yanashabihiana na utafiti alioufanya Moreno (2008) kuhusu vijana wa Kikatalunya waliojua lugha hii kwa kiwango cha chini na hawangeweza kufanya baadhi ya mambo kama vile kuimba na kusimulia hadithi kwa kutumia lugha hiyo.


Sababu walizotoa kueleza udhaifu huu zilikuwa kama vile kiwango chao cha umilisi pevu ni finyu mno kutokana na kuwa katika mfumo wa shule za kuishi kwa muda mrefu, athari ya Kiswahili na Kiluo katika kujua na kutumia Kimaragoli, hadithi za Kimaragoli kukosa mtindo mzuri wa kimasimulizi. Sababu hizi za kupoteza umilisi pevu wa lugha miongoni mwa vijana zinaenda sambamba na utafiti wa O'Riagain (2008b) kuwa shule na kazi zina mchango mkubwa katika kudidimiza umilisi wa vijana. Waliosema hawana tatizo lolote katika kujieleza kwa Kimaragoli walijitetea kwa kusema Kimaragoli ni

lugha ambayo walizaliwa nayo, hivyo wanaionea fahari, wanaipenda na wanataka kuiendeleza. Pia, wengine wakadai kuwa vizazi vya awali (babu/nyanya na baba/mama zao) vilizungumza, hivyo, faradhi wao kuzungumza Kimaragoli.

### 4.4.3 Umilisi na Utendaji miongoni mwa Makamo na Wazee

Watafitiwa wa miaka 36 na zaidi walipoulizwa waeleze kiwango chao cha Kimaragoli, walikuwa na majibu yafuatayo: 52 (60.4%) walisema ni kizuri sana, 29 (33%) walisema ni kizuri, 4 (4.4%) walisema ni kizuri kidogo na 2 (2.2%) walisema ni kibaya. Takwimu hizi zimewasilishwa katika Kielelezo 4.3.

**Kielelezo 4.3: Umilisi na Utendaji miongoni mwa Makamo na Wazee**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na kielelezo hiki, utafiti ulithibitisha kwamba watafitiwa waliozidi miaka 36 walikuwa na kiwango cha juu kabisa cha umilisi, wakiwa na jumla ya 93.4% ikilinganishwa na makundi ya watoto na ya vijana. Pamoja na hayo, utafiti ulitaka kujua ikiwa kundi hili, licha ya kuwa na umilisi wa juu, liliweza kuimba, kusimulia hadithi na au kueleza mambo mbalimbali katika Kimaragoli. Matokeo yalionyesha kwamba watafitiwa 84 (96.6%) walisema hawana tatizo lolote la kujieleza katika lugha hii. Baadhi yao walisema kwamba wanaweza kusimulia hadithi kama vile za Kibibilia, za

asili ya Mulogoli na za tohara zilizotokea miaka mingi iliyopita. Wengine walisema kwamba wanaweza kuimba nyimbo za injili kwa Kimaragoli, nyimbo za tohara na nyimbo za kitamaduni. Watafitiwa 3 (3.4%) walisema wana matatizo katika kuomba kwa Kimaragoli.

Matokeo ya utafiti huu kwa upande mmoja yanawiana na ya Odero (2013) na Birman na Poff (2011) waliotambua kwamba katika makundi yote ya wasemaji wa Kielmolo na wahamiaji wa nchi za Marekani wazee ndio walikuwa na umilisi mkubwa. Hata hivyo, tofauti na utafiti wao, utafiti huu umetambua kwamba kuna kiwango cha kuridhisha cha umilisi miongoni mwa vijana kutokana na juhudi za wazee hawa kurithisha vijana na watoto wao maarifa ya Kimaragoli waliyo nayo.

Utafiti huu ulitaka kujua kati ya wazee, vijana na watoto, nani wanaongea Kimaragoli vizuri. Watafiti wote 244 (100%) katika makundi yote walikubali kwamba wazee ndio wana umilisi wa kiwango cha juu. Sababu walizotoa zilikuwa ni kuwa wazee ndio magwiji wa lugha na hao ndio hufundisha watu wengine, hao ndio walikuwa kizazi cha pili katika eneo la Uriri hivyo wanafahamu Kimaragoli kwa undani, wazee ndio wataalamu wa utamaduni wa Mmaragoli miongoni mwa sababu nyinginezo. Kwa upande wao, wazee waliwakashifu vijana na watoto kwa kusema kwamba kwanza, kiwango chao cha lugha kiko chini kwa sababu wanachanganya Kiluo, Kiswahili na Kiingereza wanapoongea (yaani, hawana umilisi wa ndani wa lugha moja), pili, vijana hawa wanadharau lugha yao. Sababu hii ya pili aidha ilijitokeza katika mahojiano na mzee 2 aliposema kwamba:

> **Mzee M**: *awaaa, yani hee, richaya! Varora ndi ruvahira havundu da.[Hapana, yaani ni kudharau tu. Wanaona kwamba (Kimaragoli) hakitawapeleka mahali popote. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kuwepo kwa mwelekeo hasi kama huu huenda ndio sababu mojawapo inayowaghafilisha vijana katika kutumia Kimaragoli. Katika mahojiano haya pia, ilikuwa wazi kwamba vijana hata wanapoulizwa waimbe kanisani kwa Kimaragoli siku ya Krisimasi wanapata tatizo na kuwafanya hata wengine kuhepa kuenda kanisani kabisa. Hii ndiyo sababu katika mahojiano na Mzee M alihofu kwamba:

> **Mzee M**: *Hambiri yaha, hafwana hadinyu kidogo. [Kutakuweko na tatizo dogo la udumishaji lugha siku za mbeleni. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani*)*

Dhana ya mielekeo hasi katika umilikaji lugha imezingatiwa mno katika nadharia ya mtagusano lugha. Wazee wanaposema kwamba vijana wadharau lugha yao, tatizo hili huathiri uamiliaji lugha na pia kiwango cha umilisi pevu. Hii ni kwa sababu mwanajamii lugha yeyote anaposema kwamba hakuna mahali lugha yake asilia itamsaidia au kumpeleka, basi inawafanya wazee kuhitimisha kwa kusema kwamba maisha ya baadaye ya lugha hii yatakuwa magumu. Kimsingi, uhai wa Kimaragoli, kama kinavyosemwa sasa, utakuwa hatarini.

## 4.5 Athari ya Kiluo kwa Kimaragoli Uriri

Utafiti huu pia ulithibitisha athari ya lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli. Wataalamu Ralli (2001), Sankoff (2001) na Hoffer (2002) walielekea kukubaliana kwamba kuna athari au matokeo matatu ya mtagusano lugha: Athari ya kifonetiki/kifonolojia; Athari ya kileksimu; athari ya kimofolojia. Thomason (2001) aliongeza ubadilishaji msimbo na uchanganyaji msimbo kama athari ya nne. Aidha, baada ya utafiti awali, utafiti huu uliongezea athari ya Kiluo katika maeneotumizi lugha ya Kimaragoli (ruwaza za matumizi lugha). Utafiti huu haukupata mabadiliko ya kifonetiki/kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika Kimaragoli kutokana na kuingiliwa na Kiluo na hivyo kupinga mawazo ya Nurse na Rottland (1991) na Lotta (2014) kuhusu athari ya lugha za Kinailoti kwa lugha za Kibantu. Hivyo katika uwasilishaji wa matokeo ya athari, vipengele hivi

havijahusishwa. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba ukosefu wa data katika vipengele hivi si suala la kuajabia kutokana na maoni ya wataalamu mbalimbali kuwa baadhi ya mitagusano lugha haizalishi aina hii ya matokeo, hasa lugha ambazo si za mnasaba mmoja. Kwa mfano, Winford (2003) anakiri kwamba wakati mwingine, ukopaji wa fonolojia kutoka lugha ya wengi hadi lugha ya wachache ni tukio nadra sana, ila si kwamba haliwezi kutokea. Maoni haya pamoja na matokeo nunge ya utafiti huu yanatiliwa mkazo na nadharia ya Mtagusano lugha inayodai kwamba tofauti za kitipolojia baina ya lugha zinazotagusana ndizo huchangia lugha kuwa na mabadiliko machache sana. Mabadiliko makubwa yanayoweza kutokea ni ya kimsamiati zaidi kuliko ya kimofolojia (Meillet, 1948 katika Stapert, 2013). Kwa hivyo, kukosekana kwa data kuhusu mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia ni kwa sababu ya kutofautiana kitipolojia kwa miundo ya lugha hizi mbili.

### 4.5.1 Maoni kuhusu Athari za Kiluo kwa Kimaragoli

Ili kubainisha athari za lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli, mtafiti alitafuta maoni ya watafitiwa kwa kuuliza ikiwa wanafikiri Kiluo kimeathiri matumizi yao ya Kimaragoli. Swali hili lilikuwa muhimu kwa sababu lilikuwa kama dira ya kufahamu athari za kijumla kwa watafitiwa binafsi katika kila kundi.

Watafitiwa wa miaka 12-17 walipoulizwa ikiwa Kiluo kimeathiri uzungumzaji wa Kimaragoli, walitoa maoni yafuatayo: 41 (54.6%) walikubaliana na swali ilhali 34 (45.4%) walilipinga. Hii ina maana kwamba kizazi kichanga, ambacho utafiti huu unakiita kizazi cha nne, kimeathirika pakubwa katika uzungumzaji wa Kimaragoli ikilinganishwa na kizazi cha tatu (miaka ya 18-35) na cha pili (miaka 36 na zaidi) kama itakavyobainika baadaye katika mjadala huu.

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, 36 (43.9%) walisema ndio huku 46 (56.1%) wakisema la. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba watafitiwa 43.9% wameathirika katika hali mbalimbali zikiwemo kuchanganya na kuhamisha ndimi, kuongea Kiluo nyumbani na wazazi au ndugu zao japo wao wote ni Wamaragoli. Athari ya kuchanganya ndimi inajitokeza katika miktadha mbalimbali kama vile nyumbani, sokoni/madukani mashambani, wakiwa njiani na shuleni. Mahojiano ya mtafiti msaidizi na vijana watatu yanatomelea hali hii waliposema kwamba:

> **K2:** *Vivuri garondekana. Uranyora kari mama Mluo, vamoromaa Llogori no Rovoo. Voosi vaveye Varogori, Llogori tsa. [Na wazazi, inategemea. Utapata mama Mluo anazungumza Kimaragoli au Kiluo. Wakiwa wote Wamaragoli, wanazungumza Kimaragoli.TY]*
>
> **K2**: *Garondekana. Yengo komoroma Llogori. Koveye mwivugana, komoroma Llogori nu Ruswahiri. Yinzi ningina mpira, paga njanganye na Rovoo. [Inategemea. Nyumbani, sisi tunazungumza Kimaragoli na Kiswahili. Mimi nikicheza kandanda, ninachanganya na Kiluo. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hizi mbili zinashadidia matokeo ya takwimu kwamba hakika vijana wanatumia lugha zote katika mazingira mbalimbali. Hii ni athari kwenye eneomatumizi.

Miongoni mwa makamo na wazee, 87.2% walisema hawajaathirika na Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli huku 12.8% wakikiri kuathirika kimazungumzo. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba umri wa miaka 36 na zaidi wanathamini lugha yao pamoja na kuilinda dhidi ya kuingiliwa na Kiluo. Ni muhimu kufahamu kwamba katika kundi hili, wengi wa watafitiwa ni wale walioishi na wazazi wao kwa muda mrefu bila kutagusana na Waluo. Pamoja na hayo, baadhi yao, walikuja na wazazi wao kutoka maeneo ya Magharibi mwa Kenya ambako walikuwa wamejifunza Kimaragoli. Kwa ujumla, 102 (41.8%) walijibu ndio huku 142 (58.2%) wakipinga kama inavyojitokeza katika jedwali 4.3:

**Jedwali 4.3: Athari Jumla za Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio | 102 | 41.8 |
| La | 142 | 58.2 |
| **Total** | **244** | **100.0** |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kwamba watoto, vijana na wazee 102 (41.8%) wanakiri kuathirika na Kiluo dhidi ya 142 (58.2%) waliokiri kutoathirika kwa namna yoyote ile. Idadi hii ni ya wastani na hivyo kuzua mahitimisho kwamba walioathirika na Kiluo miongioni mwa Wamaragoli ni wengi na huenda wataongezeka zaidi siku za baadaye.

Takwimu hizi zinatomelewa na matokeo ya mahojiano na Mzee 2 na Nyanya 1, walioweka wazi kwamba athari hizi ingawa hazitokei katika kila boma, ni tukio la kawaida katika baadhi ya nyumba za Wamaragoli na mahusiano ya Wamaragoli-Wamaragoli:

Mtafiti: *Na veveye varogori vene ku vene?* [Na wakiwa Wamaragoli kwa Wamaragoli]

> **Mzee M:** *Vene ku vene uranyora vamoroma Llogori, kandi rujaluo. Vala vamoromaaLlogori, na vandi kari onyora vamoromaza Rovoo. Uranyora Mrogori kumrogori amoromaa rovoo. Unyara kari kuhula vamoroma rovoo vaveye hano, vaturaho visundi hambiri, uhula vagirunganyi vamoroma llogori. Nindyo sya vakoraa.[Wenyewe kwa wenyewe utapata wanaongea Kimaragoli na Kiluo. Wengine wanaongea Kimaragoli tu kabisa, na wengine wanaongea Kiluo tu. Utapata Mmaragoli kwa Mmragoli wanaongea tu Kiluo. Utawasikia wakiongea Kiluo wakiwa hapa, wakisonga mbele kidogo, wanabadili ndimi na kuongea Kimaragoli. Hivyo ndivyo wanafanya. TY]*
>
> **Nyanya 2***: Koveye na Varogori vala vamenyi Ombo wamoromaza Rovo. Kari vaveye yengo na Varagori vavo. Kindu kerombatsa umanya hano na hango hu Mrogori ni ryumbaka ryi tsinyumba tsyavo; kigira zifwanana na tsya Vavo dave. Nuwingiraho ma omorome Llogori, varakujiba mu Llogori.[Kuna baadhi ya Wamaragoli ambao wanaishi Ombo wanaongea tu Kiluo, hata wakiwa nyumbani wao kwa wao. Kitu kitakachokufanya utambue ni nyumbani kwa Wamaragoli, ni muundo wa nyumba zao kwa sababu hazifanani na za Waluo. Ukiingiatu hapo na uongee Kimaragoli, watakujibu kwa Kimaragoli. TY]*(Chanzo: Data ya nyanjani)

Mahojiano haya yanaonyesha jinsi ambavyo Kiluo kimeathiri uzungumzaji wa Kimaragoli katika vikundi mbalimbali vya kiumri. Tofauti za viwango zinatokana na sababu kadhaa: kwanza, watoto katika kikundi hiki wamezaliwa katika kipindi ambacho Kiluo kimeingia mno katika maeneotumizi ya Kimaragoli, hivyo wanapokuwa na wazazi, hakuna msisitizo mkubwa katika kusema Kimaragoli. Pili, kuweko kwa uhuru wa utangamano kati yao na Waluo kumesababisha ujifunzaji wa Kiluo kwa kiwango kikubwa na hivyo kuathiri uzungumzaji wa Kimaragoli. Ni muhimu kufahamu kwamba katika mahojiano, wazee walisema mara ya kwanza walipoingia maeneo ya Migori, kulikuweko na sheria kwamba hakuna kutangamana kindoa kati ya Mmaragoli na Mluo. Mapatanao haya yalivunjwa na kizazi cha pili na tatu hivi kwamba ndoa zilizidi kuwa nyingi na mahusiano yakawa huru zaidi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha, kuweko kwa athari hizi kunatokana na kulegea kwa mtandao wa kimahusiano miongoni mwa Wamaragoli. Hii ni kwa sababu kizazi cha kwanza (ambacho kiliaga kati ya miaka ya 1950-1980) kilidumisha lugha yao kwa kuwa hiyo ndiyo waliyoijua peke yake. Kizazi cha pili, ambacho kilikuwa na umri wa chini ya miaka 15 mwaka wa 1940, kingalipo ila wazee wachache ambao ni zaidi ya miaka 80 sasa. Hao walidumisha Kimaragoli kwa kuwa walipewa ardhi yao, ambako hakukuweko na Waluo. Hii ilisaidia kutilia nguvu mtandao wa kijamii. Kizazi cha tatu, ambacho sasa ni kati ya miaka 18-35 kimeshuhudia mabadiliko makubwa kwenye mtandao wao kwa sababu wanasoma na Waluo, wanaishi nao ujirani, wanaona na kufanya shughuli zote kwa pamoja. Hii imedhalilisha mtandao huu na hivyo kusababisha mpenyezo wa Kiluo katika Kimaragoli na maeneotumizi yake. Kizazi cha nne, ambacho ni cha umri wa chini ya miaka 17, ndicho kinaathirika zaidi kwa sababu mtandao huu unazidi kudhoofika.

### 4.5.2 Athari ya Kileksimu

Wataalamu mbalimbali wanakubaliana kwamba athari ya kwanza na ya kimsingi lugha mbili au zaidi zinapotagusana huwa ni kuingizwa kwa maneno mapya kupitia mbinu ya ukopaji na utohozi. Uingizaji huu huanza kufanyika baada ya kipindi kirefu cha mtagusano (Nagy, 1996; 2010) na huhusisha nomino na vitenzi (Poplack na wenzake, 1998) na majina ya vyakula (T'sou, 2001).

Kimaragoli kutagusana na Kiluo kwa muda mrefu (takribani miaka 78) kulisababisha mtafiti kutaka kujua ikiwa kuliweko na maneno ya Kiluo yaliyokopwa na kuingizwa katika Kimaragoli. Ili kupata taswira halisi kuhusu athari ya Kiluo kwa Kimaragoli, watafitiwa waliulizwa ikiwa Kimaragoli wanachozungumza katika kizazi hiki ni kama kizazi cha zamani. Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, 56 (68.3%) walisema Kimaragoli wanachozungumza ni kama cha zamani huku 26 (31.7%) wakisema kina maneno ya Kiluo siku hizi. Kwa ujumla watafitiwa 60.6% wanahisia kwamba Kimaragoli wanachozungumza sasa ni kama cha zamani huku 39.4% wakisema kina maneno ya Kiluo siku hizi. Jedwali 4.4 limewasilisha matokeo haya:

**Jedwali 4.4: Maneno ya Kiluo katika Kimaragoli**

| | **Miaka 12-17** | | **Miaka 18-35** | | **Makamo/Wazee** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Umaratokezi** | **Asilimia** | **Umaratokezi** | **Asilimia** | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
| Ni kama cha zamani | 48 | 64 | 56 | 68.3 | 56 | 64.4 |
| Kina maneno ya Kiluo | 27 | 36 | 26 | 31.7 | 31 | 35.6 |
| **Jumla** | **75** | **100.0** | **82** | **100** | **87** | **100.0** |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, watafitiwa 48 (64%) kati ya miaka 12-17 walikiri Kimaragoli cha sasa ni kama cha zamani huku 27 (36%) wakikiri kina maneno ya Kiluo. Katika kundi la watafitiwa wa miaka 18-35, 56 (68.3%) walikiri kuwa ni kama cha zamani huku 26 (31.7%) wakidai kina maneno ya Kiluo. Watafitiwa 56 (64.4%) katika kundi la

makamo na wazee walikiri kuwa hakuna athari yoyote ya Kiluo kwa Kimaragoli huku 31 (35.6%) wakikubali kuna maneno ya Kiluo katika dafina ya Kimaragoli.

#### 4.5.2.1 Maoni ya watoto kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba 48 (64%) ya watafitiwa wa miaka 12-17 walidai Kimaragoli wanachozungumza ni kama cha zamani huku 27 (36%) wakisema kina maneno ya Kiluo siku hizi. Hii ina maana kwamba watoto wengi katika kikundi hiki hawaamini kuna maneno ya Kiluo yaliyoingizwa katika Kimaragoli. Jedwali 4.5 linaonyesha maneno ambayo baadhi ya wasemaji katika kundi hili walitaja kama mkopo kutoka kwa Kiluo.

**Jedwali 4.5: Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa watoto**

| **Aina ya neno** | **Mifano** | **Tafsiri kwa Kiswahili** | **Kisawe cha Kimaragoli** |
|---|---|---|---|
| Nomino | nyoyo, anyuola, chira, jaber, ong'enge, lang'o, mwalo, | Pure; jamaa/familia; mwiko; binti; seng'enge; Mkalenjin; chini | Mahengere; amitu; miruka;roseng'enge; mkalenjini, kivanda |
| Vitenzi | Bika, wantie, wadhio, | Njoo hapa; tuko; twende; | Hamba; koveye ho,kutsyie |
| Vihisishi | Yawa | jamani | maguu |
| Salamu | Nang'o, oyaore | Vipi; habari za asubuhi | Ndi,vuchee |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hli, ni wazi kwamba watoto wana mifano mingi (7) ya nomino kama maneno ya mkopo kutoka kwa Kiluo hadi kwa Kimaragoli. Hii inaendana na maoni ya wataalamu Poplack na wenzake (1998) na T'sou (2001) wanaosema kuwa nomino ndizo huwa za kwanza na za haraka kukopwa katika mtagusano wa lugha. Nomino ndizo huwa pia nyingi kuliko aina nyingine ya maneno.

#### 4.5.2.2 Maoni ya vijana kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, 56 (68.3%) walisema kwamba Kimaragoli wanachozungumza ni kama cha zamani huku 26 (31.7%) wakisema kina maneno ya Kiluo siku hizi. Hii ina maana kwamba vijana wengi hawaaamini Kimaragoli kimekopa maneno ya Kiluo na kwamba maneno ya Kiluo yanayotumiwa ni ya muda tu au ya kufidia mawasiliano kisha yakatoweka lakini si ya kudumu na kuwa sehemu ya Kimaragoli. 26 (31.7%) waliosema si kama cha zamani walitaja maneno katika jedwali 4.6 kuwa ni sehemu ya kongoo ya Kimaragoli:

**Jedwali 4:6: Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli**

| **Aina ya neno** | **Mifano** | **Tafsiri kwa Kiswahili** | **Kisawe cha Kimaragoli** |
|---|---|---|---|
| Nomino | Okombe, nyoyo omena/zimena, alot, apoth, anyuola | Kikombe; pure; dagaa; mboga; mlenda; jamaa/familia | Kekombe;mahengere;vwuni;tsinguza; mtere;amitu |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kundi hili halikutaja maneno mengine kama vile vitenzi, vivumishi au viingizi isipokuwa nomino katika jedwali hilo. Katika baadhi ya maneno kama vile nyoyo na omena, utohozi umetumika kwa kufuata kanuni za fonolojia ya Kimaragoli ambapo neno linaanza na irabu katika utamkaji na pia kuongezwa sauti /z/ katika omena. Sauti hii /z/ na vivuli vyake /dz/ na /ts/ ni kawaida katika Kimaragoli na hutumika kimpishano katika baadhi ya maneno.

#### 4.5.2.3 Maoni ya Makamo na Wazee kuhusu kuwepo kwa leksimu za Kiluo katika Kimaragoli

Miongoni mwa watafitiwa wa makamo na wazee, 56 (64.4%) walikiri kuwa Kimaragoli kimekopa maneno ya Kiluo huku 31 (35.6%) wakikiri kuwa hakuna maneno ya Kiluo katika Kimaragoli. Waliokiri kuna maneno ya Kiluo walitoa mifano mbalimbali

kuthibitisha dai lao. Jedwali 4.7 linaonyesha maneno ambayo kundi hili lilitaja kuwa ya mkopo kutoka kwa Kiluo.

**Jedwali 4.7: Leksimu za Kiluo katika Kimaragoli**

| Aina ya neno | Mifano | Tafsiri kwa Kiswahili | Kisawe kwa Kimaragoli |
|---|---|---|---|
| Nomino | Omena, nyoyo, anyuola, ekigwengu, omera, nyuol ber, apiel nade; kuon | Dagaa; pure; jamaa/familia, kutenda mambo kulingana na desturi za kijiji; bwana; sufuria kubwa; surupwenye; ugali | Vwuni; mahengere; amitu; mnyaa;gufuria; riovarol; vukima; |
| Vitenzi | Awachokama, wek bwoga, wantie, wachieo, abiro | Nasema hivi; Umenishtua; tuko; tumeamka; naja | Mbora ndi; undihitsi;kuvuki;nzitsa |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Watafitiwa 56 (64.4%) wa miaka 36 waliokiri kwamba kuna mabadiliko, walitoa mifano katika jedwali hili kama ishara tosha kwamba maneno haya yanatumika kila mara katika lugha ya Kimaragoli. Watafitiwa 31 (35.6%) wanaamini kwamba haya ni maneno ya msimu na hutokea kutegemea muktadha. Wanaamini kwamba maneno haya si sehemu ya hazina ya msamiati wa Kimaragoli. Kutokana na uchanganuzi wa mifano iliyotolewa, idadi kubwa ya maneno mkopo ni nomino (7), vitenzi (5), viingizi (2) na kisha kivumishi kimoja. Mtafiti alipokuwa anachunguza matumizi ya Kimaragoli katika eneo la Thim Jope, alikumbana na haya maneno ambayo yanatumika kila mara katika eneo hili: *Izim/kitsimi (Thim)* lenya maana ya kichaka kwa Kiluo na *kwoni (kuon)* lenye maana ya ugali. Maneno haya baada ya kukopwa, yalitoholewa ili kuchukua muundo wa fonolojia ya Kimaragoli ambao huchukua muundo wa IKIK (Izim). Pamoja na hayo, kwa kuwa Kimaragoli hakina sauti /ð/, inatohoa neno hili kwa kulipa sauti /z/ ambayo imesharabu katika maneno ya Kimaragoli. Katika mahojiano na Mchungaji, alikiri kwamba kweli maneno haya yamo katika Kimaragoli hasa maeneo ya Thim Jope:

> **Mchungaji:** *Hii gaveyeku mu. Kuri Thim Jope, Varogori vavora Kitsimi. Mu Llogori ni kisaka. Ku makovore mu Rovo dave. Ku llomba riva ryu Llogori. Mang'ana kuri nyoyo, kuon, kandi gatumika sana. [Ndio, kuna maneno ya Kiluo. Kwa mfano, Thim Jope, Wamaragoli wanasema Kitsimi. Kwa Kimaragoli, ni kisaka. Sasa hatuwezi kusema ni ya Kiluo sasa. Kubadilisha neno hili kunalifanya*

*kuwa la Kimaragoli. Maneno kama vile nyoyo, kuon, pia yanatumika. TY]*
(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na takwimu na mifano iliyotolewa ya maneno ya Kiluo katika Kimaragoli, mambo yafuatayo yanadhihirika: kwanza, kama walivyosema wataalamu (Nagy, 1996; 2010; Poplack na wenzake, 1998 na T'sou, 2001) nomino ndizo zinazokopwa kwa wingi. Pili, katika baadhi ya maneno ya Kiluo, pamekuwepo na utohozi kamili hivi kwamba neno limepitia mfumo wa kifonolojia wa Kiluo na kuingia katika ule wa Kimaragoli. Maneno kama vile *enyoyo/amanyoyo/zinyoyo* na *izim/kitsimi* (kichaka) yamechukuliwa kuwa sehemu ya Kimaragoli na hivyo yanatamkwa namna ambavyo maneno mengine ya Kimaragoli hutamkwa. Kitenzi "*wek bwoga"* (umenishtua) vilevile kinaambishwa na kutamkwa namna ambavyo vitenzi vya Kimaragoli huambishwa na hutamkwa ambapo viambishi vinaongezwa na kuwa ***wa***kumbwoga.

Katika kueleza kwa nini wanaingiza maneno ya Kiluo katika Kimaragoli, sababu zilizokuwa maarufu zilijumuisha: kwanza, kukosa visawe vya Kimaragoli katika miktadha maalumu. Mfano ambao ulitolewa kutomelea sababu hii ni "nyuor ber" (sufuria kubwa) ambao kwa maoni yao, hakuna neno la Kimaragoli linaloweza kutosheleza dhana hii. Hata hivyo, Kimaragoli kina neno halisi la sufuria kubwa ambalo ni "Gufuria" Sababu ya pili waliyotoa ni kuwepo kwa mazoea miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli kutokana na kutangamana na Waluo kwa muda mrefu. Takwimu na mifano hii inahimiliwa na nadharia ya mtagusano lugha inayodai kuwa katika lugha ambazo hazina mnasaba mmoja, neno pwekepweke ndilo hukopwa na kutumika badala ya neno linalostahili kutumika.

Tofauti iliyopo kiasilimia kati ya haya makundi matatu ni ndogo mno. Makundi yote yanakubali kwa zaidi ya 64% kuwa Kimaragoli kina maneno mapya ya Kiluo katika

kongoo yake huku watafitiwa waliokuwa na maoni tofauti wakiwa kati ya 31.7%-36%. Vilevile, maneno ambayo yanajitokeza katika makundi yote ni enyoyo/amanyoyo/zinyoyo, omena/zimena na anyuola. Maneno mengine yalitofautiana kimakundi kuonyesha kwamba kuna maneno ambayo yanavumishwa katika kundi maalumu au yanafahamika na kundi maalumu kuliko kundi jingine.

Kulingana na nadharia ya mtagusano lugha, kuwepo kwa leksimu pweke za Kiluo katika Kimaragoli kunatokana na wazo kwamba ni rahisi kuhamisha leksimu pweke au vipengele huru kutoka lugha moja hadi nyingine kuliko kuhamisha mfumo mzima wa kifonolojia, mofolojia au sintaksia. Hii ni kwa sababu vipengele hivi pweke ndivyo dhaifu katika mfumo mzima wa lugha ya binadamu. Ni muhimu kutaja kwamba maneno ya Kiluo katika Kimaragoli ni machache sana licha ya kuwepo kwa asilimia kubwa ya wanaokubali athari hii ipo. Ni bayana kwamba pia mtagusano wa muda mrefu kati ya Kiluo na Kimaragoli haujakuwa na athari kubwa katika kiwango cha uingizaji wa leksimu za Kiluo ndani yake.


### 4.5.3 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo

Utafiti huu ulitaka kuthibitisha ikiwa kulikuweko na uchanganyaji na uhamishaji msimbo miongoni mwa Wamaragoli wanaoishi eneobunge la Uriri. Uchanganyaji na uhamishaji msimbo ulikuwa muhimu katika kubainisha ikiwa Kimaragoli kinadumishwa au la. Hii ni kwa sababu, vipengele hivi viwili vya kiisimujamii ni sehemu ya tabia ya matumizi lugha na kigezo muhimu katika kutambua ikiwa lugha inadumishwa au wasemaji wake wanaguria lugha nyingine. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kutegemea umri wa wasemaji.

#### 4.5.3.1 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Watoto

Watafitiwa wa miaka 12-17 walipoulizwa ikiwa wao huingiza maneno ya Kiluo wakati wa kuongea Kimaragoli 42 (56.1%) walisema ndio huku 33 (43.9%) wakisema la. Kielelezo 4.4 kinaonyesha hali hii:

**Kielelezo 4.4. Uingizaji wa maneno ya Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa watoto**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kielelezo hiki kinaonyesha jinsi ambavyo watoto wa miaka 12-17 wanavyoonekana kuthamini lugha ya Kiluo katika mazungumzo yao bila kujali kama ni mazungumzo baina ya Mmaragoli-Mmaragoli au Mmaragoli-Mluo. Kwa mujibu wa Jamai (2008) ubadilishaji na uhamishaji msimbo ni kiashiria kikubwa cha jinsi kundi fulani la wanajamiilugha wanavyoiheshimu lugha maalumu kiasi cha kuipa nafasi kiuamilifu katika maisha yao. Matokeo ya utafiti wake yanalingana na ya utafiti huu kwani alitambua kwamba watoto na vijana walikuwa na kiwango cha juu cha ubadilishaji na uhamishaji msimbo ikilinganishwa na wazee.

Vilevile, mtafiti alitaka kujua maeneotumizi ya lugha ambako Wamaragoli huchanganya na kuhamisha ndimi: wengi walisema wao huchanganya lugha wakiwa nyumbani, sokoni na mazungumzo na marafiki. Matokeo ya takwimu hizi hayakujifunga kwa wale waliokubali (56.1%) kuchanganya na kuhamisha lugha bali yalijumuisha watafitiwa

wote. Hii ni kwa sababu mtafiti alitaka kujua maoni ya kijumla kuhusu hali ya uchanganyaji na uhamishaji msimbo eneobunge la Uriri. Jedwali 4.8 linaonyesha hali halisi ya majibu yao:

**Jedwali 4.8: Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa watoto**

| Wakati/mahali wasemaji wa Kimaragoli huchanganya Kimaragoli na Kiluo | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Mazungumzo na Marafiki** | 52 | 69.3 |
| **Sokoni** | 47 | 62.7 |
| **Michezoni** | 46 | 61.3 |
| **Barabarani/Njiani** | 36 | 48 |
| **Shambani/Kazini** | 32 | 42.7 |
| **Mikutanoni** | 30 | 40 |
| **Nyumbani** | 29 | 38.7 |
| **Shuleni** | 27 | 36 |
| **Kanisani** | 20 | 26.7 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Jedwali hili linaonyesha kwamba watafitiwa 52 (69.3%) huchanganya na kuhamisha msimbo wakiwa na mazungumzo na marafiki, 47 (62.7%) wakiwa sokoni, 46 (61.3%) wakiwa michezoni, 36 (48%) wakiwa njiani na marafiki na 32 (42.7%) wakiwa shambani au kazini. Vilevile, 30 (40%) huchanganya na kuhamisha wakiwa katika mikutano mbalimbali kama vile ya vijana na ya kanisa, 29 (38.7%) wakiwa nyumbani kwao, 27 (36%) wakiwa shuleni na 20 (26.7%) wakiwa kanisani.

Matokeo ya uchunzaji katika masoko na maduka ya Bware, Thim Jope na Arambe yalionyesha kwamba uchanganyaji na uhamishaji ndimi ulikuwa unafanyika sana. Sababu kubwa ilikuwa kuwepo kwa wauzaji na wanunuzi kutoka jamii hizi mbili. Matokeo ya uchunzaji wa mtafiti msaidizi katika eneo la Kajulu I yalionyesha kwamba Kiluo kilitumika sana kuliko Kimaragoli na pia zaidi kuliko uchanganyaji wa lugha hizi mbili. Tofauti kati ya matokeo haya inatokana na sababu kwamba Wamaragoli wengi wanapatikana upande wa Thim Jope, Arambe, Bware, na zaidi, Lwala kuliko upande wa

Kajulu I. Takwimu na idhibati hizi zinamaanisha kwamba Kiluo kimekita mizizi katika sehemu na miktadha ambamo Kimaragoli kinastahili kutamalaki. Kwa mujibu wa Jamai (2008), hii ni ishara kwamba wanaodumisha lugha ni wachache ikilinganishwa na wanaoathirika na hawa wanaoathirika, hatimaye, wasiporekebisha, wataguria Kiluo.

Kwa kuwa eneotumizi la nyumbani ni muhimu na la kimsingi katika kudumisha lugha, mtafiti aliuliza watafitiwa ikiwa wao huchanganya/kuhamisha lugha wakiwa nyumbani na watu mbalimbali. Hii ilikuwa muhimu kwa sababu ilitoa mwanga kamili wa ruwaza ya matumizi ya Kimaragoli nyumbani. Matokeo haya yamewasilishwa kitakwimu katika jedwali 4.9

**Jedwali 4.9: Ruwaza za uchanganyaji/Uhamishaji Msimbo nyumbani miongoni mwa watoto**

| Mahusiano ya nyumbani na matumizi ya Kimaragoli | Kimaragoli | | Kiluo | | Zote (Uchanganyaji/Uhamishaji) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % |
| Na Nyanya/babu | 66 | 88 | 9 | 12 | 1 | 1.3 |
| Wazazi | 64 | 85.3 | 9 | 12 | 3 | 4 |
| Watu wa ukoo | 49 | 65.3 | 9 | 12 | 16 | 21.3 |
| Ndugu zao | 51 | 68 | 9 | 12 | 15 | 20 |
| Majirani | 38 | 50.7 | 9 | 12 | 28 | 37.3 |
| Watoto wengine | 38 | 50.7 | 9 | 12 | 27 | 36 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, uchanganyaji na uhamishaji msimbo ni hali inayokumba sana watoto wa umri wa miaka 12-17 wanapotangamana na watu wao wa ukoo 16 (21.3%) kama vile mjomba, shangazi, wapwa na mashemeji zao. Wanapowasiliana na ndugu wa tumbo moja, 15 (20%) huchanganya na kuhamisha lugha. Sababu iliyobainika kueleza hali hii ni kuwepo kwa mahusiano ya kindoa kati ya Wamaragoli na Waluo ambako kumezalisha na kushamirisha matumizi ya lugha zote mbili kama mkakati wa kukamilisha mawasiliano. Kiluo kuanza kutumika katika ukoo ambako Kimaragoli kinatarajiwa kutumika ni hali ya hatari katika udumishaji wa lugha hii siku za baadaye. Maoni ya Jamai (2008) na msingi wa nadharia unatilia mkazo wazo hili kwa kudai kuwa

lugha moja inapovamia nyingine na kuchukua nafasi yake kimatumizi, iliyovamiwa hudhoofika. Hii ni hali halisi kwani Kiluo kimeanza kudhoofisha mfumo wa kimahusiano ambako wasemaji wanatarajiwa kutumia Kimaragoli bila tatizo lolote. Na Ndiyo sababu kuna maneno ya Kiluo katika mfumo wa Kimaragoli. Miaka ya 1940 hadi 1970, Kimaragoli kilikuwa kinatumika bila kuingiliwa na Kiluo, hali sasa imebadilika. Katika uchunzaji wa mtafiti, hali hii ilikuwa bayana katika familia ambazo mama ni Mluo na baba ni Mmaragoli, hivyo watoto wanachanganya na kuhamisha Kimaragoli na Kiluo.

Kuwepo kwa majirani wa Kiluo kunasababisha watoto 28 (37.3%) kuchanganya na kuhamisha Kimaragoli na Kiluo. Watoto wa Kimaragoli wanapokutana na watoto wengine katika mazingira ya nyumbani 27 (36.5%) watachanganya na kuhamisha lugha ili kukamilisha mawasiliano yao. Hali hii pia inaenda sambamba na watoto wa Kimaragoli wanapoenda kutembelea wenzao wa Kiluo katika maboma zao. Katika uchunzaji wetu, mtafiti na msaidizi wake walitambua kwamba watoto Wamaragoli na Waluo wanapokwenda kucheza, malishoni au kuogelea, wanachanganya lugha hizi zote. Hali ilikuwa ileile tulipochunguza watoto wakicheza katika eneo la Thim Jope. Kwa mfano, katika mazungumzo aliyorekodi mtafiti, watoto walikuwa wanachanganya na kuhamisha ndimi kama ilivyonukuliwa hapa:

> **Mtoto A:** *Waa, tsiswa tsituraa…Awilo, hambi kuryi tsiswaa…bika weee..[Waa, kumbekumbe wanatoka ardhini…Awilo, njooni tule kumbekumbe…njoo wewe…TY na TYMS]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Mazungumzo haya kati ya watoto waliokuwa wanacheza nje muda wa jioni saa kumi na mbili na dakika ishirini yanaonyesha jinsi ambavyo watoto wana mazoea ya kuchanganya na kuhamisha ndimi.

#### 4.5.3.2 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Vijana

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, 36 (43.9%) walikubali kwamba huchanganya maneno ya Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli huku 46 (56.1%) wakipinga. Takwimu hizi zimewasilishwa katika Jedwali 4.10:

**Jedwali 4.10: Uingizaji wa maneno ya Kiluo katika Kimaragoli miongoni mwa vijana**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndio | 36 | 43.9 |
| La | 46 | 56.1 |
| **Asimia** | **82** | **100.0** |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na takwimu hizi, vijana wanaochanganya au kuhamisha lugha ni 36 (43.9%) huku 46 (56.1%) wakidai kutochanganya au kuhamisha lugha wanapowasiliana. Idadi ya wanaohamisha na kuchanganya lugha japo ni ndogo ikilinganishwa na wanaopinga, inaonyesha kwamba vilevile, kundi hili linathamini matumizi ya Kiluo katika mazingira ambamo Kimaragoli kinastahili kutumika. Hii ina maana kwamba uwezo wa Kimaragoli kudumishwa unayumba kwa kiasi katika kundi hili. Na kama alivyosema Jamai (2008), hii si ishara nzuri katika udumishaji wa lugha.

Ili kuelewa zaidi hali hii ya ubadilishaji na uhamishaji msimbo katika kundi hili, mtafiti alitaka maeneotumizi ambako Kimaragoli kilibadilishwa au kuhamishwa na Kiluo. Maoni yao yamewasilishwa katika Jedwali 4.11.

**Jedwali 4.11: Uchanganyaji wa Kimaragoli-Kiluo miongoni mwa vijana**

| **Wakati/mahali wasemaji wa Kimaragoli huchanganya na kuhamisha Kimaragoli na Kiluo** | **Umaratokezi** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Sokoni | 67 | 81.7 |
| Mazungumzo na Marafiki | 66 | 80.5 |
| Barabarani/njiani | 63 | 76.8 |
| Mikutanoni | 54 | 65.9 |
| Shambani/Kazini | 54 | 65.9 |
| Michezoni | 37 | 45.1 |
| Nyumbani | 26 | 31.7 |
| Kanisani | 24 | 29.3 |
| Shuleni | 21 | 25.6 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo haya yanaonyesha kwamba Kimaragoli kinachanganywa au kubadilishwa na Kiluo sana katika maeneo ya sokoni 67 (81.7%), mazungumzo na marafiki 66 (80.5%), barabarani 63 (76.8%), mikutanoni 54 (65.9%), shambani/kazini 54 (65.9%), michezoni 37 (45.1%), nyumbani 26 (31.7), kanisani 24 (29.3%) na shuleni 21 (25.6%). Maeneo ya sokoni, kuwa na marafiki, barabarani, mikutanoni, shambani/kazini na michezoni kwa kuwa yanavutia watu kutoka jamiilugha hizi zote, ni jambo linaloeleweka ikiwa asilimia hizi ni za kiwango cha juu. Vijana waliohojiwa na mtafiti msaidizi walikiri kwamba uchanganyaji na uhamishaji ndimi ni suala la kawaida katika maeneotumizi yaliyotajwa na wakatoa mifano wanakohamisha na kuchanya ndimi:

> **K2**: *Gatemea. Yengo komoroma Llogori. Koveye mwivugana, komoroma Llogori nu Ruswahiri. Yinzi ningina mpira, paga njanganye na Rovoo. [Inategemea. Nyumbani tunaongea Kimaragoli. Tukiwa kanisani, tunaongea Kimaragoli na Kiswahili. Mimi nikicheza mpira, lazima nichanganye na Kiluo. TY]*
>
> **K3**: *Kunyi rwakwatsia Kakamega, kwamoroma Llogori lakini sasa kwavikamu Rovoo nikwenya vavuri kumanya chakovora. Manyingi kwamoroma Llogori. [Sisi tulipoenda Kakamega, tuliongea Kimaragoli lakini pia tunahamisha kwa Kiluo wakati hatukutaka wajue tunasema nini. Lakini mengi tuliongea kwa Kimaragoli. TY]*
>
> **K3**: *Koveye msogoni yo makivula rigari. Kuzuganya tsiosi. [Tukiwa sokoni ndio mbaya zaidi. Tunachanganya sana zote.TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kwa mfano, mazungumzo yafuatayo yalirekodiwa katika soko la Nyasoko:

> **Mnunuzi 1**: *Gigo omako wang'i [Hizo zimekushangaza]*
> **Mnunuzi 2**: *Ole omiya discount..[Haki amenipa punguzo la bei]*

**Mnunuzi 1**: *Si mangoovoola…bedni an gi twelve tin..imiya discount [Si huwa nakuambia…hata nikiwa na gorogoro kumi na mbili, napewa punguzo.]*
**Mnunuzi 2:** *Kono emomiye girege..[Huko ndio sababu watu husagia huko]*
**Mnunuzi 1**: *Ndatsa nzizange weneyo…[Nitakuwa nakuja huko]*
**Mnunuzi 2**: *Naaa min Kesi ng'ado maduma? [Na mama Kesi hupimia (watu) mahindi kidogo?]*
**Mnunuzi 1**: *Manyi mba, kata gege ni kidogo sana [Sijui lakini yake huonekana kidogo sana]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Mazungumzo kati ya Mnunuzi 1 na Mnunuzi 2 yanaonyesha hali iliyokuwa imezagaa katika soko la Nyasoko. Ubadilishaji na uchanganyaji msimbo ni hali ya kawaida kama inavyoonekana katika dondoo hili baina ya wanawake wanunuzi. Hali ilikuwa hivyo hivyo miongoni mwa vijana waliokuwa wanapanga kutazama mchezo wa kandanda wakinywa pombe:

**Kijana 3**: *Omera, umanyi karunu ni Champions League…[Bwana, wajua leo ni siku ya Ligi Kuu ya Mabingwa wa Ulaya…]*
**Kijana 4**: *Kata an abiro kuwatch madho kong'o [Hata mimi nitakuja kutazama nikinywa pombe]*
**Kijana 3**: *Na bets hatujawekelea…*
**Kijana 4**: *Sato PSG vang'ora mang'ana, onge pesa kawuono [Jumamosi timu ya PSG iliniangusha, sina pesa leo]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Mazungumzo haya baina ya vijana wawili katika soko la Nyasoko pia yalidhihirisha dhana ya uchanganyaji na uhamishaji msimbo. Hata hivyo, uchanganyaji huu haukutokea kwa lugha za Kimaragoli na Kiluo pekee bali pia Kiswahili na Kiingereza.

Ili kupata undani wa hali halisi ya uchanganyaji na uhamishaji, mtafiti aliuliza watafitiwa lugha wanayotumia wakiwa na watu mbalimbali nyumbani. Majibu yao yamewasilishwa katika jedwali 4.12:

**Jedwali 4.12: Ruwaza za uchanganyaji/Uhamishaji Msimbo nyumbani miongoni mwa Vijana**

| Mahusiano ya nyumbani na matumizi ya Kimaragoli | Kimaragoli | | Kiluo | | Zote (Uchanganyaji/Uhamishaji) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % |
| **Babu/Nyanya** | 74 | 90.2 | 1 | 1.2 | 2 | 2.4 |
| **Wazazi** | 73 | 89 | 0 | 0.00 | 6 | 7.3 |
| **Watu wa ukoo** | 36 | 43.9 | 0 | 0.00 | 29 | 35.4 |
| **Ndugu zako** | 63 | 76.8 | 2 | 2.4 | 14 | 17.1 |
| **Watoto wako** | 64 | 78 | 1 | 1.2 | 9 | 11 |
| **Majirani** | 42 | 51.2 | 1 | 1.2 | 36 | 43.9 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Takwimu katika jedwali hili zinaonyesha kwamba kiwango cha uchanganyaji na uhamishaji msimbo katika eneo la nyumbani kinatofautiana kutegemea uhusiano wa washiriki. Watafitiwa wanaonyesha kwamba washiriki wanapokuwa na babu/nyanya, kiwango cha uchanganyaji kitakuwa cha chini mno 2 (2.4%) kikifuatwa na kile cha wazazi 6 (7.3%). Kiwango hiki cha chini kinamaanisha kuwa vijana wanapowasiliana na nyanya/babu na wazazi wao, watapendelea kuongea Kimaragoli kuliko Kimaragoli-Kiluo. Mahusiano haya yanapohusisha watu wa ukoo, kiwango cha uchanganyaji lugha kinapanda hadi 29 (35.4%) kuonyesha kuwa watafitiwa wana uhuru mkubwa wa kuongea Kimaragoli-Kiluo wakiwa na mashemeji, wajomba, mashangazi, wapwa miongoni mwa watu wengine wa ukoo mmoja nao. Kama ilivyotajwa awali, sababu kubwa ya kuwa na aina hizi za takwimu ni ya mitandao ya ndoa baina ya Wamaragoli-Waluo. Kwa mfano, katika mazungumzo na vijana, mtafitiwa msaidizi aliambiwa kwamba:

> **K2**: *Vivuri garondekana. Uranyora kari mama Mluo, vamoromaa Llogori no Rovoo. Voosi vaveye Varogori, Llogori tsa. [Na wazazi , inategemea. Unapata mama akiwa Mluo, watazungumza Kimaragoli na Kiluo. Wote wakiwa Wamaragoli, wanatumia Kimaragoli. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kwa mfano, katika mazungumzo yaliyorekodiwa na mtafiti msaidizi, hali hii ya mama Mluo na mtoto wake Mmaragoli walikuwa wanaongea Kiluo. Kwa dakika zaidi ya kumi, mazungumzo yalitumia Kiluo huku maneno ya Kimaragoli yakiwa machache. Mawasiliano yalibadilika na kutumia Kimaragoli baada ya mtoto wa kiume (mtoto wake mama Mluo) kuwasili katika sebule. Mfano wa nukuu huu hapa:

> **Mama**: *Pigcha kare pod enful, mane e sky maa mbele cha [kumbe maji yale bado yamejaa, yaleo yako kwa mtungi wa huko mbele..TYM]*
> **Binti**: *Idwaa lwoko dendi koso mana wiyi? [Unataka kuoga mwili ama kuosha kichwa peke yake…? TYM]*
> **Mama**: *Oh Bebi nenika…[Bebi alikuwa hapa TYM]*
> **Binti**: *Nobiro kar saa adi? [Alikuja saa ngapi hivi? TYM]……*
> **Kaka** : *Vindu yivi vitura hayi? [Vitu hivi vinatoka wapi? TY]*
> **Binti**: *Kiryango chari charamu…[mlango ulikuwa wazi…TY]*
> **Kaka**: *Ondetee ribeteri? Heeee? [Ulinileteea batri..heee? TY]*
> **Binti**: *Kata nzyii Stella mba. [Hata sikuenda Stella. TY]*
> (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na mazungumzo haya kati ya watu wa familia moja, ilikuwa wazi kwamba mama alipendelea kutumia Kiluo anapoongea na mtoto wake wa kike na mtoto wa kiume anapoingia, mama anakimya na ndugu wawili wanaanza kuzungumza kwa Kimaragoli. Hata hivyo, katika mawasiliano hayo, mama anazungumza Kimaragoli lakini kwa nadra sana kwa kuwa mazungumzo yanaelekea kuwa na mada inayomtenga. Mtoto wake mvulana anapoondoka, mama na binti wanazungumza kwa Kiluo lakini kwa dakika chache kwa kuwa wajukuu wanaanza kuzungumza na kuwalazimu wao wote watumie Kiswahili kuzungumza nao.

Watafitiwa 14 (17%) walikiri kuchanganya au kuhamisha msimbo wakiwa na nduzu zao wa damu moja. Hii ina maana kwamba ndugu wakiwa na mzazi mmoja wa Kimaragoli na mwenzake wa Kiluo, uwezekano mkubwa upo wa wao kujifunza lugha zote na kuzitumia kimpishano. Pamoja na kadhia kama hii ya mzazi mmoja Mluo mwingine Mmaragoli, utafiti ulitambua kwamba hata vijana wa Kimaragoli huchanganya na

kuhamisha ndimi wao kwa wao. Katika harakati za uchunzaji maeneo ya Arambe, mtafiti alirekodi mazungumzo yafuatayo kati ya dada wawili ambao mama ni Mluo na baba Mmaragoli:

> **Dada A***: Umanyi kokore vwangu mnya…kawachopo kono to wadeko wadhitimo nono [Wewe hebu tuharakishe…tukifika huko kama tumechelewa tutakuwa tumefanya kazi bure. TY na TYMS]*
> **Dada B***:Haraka en mar ango to en mana loka cha. Ohinyore marach [Haraka ya nini na ni hapo ng'ambo. Haraka haraka haina Baraka TYMS]*
>
> (Chanzo: Data ya Mtafiti)

Kauli hizi zinathibitisha kwamba uhamishaji msimbo kati ya vijana wa mzazi mmoja Mmaragoli na mwingine Mluo ni jambo lisiloepukika. Watoto waliozaliwa katika mazingira haya ya wingilugha (Kimaragoli, Kiluo na Kiswahili) wanajikuta wametumia lugha hizi zote. Takwimu hizi pia zilishadidiwa na matokeo ya uchunzaji katika eneo la Bware ambapo mtafiti alishuhudia dada wawili wa mama Mluo na baba Mmaragoli wakiongea Kimaragoli kisha wakahamisha msimbo na kuongea Kiluo. Katika vijiji vya Ombo, mtafiti alishuhudia vijana wa Kimaragoli wa kuendesha bodaboda wakichanganya lugha zote kwa sababu ya wateja waliokuwa wanaelekea barabara kuu ya kuenda Migori kutoka ndani ya vijiji. Eneo la Ombo lilionyesha kiwango kikubwa pia cha uhamishaji msimbo na katika baadhi ya nyumba, mtafiti na msaidizi wake walitambua maboma ya Wamaragoli waliokuwa wanaongea Kiluo tu. Katika mahojiano na watafitiwa mbalimbali, eneo hili pia lilitajwa. Mmoja wa wazee alisema kwamba:

> **Guuga 2:** *Anza he mwanange, kwatsya ku havundu Ombo yira konyora vijana vyumbaka inyumba. Mryango gwari gohenzi iruhya ku imbarabara. Nikumanya, yava na Varogori na kandi mugitsi gunu gwu Mrogori. Ku kwavateva kigira ki vamoroma Rovoo, voombi viruka. Ole viruka voombi. Viruka vatsya kwihanira mmba. Kukwama kuvita ho kande kaare, vakocheritsa mu Llogori. Vakovola ndi, vagoyana na vakuhula vuvi kogotitsa miima gyavo.*
> **Babu 2:** *Angalia mtoto wangu, tuna mahali tulienda Ombo tukapata vijana wanajenga nyumba. Mlango ulikuwa umeangalia mbele ya barabara. Tukajua, hawa ni Wamaragoli na tena ni boma la Mmaragoli. Tulipowauliza kwa nini wanaongea Kiluo, wote walitoroka. Walitoroka wakaenda kujificha ndani ya nyumba na wakafunga milango. Tulipoenda na kupitia pale baadaye, walitusalimia sasa kwa Kimaragoli. Wakatuambia wamechanganyikiwa kwa*

*kuwa wanahisi walikuwa wanapoteza utamaduni na lugha yao. TY]*

(Chanzo: Data ya nyanjani*)*

Kauli hizi zinashadidia yale ambayo mtafiti na msaidizi wake walishudia nyanjani Ombo na pia katika maeneo ya Kajulu I.

Watafitiwa 9 (11%) walisema wanachanganya na kuhamisha ndimi wanapowasiliana na watoto wao. Data ya kimsingi ilionyesha kwamba wazazi hawa 9 (11%) wote walikuwa wa kike na lugha yao asili ilikuwa Kiluo. Hii ina maana kwamba walikuwa Waluo walioolewa kwa Wamaragoli. Hii ina maana kwamba kutofahamu lugha ya Kimaragoli vizuri ndiyo sababu ya wao kuzungumza lugha zote. Kukosa umilisi katika lugha ya Kimaragoli ndicho chanzo kikubwa cha kuchanganya na kuhamisha Kimaragoli hadi kwa Kiluo.

Idadi kubwa 36 (43.9%) ilikiri kuzungumza Kimaragoli na Kiluo kwa wakati mmoja wanapowasiliana na majirani zao. Hii ni kwa sababu Wamaragoli wanapakana na Waluo katika vijiji mbalimbali isipokuwa maeneo ya Bware na Lwala ambako kwa kiasi kikubwa, Wamaragoli wana ujirani na wenzao.

#### 4.5.3.3 Uchanganyaji na Uhamishaji Msimbo miongoni mwa Makamo na Wazee

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 36 na zaidi, 23 (26.4%) walikubali kwamba wamewahi kuingiza maneno ya Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli huku 64 (73.6%) wakipinga kama inavyowasilishwa katika jedwali 4.13

**Jedwali 4.13. Uingizaji wa maneno ya Kiluo miongoni mwa makamo na wazee**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio | 23 | 26.4 |
| La | 64 | 73.6 |
| Jumla | 87 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Takwimu hizi zinaashiria kwamba kundi la makamo na wazee wanajizatiti kudumisha lugha yao kwa kutohamisha au kuichanganya na Kiluo. Hii inatokana na maoni ya Odero (2013), Birman na Poff (2011) na Kipp (2009) kwamba kundi hili lina umilisi tosha wa kuweza kuzungumza bila kutatizika au kusahau msamiati na hivyo kushinikiza uchanganyaji ndimi. Kwa watafitiwa waliokiri kuchanganya na kuhamisha lugha, 20 (87%) walikuwa wa umri wa chini ya miaka 55 huku waliosalia 3 (13%) wakiwa na zaidi ya 55.

Mtafiti pia alitaka kujua ni sehemu gani ambazo wasemaji wa Kimaragoli huchanganya na kuhamisha lugha. Jedwali 4.14 linaonyesha msambao wa takwimu hizi:

**Jed.4.14: Uchanganyaji na Uhamishaji lugha miongoni mwa Makamo na Wazee**

| Wakati/mahali wasemaji wa Kimaragoli huchanganya Kimaragoli na Kiluo | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Sokoni** | 59 | 67.8 |
| **Mazungumzo na Marafiki** | 57 | 65.5 |
| **Barabarani/njiani** | 54 | 62.1 |
| **Mikutanoni** | 48 | 55.2 |
| **Shambani/Kazini** | 43 | 49.4 |
| **Kutazama/Kushiriki Michezo** | 32 | 36.8 |
| **Nyumbani** | 29 | 33.3 |
| **Kanisani** | 18 | 20.7 |
| **Shuleni** | 18 | 20.7 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni ya watafitiwa yanaonyesha kwamba wasemaji wa Kimaragoli wamezoea sana kuchanganya na kuhamisha lugha wakiwa sokoni 59 (67.8%), wakiwa na mazungumzo na marafiki 57 (65.5%), wakiwa njiani 54 (62.1%), wakiwa mikutanoni 48 (55.2%) na wakiwa kazini/mashambani 43 (49.4%). Wachache wanachanganya na kuhamisha lugha wakiwa michezoni 32 (36.8%), nyumbani 29 (33.3%), kanisani 18 (20.7%) na shuleni 18 (20.7%). Hizi ni hali ambazo kwa kawaida, hazina ulazima wa kutumia lugha moja kwa sababu sokoni na njiani ni sehemu zinazovutia wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo. Masoko ya Bware, Nyasoko na Thim Jope yalipochunguzwa na mtafiti na msaidizi wake,

yalijumuisha wasemaji wa lugha hizi mbili hivyo inaruhusiwa kuchanganya na kuhamisha lugha. Tatizo kubwa lipo katika uchanganyaji lugha maeneo ya nyumbani na mashambani. Hii ni kwa sababu maeneo haya aghalabu ni ya watu wa lugha moja au wanaostahili kutumia lugha ya Kimaragoli kila mara. Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha, kizio kidogo kabisa cha udumishaji lugha ni maeneo ya nyumbani au ya kifamilia na nyumba hizi zinapokaribiana, zinaunda mfumo dhabiti ambao hauwezi kuvunjwa kwa urahisi na lugha nyingineyo. Hivyo, Kiluo kinapoingia katika eneotumizi lugha ya Kimaragoli, basi ni ishara tosha kwamba lugha inayovamiwa imeanza kupoteza uwezo wake wa kutumika. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulitaka kujua ruwaza ya matumizi lugha katika eneo la nyumbani. Matokeo yake yamewasilishwa katika jedwali 4.15:

**Jedwali 4.15: Ruwaza za uchanganyaji/uhamishaji Msimbo nyumbani miongoni mwa Makamo na Wazee**

| Mahusiano ya nyumbani na matumizi ya Kimaragoli | Kimaragoli | | Kiluo | | Zote (Uchanganyaji/ Uhamishaji) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % | Umaratokezi | % |
| **Wajukuu** | 69 | 79.3 | 0 | 0.00 | 18 | 20.7 |
| **Wazazi** | 87 | 96.7 | 1 | 1.1 | 2 | 2.3 |
| **Watu wa ukoo** | 63 | 77.8 | 1 | 1.1 | 18 | 20.7 |
| **Ndugu zao** | 82 | 91.1 | 0 | 0.0 | 8 | 9.2 |
| **Watoto wako** | 72 | 80 | 0 | 0.0 | 16 | 18.4 |
| **Majirani** | 49 | 53.8 | 1 | 1.1 | 41 | 47.1 |
| **Makamo na wazee wenzako** | 70 | 76.9 | 0 | 0.0 | 19 | 21.8 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Takwimu zinathibitisha kwamba upo uchanganyaji na uhamishaji ndimi kati ya wazee na wajukuu 18 (20.7%). Katika hali ya kawaida, inatarajiwa kuwa wazee wanapozungumza na wajukuu wao wanastahili kutumia Kimaragoli. Maoni ya Mzee 2 katika mahojiano yanaeleza kwa nini wazee hawa wanahamisha na kubadilisha msimbo:

> **Mzee M**: *Kuzyii hango konyoraza vatumikira LLogori. Navutswa, Llogori rutumika sana ku vasakukuru na vivuri, ma na vandu vahindira ku. Lakini nonyora vana kindu 10, 12 kari 14, nivaa varazaa mmba ma vavatumii kindu, uranyora vivuri vavo vavatumira mu Ruswahili noho Rovo. Vana vitu ku mihiga yigyi, vahula Llogori, navutswa komoromakuvaregel'a. Ku mwivuri arora,*

*havogono hu kumsumbura mwana, afadhali amoromee ruswahili noho Rovo kumwanguhizira.[Tukienda nyumbani utapata wanatumia Kimaragoli. Lakini Kimaragoli kinatumika sana kwa wazee na wazazi, na watu wa makamo zaidi. Lakini kupata watoto wa miaka 10, 12 na hata 14, kama watakuja kwanyumba kisha watumwe kitu, utapata wazazi wao wanatumia Kiswahili au Kiluo. Watotowetu kwa hiki kizazi, wanasikia Kimaragoli, lakini kuongea kunawashinda. Hivyo, mzazi anaona badala ya kumsumbua mtoto wake, afadhali aongee Kiswahili au Kiluo kurahisisha mawasiliano.TY]*

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Sababu ya makamo na wazee kuchanganya na kuhamisha lugha ni kuwa wanapenda kurahisisha mawasiliano kati yao na watoto, wajukuu na vitukuu wao katika mazingira ya nyumbani. Kizazi hiki kichanga kwa kuwa hakina muda wa kutosha na wazazi wao, ni vigumu wao kuketi chini na kufundishwa Kimaragoli. Tatizo hili ni sawia kwa wazazi wanapoongea na watoto wao katika mazingira ya nyumbani kwani 16 (18.4%) walikiri kuchanganya na kuhamisha lugha wanapowasiliana nao.

Vilevile, takwimu hizi zinaonyesha kwamba watafitiwa 8 (9.2%) wa miaka 36 na zaidi wanapowasiliana na ndugu zao katika mazingira ya nyumbani, wanachanganya na kuhamisha lugha. Wanapowasiliana na wazazi wao, 2 (2.3%) wanachanganya na kuhamisha ndimi. Wanapowasiliana na watu wa ukoo kama vile mashemeji, wajomba, wapwa na kadhalika, watafitiwa 18 (20.7%) huchanganya na kuhamisha ndimi. Kuwepo kwa 18 (20.7%) ya Wamaragoli wanaochanga na kuhamisha ndimi ni kuwepo kwa ndoa za Wamaragoli-Waluo zinazowalazimisha baadhi yao kuzungumza lugha zote kwa wakati mmoja. Kama ilivyotajwa hapo awali, ndoa ni kipengele muhimu sana katika kudhoofisha au kuimarisha udumishaji lugha na ndiposa nadharia ya Mtagusano Lugha inatilia mkazo udhabiti wa mfumo wa mahusiano wa lugha inayodumishwa. Ndoa inaposababisha uchanganyaji na uhamishaji wa msimbo, hatima yake ni kuhamia lugha ya wengi (Jamai, 2008).

Kuwepo kwa ujirani ni suala la kawaida miongoni mwa binadamu, hata hivyo, katika kipengele hiki, ni wazi kwamba watafitiwa 41 (47.1%) wanaathirika na ujirani huu kwa mujibu wa wanavyojiwasilisha. Katika vijiji vya Thim Jope, Arambe, Kajulu II na Kawere II, idadi ya Wamaragoli wanaoishi ujirani na Waluo iko juu zaidi ikilinganishwa na maeneo ya Bware na Lwala ambayo wengi ni Wamaragoli. Hii ni kwa sababu maeneo haya mawili Bware na Lwala ndiyo yalikuwa kitovu cha msambao ambako Wamaragoli waligawiwa kama urithi miaka ya 1940 na hakukuwepo na Mluo isipokuwa walipoanza kuolewa na kununua mashamba sehemu hizi miaka ya baadaye.

Makamo na wazee wanapokutana na wenzao katika sehemu mbalimbali, 19 (21.8%) walikiri kuchanganya na kuhamisha msimbo. Aghalabu, mikutano ya walikulima, siasa, kanisa, kunywa pombe na mikutano ya kawaida sokoni/madukani huvutia watu wa jamii hizi mbili na hivyo, wasemaji wanajikuta katika hali ya kulazimika kuongea lugha zote.

### 4.6 Mielekeo Katika Udumishaji wa Kimaragoli

Udumishaji lugha ni suala ambalo hutegemea mielekeo ya wasemaji pamoja na jamii-lugha zilizo katika mtagusano mmoja. Mielekeo inapokuwa chanya, uwezekano wa lugha kudumishwa vizazi hadi vizazi huwepo, na panapokuwa na mielekeo hasi, lugha hiyo huwa katika hatari ya kutoweka kwa sababu haipendwi, haithaminiwi wala kutumika kila mara na kila mahali na wasemaji wake. Hii ndiyo ilikuwa sababu kuu ya kufanya utafiti, kwanza, kuhusu mielekeo ya Wamaragoli kuhusu lugha yao, na pili, kubainisha mielekeo ya Waluo kuhusu lugha ya Kimaragoli.

Mielekeo ya Wamaragoli kuhusu lugha yao imejadiliwa kwa kuzingatia makundi matatu ya utafiti huu, yaani, kundi la watoto wa miaka 12-17, kundi la vijana wa miaka 18-35 na

kundi la makamo na wazee (miaka ya 36 na zaidi). Mwisho utafiti umejadili mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli. kwa kutumia data ya mahojiano.

### 4.6.1 Mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli


Ili kubaini mielekeo ya uzungumzaji wa Kimaragoli miongoni mwa watoto wa miaka 12-17, vijana wa miaka 18-35 na miaka 35 na zaidi, kauli mbalimbali zilitolewa kwa lengo la kubainisha hisia zao kuhusu Kimaragoli. Watafitiwa walitakiwa kutoa jibu kulingana na kiwango wanachokubali kauli tofauti, yaani, kwa kuonyesha ikiwa wanakubali kabisa, wanakubali, hawana hakika, hawakubali na hawakubali kabisa. Matokeo yamejadiliwa katika vipengele mbalimbali vinavyobainisha mielekeo ya lugha. Kwa kila kipengele cha mwelekeo, utafiti umejadili kila kundi na kisha kutoa maoni ya wataalamu mbalimbali na kuonyesha pia jinsi vinaingiliana na nadharia za utafiti.

#### 4.6.1.1 Fahari miongoni Wamaragoli

Fahari ni mojawapo ya kipengele muhimu cha kutathmini iwapo mwelekeo ni chanya au hasi. Aghalabu, watu wanapoionea fahari lugha yao huwa ishara tosha kwamba wana mwelekeo chanya kuihusu.

Watafitiwa wa miaka 12-17 walipoulizwa maoni yao kuhusu kauli, "Najivunia kuongea Kimaragoli hata kama sisi tuko wachache Uriri", 47 (62.7%) walikubali kabisa, 15 (20%) walikubali, 4 (5.3%) hawakuwa na hakika, 1 (1.3%) hawakukubali, 8 (10.7%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya yamewasilishwa katika Kielelezo 4.5:

**Kielelezo 4.5: Najivunia kama mtoto kuongea Kimaragoli**




(Chanzo: data ya utafiti)

Kielelezo hiki kinaonyesha kwamba watoto wengi wa Kimaragoli 62 (82.7%) wanajivunia kuzungumza lugha yao japo kuna tofauti kubwa kati ya wale wanaojivunia sana (62.7%) na wale wanaojivunia (20%). Takwimu hizi za juu zina maana kwamba kundi hili la kiumri limetambua umuhimu wa lugha yao na haja ya kuiendeleza. Matokeo haya miongoni mwa watato yanathibitishwa na tafiti za Kuncha na Bathula (2004) na Jamai (2008), waliodai kuwa udumishaji wa lugha ni tendo linalohitaji watoto kuonea fahari lugha yao bila kujali idadi ya wazungumzaji, kiwango cha kiuchumi au hata taifa ambamo wasemaji hao wamehamia.

Vilevile, watafitiwa katika kundi hili waliulizwa ikiwa wataona aibu iwapo wenzao wa Kiluo watajua Kiluo na wao wenyewe hawajui Kimaragoli. Matokeo ya majibu yao yamewasilishwa katika jedwali 4.16:


**Jedwali 4.16: Aibu ya kutojua Kimaragoli**

| | Umarataukizi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 35 | 46.7 |
| Nakubali | 9 | 12 |
| Sina hakika | 4 | 5.3 |
| Sikubali | 13 | 17.3 |
| Sikubali kabisa | 14 | 18.7 |
| Jumla | 75 | 100.0 |

Kutokana na jedwali hili, waliokubali kabisa walikuwa 35 (46.7%), waliokubali wataona aibu ni 9 (12%), waliokosa uhakika walikuwa 4 (5.3%), walikosa kukubaliana na kauli walikuwa 13 (17.3%) na waliokosa kukubaliana na kauli kabisa walikuwa 14 (18.7%). Jumla ya watafitiwa 44 (58.7%) walisema wataona aibu huku 5.3% wakikosa uhakika. Jumla ya watafitiwa 27 (36%) hawataona aibu kabisa wakikosa kujua na kuongea lugha yao. Kuwepo kwa idadi hii ya 58.7% kunaonyesha kwamba katika kundi hili, mwelekeo chanya ni wastani na hiki si kiwango kizuri katika kudumisha lugha ya Kimaragoli kwa siku zinazokuja. Vilevile, wengi wao kuzungumza Kiluo kunawafanya kutothamini na kuonea fahari Kimaragoli kwa kuwa wanaamini alimuradi wamewasiliana na wenzao, hakuna tatizo. Hii ndiyo sababu asilimia 6.7% walisema kwamba japo Kimaragoli ni lugha yao ya kwanza, wanapendelea Kiswahili katika kuwasiliana na wenzao.

Watafitiwa hawa pia walipoulizwa kutoa maoni yao kuhusu kauli “Nitahisi vibaya sana ikiwa sisi tutawacha kuongea Kimaragoli kabisa na kuongea Kiluo”, 34 (45.4%) walikubali kabisa, 10 (13.3%) walikubali, 4 (5.3%) hawakuwa na hakika, 7 (9.3%) hawakukubali, 20 (26.7%) hawakukubali kabisa. Maoni yao yamewasilishwa katika Kielelezo 4.6:

**Kielelezo 4.6: Hisia kuhusu Kimaragoli kukoma kuzungumzwa Uriri**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo haya yanaonyesha kwamba jumla ya watafitiwa 44 (58.7%) watahisi vibaya iwapo lugha yao itapotea siku za baadaye huku watafitiwa 27 (36%) wakisema kwamba hawataona tatizo lolote. Watafitiwa 4 (5.3%) hawakuwa na hakika ya jinsi watakavyohisi iwapo lugha ya Kimaragoli itapotea au itazidi kudumishwa. Asilimia 58.7% ya wanaoonyesha mwelekeo chanya kuhusu lugha yao inaonekana kutokuwa ya kuridhisha kwa sababu kadhaa: kwanza, katika jumla ya watafitiwa 36%, kuna wasemaji wa Kiluo ambao wamelelewa na Kiluo kama lugha ya kwanza. Kwa kuwa wamelelewa na mzazi mmoja Mluo na mwingine Mmaragoli, hawaonyeshi hisia chanya kuhusu kuendeleza lugha ambayo wanahisi si yao kwa sababu mama au baba yao haizungumzi. Maoni yao yanaonyesha hisia hizi:

> **Mtoto A**: *Sisi tunaongea Kiluo hata hapa nyumbani na shuleni (miaka 12)*
> **Mtoto *B***: *hakinipendezi na sikielewi*
> **Mtoto C**: *Sijui Kimaragoli kwa sababu mama ni Mluo na baba ni Mmaragoli kwa hivyo mimi hukaa sana karibu na mama ndiposa nakijua Kiluo bila kujua Kimaragoli* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni haya yanaonyesha kwamba kuwepo kwa mwelekeo hasi kuhusu kudumishwa au kutodumishwa kwa Kimaragoli siku za baadaye kunatokana na baadhi ya watafitiwa

kutopenda Kimaragoli, wengine kuwa na mazoea ya kuzungumza Kiluo nyumbani na shuleni na wengine kwa sababu ya kukaa na mama Mluo zaidi ya baba Mmaragoli. Hizi ndizo sababu zinazochangia baadhi yao kudai kwamba hawatahisi chochote iwapo Kimaragoli kitakoma kuzungumzwa siku za baadaye.

Pili, katika asilimia hii pia, kunao watafitiwa ambao walidai kupendelea kuzungumza Kiswahili badala ya Kimaragoli. Hisia zao zinajitokeza kupitia kwa maoni haya:

> **Mtoto C***: Ni vizuri kuongea Kiswahili kuliko Kimaragoli na Kiluo (miaka 14)*
> (Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni haya yanaonyesha kwamba mawazo ya kudhalilisha lugha asilia na kupendelea Kiswahili yangali katika wanajamii. Huenda hii inatokana na sera za shule zinazosisitiza matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kuliko lugha asilia kama Kimaragoli. Tatu, kuna watafitiwa ambao wanazungumza Kimaragoli na Kiluo kwa umilisi sawa na hawana tatizo ikiwa lugha moja itapotea. Kwa mujibu wao, mawasiliano yataendelea.

Walioonyesha hisia chanya kuhusu kudumishwa kwa Kimaragoli walisema ni lugha yao ambayo wanaienzi; ni lugha kama zingine nchini Kenya na inastahili kudumishwa. Baadhi ya maoni ya watafitiwa yamenukuliwa:


> **Mtoto D***: Nazungumza Kimaragoli kwa sababu ni kizuri kwangu na pia najivunia sana (miaka 17)*
> **Mtoto E***: Ni lugha yangu ya urithi kutoka kwa wazazi wangu (miaka 17)*
> **Mtoto F***: Ni lugha yangu na ni lazima niidumishe (miaka 14)*
> (Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni haya yanadhihirisha mielekeo chanya iliyopo katika kundi hili la kiumri. Inatokea wazi wazi kwamba wanajivunia urithi ambao wazazi wao wamewapa katika umri huu mchanga. Kuwepo kwa maoni tofautitofauti miongoni mwa watafitiwa hawa kunaonyesha kwamba kundi hili la miaka 12-17 lina mielekeo kinzani kuhusu Kimaragoli. Kwa mujibu wa nadharia ya mtagusano lugha, kundi hili ndilo nyeti katika

kubadilisha mkondo wa udumishaji au uhamiaji kwa lugha nyingine. Nadharia hii inashikilia kuwa watoto wanaobaleghe na waliobaleghe ndio mawakala wakubwa wa kubadilisha mkondo wa lugha yao. Hii ni kwa sababu wengi wao wanajifundisha lugha na mielekeo ya lugha kutoka kwa wenzao ambao wanaweza kuwapotosha au kuwajenga kutegemea jinsi wanavyohisi kuhusu lugha maalumu. Vilevile, kwa kuwa walimu wao shuleni wanawalazimisha kuzungumza Kiswahili au Kiingereza, wanadharau lugha ya Kimaragoli kwa kuwa haina fahari au mchango katika maazimio ya kimasomo.

Watafitiwa katika kundi la miaka 18-35 walipoulizwa maoni kuhusu, “Najivunia kuongea Kimaragoli hata kama sisi tuko wachache Uriri”, 65 (79.3%) walikubali kabisa, 14.6% walikubali, 1.2% hawakukubali, 4.9% hawakukubali kabisa. Takwimu hizi zimewasilishwa katika Kielelezo 4.7

**Kielelezo 4.7 Najivunia kama kijana kuongea Kimaragoli**





(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo haya yanaonyesha kwamba wasemaji wengi (93.9%) wa Kimaragoli katika kiwango hiki cha umri wana mwelekeo chanya kuhusu lugha yao huku wachache (6.1%) wakiwa na mwelekeo hasi. Kuonea fahari lugha asilia ni mojawapo ya kigezo cha

kukadiria mwelekeo na mwelekeo ni kipengele muhimu cha kubainisha ikiwa lugha inadumishwa au inatoweka. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti wa Jamai (2008) aliyetafitia udumishaji wa lugha asilia za Kimoroko na kutambua kwamba wasemaji wanapoonea fahari lugha yao, hulazimika kuidumisha. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhuishaji Kiethnoisimu, fahari ya lugha na utamaduni maalumu hudhihirika kupitia kwa jinsi wasemaji wa kundi wanavyohusiana, wanavyozungumza na wanavyojitafutia uhuru wa kujitawala na kuendeleza lugha yao. Wasemaji wa Kimaragoli wa miaka 18-35 wameonyesha fahari hii kupitia kwa matendo kama vile mahusiano katika siku ya utamaduni, matanga, sherehe za kuzaliwa kwa watoto na kuwapa majina, ibada za kanisani, hasa za vijana, kutumia Kimaragoli mashambani na hata michezo wakati wanatagusana na vijana wenzao. Kwa mujibu wa nadharia ya mtagusano lugha, mhimili wa isimunafsia ni muhimu sana kwani kila msemaji wa lugha anawajibikia kudumisha lugha yake binafsi licha ya kuwa katika kundi.

Watafitiwa katika kundi hili la vijana walipoulizwa maoni kuhusu kauli, “Mimi huona aibu kuona vijana wa Kiluo wanajua kuongea lugha yao na mimi sijui Kimaragoli”, 50 (61%) walikubali kabisa, 8 (9.8%) walikubali, 5 (6.1%) hawakuwa na hakika, 6 (7.3%) hawakukubali, na 13 (15.8%) hawakukubali kabisa kama inavyoonyeshwa katika kielelezo 4.8

**Kielelezo 4.8: Mimi huona aibu kuona vijana wa Kiluo wanajua kuongea lugha yao na mimi sijui Kimaragoli**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo haya yanaonyesha watafitiwa wengi (70.8%) wanapenda lugha yao kiasi kwamba wataona aibu ikiwa wenzao wa Kiluo watajua kuongea na kujieleza kwa Kiluo na wao wakashindwa kufanya hivyo kwa Kimaragoli. Watafitiwa 23.1% walihisi kwamba hawataona aibu iwapo wenzao wa Kiluo wanazungumza Kiluo zaidi kuliko wao kuzungumza Kimaragoli. watafitiwa 5 hawakuwa na uhakika wowote kuhusu kauli hii. Hii inaonyesha kwamba wanaoonyesha mwelekeo chanya kuhusu Kimaragoli ni wengi ikilinganishwa na wale walio na mwelekeo hasi. Waliokosa uhakika ni kwa sababu wao wanazungumza Kiluo kama lugha yao ya kwanza kwa kuwa mzazi mmoja ni Mluo, hasa baba. Aidha, baadhi ya Wamaragoli kwa kuwa wanazungumza Kiluo vizuri zaidi, hawaoni tatizo lolote iwapo hawatajua Kiluo kwa sababu wana lugha wanayoweza kutumia kuwasiliana.

Watafitiwa pia waliulizwa maoni yao kuhusu kauli: Nitahisi vibaya ikiwa Kimaragoli kitakoma kuzungumzwa Uriri. Matokeo yanaonyesha kwamba 60 (73.2%) walikubali kabisa, 7 (8.5%) walikubali, 5 (6.1%) hawakukubali, 5 (6.1%) hawakukubali kabisa na 5


(6.1%) hawakuwa na uhakika. Kijumla, matokeo haya yanaonyesha kwamba watafitiwa wengi 67 (81.7%) katika kundi hili la 18-35 walionyesha mwelekeo chanya kuhusiana na fahari ya Kimaragoli huku wachache 10 (12.2%) wakidhihirisha mwelekeo hasi. Watafitiwa 10 (12.2%) walikosa uhakika kwa sababu kadhaa, kwanza, wao ni wazawa wa Kiluo kwa kuwa baba ni Mluo na mama Mmaragoli. Hivyo, Kimaragoli kikitoweka eneo la Uriri si tatizo. Pili, kunao baadhi ya Wamaragoli ambao wanazungumza Kiluo, wanajinasibisha na Kiluo zaidi, hivyo, hawatilii Kimaragoli maanani. 5 (6.1%) waliokosa uhakika ni Wamaragoli wanaozungumza Kiluo ila mwelekeo wao unayumba kiasi cha wao kutojua hisia zao iwapo lugha hii itakoma kuzungumzwa. Pia, kuna baadhi ya Wamaragoli ambao wanahisi Kiswahili ni bora kuliko Kimaragoli kwa kuwa ni lugha ya Wakenya, hivyo, hata Kimaragoli kikitoweka, watakuwa na njia ya kuwasiliana na wengine. Kwa mujibu wa Mufwene (2014), kuwepo kwa baadhi ya wasemaji wa lugha asilia wasiojivunia lugha yao ni chanzo cha uhamaji lugha. Kukosa kuzungumza lugha ya Kimaragoli na kutoona aibu ni chanzo cha baadhi ya Wamaragoli kupoteza mwelekeo chanya wa lugha yao na hivyo siku za usoni, ufifiaji wa lugha utaanza kujitokeza katika kundi hili. Kwa mujibu wa mahojiano na mzee mmoja, ilikuwa wazi kwamba baadhi ya vijana wanahamia lugha ya Kiluo, hasa maeneo ya Ombo.

> **Babu 2**: *Anza he mwanange, kwatsya havundu havaranganga Ombo konyora vang'ele vumbaka inyumba. Mryango gwari gohenzi ku imbarabara nikumanya, yava na Varogori na kandi na hango hu Murogori. Rwa kwavateva kigira ki vamoroma Rovo, voosi viruka. Viruka vatsya kwivisa mmba, vahana miryango. Rwa kwavita ho ing'inga yindi, vakocheritsa mu Llogori. Ni vakovola, vagoyana na kandi vahula esoni kogotitsa miima ne lulimi lwavo. [Angalia mtoto wangu, tuna mahali tulienda Ombo tukapata vijana wanajenga nyumba. Mlango ulikuwa umeangalia mbele ya barabara. Tukajua, hawa ni Wamaragoli na tena ni boma la Mmaragoli. Tulipowauliza kwa nini wanaongea Kiluo, wote walitoroka. Walitoroka wakaenda kujificha ndani ya nyumba na wakafunga milango. Tulipoenda na kupitia pale baadaye, walitusalimia sasa kwa Kimaragoli. Wakatuambia wamepotoka kwa kuwa wanahisi walikuwa wanapoteza utamaduni na lugha yao. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hii inaonyesha kwamba baadhi ya Vijana Wamaragoli wanafahamu lugha yao lakini kasumba ya kupenda Kiluo inawasukuma kukizungumza katika maeneo ambamo Kimaragoli kinastahili kuchukua nafasi kamili. Hata hivyo, wao wenyewe wanaona aibu kwa kupotoka na kuona aibu kubwa ya kutozungumza lugha yao katika mazingira ya nyumbani.

Miongoni mwa kundi la makamo na wazee (miaka 36 na zaidi), watafitiwa 71 (81.6%) walikubali kabisa, 8 (9.2%) walikubali, 5 (5.7%) hawakuwa na hakika, 1 (1.2%) hawakukubali, 2 (2.3%) hawakukubali kabisa. Kwa ujumla, makamo na wazee 79 (90.8%) walikiri kujivunia kuzungumza lugha yao huku 3 (3.5%) wakionyesha kutojivunia. Takwimu hizi zimewasilishwa katika Kielelezo 4.9:

**Kielelezo 4.9: Najivunia kama makamo na mzee kuongea Kimaragoli**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Idadi hii ya juu inaashiria mwelekeo chanya miongoni mwa wasemaji wa kundi hili kuhusiana na kujivunia Kimaragoli. Asilimia hii ya 90.8% inaonyesha kwamba udumishaji Kimaragoli uko imara katika kundi hili la makamo na wazee. Matokeo haya yanathibitishwa na tafiti zilizofanywa na Thomason (2001) na Perlin (2009). Kwa mfano, Perlin (2009) alitambua kwamba wazee walipendelea Kitirung zaidi na walionyesha

mwelekeo chanya ikilinganishwa na vijana na watoto waliopenda Kichina kwa sababu kiliwapa uwezo wa kupigana kiuchumi na kijamii. Katika kueleza 3 (3.5%) waliosema hawajivunii Kimaragoli ni kwamba, watafitiwa hawa watatu, wawili wa jinsia ya kike na mmoja wa kiume, walio kati ya miaka 35-49 walikuwa na asili ya Kiluo na hivyo waliongea zaidi Kiswahili wanapowasiliana na wenzao wa Kimaragoli hivyo hawakuonea Kimaragoli fahari. Kwa kuwa Kiluo ndiyo lugha yao ya kwanza, hawakuwa na haja ya kuzungumza Kimaragoli wala kukionea fahari.

Vilevile, mtafiti alitaka maoni ya watafitiwa hawa kuhusu kauli "Mimi huona aibu kuona vijana na watoto wa Kiluo wanajua kuongea lugha yao na watoto na vijana wetu hawajui Kimaragoli". Matokeo yao yamewasilishwa katika Jedwali 4.17:

**Jedwali 4.17: Mimi huaibika nikiona watoto wa Kiluo wanajua kuongea lugha yao na wetu hawajui Kimaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 50 | 57.5 |
| Nakubali | 15 | 17.3 |
| Sina hakika | 8 | 9.2 |
| Sikubali | 5 | 5.7 |
| Sikubali kabisa | 9 | 10.3 |
| Jumla | 87 | 10 0.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, watafitiwa 50 (57.5%) walikubali kabisa, 15 (17.3%) walikubali, 8 (9.2%) hawakuwa na hakika, 5 (5.7%) hawakukubali na 9 (10.3%) hawakukubali kabisa. Kijumla, watafitiwa 65 (74.8%) walionyesha mwelekeo chanya ikilinganishwa na 14 (16%) waliokuwa na mwelekeo hasi. Kuwepo kwa idadi kubwa ya makamo na wazee wanaoona aibu watoto wao wanaposhindwa kuzungumza Kimaragoli ni ishara kwamba wanajali kudumishwa kwa lugha yao siku za usoni. Hata hivyo, 14 (16%) hawaonyeshi mwelekeo huu chanya kwa sababu mbili kuu: kwanza, baadhi ya makamo na wazee kama ilivyokwisha kuwasilishwa katika tasnifu hii, wanatumia Kiswahili au Kiluo kuzungumza na wao badala ya Kimaragoli; pili, baadhi ya makamo

na wazee hawa wanazungumza Kiluo kama lugha yao ya kwanza hivyo hawana tatizo lolote ikiwa watoto wao au wajukuu wao watazungumza Kiluo. Matokeo haya yanalingana na mawazo ya Mohochi (2005) anayedai kwamba wazazi wana jukumu kubwa katika kuvyaza mielekeo ya lugha ya watoto wao. Wanapowahimiza au kusisitiza lugha maalumu, watoto wao huitumia na wanapoonyesha kupendelea lugha nyingine tofauti na ya asili yao, basi watoto hukua wakithamini lugha hiyo, na katika hali hii, Kiluo au Kiswahili.

Mtafiti pia alitaka kujua maoni ya watafitiwa wa makamo na wazee kuhusu kauli "Nitahisi vibaya sana ikiwa sisi tutawacha kuongea Kimaragoli kabisa na kuongea Kiluo", 71 (81.6%) walikubali kabisa, 8 (9.2%) walikubali, 5 (5.7%) hawakuwa na hakika, 1 (1.2%) hawakukubali na 2 (2.3%) hawakukubali kabisa. Jedwali 4.18 limewasilisha matokeo haya:

**Jedwali 4.18: Nitahisi vibaya sana ikiwa sisi tutawacha kuongea Kimaragoli kabisa na kuongea Kiluo**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 71 | 81.6 |
| Nakubali | 8 | 9.2 |
| Sina Hakika | 5 | 5.7 |
| Sikubali | 1 | 1.2 |
| Sikubali Kabisa | 2 | 2.3 |
| Jumla | 87 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Takwimu hizi zinaonyesha wasemaji wa Kimaragoli katika umri huu wana hisia chanya na hivyo mwelekeo chanya kuhusu lugha yao ya Kimaragoli. Hii ni kwa sababu jumla ya watafitiwa 79 (90.8%) walikuwa na mwelekeo chanya unaoashiria kupendelea kudumisha Kimaragoli huku 3 (3.5%) wakiwa na mwelekeo hasi. Watafitiwa 5 (5.7%) hawakuwa na hakika jinsi wangehisi ikiwa Kimaragoli kitakoma kuzungumzwa kabisa.

#### 4.6.1.2 Thamani ya Kimaragoli

Thamani ya lugha hudhihirisha mielekeo ya wasemaji wa lugha mahsusi au lugha wanayotagusana nayo. Wasemaji wanapothamini lugha yao, huona haja ya kujifunza na kuiongea, kuirithisha kwa vizazi vya baadaye, kuidumisha, kusikiliza kupitia kwa redio na kuitumia katika maeneo mbalimbali. Utafiti huu uliazimia kuchunguza kipengele cha thamani miongoni mwa watafitiwa wa miaka 12-17, 18-35 na 35 na zaidi, na matokeo yake yamewasilishwa katika sehemu inayofuata. Kulikuweko na kauli 3 : hakuna haja ya kuongea Kimaragoli ; naongea Kimaragoli kwa ajili ya kukidumisha na tunafahamu Kiluo kwa sababu ya uchumi. Kauli hii ya mwisho ililenga watu wa miaka 18 na zaidi kwa kuwa ndio umri halali wa kufanya kazi nchini Kenya.

Kipengele cha kwanza chini thamani ya lugha ambacho mtafiti alichunguza miongoni mwa watoto wa miaka 12-17 kilikuwa ni kuwepo kwa haja ya kuongea Kimaragoli eneo la Uriri. Majibu yao yamewasilishwa kiumaratokezi na kiasilimia katika Jedwali 4.19:

**Jedwali 4.19: Hakuna haja ya mimi kuongea Kimaragoli hapa Uriri**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 13 | 17.3 |
| Nakubali | 4 | 5.3 |
| Sina hakika | 15 | 20 |
| Sikubali | 7 | 9.4 |
| Sikubali kabisa | 36 | 48 |
| Jumla | 75 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Watafitiwa 13 (17.3%) walikubali kabisa na kauli, 4 (5.3%) walikubali, 15 (20%) hawakuwa na hakika, 7 (9.4%) hawakukubali, 36 (48%) hawakukubali kabisa. Jumla ya watafitiwa 17 (22.6%) walikubali kwamba hakuna haja ya wao kuzungumza Kimaragoli katika eneo la Uriri ambako Waluo ndio wengi. Jumla ya watafitiwa 43 (57.4%) waliamini kwamba kuna haja ya wao kuzungumza Kimaragoli katika eneo hili na watafitiwa, 20% hawakuwa na hakika. Asilimia 22. 6% hawaoni haja ya Kimaragoli

kuzungumzwa eneo la Uriri. Baadhi ya watafitiwa katika kundi hili la watoto walioonyesha mwelekeo chanya walisema kwamba ni muhimu kuzungumza Kimaragoli Uriri kwa sababu ndiyo lugha yao, wanaipenda, wanaijua vizuri, inatunza siri zao, ni sehemu ya kitambulisho, ni lugha ya kwanza miongoni mwa sababu nyinginezo. Waliodai kuwa hakuna haja ya wao kuzungumza Kimaragoli walisema kwamba Kiswahili ndicho kinapendelewa katika shule na pia wakiongea Kimaragoli ni aibu kwa sababu hawakijui vizuri. Wengine walidai kuwa wanajua Kiluo vizuri kuliko Kimaragoli kwa sababu mmojawapo wa wazazi wao ni Mluo.

Kundi hili la watoto wa miaka kati ya 12-17 pia waliulizwa maoni kuhusu kauli: naongea Kimaragoli ili kukidumisha. Takwimu zifuatazo zinaonyesha maoni yao: watafitiwa 43 (57.3%0 walikubali kabisa, 20 (26.7%) walikubali, 5 (6.7%) hawakuwa na hakika, 2 (2.6%) hawakukubali na 5 (6.7%) hawakukubali kabisa. Kijumla, 63 (84%) walionyesha mwelekeo chanya kuhusiana na kauli hii huku 7 (9.3%) walionyesha mwelekeo hasi. Watafitiwa 2 hawakuwa na uhakika kwa nini wanaongea Kimaragoli. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba wazungumzaji wengi wa Kimaragoli katika eneo la Uriri na Migori kwa ujumla wanazungumza Kimaragoli kwa lengo la kuhakikisha kwamba lugha yao inazidi kujidumisha. Baadhi yao walitoa maoni kwa kusema kwamba ni lugha ya mababu zao, ni nzuri na sehemu ya kuendeleza mila na desturi, ambazo ni za kipekee katika kaunti ya Migori. Watafitiwa 7 (9.3%) huenda wanazungumza Kimaragoli ila si kwa lengo la kuidumisha au ni wasemaji wa Kiluo ambao mzazi mmoja, hasa baba ni Mluo.

Watafitiwa wa miaka ya 18-35 walipoulizwa maoni kuhusu kauli, “tunajua Kiluo kwa sababu ya uchumi na kazi hapa Uriri”, 26 (31.7%) walikubali kabisa, 27 (32.9%) walikubali, 24 (29.3%) hawakuwa na hakika, 3 (3.7%) hawakukubali na 2 (2.4%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya yamewasilishwa katika jedwali 4.20

**Jedwali 4.20: Tunajua Kiluo kwa sababu ya uchumi hapa Uriri**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 26 | 31.7 |
| Nakubali | 27 | 32.9 |
| Sina hakika | 24 | 29.3 |
| Sikubali | 3 | 3.7 |
| Sikubali Kabisa | 2 | 2.4 |
| Jumla | 82 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya Utafiti)

Matokeo haya yanaonyesha kwamba Kiluo kina thamani kubwa katika uchumi wa Uriri ikilinganishwa na Kimaragoli. Hii ni kwa sababu Uriri, na hasa wanakoishi Wamaragoli, lugha ya Kiluo ndiyo inazungumzwa kwa wingi na ndiyo inatawala mfumo wa uzalishaji mali zaidi. Wazungumzaji wa Kimaragoli wanapokwenda kutafuta kazi za ukulima katika mashamba ya Waluo, inawalazimu kuzungumza Kiluo. Vilevile, vijana wa boda boda wanapotafuta wateja, inawalazimu kuzungumza au kujibu kwa Kiluo. Kiluo vilevile kinatumika katika baadhi ya afisi, shuleni, sokoni na maeneo mengine ya kiuchumi. Hata hivyo, ilikuwa wazi kwamba matumizi ya Kiluo katika baadhi ya maeneo haya si suala rasmi wala la kisheria ila kwa sababu wafanyakiza wengi ni wa asili ya Kiluo. Katika uchunzaji wetu, ilikuwa wazi kwamba vijana wa boda boda katika eneo la Bware na Thim Jope walikuwa wanazungumza Kimaragoli au Kiluo kutegemea lugha ya wateja. Mteja akiwa Mluo, walikuwa wanazungumza kwa Kiluo wakisema, “Wadhi (Jatelo)?” na akiwa Mmaragoli, “Hamba kutsyi.” Akiwa mtu wasiyemfahamu, walikuwa wanatumia Kiswahili. Hata hivyo, licha ya kwamba Kiluo ndicho kinatumika sana kiuchumi, Kimaragoli hakimo katika hatari kubwa ya kuangamia. Hii ni kwa sababu kingali kinatumika katika maeneotumizi mengine kama vile nyumbani, sokoni na kadhalika. Aidha, Kimaragoli kinatumika kwa kiwango cha kuridhisha japo kwa kuchanganywa na Kiluo.

Kigezo mojawapo cha kupima thamani ni matumizi ya lugha katika maeneo ambayo yametamalakiwa na lugha nyingine. Hii ndiyo sababu mtafiti alitaka kujua ikiwa

Wamaragoli wa kati ya miaka 18-35 wanaona umuhimu au haja ya kuzungumza lugha yao maeneo ya Waluo. Matokeo ya maoni yao yamewasilishwa katika jedwali 4.21:

**Jede 4.21: Hakuna haja ya mimi kijana kuongea Kimaragoli hapa Uriri**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 7 | 8.5 |
| Nakubali | 3 | 3.7 |
| Sikubali | 10 | 12.2 |
| Sikubali kabisa | 62 | 75.6 |
| Jumla | 82 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, watafitiwa 7 (8.5%) walikubali kabisa, 3 (3.7%) walikubali, 10 (12.2%) hawakukubali, 62 (75.6%) hawakukubali kabisa. Jumla ya watafitiwa 72 (87.8%) wanaonyesha mwelekeo chanya kwa kutambua thamani iliyomo katika kuzungumza Kimaragoli ikilinganishwa na wachache 12.2% waliokuwa na maoni tofauti. Matokeo haya yanathibitisha mawazo ya Cummins (1994) aliyedai kwamba kuzungumza lugha asilia kunachangia katika ujenzi wa kitambulisho cha mtu binafsi, hivyo basi kumfundisha kuthamini utamaduni na turathi zake. Mtu anapothamini utamaduni wake, basi huchangia mwelekeo chanya. Aidha, uzungumzaji wa lugha asilia nyumbani au katika maeneo yanayostahili husaidia kuimarisha mfumo wa kijamii wa wasemaji wake hivyo basi kutomelea mawazo ya nadharia ya Mtagusano wa Isimu kwamba lugha hudumishwa inapozungumzwa katika mfumo wa kimahusiano wa jamii moja.

Mtafiti pia alitaka maoni ya kundi hili la vijana kuhusu kauli: naongea Kimaragoli ili kukidumisha. Takwimu zifuatazo zinaonyesha majibu yao: 65 (79.3%) walikubali kabisa, 10 (12.2%) walikubali, 3 (3.7%) hawakuwa na uhakika, 2 (2.4%) hakukubali na 2 (2.4%) hakukubali kabisa. Kijumla, takwimu hizi zinaonyesha kwamba Wamaragoli wengi 75 (91.5%) katika kundi hili wanazungumza Kimaragoli kwa ajili ya kuidumisha

ikilinganishwa na 4 (4.8%) waliodhihirisha mwelekeo hasi. Watafitiwa hawa huenda wanawakilisha wazungumzaji wa Kimaragoli ambao wanazungumza tu Kimaragoli bila kufahamu kwamba wanaendeleza lengo la udumishaji. Aidha, asilimia hii inawakilisha baadhi ya wakaazi wa Uriri ambao wana lugha zao kama vile Kiluo na hawaoni haja ya kuzungumza Kimaragoli au wanapokizungumza, lengo lao si kukidumisha. Asilimia 3.7% ambao hawakuwana uhakika ni wakaazi wa Uriri ambao huenda ni Wamaragol wasiojua lengo la kuzungumza Kimaragoli au ni wazawa wa ndoa mseto.

Kwa mujibu wa utafiti za Jagodic (2011) makamo na wazee huonyesha thamani kubwa kuhusu lugha yao ikilinganishwa na makundi mengine ya kiumri. Mtafiti alitaka kuthibitisha ukweli wa tafiti hizi kwa kuuliza watafitiwa wenye miaka zaidi ya 36 maoni yao kuhusu kauli mbalimbali za thamani. Kwanza, Watafitiwa waliulizwa maoni yao kuhusu kauli "Hakuna haja ya mimi kuongea Kimaragoli hapa kwa Waluo". Matokeo yamewasilishwa katika jedwali 4.22.

**Jedwali 4.22: Hakuna haja ya mimi Mzee kuongea Kimaragoli hapa Uriri**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 4 | 4.6 |
| Nakubali | 13 | 14.9 |
| Sina hakika | 6 | 6.9 |
| Sikubali | 15 | 17.2 |
| Sikubali kabisa | 49 | 56.4 |
| Jumla | 87 | 100.0 |


(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, 4 (4.6%) wanakubali kabisa, 13 (14.9%) wanakubali, 6 (6.9%) hawana hakika, 15 (17.2%) hawakubali na 49 (56.4%) hawakubali kabisa. Matokeo yanaonyesha kwamba kwa ujumla, watafitiwa 64 (73.6%) walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu kuzungumza lugha ya Kimaragoli katika eneo la Waluo huku 17 (19.5%) wakiwa na mwelekeo hasi. Watafitiwa 6 (6.9%) hawakuwa na uhakika. Hii ina maana kwamba wasemaji 64 (73.6%) wa Kimaragoli katika kundi hili wanaona haja ya

kuzungumza Kimaragoli licha ya kuwa wachache ikilinganishwa na Waluo. Aidha, wanafahamu kuzungumza lugha yao ni kudumisha mila na utamaduni, ni njia ya kuwatambulisha na kuwatofautisha na wasemaji wa Kiluo pamoja na kuwa na haki ya kuendeleza lugha hii kama wanavyoruhusiwa kikatiba. Hii ndiyo sababu asilimia kubwa ya watoto na vijana walikubali wazee wana umilisi mkubwa wa lugha na pia hao ndio wanaizungumza zaidi katika miktadha yote. Kuwepo kwa watafitiwa 17 (19.5%) waliodhihirisha mwelekeo hasi ni kutokana na kwanza, baadhi ya wazazi katika kundi hili walipendelea kuzungumza na watoto au wajukuu zao Kiluo. Pili, baadhi yao wanapendelea Kiswahili kuliko Kimaragoli hata katika mazingira ya nyumbani. Hii inaonyesha kwamba hawathamini lugha yao. Mwelekeo huu hasi ndio umeathiri watoto na vijana wao. Kuwepo kwa 6 (6.9%) ya makamo na wazee waliokosa kuwa na hakika kuhusu dhima ya kuzungumza lugha asilia na pia baadhi ya wazazi ni wazawa wa Kiluo.

Lugha inapokuwa na thamani miongoni mwa wasemaji wake, wao huhakikisha kwamba wanaizungumza na kuidumisha. Hii ndio maana mtafiti alitaka kujua maoni ya makamo na wazee kuhusu kauli, “Naongea Kimaragoli ili kukidumisha”. Matokeo yamewasilishwa katika Kielelezo 4.10:


**Kielelezo 4.10: Tunaongea Kimaragoli ili kukidumisha**



Takwimu zinaonyesha kwamba watafitiwa 71 (81.6%) walikubali kabisa, 8 (9.2%) walikubali na 8 (9.2%) hawakukubali kabisa. Kwa ujumla, watafitiwa wengi 79 (90.8%) walio na zaidi ya miaka 35 wana mwelekeo chanya kuhusu udumishaji wa Kimaragoli kupitia njia ya mazungumzo. Utafiti huu unathibitisha matokeo ya Odero (2013) kuhusu makamo na wazee kudumisha lugha yao kuliko makundi ya vijana na watoto. Hakika, kutumia mazungumzo ndiyo njia pekee ya kudumisha lugha ambayo imetumika vizazi baada ya vizazi hata kabla ya kutokea kwa maandishi. Lengo kubwa la kuzungumza lugha, mbali na kuwasilisha ujumbe, ni kudumisha vipopo na hazina ya lugha hiyo. Hii ndiyo sababu Campbell (2016) anaeleza kwamba njia ya kudumisha lugha ni kuifunza na kuhakikisha inazungumzwa katika miktadha mbalimbali.

Mara nyingi, katika jamii zote, lugha hupewa thamani kubwa katika mfumo wa kiuchumi. Hii ina maana kwamba inamlazimu mkaazi katika jamii hiyo kufahamu lugha hiyo ndiposa aweze kupata kazi au kushiriki katika shughuli za kiuchumi ipasavayo. Hii ndiyo sababu mtafiti alitaka kujua ikiwa uchumi ndio kichocheo cha kufahamu Kiluo miongoni mwa Wamaragoli wa miaka 36 na zaidi. Matokeo yamewasilishwa katika Kielelezo 4.11.

**Kielelezo 4.11: Tunafahamu Kiluo kwa sababu ya uchumi hapa Uriri**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Watafitiwa 23 (26.5%) katika kundi la makamo na wazee walikubali kabisa kwamba wanajua Kiluo kwa sababu ya uchumi, 29 (33.3%) walikubali, 29 (33.3%) hawakuwa hakika, 4 (4.6%) hawakukubali na 2 (2.3%) hawakukubali kabisa. Kijumla, watafitiwa 52 (59.8%) walikiri kujua Kiluo kwa sababu ya kazi huku 6 (6.9%) wakikosa kukubaliana na kauli. Watafitiwa 29 (33.3%) hawakuwa na uhakika ikiwa wanajua Kiluo kwa sababu ya uchumi au zipo sababu nyinginezo. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba lugha ya Kiluo, kwa kuwa ndiyo ya wengi, inatamalaki uzalishaji kiuchumi Uriri na kaunti ya Migori kwa kiasi kikubwa. Hivyo, baadhi ya Wamaragoli 52 (59.8%) walilazimika kujifunza Kiluo ili wawe na nafasi kubwa ya kupata kazi. Hii ina maana kwamba kiuchumi, ni lazima Mmaragoli ajitambulishe na lugha ya Kiluo ndiposa aweze kupata kazi. Thamani ya Kiluo kiuchumi ikilinganishwa na Kimaragoli ni ya juu. Hata hivyo, Wamaragoli wengine wanahisi kwamba wanajua Kiluo kwa sababu ya mawasiliano ya kawaida na sababu nyinginezo ila si kwa sababu ya kazi. Kwa mfano, baadhi ya kazi ambazo zinamlazimisha Mmaragoli kujifunza Kiluo ni kama vile kuendesha 'bodaboda', kufanya kazi katika mashamba na maboma ya Waluo, kumiliki maduka au kuuza bidhaa sokoni na kadhalika. Hizi kazi kwa kuwa hazihitaji mtu kuwa na wasifu kazi maalumu

kama ilivyo afisini, kuzungumza Kiluo kunaweza kuwa tosha. Katika mahojiano na vijana wawili wa bodaboda, sababu hii ilikuwa wazi :

> **Kijana 1** : *Umanyi wenya unyare mmbo, wigi romora rwirwe. Ndio aravugila umgingi ku kibigibigi chichyo. [Unajua ukitaka kumweza Mluo, jifunze lugha yake. Hivyo, atakubali umbebe kwa pikipiki yako. TY]*
> **Kijana 2** : *Kari vutswa, yenya akutume, arakuranga mu Rovo. So ni lazima wigi kuonyore churya.[Hata akitaka kukutuma, atakuita kwa Kiluo. Hivyo, ni lazima ujifunze ili upate chakula chako. TY]* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Mbali na kujua Kiluo kwa sababu za kiuchumi, wapo wanaokijua kwa sababu nyinginezo. Katika mahojiano na Mzee 2, alidai kwamba walijua Kiluo kwa sababu Mluo ni mtu anayependa watu wanaojua lugha yake. Pamoja na hayo, alisema kwamba Mmaragoli anapofahamu Kiluo, Mluo hufungua moyo wake na kumweleza siri kubwa ambazo hawezi kuzieleza kwa Kiswahili au mtu anayeonekana kuwa wa ‘nje’. Vilevile, katika mahojiano na Nyanya 1, kujua Kiluo huwa ni kwa wale ambao wanajishengesha katika afisi za utawala wakiomba kuwezeshwa kiuchumi au kwa Wamaragoli ambao wanapenda kulimia Waluo katika mashamba yao makubwa. Pia, Kiluo hutumiwa na Wamaragoli ambao wangependa kukodisha mashamba ya Waluo kwa sababu wao wenyewe hawana bidii ya kuyalima. Mbali na hiyo, katika siasa, wanaowania nyadhifa mbalimbali hulazimika kuzungumza Kiluo kwa wapiga kura walio na asili ya Kiluo ili wapate kura zao.

Kulingana na nadharia ya uhuishaji kiethnoisimu, uwezeshwaji wa lugha katika mfumo wa uzalishaji uchumi huwa muhimu katika udumishaji wa lugha. Kutamalaki kwa Kiluo kuliko Kimaragoli katika mfumo wa uzalishaji mali unaonyesha kwamba wasemaji wa Kimaragoli huenda watahamia Kiluo siku za baadaye na kukoma kuzungumza lugha yao. Kwa mujibu wa Hamde (2005) mfumo wa uchumi-jamii huchangia sana katika udumishaji au uhamaji wa lugha katika jamii. Wasemaji wa lugha wanapokuwa katika mazingira ya kiuchumi ambapo lugha yao haitumiki sana, wao huhamia lugha ya uchumi


huo. Hii ndiyo sababu wasemaji wa Kimaragoli wanaelekea kupendelea kujifunza na kutumia Kiluo kwa sababu ya uchumi na kazi Uriri.

#### 4.6.1.3 Kupendelea matumizi ya Kimaragoli

Kwa mujibu wa Mohochi (2005) njia moja ya kupima mielekeo ni kupitia kwa vipengele kama vile mapendeleo ya matumizi lugha. Lugha, kama kipengele tendaji, hudhihirisha mielekeo chanya au hasi. Mielekeo chanya hudhihirika lugha inapotumiwa sana huku mwelekeo hasi ukidhihirishwa katika matumizi ya lugha nyingine badala ya lugha inayomlea msemaji huyo. Hivyo, utafiti huu ulitaka kujua uhalisia wa mapendeleo ya Kimaragoli kwa kutaka maoni ya watafitiwa wa miaka 12-17, 18-35 na zaidi ya 36 kuhusu kauli zifuatazo: tunaongea Kimaragoli zaidi na watu wa ukoo na pia, tunapendelea idhaa za Kimaragoli.

Kupendelea kutumia Kimaragoli wakati wa kuhusiana na watu mbalimbali wa ukoo kunaonyesha mwelekeo chanya katika kutilia nguvu mfumo wa kimahusiano na hivyo kusaidia kudumisha lugha. Katika kutaka kujua ikiwa watafitiwa wa miaka 12-17 walikuwa wanatumia Kimaragoli kati yao na ukoo wao, mtafiti aliuliza maoni yao na matokeo yake yamewasilishwa katika Kielelezo 4.12.

**Kielelezo 4.12: Tunaongea Kimaragoli na watu wa ukoo**





(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo yanaonyesha kwamba 27 (36%) walikubali kabisa, 31 (41.3%) walikubali, 9 (12%) hawakuwa na hakika, 3 (4%) hawakukubali, 5 (6.7%) hawakukubali kabisa. Kijumla, watafitiwa 58 (77.3%) walikubali kauli kwamba wao hutumia Kimaragoli kuwasiliana na ukoo wao huku 8 (10.7%) wakikosa kukubali kauli. Kuzungumza na ukoo ni tendo muhimu katika kuendeleza lugha ya Kimaragoli na linadhihirisha mwelekeo chanya miongoni mwa watafitiwa wa kundi hili. Hata hivyo, wazazi wana jukumu la kuhakikisha kwamba watoto wengi zaidi wanatangamana na ukoo wao kwa lengo la kudumisha Kimaragoli. Baadhi ya watu wa ukoo ambao watafitiwa walikiri kuwasiliana nao kwa Kimaragoli ni nyanya, babu, wajomba, mashangazi na wapwa zao. Mawasiliano haya hutendeka wanapotembelewa kwao nyumbani, wanapotembelea nasaba zao maeneo mbalimbali wanakoishi au kutumia simu tamba kuzungumza nao.

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, mtafiti aliuliza maoni ya watafitiwa kuhusu lugha ambayo wanaongea zaidi kati yao na watu wa ukoo. Majibu yao yamewasilishwa katika Kielelezo 4.13:

**Kielelezo 4.13: Tunaongea Kimaragoli zaidi kuliko Kiluo**




(Chanzo: Data ya nyanjani)


Watafitiwa 59 (72%) walikubali kabisa, 16 (19.4%) walikubali, 4 (4.9%), hawakukubali na 3 (3.7%) hawakukubali kabisa. Kwa ujumla, watafitiwa 75 (91.4%) walikiri kuzungumza Kimaragoli zaidi wanapokuwa na ndugu zao huku 7 (8.6%) wakiwa na maoni kinyume. Kuwepo kwa watafitiwa wengi wanaozungumza Kimaragoli kushinda Kiluo kunadhihirisha mwelekeo chanya katika kundi hili na hivyo kuchapuza udumishaji wa Kimaragoli. Kwa mujibu wa Jamai (2008) kupendelea lugha asilia miongoni mwa watu wa familia moja kunaonyesha mwelekeo chanya na hivyo kuboresha uwezo wa lugha hiyo maalumu kujidumisha. Sababu ya kuwa na Watafitiwa 7 (8.6%) walio na maoni tofauti ni kwamba kwanza, wapo walioolewa na Wamaragoli na hivyo wanapoenda kuwatembelea ndugu zao, wanatumia Kiluo kwa kuwa ndiyo lugha yao ya kwanza. Pili, baadhi ya watafitiwa walisema japo Kimaragoli ni lugha yao ya kwanza, hawana umilisi mkubwa wa kuzungumza, hivyo wanapendelea Kiswahili zaidi kuwasiliana na wenzao. Haya pia yalijitokeza katika mahojiano ya Mzee 2 aliyekiri kwamba watoto na vijana hawajui Kimaragoli vizuri, na kwa ajili ya kuwarahisishia mawasiliano, wanakubali kuzungumza Kiswahili. Ingawa idadi ya wanaozungumza Kimaragoli zaidi na ndugu zao ingali juu, huenda kukawa na mabadiliko siku za baadaye

kutokana na hata wazazi wenyewe kuwapa watoto wao uhuru wa kuzungumza kwa Kiswahili au Kiluo. Hii huenda itasababisha uhamiaji Kiswahili au Kiluo na hivyo kuathiri udumishaji wa Kimaragoli. Kulingana na nadharia ya isimu mtagusano, kadiri wasemaji wanavyozidi kuzungumza lugha yao katika mfumo wa kimahusiano, ndivyo lugha hiyo inavyozidi kuimarika na pindi mabadiliko yanapoanza kushuhudiwa, basi mfumo huu hulegea na hatimaye kuzalisha uhamiaji lugha.

Watafitiwa pia waliulizwa maoni yao kuhusu kauli: tunaongea Kimaragoli na watu wa ukoo". Maoni yao yamewasilishwa kitakwimu kama ifuatavyo: 40 (48.8%) walikubali kabisa, 6 (7.3%) walikubali, 28 (34.1 %) hawakukubali na 8 (9.8%) hawakukubali kabisa. Takwimu hizi zinadhihirisha mwelekeo chanya miongoni mwa vijana kwa kuwa ina jumla ya asilimia kubwa (56.1%) ikilinganishwa na wale walioonyesha mwelekeo hasi (43.9%). Hakuna watafitiwa walioonyesha ukosefu wa uhakika kuhusu kauli hii. Kuwepo kwa idadi hii ya kadiri ya wanaozungumza Kimaragoli na watu wa ukoo kunatokana na sababu kadhaa. Kwanza, wapo Wamaragoli ambao katika ukoo wote, hakuna Mluo aliyeolewa ndani yao. Pili, kwa kuwa wote ni Wamaragoli, ni rahisi wao kuwasiliana kwa Kimaragoli. Idadi ya walio na mwelekeo hasi katika kundi hili inatokana na sababu kwamba baadhi ya Wamaragoli wanazungumza Kiswahili ndani ya nyumba zao, hii ikihusisha watu wa ukoo. Pili, wapo Waluo ambao walishaolewa kwa Wamaragoli hivyo, mazungumzo katika ukoo mzima unaambatana na aina ya lugha ambayo washiriki wanajua vyema. Hivyo, baadhi ya washiriki wa mazungumzo katika ukoo wataamua kuzungumza Kiluo, hasa familia ya msichana Mluo aliyeolewa kwa Mmaragoli.

Miongoni mwa makamo na wazee (miaka zaidi ya 36) watafitiwa wengi 74 (85.1%) walikubali kabisa, 9 (10.3%) walikubali na 4 (4.6%) hawakukubali kabisa kwamba wao huzungumza Kimaragoli sana na watu wao wa ukoo. Matokeo haya yamewasilishwa katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo 4.14 Tunaongea Kimaragoli na ukoo wetu**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo yanaashiria wasemaji wa makamo na wazee wa Kimaragoli wana mwelekeo chanya kuhusu lugha yao katika mazungumzo ya ndugu kwa ndugu katika mazingira ya nyumbani au kwingineko. Kwa kuwa kizio kidogo na muhimu katika udumishaji lugha ni familia, basi Kimaragoli kinapotumiwa baina ya ndugu na ndugu kinadumishwa. Hiki ni kinyume na watafitiwa wachache 4 (4.6%) waliokubali kuzungumza Kiluo na ndugu zao. Asilimia hii ndogo inajumuisha wanawake wa Kiluo walioolewa kwa Wamaragoli na wanapoenda kwao au wanapotembelewa, hawana sharuti yoyote kuzungumza Kimaragoli. Wao huzungumza Kiluo kwa kuwa ndiyo lugha yao ya kwanza.

Mielekeo pia hudhihirika kupitia mapendeleo ya kutumia lugha katika vyombo vya habari. Hii ndiyo sababu mtafiti aliuliza maoni ya watafitiwa kuhusu usikizaji wa idhaa za Kimaragoli. Matokeo ya kundi la watoto yamewasilishwa katika jedwali 4.23:

**Jedwali 4.23: Tunapenda kusikiza idhaa za Kimaragoli**


| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 59 | 67.8 |
| Nakubali | 14 | 16.1 |
| Sina hakika | 5 | 5.7 |
| Sikubali | 4 | 4.7 |
| Sikubali kabisa | 5 | 5.7 |
| Jumla | 87 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Jedwali hili linaonyesha kwamba watafitiwa 59 (67.8%) wanakubali kabisa, 14 (16.1%) wanakubali, 5 (5.7%) hawakuwa na hakika, 4 (4.7%) hawakukubali na 5 (5.7%) hawakukubali kabisa. Matokeo yanaonyesha kwamba watafitiwa wengi 73 (83.9%) walionyesha mwelekeo chanya kwa kukubali wao husikiza idhaa za Kimaragoli kwa lengo la kujifundisha, kujikumbusha na kuendeleza Kimaragoli. Watafitiwa 5 (5.7%) hawakuwa na hakika kuhusu sababu inayowafanya kusikiza idhaa hizi huku 9 (10.4%) wakiwa maoni kwamba hawasikizi idhaa hizi kwa lengo la kujifundisha, kujikumbusha na kudumisha Kimaragoli

Miongoni mwa vijana wa miaka 18-35, watafitiwa 58 (70.7%) walikubali kabisa, 9 (11%) walikubali, 5 (6.1%) hawakuwa na hakika, 6 (7.3%) hawakukubali na 4 (4.9%) hawakukubali kabisa. Matokeo yamewasilishwa katika kielelezo 4.15:

**Kielelezo 4.15: Tunapenda kusikiliza idhaa za Kimaragoli**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Wengi wa watafitiwa 67 (81.7%) walikiri kusikiliza sana idhaa za Kimaragoli kwa lengo la kujifundisa, kujikumbusha na kudumisha Kimaragoli. Hii ina maana kwamba idhaa zinazotangaza kwa Kimaragoli kama vile Mulembe na Vuka ndizo maarufu sana katika maeneo haya kama ilivyobainishwa katika madhumuni ya kwanza. Wachache 10 (12.2%) walikuwa na maoni kinyume huku 5 (6.1%) wakikosa kuwa na uhakika. Matokeo haya yanathibitisha kuwepo kwa mwelekeo chanya miongoni mwa vijana Wamaragoli wanaoamini kuwa usikilizaji wa idhaa za Kimaragoli unachangia kuendelezwa kwa lugha yao.

Miongoni mwa kundi la watoto, watafitiwa 50 (66.7%) walikubali kabisa kwamba wanasikiliza idhaa za Kimaragoli, 5 (6.7%) walikubali, 1 (1.2%) hakuwa na uhakika, 14 (18.7%) hawakukubali na 5 (6.7%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya yanaonyesha kwamba watoto wengi wa Kimaragoli wanapenda kusikiliza idhaa za Kimaragoli zaidi dhidi ya wale ambao hawapendi. Mmoja tu alionyesha ukosefu wa uhakika wa kauli hii. Watoto wengi wanaosikiliza huenda inatokana na wazazi wao kusikiza idhaa hizi kwa kuwa redio inayotumika ndani ya nyumba ni moja. Mzazi anapoweka idhaa kama vile Vuka au Mulembe, watoto na vijana walio ndani ya nyumba wanalazimika kusikiza pia. Wasiopendelea ina maana kwamba wazazi wao au wao wenyewe wanasikiza idhaa nyinginezo za Kiswahili, Kiingereza na Kiluo hivyo za Kimaragoli hazipewi nafasi sana.

Matokeo ya utafiti huu yanaingiliana na utafiti wa Obiero (2008) aliyebainisha kwamba Kisuba kilihuishwa na kudumishwa kupitia teknolojia ya redio. Kwa mujibu wa nadharia ya Uzalishaji Kijamii, matumizi ya redio ni mkakati unaopangwa na wasemaji wa lugha kwa ajili ya kurithisha amana maalumu kwa wasikilizaji wake. Aidha, nadharia ya Uhuishaji wa Kiethnosimu, inadai kuwa kuwepo kwa msaada wa kitaasisi na kiasasi ni sehemu muhimu ya kudumisha lugha. Vyombo vya habari ni asasi muhimu inayosaidia kudumisha Kimaragoli miongoni mwa vijana. Haiwezekani kuanzisha idhaa za redio za Kimaragoli iwapo wasemaji wake hawaoni thamani yake na vivyo hivyo, haiwezekani wao pia kusikiliza iwapo hawaoni umuhimu wake katika maisha yao.

Kwa mujibu wa Obiero (2008) redio ni kifaa muhimu katika kuendeleza na kudumisha lugha asilia. Hivyo basi, matokeo haya yanathibitisha mahitimisho aliyofanya Obiero kuhusu matumizi ya redio kudumisha Kisuba kwamba kufufuka na kudumishwa kwa Kisuba kulitokana na mkakati wa kutumia redio kupitia vipindi mbalimbali vya mazungumzo na mafundisho katika Kisuba. Kuwepo kwa mwelekeo chanya wa


kupendelea matumizi ya redio miongoni mwa Wamaragoli ni ishara nzuri ya udumishaji wake.

#### 4.6.1.4 Uamiliaji na Ujifunzaji usio rasmi wa Kimaragoli

Kuamilia au kujifundisha lugha kusiko rasmi ni sehemu muhimu ya kutathmini mielekeo. Hii ndiyo sababu Pap (1979) katika Mohochi (2005) anasema kwamba mielekeo hujumuisha ujifunzaji/uamiliaji wa lugha. Hivyo, katika utafiti huu, ilikuwa muhimu kutathmini mielekeo kwa kuangalia namna watafitiwa walivyohisi kuhusu kujifunza au kufundishwa Kimaragoli, sasa na siku za baadaye. Katika sehemu hii, kauli zilikuwa tatu : ya kwanza ililenga watoto na vijana pekee kwa kuwa inachukuliwa kwamba wao ndio wanajifunza na kuamilia lugha zaidi ya makamo na wazee. Mtafiti alitaka kujua hali halisi ya lugha hii siku za usoni. Kauli ya pili ilizungumzia ufundishaji/uamiliaji na urithishaji wa Kimaragoli. Hii ilijumuisha makundi yote matatu. Kauli ya tatu aidha ilizingatia makundi yote. Hata hivyo, miongoni mwa vijana, swali lilibadilishwa kidogo kulenga ufundishaji/uamiliaji wa Kimaragoli siku za baadaye watakapoolewa.

Kwanza kabisa, miongoni mwa watafitiwa wa umri wa miaka 12-17, mtafiti alitaka maoni kuhusu kauli hii “Mimi sina muda kujifunza Kimaragoli”. Matokeo ya maoni yao yamewasilishwa katika Kielelezo 4.16:

**Kielelezo 4.16: Sina muda wa kujifunza Kimaragoli**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na maoni yao, watafitiwa 8 (10.7%) walikubali kabisa, 3 (4%) walikubali, 5 (6.7%) hawakuwa na hakika, 15 (20%) hawakukubali, 44 (58.6%) hawakukubali kabisa. Kwa ujumla, watafitiwa 59 (78.6%) walikiri kuwa na muda wa kujifunza Kimaragoli huku 11 (14.7%) wakikiri kukosa muda wa kijifunza Kimaragoli. Sababu kubwa ya watafitiwa kukiri kukosa muda ni mfumo wa elimu ambao unawatenga na wazazi au wanafunzi wenzao kwa muda mrefu. Hii ina maana kwamba baadhi ya wanafunzi wanasoma katika shule za mabweni ambako hawatangamani na wazungumzaji wa Kimaragoli. Vilevile, kwa kuwa hakuna somo la lugha za kiasili katika mfumo wa elimu wa Kenya kama ilivyokuwa hapo awali, wanafunzi wengi wanajikuta katika hali ngumu inayowalazimu kuzungumza Kimaragoli wakiwa nyumbani peke yake. Tatizo hili limejitokeza katika mahojiano na Mzee wa 2 aliyesema kwamba:


> **Mzee M**: *Hii kuvavolaku navutswa time yu kudinyirizaa mwana mu Llimi yiru y'oitaveho dave. Niva kurava navo mwivugana, mu commitees, onyoraza kutumikirii ruswahili. (Naam, tunawambia (wajifunze Kimaragoli) lakini muda wa kuwafundisha na kuwahimiza ndio mchache. Tukiwa nao kanisani, katika Kamati,unapata tunatumia Kiswahili. TY)* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Watoto wanapokosa watu wa kuwafunza lugha yao, huathirika kimwelekeo hivi kwamba wanaishia kupenda na kutumia lugha nyingine ambayo wana umilisi mkubwa. Hii ndio

maana Mohochi (2005) anakiri kwamba wazazi wanavyaza pakubwa mielekeo ya watoto wao. Mawazo haya yanathibitisha maoni ya mtafitiwa mmoja aliyesema kwamba ingawa baba ni Mmaragoli, amejifunza Kiluo kwa kuwa anakaa na mama kwa karibu mno. Waliokiri kuwa na muda wa kujifunza Kimaragoli walisema kwamba wamejifundisha lugha hii wakiwa nyumbani na wazazi wao pamoja na kukaa karibu na nyanya au babu. Ingawa mfumo wa shule unawazuia kukaa muda mrefu na wazazi wao, hauwanyimi kabisa fursa ya kujifunza Kimaragoli. Katika matokeo ya uchunzaji, mtafiti alitambua kwamba katika siku ya utamaduni wa Wamaragoli, wazee walikuwa wanafunza watoto masuala mbalimbali ya kale. Hata hivyo, tamasha hii ya utamaduni hutokea mara moja tu baada ya miaka 7 au 10 na hivyo si muda wa kutosha kufunza Kimaragoli kwa undani.

Pili, mtafiti pia alitaka kufahamu maoni ya watafitiwa kuhusu kauli "Kimaragoli kinafaa kuendelea kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee". Watafitiwa 49 (65.4%) katika kundi la watoto walikubali kabisa, 17 (22.7%) walikubali, 2 (2.6%) hawakuwa na hakika na 1 (1.3%) hawakukubali na 6 (8%) hawakukubali kabisa kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 4.17.

**Kielelezo 4.17: Kimaragoli kiendelee kufundishwa na kurithishwa**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kijumla, watafitiwa wengi 66 (88.1%) wanaelekea kukubali kwamba Kimaragoli kinastahili kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee siku za baadaye huku wachache 7 (9.3%) wakikosa kukubaliana na kauli hii. Watafitiwa 2.6% hawakuwa na hakika ikiwa Kimaragoli kinastahili kufundishwa na kurithishwa kwa vizazi vya baadaye. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba watafitiwa wengi wanaonyesha mwelekeo chanya kuhusu udumishaji wa lugha yao. Kizazi kichanga kinapoonyesha mwelekeo chanya kama huu inadhihirisha uwezo wa Kimaragoli kujidumsha siku za baadaye licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Sababu kubwa ya wachache kupinga uchanya wa kauli hii ni kuwepo kwa baadhi ya watoto ambao wazazi wao wanajali Kiluo zaidi ya Kimaragoli na hawaoni haja ya kuwepo kwa Kimaragoli.

Tatu, mtafiti aliuliza maoni yao kuhusu kauli "Mimi hufundisha watoto wetu na marafiki Waluo Kimaragoli". Watafitiwa 33 (44%) walikubali kabisa, 15 (20%) walikubali, 13 (17.3%) hawakuwa na hakika, 8 (10.7%) hawakukubali, 6 (8%) hawakukubali kabisa kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 4.24:

**Jedwali 4.24: Mimi hufundisha watoto wetu na marafiki Waluo Kimaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 33 | 44 |
| Nakubali | 15 | 20 |
| Sina hakika | 13 | 17.3 |
| Sikubali | 8 | 10.7 |
| Sikubali kabisa | 6 | 8 |
| Jumla | 75 | 100.0 |


(Chanzo: Data ya nyanjani)

Maoni ya wengi 48 (64%) ni kwamba wanajizatiti kufunza watoto wao, wakiwemo wanaozungumza Kiluo, lugha ya Kimaragoli huku 13 (17.3%) wakikosa kuwa hakika na 14 (18.7%) wakikiri kutofunza watoto wao na marafiki wa Kiluo lugha ya Kimaragoli. Uamiliaji na ufundishaji usorasmi wa Kimaragoli miongoni mwa watafitiwa katika kundi hili inajumuisha kuwasaidia kufahamu salamu za Kimaragoli, majina ya viumbe na

mimea na kadhalika. Vilevile, watoto wanapocheza na wenzao, wanahakikisha kwamba mazungumzo yanafanyika katika Kimaragoli. Kutokana na mfumo wa elimu unaowafungia wengi shuleni, uamiliaji na ufundishaji huu usorasmi hufanyika wakiwa njiani wakitoka shuleni, wakiwa malishoni, nyumbani, wakiogelea, wakiwinda na kadhalika. Wanaosomea shule za mabweni husubiri wafunge shule ndipo waweze kutagusana na lugha hii ya Kimaragoli. Katika uchunzaji wetu, hasa maeneo ya Lwala na Bware, mtafiti alitambua kwamba watoto wanaozungumza Kimaragoli walikuwa wanacheza na wenzao wa jamii ya Luo kwa kutumia Kimaragoli. Hili linajitokeza katika mahojiano na mojawapo ya Mzee, aliyetilia hoja hii mkazo kwa kudai kwamba watoto wa jamii hizi mbili hawana tatizo la kuzungumza lugha hizi mbili. Wanapotumia lugha hizi kwa mpishano, basi wanafundishana maneno na matumizi yake katika lugha hizi zote. Kwa kuwa kiwango chao cha kubwia msamiati ni kizuri, wanaishia kufahamu maneno ya Kimaragoli na kuyatumia hata wanapokua siku za baadaye.

Kutokana na takwimu za kidemografia katika kundi hili la miaka ya 18-35, watafitiwa 57 walikuwa wameolewa hivyo hawakujibu swali hili. Mtafiti alilenga hasa watafitiwa ambao walikuwa hawajaoa au kuolewa. Majibu yao yamesilishwa katika kielelezo 4.18:

**Kielelezo 4.18: Nikioa/olewa haitakua lazima watoto wangu wajue Kimaragoli**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Watafitiwa 2 (8%) walikubali kabisa, 3 (12%) walikubali, 3 (12%) hawakuwa na hakika, 5 (20%) hawakukubali, 12 (48%) hawakukubali kabisa. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba idadi ya watakaowapa watoto wao uhuru wa kujifunza au kutojifunza lugha ya Kimaragoli ni 20% dhidi ya 68% waliokubali kwamba watoto wao lazima wajue Kimaragoli na 3 (12%) hawajui kama watawapa watoto wao uhuru au watawashurutisha kujua Kimaragoli. Katika 3 (12%) ya waliokosa uhakika, wote walikuwa wa jinsia ya kike. Kutokuwa na hakika huku kunamaanisha kwamba wasichana hawa watapofika umri wa kuchumbiwa, hawajui kama wataolewa hatimaye kwa Mluo au Mmaragoli. Katika jumla ya watafitiwa 5 (20%) ambao walikiri haitakuwa lazima, wanne waliteua Kiswahili kama lugha ambayo wana umilisi mkubwa kuliko Kimaragoli huku mmoja akisema lugha yake ya kwanza ni Kiluo licha ya kwamba mzazi wake mmoja ni Mmaragoli. Hii ina maana kwamba baadhi yao kukosa kuzungumza au kuwa na umilisi tosha wa Kimaragoli katika ujana wao huenda ukaathiri lugha ambayo itatumika katika ndoa na hivyo kutoonyesha uhakika kuhusu kufundisha watoto wao Kimaragoli.

Ujifunzaji wa lugha huhitaji muda wa kutosha. Wasemaji wanapotenga muda wa kukaa na wazazi, vijana, wazee na watu wengine kwa ajili ya kuzungumza na kuamilia lugha huwa ishara ya mwelekeo chanya wa lugha. Katika kutambua mwelekeo wa vijana wa Kimaragoli kuhusu lugha yao, mtafiti alitaka maoni yao kuhusu wao kuwa au kutokuwa na muda wa kujifunza Kimaragoli. Majibu yao yamewasilishwa katika jedwali 4.25:

**Jedwali 4.25: Mimi kama kijana sina muda wa kujifunza Kimaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 13 | 15.9 |
| Nakubali | 17 | 20.7 |
| Sikubali | 8 | 9.8 |
| Sikubali kabisa | 44 | 53.6 |
| Jumla | 82 | 100.0 |


(Chanzo: Data ya nyanjani)

Jedwali hili linaonyesha kwamba watafitiwa 13 (15.9%) walikubali kabisa, 17 (20.7%) walikubali, 8 (9.8%) hawakukubali na 44 (53.6%) hawakukubali kabisa. Kijumla, watafitiwa 30 (36.6%) walikiri kukosa muda wa kujifunza Kimaragoli dhidi ya 52 (63.4%) waliosema wana muda wa kujifunza Kimaragoli. Hii ina maana kwamba asilimia kubwa ya vijana wanaozungumza Kimaragoli wana mwelekeo chanya kuhusu lugha yao. Kukosa muda wa kujifunza Kimaragoli kunatokana na sababu mbalimbali zikiwemo kukaa katika mfumo wa elimu unaowanyima muda wa kutosha kukaa nyumbani na wazazi au ndugu zao; kuzaliwa na kukulia mijini; baadhi ya wazazi kutojali Kimaragoli kutokana na sababu ya mzazi mmoja kuzungumza Kiluo na kadhalika. Hii basi ina maana kwamba mtagusano wao na wazee au watu walio na umilisi mkubwa wa Kimaragoli ni finyu kutokana na kukosa muda. Watafitiwa 63.4% waliokuwa na maoni tofauti walikiri wana muda wa kutosha kujifunza Kimaragoli kwa sababu katika kukua kwao siku nyingi, wameishi na wazazi, maajuza na watu wa ukoo ambao waliwafunza Kimaragoli. Hata mtafitiwa mmoja alikiri kuishi maeneo ya Chavakali (Kaunti ya Vihiga) kwa muda mrefu ujombani alikojifunzia Kimaragoli kabla ya kurudi kwao Uriri.

Hii ndiyo sababu walipoulizwa wapi wamejifundishia Kimaragoli, asilimia kubwa walikiri kujifundishia nyumbani. Hivyo basi, licha ya kuwa katika shule za bweni, kufanya kazi za boda boda, ukulima, hii haiwanyimi fursa ya kujifundisha na kuongea Kimaragoli. Njia nyepesi ambayo wametumia kujifundisha Kimaragoli ni kupitia kwa mazungumzo na wenzao. Matokeo haya yanathibitisha utafiti aliofanya Obiero (2008) kuhusu uhuishaji wa Kisuba kwamba wazee walichukua muda mrefu kufundisha vijana lugha yao, wakaihuisha na hadi sasa, wanaidumisha.

Watafitiwa waliulizwa maoni yao kuhusu kauli "Kimaragoli kinafaa kuendelea kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee" na maoni yao yamewasilishwa katika kielelezo 4.19:

**Kielelezo 4.19: Maoni ya Vijana kuhusu Kimaragoli kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na kielelezo hiki, watafitiwa 66 (80.5%) walikubali kabisa, 9 (11%) walikubali, 2 (2.4%) hawakukubali na 5 (6.1%) hawakukubali kabisa. Jumla ya wanaokubali Kimaragoli kiendelee kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee ni 91.5% dhidi ya 8.5% wanaopinga kauli. Hii ina maana kwamba vijana wengi katika eneobunge

la Uriri kwa jumla wanaamini kwamba njia bora ya kudumisha Kimaragoli ni kuhakikisha kinafundishwa na kurithishwa kizazi baada ya kizazi. Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Strubell (2001) aliyetambua kwamba njia nzuri ya kudumisha lugha asili kizazi baada ya kizazi ni kuhakikisha kwamba inafundishwa na kuzungumzwa. Hata hivyo, yanapinga matokeo ya Perlin (2009) kwamba vijana wanaozungumza Kitirung hawakupendelea kufundishwa wala kudumisha lugha yao na badala yake, waliamua kujifunza na kudumisha Kichina. Kwa mujibu wa nadharia ya Uzalishaji Kijamii, lugha kama amana ya jamii hudumu muda mrefu inaporithishwa kupitia kwa mazungumzo ya kila mara. Hii ndiyo sababu watafitiwa wa kundi hili walikiri kujifunza lugha hii na kuitumia wakiwa katika mazingira ya nyumbani.

Katika kundi la makamo na wazee, watafitiwa waliulizwa kutoa maoni kuhusu kauli "Mimi hufundisha watoto wangu na marafiki Waluo Kimaragoli". Matokeo yanaonyesha kwamba 66 (75.8%) walikubali kabisa na kauli, 14 (16.1%) walikubali, 4 (4.7%) hawakukubali na 3 (3.4%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.26: Mimi hufundisha watoto wangu na marafiki Waluo Kimaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 66 | 75.8 |
| Nakubali | 14 | 16.1 |
| Sikubali | 4 | 4.7 |
| Sikubali kabisa | 3 | 3.4 |
| Jumla | 87 | 100.0 |


(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo haya yanadhihirisha mielekeo chanya kuhusu makamo na wazee kufundisha watoto wao Kimaragoli pamoja na marafiki zao wa Kiluo. Kwa ujumla, watafitiwa 80 (91.9%) walikiri kufundisha watoto wao na marafiki zao Kimaragoli. Asilimia hii ya juu inaenda sambamba na swali lililoulizwa ikiwa marafiki wa Kiluo wa watafitiwa

wanaongea Kimaragoli. Kijumla, watafitiwa walisema kwamba 62.1% ya marafiki zao wa Kiluo wanaongea Kimaragoli huku 37.9% wakisema hawaongei Kimaragoli. Walipoulizwa waseme hawa marafiki zao walijifunzia wapi, maoni ya wengi yalionyesha kwamba walijifundishia shuleni miaka mingi Kimaragoli kilipokuwa kinafundishwa. Aidha, walijifunza kutoka kwa majirani, marafiki wakiwa vikaoni kama vile sehemu za burudani, wakiwa mawindoni na kuogelea siku zao za utotoni. Pia, wengine waijifunzia kanisani na kazini. Hii inaonyesha kwamba kudumishwa kwa Kimaragoli kumefaulu tangu siku za kale hadi sasa kutokana na kuwa na mwelekeo chanya kuhusu Kimaragoli kiasi cha kufunza watoto wao pamoja na marafiki wa Kiluo.

Lugha inapoendelea kufundishwa na kurithishwa vizazi baada ya vizazi, huwa ni ishara nzuri ya mwelekeo chanya miongoni mwa wasemaji wake. Hivyo basi, mtafiti alitaka maoni ya watafitiwa wa kundi la makamo na wazee (miaka 36 na zaidi) kuhusu kufundishwa na kurithishwa Kimaragoli ili kisipotee. Kielelezo 4.20 kinaonyesha matokeo ya kauli hii.

**Kielelezo 4.20 Maoni ya makamo na wazee kuhusu Kimaragoli kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo yanaonyesha kwamba watafitiwa wengi 76 (87.4%) walikubali sana na kauli, 4 (4.6%) walikubali na 7 (8%) hawakuwa na hakika na kauli. Kijumla, watafitiwa 80 (92%) walidhihirisha mwelekeo chanya kwa kukubaliana na kauli huku 7 (8%) wakikosa uhakika. Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watafitiwa wanaotaka Kimaragoli kiendelee kufundishwa na kurithishwa ili kisipotee inadhihirisha mwelekeo chanya kuhusiana na udumishwaji wa lugha hii. Hii pia ina maana kwamba kundi hili la watafitiwa linafanya kila juhudi kuhakikisha vizazi vinavyofuata vinaweza kuzungumza lugha hii. Watafitiwa 7 (8%) waliopinga kauli wanajumuisha wazawa wa Kiluo ambao wameolewa kwa Wamaragoli. Kwa kuwa wana lugha yao ya Kiluo, hawaoni haja ya kuendeleza na kurithisha lugha ambayo hawajui kuizungumza vyema.

#### 4.6.1.5 Heshima ya lugha miongoni mwa wasemaji wa Kimaragoli

Kwanza, katika utafiti huu, watafitiwa wa miaka kati ya 12-17 walitakiwa kutoa jibu kuhusu kauli, "Kiluo kinatupa heshima kubwa kuliko Kimaragoli". Jedwali 4.27 linaonyesha majibu yao:

**Jedwali 4.27: Kiluo kinatupa heshima kubwa kuliko Kimaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 7 | 9.4 |
| Nakubali | 6 | 8 |
| Sina hakika | 17 | 22.6 |
| Sikubali | 11 | 14.7 |
| Sikubali kabisa | 34 | 45.3 |
| Jumla | 75 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kutokana na jedwali hili, watafitiwa 7 (9.4%) walikubali kabisa, 6 (8%) walikubali, 17 (22.6%) hawakuwa na hakika, 11 (14.7%) hawakukubali, 34 (45.3%) hawakukubali kabisa. Kwa jumla, wale ambao wanahisi Kiluo kinawapa heshima kubwa kuliko Kimaragoli ni 13 (17.4%) huku 45 (60%) wakihisi tofauti na 17 (22.6%) wakikosa uhakika wa lugha inayowapa heshima maeneo ya Uriri. Idadi hii kubwa ya wanaohisi Kimaragoli kinawapa heshima kubwa katika eneo la Uriri ni kutokana na wao kutambua


thamani ya Kimaragoli kama kitambulisho chao halisi. Hii ndiyo sababu katika maoni yao, baadhi walisema kwamba:

> **Mtafitiwa D**: *Kwa sababu nafuata kimila cha baba na mama (miaka 14)*
> **Mtafitiwa E***: Kwa sababu nafuata kimila cha ukoo (miaka 13)*
> (Chanzo: Data ya Mtafiti)

Maoni ya watafitiwa hawa yanaonyesha jinsi ambavyo wanapenda kujitambulisha na lugha ambayo imekuwa kitambulisho cha ukoo wao kuanzia miaka ya kale. Watafitiwa 17.4% waliokiri Kiluo kinawapa heshima ni kwa sababu kwanza, baadhi yao wamekuwa wakitangamana na Waluo katika nyanja zote za maisha yao-kanisani, michezoni, shuleni, njiani, sokoni, malishoni, kuogelea kwa pamoja na kadhalika. Pili, baadhi ya wazazi wa watoto hawa hawaonyeshi ari ya kuendeleza Kimaragoli, na badala yake, wanaongea Kiluo. Hii ndiyo maana hawaamini kwamba Kimaragoli ambacho hawaongei au hawajui, kinaweza kuwapa heshima maeneo haya ya Uriri. Watafitiwa 22.6% waliokosa uhakika huenda ni kwa sababu wameanza kutilia shaka nafasi ya Kimaragoli katika eneo la Uriri lakini bado hawajakubali lugha ya Kiluo.

Mbali na kutaka kujua ikiwa Kiluo kinawapa heshima eneo la Uriri, mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa watoto wa umri wa kati ya miaka 12-17 ikiwa jamii zingine zinaheshimu Kimaragoli katika eneo la Uriri. Majibu yao yamewasilishwa katika Kielelezo kifuatacho:

**Kielelzo 4.21: Kimaragoli kinaheshimiwa na kabila zingine Uriri**




(Chanzo: Data ya nyanjani)


Kutokana na kielelezo hiki, 20 (26.7%) walikubali kabisa, 15 (20%) walikubali, 12 (16%) hawakuwa na hakika, 16 (21.3%) hawakukubali, 12 (16%) hawakukubali kabisa. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba lugha ya Kimaragoli inaheshimiwa na jumla ya watafitiwa 35 (46.7%) huku wanaoamini Kimaragoli hakina heshima miongoni mwa makabila mengine wakiwa 28 (37.3%). Kuwepo kwa heshima ni kwa sababu ya uhusiano mwema uliopo kati ya Wamaragoli na wasemaji wa lugha zingine kama vile Kiluo, Kikurya na kadhalika. Kuwepo kwa watafitiwa wanaodai Kimaragoli hakipewi heshima ni kwa sababu baadhi yao walidai kwamba Kimaragoli ni lugha chafu. Watafitiwa 12 (16%) ambao walikosa uhakika huenda ni kutokana na wao kuwa katika familia ambayo mzazi mmoja ni Mluo na mwingine ni Mmaragoli hivyo hawajafanya uamuzi dhabiti kuhusu mwelekeo wao kwa Kimaragoli.

Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Odero (2013) aliyetambua kwamba Waelmolo walihisi kutopewa heshima na Wasamburu na hivyo kusababisha wao kuhamia lugha ya Kisamburu. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wa Odero kwa sababu japo Wamaragoli wanahisi Kiluo kinawapa heshima, hawajahamia lugha ya Kiluo bali

wanadumisha lugha yao. Katika mchakato wa udumishaji lugha, kadiri jamii na lugha yake inapozidi kupewa heshima, ndivyo inavyozidi kujidumisha na heshima inapopungua, uwezekano mkubwa wa kuhamia lugha nyingine ya satua kubwa huwepo. Heshima hii inatokana na Kimaragoli kutumika katika siasa na nyadhifa mbalimbali za utawala wa Kaunti, wasemaji wake kuwa viongozi wakubwa kanisani, kuonyesha mfano bora unaopendeza wanajamii wengine miongoni mwa matendo mengine yanayoweza kukweza Kimaragoli na wasemaji wake.

Ilikuwa muhimu pia kujua ikiwa Wamaragoli wanaheshimu lugha na jamii nyingine katika eneo la Uriri. Majibu yao yamewasilishwa katika chati duara ifuatayo:

**Kielelezo 4.21: Heshima ya Wamaragoli kwa lugha zingine**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba watafitiwa 21 (28%) walikubali kabisa, 26 (34.7%) walikubali, 2 (2.6%) hawakuwa na hakika, 4 (5.3%) hawakukubali, 22 (29.4%) hawakukubali kabisa na kauli ya utafiti. Kijumla, watafitiwa 47 (62.7%) wanaheshimu lugha nyinginezo huku 26 (34.7%) wakikiri kukosa kuheshimu lugha nyinginezo na asilimia ndogo (2.6%) wakikosa uhakika. Udumishwaji wa lugha katika eneo maalumu la wingilugha hutegemea sana jinsi wanajamii wanavyohusiana kila siku. Panapokuwa na


heshima pande zote, lugha zote hudumishwa, na heshima inapopungua, kiwango cha udumishwaji lugha huanza kuyumba na kusababisha kundi dogo kuhamia lugha ya wengi. Kuwepo kwa heshima kati ya Kimaragoli na lugha zingine na lugha hizi na Kimaragoli ni sababu mojawapo ya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa Uriri. Kuwepo kwa baadhi ya watafitiwa wanaokosa kuheshimu lugha nyinginezo kunatokana na mielekeo hasi ya kijamii inayosababishwa na mambo kama vile siasa zinazozua vita, kubeza Kimaragoli kuwa ni lugha chafu na kutopendwa kwa kuwa wao ni walowezi wanaostahili kurudishwa kwao. Sababu hizi zinachangia Wamaragoli kukosa kuheshimu lugha ya Kiluo.

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, mtafiti alitaka kujua iwapo Kiluo kinawapa heshima kuliko Kimaragoli. Watafitiwa 2 (2.4%) walikubali kabisa, 5(6.1%) walikubali, 3 (3.7%) hawakuwa na uhakika, 12 (14.6%) hawakukubali na 60 (73.2%) hawakukubali kabisa. Kijumla, matokeo haya yanaonyesha kwamba watafitiwa 72 (87.8%) walikaaa kwamba Kiluo kinawapa heshima eneo la Uriri dhidi ya 7(8.2%) waliopata heshima kutokana na kujua na kuzungumza kiluo na 12 (14.6%) waliokosa uhakika. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba wanaoamini Kimaragoli kinawapa heshima kuliko Kiluo ni wengi na hivyo ishara ya mwelekeo chanya. Waliokiri kupata heshima kutokana na Kiluo ni kwa sababu baadhi baba ni Mluo huku mama akiwa Mmaragoli na pia baadhi wanajinasibisha na Kiluo zaidi ya Kimaragoli. Hii inaendana na hoja ya uchumi kwamba wanapozungumza Kiluo wanapotafuta kazi, wanaheshimiwa na hivyo uwezekano wa kupata kazi au pato ni wa juu.

Miongoni mwa watafitiwa wa miaka 18-35, mtafiti alitaka kujua iwapo Kimaragoli kinaheshimiwa na jamii zingine Uriri. Watafitiwa 19 (23.3%) walikubali kabisa, 23

(28%) walikubali, 27 (32.9%) hawakuwa na hakika, 6 (7.3%) hawakukubali, 7 (8.5%) hawakukubali kabisa kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo 4.22

**Kielelezo 4.22: Maoni ya Makamo na Wazee kuhusu Kimaragoli kuheshimiwa na kabila zingine hapa Uriri**




(Chanzo: Data ya nyanjani**)**

Kwa ujumla, wanaokubali kwamba Kimaragoli kinaheshimiwa Uriri ni 42 (51.3%) huku 13 (15.8%) wakipinga kauli hii na 27 (32.9%) wakikosa uhakika. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba Wamaragoli 42 (51.3%) wanahisi kuwa wasemaji wa lugha za Kiluo, Kikurya na kadhalika wana mwelekeo chanya kuhusu udumishaji wa lugha ya Kimaragoli ikilinganishwa na 13 (15.8%) wanaohisi kuwa jamii zingine haziheshimu Kimaragoli na hivyo kuwa na mwelekeo hasi kwacho. Kuheshimiwa huku kunatokana na ushirikiano wa kidini na kiuchumi kati ya wasemaji wa Kimaragoli na lugha nyinginezo, hasa Kiluo na pia uhusiano mwema ambao umedumu katika ya Wamaragoli na jamii zingine. Kukukosa kuheshimiwa kunatokana na kuwa na mila tofauti na jamii ya Waluo. Mahojiano na Nyanya 2 yalionyesha kwamba Waluo wanadharau Wamaragoli kwa kuwaita “Jomwa”, “mwache” na “jamarandeu” (wale watu), majina ambayo wanahisi yanaendeleza mwelekeo hasi kwa kuwa ni maneno ya madharau. Aidha, wengine wanaita lugha ya Kimaragoli, “lugha chafu”. Sababu mojawapo iliyowafanya

Wamaragoli kufukuzwa katika maeneo ya Katieno na Kawere ni kutokana na kudharauliwa kisiasa, kiuchumi na kitamaduni na kuchukuliwa kama ‘walowezi’ waliokuja kuwanyang’anya wenyeji mashamba yao. Idadi kubwa ya wasemaji wa Kimaragoli ambao hawana uhakika kuhusu heshima ya Kimaragoli huenda ni kwa sababu 27 (32.9%) hawathamini Kimaragoli au hawafahamu dhana ya heshima kwa lugha.

Kwa kuwa heshima ni tendo la kuchagizana, mtafiti alitaka kujua ikiwa Wamaragoli nao wanaheshimu lugha zingine na jamii zao kwa ujumla. Majibu ya watafitiwa wa umri wa kati ya 18-35 yamewasilishwa kiumaratokezi katika jedwali 4.28:

**Jedwali 4.28: Wamaragoli tunaheshimu lugha zingine Uriri**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 22 | 26.8 |
| Nakubali | 16 | 19.5 |
| Sina hakika | 29 | 35.4 |
| Sikubali | 5 | 6.1 |
| Sikubali kabisa | 10 | 12.2 |
| Jumla | 82 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Watafitiwa 22 (26.8%) walikubali kabisa, 16 (19.5%) walikubali, 29 (35.4%) hawakuwa na hakika, 5 (6.1%) hawakukubali, 10 (12.2%) hawakukubali kabisa. Kutokana na majibu yao, jumla ya watafitiwa 38 (46.3%) wakikiri kuheshimu Kiluo, Kikisii, Kikurya, Kisomali na lugha nyinginezo. Watafitiwa 15 (18.3%) walikiri kutoziheshimu lugha hizi na 29 (35.4%) hawakuwa na hakika. Matokeo haya yanaonyesha kwamba heshima ni suala la nipe nikupe. Wanaohisi Kimaragoli hakiheshimiwi ni wale wale ambao hawaoni haja ya kuheshimu lugha zingine. Kwa mujibu wa Mohochi (2008) ujenzi wa mielekeo hasi kuhusu jamii moja na lugha yao hutokana na jinsi wanavyotazama jamii nyinginezo. Aidha, hutokana na mahitimisho ambayo wasemaji wake hufanya kutokana na maneno

wanayosikia na matendo wanayoshuhudia wakifanyiwa na jamii nyinginezo. Mielekeo hii hivyo basi inapoumbika, huhamishwa kwa jamii inayowadharau. Katika muktadha huu, Wamaragoli wanaohisi Kimaragoli kinadharauliwa huhamisha hisia hizo za madharau kwa jamii ya Waluo. Katika mahojiano na watafitiwa mbalimbali, hakukuwepo jina la madharau kwa Waluo kama yalivyokuwa majina kadhaa yanayoonyesha Waluo wakikejeli na kudharau Wamaragoli. Wanaohisi Kimaragoli kinaheshimiwa kwa sababu kinatumiwa katika siasa, dini, biashara, sherehe za kijamii na maeneo mengine ambako Kiluo kinatumika, vilevile, wanahamisha hiyo heshima kwa Kiluo na lugha zingine kama vile Kikurya na Kikisii.


Matokeo ya kauli hii na iliyotangulia yanaonyesha mfanano mkubwa. Kwanza, watafitiwa chini ya 50% wanaonyesha kwamba wanaheshimu lugha zingine na Kimaragoli kinaheshimiwa. Pili, 32.9% hawakuwa na uhakika ikiwa Kimaragoli kinaheshimiwa na hii si tofauti mno na wale (35.4%) ambao hawana uhakika ikiwa wanaheshimu lugha zingine. Tatu, 46.3% wanaamini kuwa Wamaragoli wanaheshimu lugha zingine dhidi ya 51.3% wanaohisi Kimaragoli kinaheshimiwa na wengine.

Katika kundi la makamo na wazee, matokeo ya kauli “Kiluo kinatupa heshima kuliko Kimaragoli”, watafitiwa 2 (2.3%) walikubali kabisa, 3 (3.4%) walikubali, 8 (9.2%) hawakukubali na 74 (85.1%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya kwa ujumla yanaonyesha kwamba wengi wa watafitiwa zaidi ya miaka 36  82 (94.3%) wanapata heshima yao kutokana na kuzungumza Kimaragoli kuliko Kiluo ikilinganishwa na 5 (5.7%) waliokiri wanapata heshima kutokana na Kiluo. Hakuna aliyekosa kuwa na uhakika katika kauli hii. Kuwepo kwa asilimia ya juu zaidi ikilinganishwa na makundi mengine ni kutokana na hali kwamba makamo na wazee aghalabu wana mazoea ya

kuzungumza Kimaragoli. Baadhi yao wamestaafu kwa muda mrefu na hivyo wamezoea kuzungumza Kimaragoli badala ya lugha nyingine.

Katika kundi la makamo na wazee, matokeo yanaonyesha kwamba katika kauli "Tunaheshimu lugha zingine", watafitiwa 77 (88.6%) walikubali kabisa na kauli, 3 (3.4%) walikubali, 6 (6.9%) hawakuwa na hakikana 1 (1.1%) hawakukubali. Matokeo haya yamewasilishwa katika kielelezo 4.23:

**Kielelezo 4.23 Tunaheshimu lugha zingine Uriri**





(Chanzo: Data ya nyanjani)

Jumla, watafitiwa 80 (92%) wanathibitisha heshima na mwelekeo chanya ulioko miongoni mwa Wamaragoli kuhusu wasemaji wa lugha nyinginezo kama vile Kiluo, Kikurya, Kisomali, Kikisii na kadhalika ikilinganishwa na 1.1% ambao walielekea kuonyesha mwelekeo hasi kabisa kuhusu lugha zingine. Hii ina maana kwamba Wamaragoli wanapoheshimu lugha zingine, pia wao wanapewa heshima katika kuzungumza lugha yao na hivyo kuidumisha. Kuwepo kwa watafitiwa wengi katika kundi hili wanaoheshimu lugha zingine huenda ni kutokana na kutangamana kwa muda mrefu na wasemaji wa lugha zingine.

Mbali na Wamaragoli kuheshimu lugha zingine, mtafiti alitaka maoni ya makamo na wazee kuhusu ikiwa wanahisi Kimaragoli kinaheshimiwa na wasemaji wa lugha zingine, hasa Kiluo. Matokeo haya yamewasilishwa katika Kielelezo 4.24:

**Kielelezo 4.24: Lugha yetu inaheshimiwa na Wengine Uriri**




(Chanzo: Data ya nyanjani)

Matokeo yanaonyesha kwamba 45 (51.7%) walikubali kabisa, 12 (13.8%) walikubali, 25 (28.7%) hawakuwa na hakika, 1 (1.1%) hawakukubali na 4 (4.7%) hawakukubali kabisa. Kwa ujumla, watafitiwa 57 (65.5%) walionyesha mwelekeo chanya kwa kudai kwamba wasemaji wa lugha zingine, hasa Waluo, wanaheshimu Kimaragoli ikilinganishwa na 5 (5.8%) waliodhihirisha mwelekeo hasi kwa kusema kwamba Kimaragoli hakiheshimiwi. Baadhi ya maoni ambayo yalitolewa katika hojaji ni: Kimaragoli ni lugha chafu, haina heshima na ni mbaya. Hata hivyo, watafitiwa waliokuwa na maoni haya hawakuonyesha uchafu au ubaya wake. Kuwepo kwa mwelekeo chanya miongoni mwa Waluo kuhusu Kimaragoli ndiko kumesaidia lugha hii kudumishwa kwa kipindi hiki kirefu tangu kuhamia eneo la Uriri.

#### 4.6.1.6 Utambulisho kama Mzungumzaji wa Kimaragoli

Msemaji kujitambulisha na lugha au jamii yake huashiria mwelekeo chanya na anapoogopa, huonyesha kwamba anaonea haya jamii yake pamoja na tamaduni zake, na

hivyo mwelekeo hasi. Hii ndiyo sababu mtafiti alitaka kujua ikiwa watafitiwa walikuwa wanapenda kujitabulisha kama Wamaragoli. Kwa kuwa utambulisho ni hali inayoendana na ukomavu wa akili tambuzi, mtafiti aliwauliza vijana na makamo na wazee pekee.

Matokeo katika kundi la vijana wa miaka 18-35 yanaonyesha kwamba watafitiwa 42 (51.3%) walikubali kabisa, 32 (39%) walikubali, 2 (2.4%) hawakukubali na 6 (7.3%) hawakukubali kabisa. Matokeo haya yamewasilishwa katika jedwali 4.29:

**Jedwali 4.29: Mimi kijana hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 42 | 51.3 |
| Nakubali | 32 | 39 |
| Sikubali | 2 | 2.4 |
| Sikubali kabisa | 6 | 7.3 |
| Jumla | 82 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kwa ujumla, watafitiwa 74 (90.3%) wanapenda kujitambulisha kama Wamaragoli huku 8 (9.7%) wakikiri kutojitambulisha kama Wamaragoli. Asilimia hii kubwa ina mwelekeo chanya kuhusu lugha yao ikilinganishwa na wachache wanaodhihirisha mwelekeo hasi. Wengi waliokubali kujitambulisha kama Wamaragoli walisema Kimaragoli kinawapa fahari kubwa wanapozungumza, kinawapa kitambulisho cha kijamii nchini na pia kinawasaidia kuwapa upekee katika sherehe za kitamaduni. Sababu ya 8 (9.7 %) kutojitambulisha kama Wamaragoli ni kwa sababu mzazi wao mmoja ni Mluo na pia hawajui kuongea Kimaragoli.

Katika kundi la makamo na wazee, matokeo yanaonyesha kwamba watafitiwa 62 (71.3%) walikubali sana na kauli, 9 (10.3%) walikubali, 1 (1.1%) hawakukubali na 15 (17.3%) hawakukubali kabisa. Kijumla, watafitiwa 71 (81.6%) walionyesha mwelekeo chanya huku 16 (18.4%) wakiwa na mwelekeo hasi kuhusu kujitambulisha kama Mmaragoli. Matokeo haya yamewasilishwa katika jedwali 4.30 :

**Jedwali 4.30: Mimi Mzee hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| Nakubali kabisa | 62 | 71.3 |
| Nakubali | 9 | 10.3 |
| Sikubali | 1 | 1.1 |
| Sikubali kabisa | 15 | 17.3 |
| Jumla | 87 | 100.0 |

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kuwepo kwa mwelekeo chanya kunamaanisha watafitiwa wanaonea fahari lugha yao kiasi cha wao kujitambulisha na jamii yao. Matokeo haya yanatomelewa na yale ya uchunzaji ambapo mtafiti alitambua Wamaragoli, hasa makamo na wazee, walikuwa wanapenda kujitambulisha kama Wamaragoli katika sherehe ya Utamaduni wa Mmaragoli na pia katika baadhi ya mikutano ya kisiasa. Mmojawapo wa mwanasiasa aliyekuwa anawania wadhifa wa Useneta alijitambulisha kama Mmaragoli ijapokuwa mzazi wake mmoja ni Mmragoli na mwingine Mkurya. Lengo kubwa la utambulisho katika siasa lilikuwa ni kutaka kuungwa mkono kama 'mtu wetu' na hivyo kuvutia wapigaji kura wengi wa Kimaragoli. Watafitiwa 16 (18.4%) waliopinga kauli hii walikuwa kwanza, wazawa wa Kiluo ambao wameolewa kwa Wamaragoli na pili, baadhi ya Wamaragoli wanaodhani kwamba kujitambulisha kama Mmaragoli ni kuendeleza ukabila hivyo wanapenda kujitambulisha kama Wakenya tu.

### 4.6.2 Mielekeo ya Waluo kuhusu Kimaragoli

Utafiti huu ulitaka kujua hali halisi ya wasemaji wa Kiluo na mchango wa mielekeo yao katika kudumisha Kimaragoli. Data ya matokeo haya ilitokana na mjadala wa kundi lengwa.

#### 4.6.2.1 Kujifunza Kimaragoli tangu utotoni

Wasemaji wengi wa Kiluo wanaoishi Uriri walionyesha ari kubwa ya kujifunza Kimaragoli wakiwa utotoni hadi utu uzima. Mwelekeo huu chanya uliokuzwa na mazingira ya kiutangamano unaonyesha kwamba lugha ya Kimaragoli haikuchukiwa wala wazazi wa Kiluo kukataza watoto wao kuizungumza. Ujifunzaji huu ulifanyika katika mazingira ya shule, nyumbani, malishoni, michezoni na kadhalika. Kwa mfano, baadhi ya wanakikundi walidai kwamba:

> **Baba M:** *Unajua ndugu yangu, sisi wengi hapa wanaume tumekua na hawa Wamaragoli wetu. Tangu tukiwa watoto. Shule moja. Kucheza mahali pamoja. Tumekula mahali pamoja na tumefanya mambo mengi sana. Sasa Kimaragoli na Kiluo ndizo zilikuwa lugha zetu sote. Tunacheza na kuongeleshana lugha zote kwa wakati mmoja.*
> **Mama F***: Mimi nimeishi Kakrao siku zangu tangu kuzaliwa. Ilikuwa bahati nzuri nikawa kanisa moja na Mama Mercy. Sasa nimekuwa nikiongea Kimaragoli kuanzianikiwa mtoto tu.*
> **Bwana L***: Watu wengi hapa tunaongea Kimaragoli kwa sababu tumeishi na Wamaragoli. Mimi nimezaliwa Lwala na huko ndiko nimeishi siku zote isipokuwa wakati nilienda shule ya Sekondari.* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli za wanakikundi hawa zinathibitisha kwamba tangu miaka ya kale, mazingira ya kujifunza Kimaragoli yamekuwa mazuri. Wahusika walipokuwa watoto wadogo, walijifunza Kimaragoli kutoka kwa wenzao wa Kimaragoli na hawakujifunga kwa mandhari mahsusi. Walikuwa na miktadha mipana ndani na nje ya shule. Katika shule zilizoanzishwa na Wamaragoli, Waluo wa kwanza walilazimika kuzungumza Kimaragoli wakati wanacheza na wenzao nje ya darasa au wakati wanaenda nyumbani baada ya shule. Hii ni kwa sababu watoto walikuwa huru kuzungumza Kimaragoli licha ya kwamba hakikuwa kinafunzwa darasani. Hivyo, kwa kuwa Waluo hawa walizungumza Kimaragoli, wenzao pia waliishia kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha hii.

#### 4.6.2.2 Ndoa kati ya Waluo na Wamaragoli

Kuwepo kwa ndoa za wasemaji lugha mbalimbali hukuza umoja na heshima miongoni mwa wasemaji wake. Waluo na Wamaragoli japo walipoanza kutangamana hakukuwepo na ndoa zozote kati yao, hali hii ilibadilika baadaye. Hatima ikawa msambao wa ndoa za Wamaragoli na Waluo. Kwa sababu ya kujengwa kwa misingi ya mapenzi na heshima, ndoa hizi zilisababisha wanawake wa Kiluo kuanza kujifunza na kuzungumza Kimaragoli. Baadhi ya wanawake walioshiriki katika mjadala wa kundi walikubali kwamba sababu mojawapo ya wao kujifunza Kimaragoli ni mwelekeo katika ndoa. Mwelekeo huu ulitokana na haja ya kujua na kuelewa wakwe. Mmoja wa wanawake alikiri kwamba:

> **Mama T***: Haaaaiyaa. Mama Mercy ni rafiki yangu na tulikutana sote huku wakati wa ndoa.Kwa kweli ni jirani yangu upande huu mlitokea na Ajema. Sasa mimi na bwanangu tunaongea Kimaragoli kwa sababu tumejifunza kutoka kwa kina Mama Mercy na watoto wake hawa wakubwa kina Mark na wengine. Bwanangu hakunifunza mimi. Halafu tukiwa na Mama Mercy, Mama F na Mama A kwa chama kimoja, tulikuwa tunahimizana sana. Kusema ukweli, kama mwanamke mgeni katika boma, unakuwa na uoga kidogo ukisikia watu wanaongea lugha nyingine na wewe hujui. Unaweza kufikiri wanakusengenya au wanakusema kwa mabaya. Pengine hukupika vizuri (wote wanacheka). Sasa tulijihimiza kujua Kimaragoli kutoka kwa watu wa boma au majirani. Wakati mwingine, kama Mama Mercy amejifunza neno jipya, tukikutana kwa chama, tunafunzana tu wenyewe kwa wenyewe. Hatukujua utamkaji vizuri lakini tulitaka kujua maneno yote ndio tujue kama wanatusengenya au wanatusifu. Sasa uoga wa kulinda nyumba zetu ulitufanya kujua Kimaragoli.*
>
> *(*Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hii inathibitisha kwamba kudumishwa kwa Kimaragoli katika eneo linalozungukwa na Waluo zaidi kulichangiwa na ndoa zilizosababisha wanawake hawa kupenda Kimaragoli kama walivyopenda mabwana na watoto wao. Baadhi ya wanawake hawa walipojua Kimaragoli zaidi ya baadhi ya Wamaragoli, walianza kufundisha watoto wao ili nao wakidumishe kama lugha ya baba zao. Utafiti huu unapinga mawazo ya Igboanusi na Wolf (2010) waliodai kuwa ndoa mseto zinasababisha uhamiaji lugha.

#### 4.6.2.3 Mwelekeo chanya kwa Wamaragoli

Uhusiano kati ya wasemaji wa lugha moja na nyingine unaweza kusaidia lugha kufa au kudumishwa. Hii ni kwa sababu, wasemaji wa lugha hizi mbili wanapozozana, uhasama huu unaweza kuangamiza lugha moja au nyingine kupitia vita, kufurushwa kwa lazima au katika baadhi ya mataifa, kutia wasemaji wake katika kambi za kuangamiza jinsi Hitler alivyowafanya Wayahudi nchini Ujerumani (Hartman, 1994). Uhusiano unapokuwa mwema, wasemaji wa lugha hizi hujihisi wako huru kuzungumza lugha zao. Hii ndiyo sababu katika mjadala, baadhi ya wasemaji wa Kiluo walidai kupenda Wamaragoli na hii ikafanya ujifunzaji wa Kimaragoli kuonekana rahisi:

> **Bwana L:** *Mimi nitasema Kimaragoli tunakipenda. Eeeh pia tunakiheshimu kwa sababu si cha watu wabaya. Ni wangwana sana.*
> **Bwana A**: *Kweli kujifunza kama mtoto, ni rahisi. Lakini kwa mtu mkubwa ni vigumu.Akili ina mambo mengi ya kufikiria. Lakini mimi nitasema Kimaragoli ni lugha ya heshima. Tena watu wake hatujapigana nao hapa kwetu.*
> **Mtafiti**: *Lakini nasikia kulikuwa na vita hata Wamaragoli wakafukuzwa…*
> **Bwana A**: *Ndio. 2002. Tena 2013 lakini ukiangalia vizuri, shida ilikuwa ya siasa tu.Mambo ya lugha hayakuwa ndani.* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Ni rahisi kutambua uhusiano mwema uliopo kati ya Wamaragoli na Waluo kupitia kwa mjadala huu. Katika dondoo tulizotumia, Waluo wanawaita Wamaragoli "si watu wabaya", "Watu wangwana" na katika mahusiano yao, wanasema kwamba "hatujapigana nao hapa kwetu" na hata baadhi yao walipopigana "mambo ya lugha hayakuwa ndani". Hili ni dhihirisho tosha kwamba japo kunaweza kutokea mzozo wa kisiasa, vita vitakavyofuata vitasalia kuwa vya kisiasa na wala si vya kikabila. Hivyo, vita vinatokana kwa sababu ya kuwa na itikadi zinazosigana kisiasa katika taifa au janibu. Kuwepo kwa mwelekeo huu chanya katika Kimaragoli umechangia pakubwa katika udumishwaji wa Kimaragoli eneobunge la Uriri.

#### 4.6.2.4 Kuzungumza Kimaragoli mara kwa mara

Njia moja ya kupima mwelekeo ni kupitia kwa mazungumzo ya mara kwa mara katika miktadha mbalimbali. Uzungumzaji wa lugha maalumu kila mara kwa upande mwingine unasaidia kudumisha lugha kwa kuwa mazungumzo yanahuisha lugha kila siku. Hii ndiyo sababu kuu ya kufanya mjadala na wazungumzaji wa Kiluo kutaka kujua ikiwa wao, japo wana lugha yao, wanazungumza Kimaragoli kila wakati. Maoni yao yalitofautiana kutoka kwa msemaji mmoja hadi kwa mwingine. Kuna wale ambao walikiri kwamba sasa hawakizungumzi japo wangali wanakikumbuka na wale ambao wangali wanakitumia kila siku kwa sababu ya kuwa katika mazingira yanayowasukuma kuzungumza. Kwa mfano, waliosema hawazungumzi sana walidai kwamba:

> **Kijana A***: Kimaragoli hatutumii sana kwa sababu watu wengi tuliosoma nao sasa wako mbali. Pengine kama tu ni salamu kidogo na maongezi kidogo tukikutana au kwa simu kama tunaongea nao. Watoto wao sasa kama wamekuja nyumbani wanisalimu kwa Kimaragoli. Lakini wakija kwangu wanajua mimi ni Mluo, sasa wanaongea tu Kiluo. Na ni watoto wa marafiki zangu ambao ni Wamaragoli.*
> **Mama C***: Mimi siongei Kimaragoli.*
> **Baba M***: Mimi nakitumia pia lakini mahali maalumu. Kwangu sikitumiii sana pengine kama rafiki wangu wa kitambo amekuja kuniona tuanze kuongea mambo yakitambo* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hizi zinaonyesha kwamba katika mazingira ya nyumbani kwa Mluo, Kimaragoli hakitumiki kwa sababu tayari ni nafasi ya Kiluo. Hata hivyo, Kimaragoli kinaweza kutumika japo kwa idadi ndogo kama anavyokiri Kijana A.

Maoni haya yalikuwa kinyume na ya wenzao waliokiri kwamba tangu wajifunze Kimaragoli utotoni au katika ndoa, wangali wanakitumia. Baadhi yao walisema kwamba:

> **Mama M***: Mimi natumia siku zote. Bwanangu ni Mmragoli. Watoto wangu wanaongea Kimaragoli na Kiluo. Lakini siku zingine tunaongea Kiluo tu hapa kwa nyumba. Nikienda kwa mama, hiyo nyumba unaona hapo chini, mama anaongea Kimaragoli na hajui Kiluo kabisa. Sasa ni lazima niongee naye Kimaragoli. Hata si Kiswahili.*

**Mama F***: Mimi bado naongea Kimaragoli kila siku. Marafiki zangu wengi wa kanisa, wa kazi, na majirani wote Kakrao wanaongea Kimaragoli tu. Sasa nakitumia kila mahali.*
**Mama T***: Mimi nakitumia karibu kila siku ingawa si kila wakati. Lakini kitambo tulikiongea sana. Tukiwa kanisani, tunasalimiana na Wamaragoli kwa Kimaragoli na pia kwa Kiluo.*
**Bwana L***: Mimi naongea Kimaragoli siku zote. Lwala ni kama kitovu cha Wamaragoli. Kwanza sisi Waluo hapo tuko wachache sana. Sasa ni kama lugha yangu kwa sababu najikuta naongea hata kushinda Kiluo siku zingine. Majirani wote ni Wamaragoli.* (Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli hizi zinadhihirisha ruwaza za matumizi ya Kimaragoli miongoni mwa Waluo. Kwanza, wanakiri kukizungumza kila siku japo si kila saa na wengine wanakizungumza kila wakati. Mandhari yanayosababisha hali hii ni kuwepo kwa mikutano ya kanisa, ujirani wa Mluo na Wamaragoli na kuwa katika kitovu cha Wamaragoli. Hii ina maana kwamba kuwepo kwa idadi kubwa ya Wamaragoli kunasababisha Waluo kuzungumza Kimaragoli.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano lugha mwelekeo huu chanya unaweza kuelezwa kwa kigezo cha isimunafsia, mhimili ambapo akili inapewa nafasi kubwa sana katika udumishaji lugha. Uwililugha au wingilugha katika maisha ya mtu binafsi au jamii maalumu unaweza kuelezwa vyema kupitia mhimili huu. Umilisi lugha wa mtu binafsi katika jamii unategemea uwezo wa akili kubwia misamiati na vipengele vingine vya kiisimu na uwezo huu unaathiriwa na umri. Hivyo, wasemaji wa Kiluo wengi wanakiri kujifunza Kimaragoli wakiwa watoto wadogo na hadi sasa msamiati waliobwia haujatoweka kwa wasemaji isipokuwa Mama C aliyekiri kuenda Nairobi na kuishi kule kwa muda mrefu kwa sababu ya kazi. Wengine wote kwa kuwa umilisi wao wa Kimaragoli ulikuwa wa juu, basi imekuwa rahisi wao kutenda kupitia kwa mazungumzo ya miktadha mbalimbali. Hii ndiyo sababu baadhi ya Waluo wanakiri kuzungumza Kimaragoli kushinda baadhi ya Wamaragoli na wengine kusema kwamba wanaweza kutumia Kimaragoli hata katika miktadha ya kisiasa na kanisani. Hii inaonyesha uwezo

wao mkubwa wa kiakili wa kujua na kutumia Kimaragoli. Pamoja na hayo, nadharia hii na ya uhuishaji kiethnoisimu, zinatilia mkazo dhana ya kuwepo kwa mahusiano dhabiti ya kimakundi yanayoweza kusababisha wasemaji wa Kimaragoli kudumisha lugha yao. Hii ni kutokana na wao kuishi kwa pamoja na badala ya kuathiriwa na Waluo na Kiluo, wao ndio wanaathiri Waluo kwa kuwafanya wao kuzungumza Kimaragoli.

## 4.7 Hitimisho

Sura hii imejadili kwa kina madhumuni manne ya utafiti huu huku ikijibu maswali ambayo utafiti huu ulidhamiria kutafutia majibu. Madhumuni haya yamegusia mikakati inayotumiwa na Wamaragoli kudumisha lugha yao, umilisi wa Wamaragoli, athari za Kiluo kwa Kimaragoli na mielekeo ya Wamaragoli na Waluo kuhusu udumishaji wa Kimaragoli eneo la Uriri. Mjadala umezingatia data wingiidadi na thamano. Katika madhumuni ya kwanza, ni wazi kwamba wasemaji wa Kimaragoli wamemakinikia udumishaji lugha yao kwa kuzingatia mikakati mbalimbali. Ingawa mikakati hii ilitofautiana kutegemea kila kundi, watafitiwa wote walionyesha kwamba udumishaji wa Kimaragoli ni muhimu. Katika madhumuni ya pili, ni wazi kwamba umilisi na utendaji miongoni mwa vizazi vitatu ungali imara. Hata hivyo, viwango vinaonekana kuzidi kushuka. Katika madhumuni ya tatu, ni bayana kwamba Kimaragoli kimeathirika kwa kiasi kikubwa katika eneobunge la Uriri. Athari hii imejitokeza katika kiwango cha msamiati, uchanganyaji na uhamishaji lugha na kadhalika. Madhumuni ya mwisho yameonyesha kwamba Kimaragoli kimedumishwa kutokana na miekeleo chanya iliyopo kati ya Wamaragoli na pia Waluo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imetoa taswira kamili ya utafiti mintarafu matokeo yaliyojadiliwa katika sura ya nne. Inatoa muhtasari wa matokeo ya tasnifu hii kutegemea madhumuni ya utafiti na pia kufanya mahitimisho kutoka kwa mjadala wa matokeo. Sura hii vilevile inatoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza, ambayo ni msingi wa utafiti inatoa vipengele vya kimsingi kuhusu tasnifu hii. Sura ya pili ni uhakiki wa maandishi yaliyo na mchango muhimu katika kuweka bayana haja ya kutendeka kwa utafiti huu. Imezingatia kwa kina watafiti mbalimbali kutoka sehemu zote za ulimwengu ikiwemo bara la Afrika na pia Kenya. Sura ya tatu imejadili njia na mbinu za utafiti. Inaeleza jinsi utafiti huu ulitendeka. Sura ya nne imejadili matokeo ya utafiti huu. Matokeo haya yamewasilishwa kwa njia mbalimbali za kigrafiki, kitakwimu na kithamano. Sura ya tano inatoa muhtasari na mahitimisho ya tasnifu nzima na pia mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo

Sehemu hii inatoa muhtasari wa sura ya nne kwa kuzingatia kila madhumuni ya utafiti huu.

### 5.3.1 Mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli Uriri

Udumishaji wa Kimaragoli Uriri unategemea mikakati mbalimbali. Mapendeleo ya mikakati hii kwa mujibu wa matokeo ya utafiti yalitofautiana kizazi kimoja na kingine. Miongoni mwa watoto, mkakati wa kufundishwa Kimaragoli nyumbani ndio ulikuwa na

asilimia kubwa (77.3%), kisha kufuatiwa na kuabudu kanisani (69.3%) na matumizi ya idhaa za *Vuka FM* na *Mulembe FM* (66.7%). Miongoni mwa vijana, kuzungumza Kimaragoli nyumbani (87.3%) ulionekana kuwa mkakati unaopendelewa sana huku kusikiliza idhaa za *VukaFM* na *Mulembe FM* (78%) na wazazi kufundisha watoto Kimaragoli nyumbani (74.4%) ikifuatana. Miongoni mwa makamo na wazee, kusikiliza idhaa za *Vuka FM* na *Mulembe FM* (82.8%), kufanya sherehe za tohara na mila za Wamaragoli (sherehe za kitamaduni) (80.5%) na kuongea Kimaragoli nyumbani (78.2%) ilikuwa mikakati waliyokubali inachangia pakubwa katika kudumisha Kimaragoli. Kulikuweko na mikakati mingine kama vile mikutano ya chama, kuongea Kimaragoli nyumbani, kutembeleana, mikutano ya kitamaduni na mabaraza za machifu. Kiwastani, mikakati mikuu iliyopendelewa na makundi haya yote ilikuwa ni matumizi ya idhaa za *Vuka FM* na *Mulembe FM* (75.8%), Wazazi kufundisha watoto Kimaragoli (73.2%) na Kuongea Kimaragoli wakiwa nyumbani (72.7%). Mikakati hii ndiyo hasa wataalamu mbalimbali walikubali ina matunda makubwa katika udumishaji wa lugha yoyote ulimwenguni. Hivyo, mafanikio ya udumishaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri, na kaunti ya Migori kwa ujumla inategemea zaidi mikakati hii mitatu.

### 5.3.2 Umilisi na Utendaji wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji wake Uriri

Ili kufahamu ikiwa Kimaragoli kinadumishwa au la, ilikuwa muhimu kutathmini kiwango cha umilisi wa kimsingi wa wasemaji wake katika makundi yote ya kiumri. Miongoni mwa watoto, kiwango cha umilisi na utendaji wa kimsingi kilikuwa 93.3%, kiwango cha umilisi na utendaji wa vijana kilikuwa 89% na kiwango cha makamo na wazee kikiwa 93.4%. Wastani wa umilisi miongoni mwa makundi yote matatu ulikuwa 91.9%. Hata hivyo, licha ya kuonyesha kwamba umilisi wa kimsingi ni wa kiwango cha juu, hasa katika makundi ya watoto na vijana, ilionekana wazi kwamba walikuwa na

tatizo la kujieleza katika baadhi ya miktadha. Miongoni mwa vijana, watafitiwa 58 (70.7%) walisema hawana tatizo lolote kwa sababu wanaweza kufanya mambo yote kwa Kimaragoli bila tatizo huku 24 (29.3%) wakikiri kwamba wanakumbana na changamoto mbalimbali wanapozungumza Kimaragoli. Miongoni mwa watoto, watafitiwa 45 (60%) walisema kwamba hawana tatizo la kujieleza katika Kimaragoli kuhusiana na masuala mbalimbali, 30 (40%) walisema wana matatizo katika baadhi ya masuala. Baadhi ya mambo waliyotaja kuwa magumu kujieleza yalijumuisha istilahi za ukoo, aina za pesa ambazo shule huhitaji kwa mfano majina ya pesa za matanga na pesa za karo, kusoma na kuomba kwa Kimaragoli, aina ya wadudu, vitu vya kiturathi, aina za vyungu, mila za jandoni, mapambo, fasihi, kusimulia hadithi, majina ya vitu mbalimbali, dira za dunia, mila, vyakula, matunda na mbari za Wamaragoli. Hata hivyo, mazungumzo ya kawaida wanaweza kuyatekeleza kwa Kimaragoli bila tatizo lolote.

### 5.3.3 Athari ya lugha ya Kiluo kwa Kimaragoli kinachozungumzwa Uriri

Miongoni mwa watoto, 53.9% walikubali kuathiriwa na Kiluo kwa namna moja au nyingine dhidi ya 46.1%. Kwa upande mwingine, 43.9% ya vijana walikiri kuathiriwa dhidi ya 56.1% waliosema kwamba hawajaathirika kwa namna yoyote ile. Miongoni mwa makamo na wazee, 87.2% walisema hawajaathirika na Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli huku 12.8% wakikiri kuathirika kimazungumzo. Kijumla, 41. 8% walikiri kuathirika ikilinganishwa na watafitiwa 58.2% waliokiri kutoathiriwa na Kiluo. Athari za Kiluo kwa Kimaragoli zilitafitiwa kwa viwango kadhaa. Kwanza, hapakuwepo na athari kubwa ya leksimu za Kiluo kuingizwa na kusharabu Kimaragoli. Maneno machache sana ndiyo yamekopwa na yanatumika. Pili, Kimaragoli kimeathiriwa pakubwa katika ruwaza za matumizi. Hii ina maana maeneotumizi yaliyokuwa ya Kimaragoli pekee miaka ya 1940 sasa yameingiliwa na Kiluo. Maeneotumizi haya ni kama vile nyumbani, kuzungumza na watu wa ukoo na mashambani. Hivi sasa uchanganyaji na uhamishaji

ndimi kati ya Kimaragoli na Kiluo unafanyika katika maeneo haya. Athari hizi zinatokana na kuwepo kwa Waluo katika ujirani na Wamaragoli, watoto kucheza na kusoma pamoja na watoto wa Kiluo, kuenda kanisa moja na hata katika maeneo ya michezo. Hii imefanya Kimaragoli kuathirika katika maeneo yanayostahili kuwa ya Kimaragoli pekee. Kundi la wazee na makamo ndilo limeonyesha kutoathirika sana wanapotumia Kimaragoli katika mazungumzo. Watafitiwa 26.4% wa kundi hili walikubali kwamba wamewahi kuingiza maneno ya Kiluo katika uzungumzaji wa Kimaragoli ikilinganishwa na 73.6% ambao hawachanganyi wala kuhamisha ndimi.

### 5.3.4 Mielekeo ya wasemaji wa Kimaragoli na Kiluo kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri

Watafitiwa wa umri wa watoto walionyesha kujivunia Kimaragoli (82.7%), 58.7% wataona aibu ikiwa watashindwa kuzungumza Kimaragoli, 58.7% watahisi vibaya iwapo Kimaragoli kitapotea, 57.4% wanaona haja ya kuzungumza Kimaragoli Uriri, 84% wanaongea Kimaragoli kwa lengo la kukidumisha, 80% wanaongea Kimaragoli zaidi ya Kiluo, 77.3% wanaongea Kimaragoli na watu wao wa ukoo, 78.6% walikiri kuwa na muda wa kujifunza Kimaragoli, 88.1% walikubali Kimaragoli kiendelee kufundishwa, 64% hujizatiti kufunza wenzao Kimaragoli, 69% walihisi Kimaragoli kinaheshimiwa na 46.7% wanaheshimu lugha nyinginezo Uriri. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba kiwastani (70.3%), Kimaragoli kina mwelekeo chanya miongoni mwa watoto. Miongoni mwa vijana, wastani wa mwelekeo chanya ni 83.4% huku wazee ikiwa pia 83.4%. Jumla ya takwimu hizi za juu zinadhihirisha kuwa udumishaji wa Kimaragoli unatokana na mwelekeo chanya ulioko miongoni mwa makundi matatu yaliyotafitiwa. Mjadala wa Kundi lengwa kati ya mtafiti na wazawa wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli unaonyesha kwamba kudumishwa kwa Kimaragoli kunatokana pia na mwelekeo chanya kati ya Kimaragoli na jamii ya Waluo na jamii nyinginezo.

Utafiti huu aidha ulitafitia mielekeo ya wazungumzaji wa Kiluo kuhusu Kimaragoli na kutambua kwamba Kimaragoli kimedumishwa kwa sababu ya kuwepo kwa mielekeo chanya miongoni mwa Waluo. Mielekeo hii chanya ilipimwa kutokana na vigezo kama vile kujifunza Kimaragoli tangu utotoni, kuwepo kwa ndoa kati ya Waluo na Wamaragoli, kuwepo kwa mwelekeo chanya wa Waluo wanaozungumza Kimaragoli na kutumia Kimaragoli mara kwa mara. Kuwepo kwa mwelekeo chanya miongoni mwa Waluo katika eneo hili kunadhihirisha mshikamano wa amani uliopo kati ya wasemaji wa lugha hizi mbili kiasi cha kuruhusu kila mmoja kuzungumza na kuendeleza lugha yake. Baadhi ya wasemaji wa Kiluo kujifunza na kuzungumza Kimaragoli tangu utotoni pia kumesaidia udumishwaji wa Kimaragoli. Hivi vipengele muhimu vya kupima mielekeo vilikuwa dira muhimu ya kuthibitisha kwamba udumishwaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri uko imara kwa kiasi kikubwa.

## 5.4 Mahitimisho

Sehemu hii inatoa mahitimisho kuhusu madhumuni manne ambayo utafiti huu ulishughulikia katika sura ya nne.

### 5.4.1 Mikakati ya udumishaji wa Kimaragoli Uriri

Kudumishwa kwa Kimaragoli Uriri ni suala ambalo litaendelea kwa muda mrefu kutokana na kujitolea kwa wasemaji wake kuzungumza na kufundishana lugha hii nyumbani. Pamoja na kusikiliza idhaa zinazotangaza kwa Kimaragoli, udumishaji wa Kimaragoli una udhabiti wa kiwango cha juu. Mikakati hii mitatu, pamoja na mingine iliyobainishwa hata hivyo inastahili kuhimizwa zaidi kwa sababu baadhi ya wasemaji wanadai kwamba hawana muda wa kukaa na wazazi au watoto wao kuwafunza Kimaragoli. Iwapo hali hii itaendelea na wasemaji wengi kukosa muda wa kujifunza

kutokana na kazi au masomo, basi, udumishwaji wake utayumba siku za usoni. Kutakuwepo na uwezekano mkubwa wa kuhamia Kiluo.

### 5.4.2 Umilisi na Utendaji wa lugha ya Kimaragoli miongoni mwa wasemaji Uriri

Utafiti huu unahitimisha kwamba umilisi wa kimsingi katika vizazi vyote vitatu, yaani, watoto, vijana na makamo na wazee ni wa kuridhisha. Wazee na makamo wameonyesha umilisi wa kiwango cha juu kutokana na wao kuishi miaka mingi wakizungumza Kimaragoli pamoja na kukitunza walipohamia Migori wakiwa watoto wadogo miaka ya 1940. Aidha, kiwango cha watoto kuwa cha juu pia kunatokana na hali kwamba wao hujifunza lugha haraka. Kwa upande wa vijana wao kuwa na kiwango cha chini cha umilisi ikilinganishwa na makundi hayo mawili ni kutokana na wao kuathirika pakubwa na Kiluo pamoja na kutoonekana kukizingatia sana katika mawasilino. Ni muhimu kufanya hitimisho kwamba Kimaragoli kitazidi kudumishwa kutokana na kiwango cha kuridhisha cha umilisi miongoni mwa wasemaji wake. Hata hivyo, udumishwaji huu utaathirika kihasi ikiwa kizazi cha watoto na vijana kitazidi kuathirika pakubwa na uchanganyaji na uhamishaji ndimi kati ya Kimaragoli, Kiluo na Kiswahili.

### 5.4.3 Athari ya Kiluo kwa Kimaragoli kinachozungumzwa Uriri

Utafiti huu unahitimisha kwamba Kimaragoli hakijaathiriwa pakubwa kileksimu na lugha ya Kiluo. Hivyo, uwezo wake wa kudumisha istilahi na maneno asilia ya Kimaragoli utakuwa amilifu katika udumishwaji wake siku za baadaye. Athari imejitokeza pakubwa katika maeneotumizi ya Kimaragoli, hasa pale ambapo Kimaragoli pekee kinastahili kutumika. Watoto na vijana ndio walioathirika mno kwani wanajikuta wanachanganya na kuhamisha ndimi wakiwa nyumbani, na wanapowasiliana na nasaba zao. Hii itaathiri kihasi juhudi za kudumisha Kimaragoli siku za baadaye kwani kadiri ya muda,

kutashuhudiwa uhamiaji Kiluo hata katika maeneo ya nyumbani ambako wasemaji ni Wamaragoli peke yake.

### 5.4.4 Mielekeo ya Wamaragoli na Waluo kuhusu uzungumzaji wa lugha ya Kimaragoli Uriri

Wamaragoli walidhihirisha mielekeo chanya kuhusiana na lugha yao. Hii imekuwa na mchango mkubwa katika udumishaji wa lugha yao kuanzia miaka ya 1940 hadi sasa. Pamoja na hayo, wasemaji wa Kiluo wameonyesha kwamba kuna heshima kati yao na Wamaragoli hivyo kuifanya lugha hii kuwa na mazingira mazuri ya kiisimu kujidumisha. Hali ni ile ile kwa lugha nyingine zinazosemwa maeneo mapana ya Migori kama vile Kikurya, Kisomali, Kisii na lahaja nyingine za Kiluhya. Hitimisho linaloweza kufanywa kutokana na hali hii ni kwamba kuwepo kwa muamala mzuri kati ya lugha kunachangia mwelekeo chanya na hivyo, kukuza mazingira mazuri ya kiisimu ya kudumisha lugha, na katika muktadha wa utafiti huu, Kimaragoli.

Utafiti huu ulihitimisha kwamba uzungumzwaji na udumishwaji wa Kimaragoli katika eneobunge la Uriri umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kwanza, mlahaka mwema uliokuwepo kati ya Waluo na Wamaragoli, na pili, kuishi vyema na kwa amani kati ya wasemaji wa lugha hizi mbili. Kwa kuwa mazingira ya kiisimu hayana uhasama wowote katika eneo hili, basi yanazipa lugha zote mbili, na hasa Kimaragoli satua na ujasiri wa kujidumisha bila kutokea tatizo la vita vya kikabila.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhuishaji kiethnoisimu, hali halisi ya Kimaragoli inaweza kuhitimishwa kwamba udumishwaji ni dhabiti japo ipo hatari ya wasemaji wake kuhamia Kiluo na Kiswahili. Mahitimisho haya yanatokana na kigezo cha UNESCO (2003) kwamba lugha hii inazungumzwa na vizazi vyote vitatu katika maeneotumizi mengi, na

kwamba urithishwaji wake umejitokeza katika vizazi vichanga. Hata hivyo, wingilugha (Kiluo na Kiswahili) katika maeneo asilia ya matumizi ya Kimaragoli umejitokeza kwa kiasi kikubwa na kuathiri miktadha ambayo Kimaragoli hutumiwa kuwasiliana.

### 5.5 Mapendekezo

Sehemu hii inatoa mapendekezo kwa kuzingatia vipengele viwili. Kipengele cha kwanza ni mapendekezo ya kisera na kiutekelezi na mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye.

#### 5.5.1 Mapendekezo ya Kisera na Kiutekelezi

Utafiti huu unapendekeza kwamba,

i. Kwa kuwa CBC imezipa lugha asili kipaumbele, marejeleo mengi yaweze kuandikwa, hasa viwango vya sekondari ya chini.
ii. Utafiti unapendekeza kwamba pawepo na vipindi maalumu kwenye redio vinavyofunza Kimaragoli ili kuimarisha umisili na utendaji miongoni mwa vijana.
iii. Utafiti unapendekeza makamo na wazee waweke watenge muda wa kufunza watoto na vijana Kimaragoli wanapokuwa likizoni.
iv. Utafiti unapendekeza kwamba uhusiano uliopo kati ya wasemaji wa Kiluo na Kimaragoli uendelee kudumishwa hasa katika maeneo ambayo wasemaji wa Kimaragoli ni wachache.

#### 5.5.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Mapendekezo yafuatayo yametolewa kwa ajili ya utafiti wa baadaye :

1. Utafiti wa baadaye uchunguze hali halisi ya Wamaragoli maeneo mbalimbali ya Kenya.
2. Kiswahili kipewe nafasi kama lugha ya kutafitia lugha nyingine za Kiafrika na maarifa yanayopatikana yaandikwe kwa Kiswahili.

3. Utafiti huu unapendekeza tafiti zifanywe katika lugha zilizoorodheshwa na UNESCO kuwa hatarini na maarifa mapya kukusanywa pamoja kwa minajili ya kuunda kiunzi cha kuziokoa. Kipengele cha kiteknolojia hasa kitiliwe maanani katika kuokoa lugha zilizo hatarini.

# MAREJELEO


Abelson, R.P., Frey, K.P na Gregg, A.P. (2004). *Experiments with people: Revalations from social psychology*. Mahwah, N.J: Lawrence Erlbaum.

Adung'o, C. (2016). Ubantu na Uarabu wa vivumishi vya Kiswahili. www.Swahilihub.com imesomwa 12/11/2016.

African Union (1995). *Statutes of African academy of languages (ACALAN*). Addis Ababa:Ethiopia.http://sa.au.int/en/sites/default/files/Statutes%20of%20Acalan.pdf imesomwa 07/09/2015.

Akuezuilo, E. O., & Agu, N. (2003). *Research and statistics in education and social sciences: method and application*, Awka: Nuel Centi Publishers and Academic Press.

Al-Badri, N. (1986). The history of Arabic lexicography. *Journal of Exeter Linguistic Studies, EVP*: pp. 36-43. imesomwa 07/09/2015.

Allard, R. & Landry, A. (1992). Ethnolinguistic vitality beliefs and language maintenance and loss, In Fase, W. et al. (eds.), *Maintenance and Loss of Minority Languages*, pp.171-195.

Allport, G. W. (1935). Attitudes. In C. Murchison (Ed.), *Handbook of social psychology* (pp. 133–175). Worcester, MA: Clark University Press.

Ang'iela, D. O. (2002). Literacy, attitudes and language revitalization. In Owino, F.R (ed) *Speaking African: African Languages for Education and Development.* Cape Town: CASAS Book Series pp 200-216.

Anyona, G. M. (2016). *Syllabic nativization of EkeGusii loanwords from English: an optimal theory approach*. (Unpublished PhD thesis Kisii University) Kenya.

Arubayi, E. O. (2003). *Research and statistics in education and social sciences*. Benin City: Ethiope Publisher.

Arka, W. (2013). Language management and minority language maintenance in (eastern) Indonesia: strategic issues. *Language Documentation & Conservation* Vol. 7, 2013: 74-105.

Aswegen, G. (2008). *Language maintenance and shift in Ethiopia: the case of Maale*. (Unpublished MA Thesis, University of South Africa) South Africa.

Babusa, O. (2012). *Ukopaji wa lugha: etimilojia na mabadiliko ya maana na utamkaji wa msamiati wa Kiarabu.* Makala ya kongamano la pili la kimataifa la Kiswahili lililoandaliwa na taasisi ya uchunguzi wa Waswahili mashariki mwa Afrika,Mombasa 25-27 Okotoba, 2012. (Haijachapishwa).

Baker, C. (1992). *Attitudes and language*. Clevedon, UK: Multilingual Matters.

Baldi, S. (2012). Arabic loans in East African languages through Swahili: a survey. *Folia Orientalia*, 49: 37-52 imesomwa 07/09/2015.

Barasa, S. (2016). Spoken code switching in written form? Manifestations of code switching in Computer Manifested communication. *Journal of Language Contact*, vol. 9(1): 49-70. imesomwa 07/09/2015

Barnes, L. & McDuling, A. (hmu). The retention of Greek language and culture in the South African Diaspora. Imesomwa 12/10/2016.

Batibo, H.M (2005) *Language decline and death in Africa: causes, consequences and challenges*. Clevedon: Multilingual matters.

Birman, D. na Poff, M. (2011). *Intergenerational differences in acculturation. encylopaedia of early childhood development.* CEECD / SKC-ECD.

Blythe, R. & Croft, W. (2012). S-Curves and the Mechanisms of Propagation. Language Change. *Language,* Volume 88, Number 2, June 2012, Pp. 269-304 imesomwa 07/09/2015.

Bokamba, E.G. (1989). Are there syntactic constraints on code-mixing? In World Englishes Vol. (8) Issue 3: https://doi.org/10.1111/j.1467-971X.1989.tb00669.x imesomwa 07/09/2015

Bortolato, C. (2012). *Language maintenance-attrition among generations of the Venetian-Italian community in Anglophone Canada.* (Unpublished PhD Thesis, Exester University) England.

Bosire, M. (2006). Immigrant identity: code switching among Kenyans in Upstate NewYork. In *Selected Proceedings of the 35th Annual Conference on African Linguistics*, ed. John Mugane et al., 44-52. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. www.lingref.com, document #1295 imesomwa 10/10/2017.

Bradley, D. (2002). Language attitudes: The key factor in language maintenance. In Bradley, D. & Bradley, M. (eds.), *Language endangerment and language maintenance.*London: Routledge Curzon, pp.1-11.

Bryman, A. (2012). *Social research methods.* London. Oxford University Press.

Campbell, R. (2016). Maintaining Japan connection: the impact of study abroad on Japanese language learners' life trajectories and ongoing interaction with Japanese speakers. *Comparative and International Education Journal* vol 45 (2) imesomwa10/10/2017.

Chambers, J. K. (1992). Dialect acquisition. *Language Journal* 68.4:673-705 imesomwa 10/10/2017.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi. Oxford University Press

Cohen, L., Manion, L., & Morrizon, K. P. B. (2000). *Research methods in education*. London: Croomhelm.

Constitution of Kenya (2010) 27th August 2010 available at https://www.refworld.org/docid/4c8508822.html imesomwa 11/10/2019.

Crystal, D. (2000). *Language death*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cummins, J. (1994). The acquisition of English as a second language. In Spangenber-Urbaschat, K na Pritchard, R. (eds). *Reading instructions for ESL students.* Delaware: International Reading association. Pp. 9-11.

Darquennes, J. na Vandenbussche, W. (2011). Language and religion as a sociolinguistic field of study: some introductory notes. *Sociolinguistic* 25/2011: pp.1-12 imesomwa 7/10/2016.

Dawson, H. C. (2003). Defining the outcome of language contact: Old English and Old Norse. *OSUWPL 57, Summer* 2003, 40–57 imesomwa 10/09/2017.

Department of Culture and Language for elders and Youth (2014). Translation policy. government of Nunavut. http://www.gov.nu.ca imesomwa 10/09/2017.

Dyers, C. (2008). Language shift or maintenance? Factors determining the use of Afrikaans among some township youth in South Africa. *Stellenbosch Papers in Linguistics, Vol. 38, 2008, 49-72* imesomwa 17/10/2017.

Eckert, P. (2008). Variation and the indexical. *Journal of Sociolinguistics* 12(4): 453-476 imesomwa 9/10/2017.

Ehala, M. (2010). Ethnolinguistic vitality and intergroup processes. *Multilingua* 29 (2010), 203-222 imesomwa 9/10/2017.

Ethnologue (2015). Maragoli Language. https://www.ethnologue.com/cloud/rag imesomwa 12/5/2015.

Fang, T. (2017). How to maintain a minority language through education. *Chinese Studiesjournals*, 6(1-11) imesomwa 9/10/2017.

Finocchiaro, C. M. (2004). *Language maintenance shift of a three-generation Italian family in three migration countries: an international comparative study*. (Unpublished PhD thesis, The University of Melbourne) Australia.

Fishman, J. (1972). *Language in sociocultural change.* Stanford: Stanford University Press.

Fishman, J. (1980). Minority language maintenance and ethnic mother tongue school. *The modern Language Journal Vol.64, Issue 2* imesomwa 9/9/2016.

Fraenkel, J. and Wallen, N. (2006). *How to design and evaluate research in education. (*6th ed). Boston: McGraw-Hill.

Gibson, H. (2013). Auxiliary placement in Rangi: A case of contact-induced change? SOAS *Working Papers in Linguistics,* Vol. 16: 153-166 imesomwa 19/2/2017.

Giles, H., Bourhis, R. Y., & Taylor, D. M. (1977) Towards a theory of language in ethnic group relations. In: H. Giles (ed.) *Language, Ethnicity and Intergroup Relations*.London: Academic Press, p. 307-348.

Grbich, C. (2007). *Qualitative data analysis. An introduction.* London: Sage Publications.

Grenoble, L. & Lindsay, W. (eds.) (1998). *Endangered languages: language loss and community response.* Cambridge: Cambridge University Press.

Grixti, J. (2006). Growing up between cultures: linguistic and cultural identity among Maltese youth and their ethnic counterparts in Australia. *Mediterranean Journal of Educational Studies,* Vol. 11(2), pp. 1-15 imesomwa 9/10/2017.

Grosjean, F. (1982). *Life with two languages: An introduction to bilingualism.* Cambridge, MA: Harvard University Press.

Gumperz, J. J. (1982a).Conversational codeswitching. In *Discourse Strategies.*Cambridge: Cambridge University Press.

Gumperz, J. J. (1982b). *Discourse strategies*. Cambridge: Cambridge University Press.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Halai, A. (2006). *Ethics in quantitave research: issues and challenges.* Working Paper no. 4 presented at the Ala Khan University, Karachi.

Hamde, K. (2005). Blin language maintenance, shift and revitalization: a study on language,culture and identity. A paper presented at the *First Conference on Blin Language and Culture* in London, 14-16 July 2005.

Hartman, G. (1994). Holocaust remembrance:the shapes of memory. Oxford: Blackwell Publishers

Haynes, E. (2010). *What is language loss*? University of California, Berkeley: Center for Applied Linguistics.

Heine, B. and Kuteva, T. (2008). *Language contact and grammatical change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Hermes, M. and King, K.A. (2013). Ojibwe language revitalization, multimedia technology, and family language learning. *Language learning and technology,* 17 (1), 125-144 imesomwa 12/10/2019.

Hildebrandt, K. A. (2004). *Manange tone: Scenarios of retention and loss in two communities.* (Unpublished Ph.D Thesis, University of Michigan) USA.

Hinton, L., Steele, N., & Vera, M. (2002). *How to keep your language alive: a commonsense approach to one-on-one language learning*. Berkeley, CA: Heyday Books.

Hoffer, B. L. (2002). Language borrowing and language diffusion: An Overview. *Intercultural Communication Studies journal XI: 4 2002, pp. 1-37* imesomwa 9/10/2017.

Hudson, R. A. (1996). *Introduction to sociolinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ianos, M. A. (2014). *Language attitudes in a multilingual and multicultural context. The case of autochthonous and immigrant students in Catalonia*. (Unpublished PhD Thesis, University of Lleida) Spain.

Iseke, J. (2013). Negotiating métis culture in michif: disrupting indigenous language shift. *Decolonization: Indigeneity, Education & Society,* 2 (2), 92-116.

Igboanusi, H. and Wolf, H. (2010). The role of ethnically mixed marriages in language shift: a case study of Nigeria's minority languages. Journal of Sociolinguistic Studies. Doi:10.1558/sols.v3i3.451

Jagodic, D. (2011). Between language maintence and shift: The Slovenian community in Italy today and tomorrow. *Slovene Research Institute* 2(1): pp.195-213 imesomwa 9/5/2015.

Jamai, A. (2008). *Language use and maintenance among the Morroccan Minority in Britain*. (Unpublished PhD thesis, University of Salford) England.

Kalmanlehto, I. (2014). Mixed domains and multilingual practices-an ethnographic study of Tanzanian university students' language use. Unpublished MA thesis. University of Tampere.

Karanja, P. (2012). Kiswahili dialects endangered the case of Kiamu and Kimvita. *International Journal of Humanities and Social Science* Vol. 2 No. 17 imesomwa 9/10/2015 pp. 95-117.

KBS (2009). *Kenya population and housing census.* Nairobi: Government of Kenya.

Kerswill, P. (1996). Children, adolescents, and language change: language variation and change. *Language Contact: The State of the Art conference Organized by the Linguistic Association of Finland (SKY), Helsinki Area & Language Studies and the CROSSLING research network Helsinki, August 28-30, 2014.*

Khan, I. (2016). Contact-induced change: Processes of borrowing in Urdu language in India. *International Journal of Scientific and Engineering Research* 7(11): 162. Imesomwa 20/9/2015

Kheirkhah, M. na Cekaite, A. (2015). Language maintenance in a multilingual family: informal heritage language lessons in parent-child interactions. *Multilingua-Journal of Crosscultural and Interlanguage Communiciation,* (34), 3, pp. 319-346. http://dx.doi.org/10.1515/multi-2014-1020 imesomwa 9/10/2015.

Kheirkhah, M. (2016). *From family language practices to family language policies:children as socializing agents.* LiU-Tryck: Linköping University.

Khrisat, A.A. na Mohamad, S.M. (2014). Language's borrowings: the role of borrowed and Arabized words in enriching Arabic language. *American Journal of Humanities and Social Sciences,* Vol. 2, 2014: 133-142 imesomwa 9/10/2015.

Kipp, D. (2009). Encouragement, Guidance and Lessons Learned: 21 Years in the Trenchesof Indigenous Language Revitalization. In Reyhner, J. and Lockard, L (eds) *Indigenous Language Revitalization Encouragement, Guidance & Lessons Learned*. Arizona: Northern Arizona University pp. 1-9.

Kipsisey, G. (2010). *Reviving marginalized languages in Kenya: a casesStudy of the Sabaot on mount Elgon.* Paper presented at the 109th Annual Meeting of the American Anthropological Association held in New Orleans on Nov. 17-21 2010.

Kombo, D.K., & Tromp, D.L.A. (2007). *Proposal and thesis writing: an introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: methods and techniques (2nd ed.).* New Delhi: New Age International Limited Publishers.

Kruegger, R.A. (1988). *Focus groups: a practical guide for applied research.* Thousands Oaks, CA, US: Sage Publications Inc.

Kuncha, R.K. na Bathula, H. (2004). The role of attitudes in language shift and language maintenance in a new immigrant community: a case study. *Working Paper No. 1.*

Lee, E. (2006). Reasons and motivations for code-mixing and code-switching. *Journal of Issues in EFL* Vol.4 No.1: pp. 43-61 imesomwa 9/10/2015.

Lee, E. (hmu). *Language Maintenance and Competing Priorities at the Portuguese Settlement, Malacca*. Sunway University.

Leeds, P. D. (1993). *Practical research: planning and design*. Upper Saddle River: Prentice-Hall Inc.

Leedy, P. D., & Ormrod, J. E. (2005). *Practical research:planning and design (8th ed.).* Upper Saddle River, NJ: Prentice Hall.

Lehmann, C. (2006). Linguistic competence theory and empiry.*Journal of Folia Linguistica* 41 (2): pp. 223-278.

Lotta, A. (2014). Contact leading to a more complex tonal system: the case of Ikoma and Datooga in North-Wes Tanzania. *In language Contact: the state of art conference Organized by the Linguistic Association of Finland (SKY), Helsinki Area & Language Studies and the CROSSLING research network Helsinki, August 28-30, 2014.*

Magga, O.H., Nicolaisen, I., Trask, M., Skutnabb-Kangas, T. na Dunbar, R. (ht). Indegenous children's education and indegenous languages. *Expert paper written for the United Nations Parmanent Forum on Indegenous Issues.* United Nations.

Maho, F.J. (2009). The online version of the New Updated Guthrie List, a referential classification of the Bantu language. *NUGL Online.* Imesomwa 09/10/2015.

Malik, L. (1994). *Sociolinguistics: a study of codeswitching*. New Delhi: Anmol.

Maracle, D. K., & Richards, M. (2002). A native language immersion program for adults: Reflections on year 1. In B. Burnaby, & J. A. Reyhner (Eds.), *Indigenous languages across the community*. Flagstaff, AZ: Northern Arizona University: Center for Excellence in Education. pp. 127-136

Marina, S. (2014). Palatalisation in L2 Irish: the extent of phonetic Interference. In *Procedia:Social and behavioural sciences,* 236:p.213-218 imesomwa 9/9/2015.

Marti-Bucknall, W. (2007). *The home-school connection: Immigrant family literacy practices and use of technology in home/first language teaching*. Canberra: University of Canberra.

Matinde, R.S (2012*). Dafina ya lugha isimu na nadharia: kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.* Serengeti Publishers: Serengeti.

Mathews, B. na Ross, L. (2010). *Research methods.* New York: Pearson Publishers.

Mazrui, A. (1995). Slang and code-switching: the case of sheng in Kenya. *Jarida la Swahili Forum, AAP* 42 (1995): 168-179 imesomwa 9/9/2015.

McCarty, T., & Watahomigie, L. (1998). Indigenous community-based language education in the USA. *Language, Culture and Curriculum* 11 (3): 309.25.

McIvor, O. (2009). Strategies for indigenous language revitalization and maintenance. In *Encyclopedia of language and literacy development).* London: CLLR. pp.1-12.

McNeil, D. (1996). Developmental psychology. In Smith, F. & Miller, G.A. (eds.). *The genesis of language: a psycholinguistic approach*. Massachusetts: The M.I.T. press.

Mesthrie, R. (2007). Language shift, cultural change and identity retention: Indian South Africans in the 1960s and beyond. *South African Historical Journal,* 2007, 57: 134-152 imesomwa 9/9/2015.

Michieka, M. (2012). Language maintenance and shift among Kenyan university students.*Selected Proceedings of the 41st Annual Conference on African Linguistics*, ed. Bruce Connell and Nicholas Rolle, 164-170. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project.

Milroy, L. and Muysken, P. (eds.) (1995).*One speaker, two languages: Cross-disciplinary* . Cambridge: Cambridge University Press.

Mohochi, S. E. (2005). *Mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili na athari zake katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa kidato cha nne katika mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya*. (Tasnifu ya Uzamifu, haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Egerton) Kenya.

Moreno, X.F. V. (2008). Catalonia and the Basque region. In O'Riagain, Williams na Moreno (eds). *Young People and Minority Languages: Language use outside the classroom Center for language and communication studies.* Trinity College, Dublin. Pp.25-38.

Muandike, M.F. (2011). *Linguistic borrowing and language vitality in Lubukusu.* (Unpublished MA Thesis, Kenyatta University) Kenya.

Mufwene, S. S. (2014). Contact languages in the Bantu area. In Nurse, D. and Philippson, G. (eds). *The Bantu languages*. Routledge: London.

Mugenda, O. M na Mugenda, A. G. (2003). *Research methods: Qualitative and quantitative methods*. Nairobi: Acts press.

Muysken, P. (1995). Code-switching and grammatical theory. In Milroy, P. Muysken (eds.) *One speaker, two languages: Cross-disciplinary perspectioves on code switching*. Cambridge: Cambridge Unievsrity Press.

Muysken, P. & Appel, R. (1987). *Language contact and bilingualism*. Amsterdam Academic Archive. Amsterdam.

Myers-Scotton, C. (2006). *Multiple voices*. Oxford: Blackwell.

Nagy, N. (1996). *Language contact and language change in the Faetar speech community.* University of Pennsylvania published PhD dissertation. IRCS Technical Report 96-08.

Nagy, N. (2010). Lexical change and language contact: Francoprovençal in Italy and Canada. *Paper presented at the Penn Linguistics Colloquium, AAAL 2010-Atlanta and ACLA 2010-Montreal.*

Nettle, D. na Romaine, S. (2000). *Vanishing voices: the extinction of the world's languages*. Oxford: Oxford University Press.

Nettle, D., & Romaine, S. (2000). *Vanishing voices. The extinction of the world's languages*. New York: Oxford University Press.

Newby, D. (2011). Competence and performance in learning and teaching: theories and practices. *Selected Papers on theoretical and applied linguistcs* Vol. 19: pp 15-32.

Ngure, K. (2012). *From Rendille to Samburu: A language shift involving two mutually unintelligible languages of Northern Kenya*.(Unpublished PhD thesis, University of Nairobi) Kenya.

Nicholas, Z. (2014). Vowel reduction in Sabellic languages: long-term effects of language contact in Ancient Italy. *Language Contact: The State of the Art conference Organized by the Linguistic Association of Finland (SKY), Helsinki Area & Language Studies and the CROSSLING research network Helsinki, August 28-30, 2014.*

Nonaka, A. (2009). Estimating size, scope, and membership of the speech/sign communities of undocumented indigenous/village sign languages: The Ban Khor Case Study. *Language and Communication journal* 29 (3):pp. 210-29 imesomwa9/10/2015.

Noori, M. (2009). Wenesh Waa Oshkii-Bmaadizijig Noondamowaad? What Will the Young Children Hear? In Jon Reyhner & Louise Lockard (eds) *Indigenous Language Revitalization Encouragement, Guidance & Lessons Learned*. Arizona: by Northern Arizona University pp. 11-32.

Norbury, C.F., et al. (2016). Younger children experience lower levels of language competence and academic progress in the first year of school: evidence from a population study. *Journal of child psychology and pyschiatry* 57 (1): pp 65-73

Nurse, D., na Rottland, F. (1991). Sonjo: description, classification, history. *Sugia* 12/13. 171–289 imesomwa 9/10/2015.

Nurse, D. and G. Philippson (2003). Introduction. In: *The Bantu languages* (D. Nurse and G.Philippson, eds.), pp. 1-12. Routledge, London & New York.

Nwogu, E. N. (2006). Utilization of information and communication technology (ICT) as a tool and strategies for improving teacher professional development for effective service delivery. *International Journal of Education,* 11 (2), 86-95

Okpanachi, D.A., & Abuh, J. (2017). Language Use and maintenance in Olawa, Dekina Local government area, Kogi State, Nigeria. *International journal of English and Linguistics research, 5*(6), 13-27.

O'Riagain, P. (1994). Language maintenance and language shift as strategies of social reproduction. *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 15(2&3):pp. 179-197

O'Riagain, P. (2008a). Republic of Ireland. In O'Riagain, Williams and Moreno (eds). *Young People and minority Languages: Language use outside the classroom.* Center for language and communication studies, Trinity College, Dublin.

O'Riagain, P., Williams, G. na Moreno, F.X.V. (2008). *Young people and minority languages:language use outside the classroom*. Center for language and communication studies, Trinity College,Dublin.

Obiero, O. J. (2008). Evaluating language revitalization in Kenya: the contradictory face andplace of the local community factor. *Nordic Journal of African Studies 17(4): 247–268*

Odero, E. O. (2013). *Sociolinguistic change in Elmolo as a dying language*. (Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.) Kenya.

Ogechi, N.O. (2002). *Trilingual codeswitching in Kenya-evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*. (Unpublished PhD thesis. Hamburg University) Germany..

Onadipe-Shalom, T.A. (2014). Attitudes in language shift and maintenance in Badagry. *Journal of the Linguistic Association of Nigeria* Vol. 17 Nos. 1 & 2 2014. pp. 75-90

Ontieri, J.O. (2013). Phonological influences of first Language on Kiswahili: a case study of Kenyan Bantu languages. *International Journal of Science and Research* (IJSR),Vol. 4(1): 2319-7064 imesomwa 9/9/2015.

Oso, W. Y., & Onen, D. (2006). *A General guide to writing research proposals and reports. A handbook for beginning researchers* (2nd Ed.). Kampala: Makerere University Press.

Ouma, M.A. (2014). *Code mixing and the learning of English as a second language: a study of selected primary schools in Migori County-Kenya.* (Unpublished MA Project, University of Nairobi) Kenya.

Pallant, J. (2002). *SPSS survival manual: a step by step guide to data analysis using SPSS for windows (version 12)*. Australia: Allen & Unwin.

Park, S. M. (2012). Religious participation in the lives of Korean immigrants in Canada. *International Journal of Innovative Interdisciplinary Research* Issue 2 2012: 11-20 .

Park, S. M., and Sarkar, M. (2007). Parents' attitudes toward heritage language maintenance for their children and their efforts to help their children maintain the heritage language: A case study of Korean-Canadian immigrants. *Language, Culture and Curriculum journal, 20(3),* 223-35 imesomwa 9/9/2015.

Patton, M. (1990). *Qualitative evaluation and research methods* (2nd ed) Newbury: London.

Paulston, C. B. (1994). Social factors in language maintenance and shift. In *Linguistic minorities in multilingual settings,* Paulston, C. B. (ed), 9-24. Amsterdam: John Benjamins.

Pauwels, A. (2004). *The handbook of language maintenance*. John Wiley & Sons Inc.London.

Perlin, R. (2009). Language attitudes of T'rung. *Journal of Linguistics of the Tibeto-Burman Area,* Volume *32(1)* imesomwa 9/9/2015 pp. 91.

Poplack, S. & Sankoff, D. (1984). Borrowing: the synchrony of integration. *Linguistic journals, 22:pp. 99-135* imesomwa 9/9/2015.

Poplack, S., & et al. (eds.) (1998). Instant loans, easy conditions: the productivity of bilingual borrowing. *Special Issue, International. Journal of. Bilingualism,* Vol. 2, no. 2, pp. 127-234 imesomwa 9/9/2015.

Prinhantoro, D. (2009) "*English loan words in Korean."* Retrieved from: http://linguistics-prihantoro.blogspot.com/2017/04/english-loanwords-inkorean.html.imesomwa 9/9/2015.

Putrayasa, I.B. (2016). The maintenance strategies of mothertongue. *Journal of Education and Social Sciences*, Vol.3 (2):84-86.

Ralli, A. (2001). Morphology in language contact: verbal loanblend formation in Asia Minor Greek (Aivaliot). In Thomas Stolz, Martine Vanhove, Hitomi Otsuka & Aina Urdze (eds.), *Morphologies in contact*. Berlin: Akademie Verlag.pp.185-201

Richards, J.C. na Schmidt, R. W. (eds.) (2002) *Longman dictionary of language teaching and applied linguistics*, Vol. 3. London: Longman Publishing Group.

Robins, R. na Eugenius, U. (eds.) (1992). *Endangered languages*. Oxford: Berg.

Robins, R.H. (1980). *General linguistics: an introductory survey 3rd* ed. London: Longman.

Romaine, S. (2002). The impact of language policy on endangered languages. *International Journal on Multicultural Societies*, Vol. 4, No. 2, 1-29. http://www.unesco.org/most/vl4n2romaine.pdf imesomwa 9/9/2015.

Sallabank, J. (2010). The role of social networks in endangered language maintenance and revitalization: the case of Guernesiais in the Channel Island. *Anthropological Linguistics* 52 NO.2: 184-205 imesomwa 9/9/2015.

Sangili, N. (2014): "Ubuntuism in the proverbs of Maragoli community of Western Kenya." In Rayson A., Susan S. D., & Sachindev P. (eds) *Culture and Media: Ecocritical Explorations* London: Cambridge Scholars Publishing. Pp. 241-257.

Sangili, K.N. S. (2017). Mitandao ya kijamii na mabadiliko ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja. *Jarida la Mwanga wa Lugha. Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika*, Chuo Kikuu cha Moi.

Sankoff, G. (2001). Linguistic outcomes of language contact. In Trudgill, P. Chambers, J. & N. Schilling-Estes (eds.) *Handbook of Sociolinguistics*. Oxford: Basil Blackwell, pp. 638-668.

Sevinc, Y. (2016). Anxiety, language use and linguistic competence in an immigrant context: a vicious cycle? *International Journal of Bilingual Education and Bilingualism*.

Stapert, E.L. (2009). Universals in language or cognition? Evidence from English language acquisition and from Pirahã. In Gil, D., Sampson, D. and Trudgill, P. (eds) *Language complexity as an evolving variable*: Oxford: OUP.

Stapert, E. (2013). *Contact-induced change in Dolgan: an investigation into the role of linguistic data for the reconstruction of a people's (pre)history*. Unpublished PhD Thesis, Universities Leiden, Geborentes Gravenhage.

Strubell, M. (2001). Catalan a decade later. In J. A. Fishman, (ed). *From theory to practice (and vice versa): review, reconsideration and reiteration,*. Clevedon: Multilingual Matters. pp. 260-284.

T'sou, K. B. (2001). Language contact and lexical innovation. In Lackner, M., Iwo A., I., and Kurtz, J. (eds.). *New Terms for New Ideas. Western Knowledge and Lexical Change in Late Imperial China*,. Koninklijke Brill: the Netherlands. pp. 35-56.

Thomason, S. G. & Kaufman, T. (1988). *Language contact, creolization, and genetic linguistics.* Berkeley / Los Angeles / London: University of California Press.

Thomason, S. G. (2001*). Language contact: an introduction.* Washington DC: Georgetown University Press

Thorold, M. (2005). *Language maintenance and language shift- a contrarian viewpoint*. Paper accesed at http://.thormay.net imesomwa 9/9/2015.

Treffers-Daller, J. (1998). Variability in code-switching styles: Turkish-German code-switching patterns. In Jacobson, R. (ed*) Code-switching Worldwide*. Berlin: Mouton de Gruyter.

Trochim, W. M.K. (2003). *The research methods knowledge base, 1st ed*. Cincinnati: Atomic Dog Publishing.

Tsitsipis, L. D. (1989). Skewed performance and full performance in language obsolescence: the case of Albanian variety. In Dorian, N. C. (ed). *Investigating obsolescence: Studies in language contractions and death.* Cambridge: Cambridge University Press.

UNESCO (2003). *Language vitality and endangerment: UNESCO ad hoc expert group on endangered languages*. Paris: UNESCO.

UNESCO (2010a). *Atlas of the world's languages in danger*. Paris: UNESCO.

UNESCO (2010b). *Why and how Africa should invest in African languages and multilingual education: an evidence-and practice-based policy advocacy brief.* UNESCO: Hamburg.

Van Hout, R., & Muysken, P. (1994). *Modeling lexical borrowability Language Variation and Change*. New York: Academic Press.

Vedernikova, E. (2014). Impact of native culture and religion on the Mari language. *ESUKA-JEFUL* 2014: 185-203 imesomwa 9/9/2015.

Verdon, S., McLeod, S. na Winsler, A. (2013). Language maintenance and loss in a population study of young Australian children. *Early childhood Research Quarterly* 29: 168-181 imesomwa 9/9/2015.

Wade, D. (1999). Vanishing cultures. *National Geographic,* 196(2): 62-89

Walsh, M. (2001). A case study of language revitalisation in 'settled' Australia. *Current Issues in Language Planning*, 2(2–3): 251–58 imesomwa 9/9/2015.

Wangia, J. I. (2014). Tense, aspect and case in Bantu and significance in translation: case of Kimaragoli Bible. *International journal of English language and translation studies,* vol 2. Issue 2: 138-158 imesomwa 9/9/2015.

Wardhaugh, R. (1992). *An Introduction to sociolinguistics.* Oxford: Blackwell.

Wardhaugh, R. (2002). *Pidgins and Creoles. an introduction to social linguistics* (fourth Ed).Blackwell.

Watera, M. E. (2014). Morphophonological changes of borrowed words from English to Lubukusu dialect of western Kenya. *International journal of English and literature*, vol. 59(2):45-51 imesomwa 9/9/2015.

Wei, L. (1994). *Three generations, two languages, one family: Language choice and language shift in chinese community in Britain*. London: Multilingual Matters.

Weinreich, U. (1953). *Languages in contact, findings and problems*. New York: Publications of the linguistics circle of New York 1.

Wichmann, S. & Wohlgemuth, J. (2008). Loan verbs in a typological perspective. In Stolz, T., Bakker, D., & Salas, P. R. (eds.). *Aspects of language contact. New theoretical, methodological and empirical findings with special focus on Romancisation processes*. Berlin/New York: Mouton de Gruyter, 89–121.

Winford, D. (2003). *An Introduction to contact linguistics*. Oxford: Blackwell.

Yagmur, K., & Kroon, S. (2003). Ethnolinguistic vitality perceptions and language revitalisation in Bashkortostan. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 24(4), 319-336 imesomwa 9/9/2015.

Yamane, T. (1967). *Statistics: an introductory analysis*. New York: Harper and Row.

Yoshiro, K. (1992). On the foreign language maintenance of the Japanese returnee students. *Intercultural Communication Studies II: 1:1992* imesomwa 9/9/2015.

Zhang, D. (2004). Home language maintenance among second-generation Chinese American children. *Working papers in educational linguistics,* 19/2: 33-53 imesomwa 9/9/2015.

## KIAMBATISHO A

## MWONGOZO WA MAHOJIANO YA KWANZA: KIONGOZI WA KANISA/KIONGOZI WA KIJIJI

1. Je, Kimaragoli kingali kinazungumzwa kwa undani? Kuna mabadiliko kwa Kimaragoli cha sasa na cha kale?

2. Kati ya Kimaragoli na Kiluo, lugha gani ambayo vijana na watoto wa Kimaragoli hujifunza haraka? Kwa nini?

3. Je, Wamaragoli walipokuja huku mwanzo mwanzo wa 1940, walikuwa na lengo gani la kuanzisha shule na makanisa ya Kimaragoli?

4. Tuna makanisa mangapi ya Kimaragoli? Yanatumia Kimaragoli katika mahubiri, matangazo, nyimbo na kadhalika?

5. Kwa miaka hii yote ambayo Wamaragoli wameishi na Waluo, je, kumekuwepo na vita au kutopatana?

6. Ukilinganisha vijana, watoto na wazee, nani wanadumisha Kimaragoli zaidi?

7. Je, kuna tatizo gani la matumizi ya Kimaragoli linalokumba vijana na watoto hapa Uriri?

8. Kitu gani kinawafanya vijana kushindwa kuongea au kuzungumza kwa Kimaragoli kila wakati?

9. Wewe kama kiongozi wa kanisa na mzee wa kijiji, unapotembelea watu wako, je wewe huwapata wakitumia lugha gani katika mazingira ya nyumbani?

10. Je, watoto na vijana wenu hujidharau wanaposhindwa kuzungumza Kimaragoli vizuri?

11. Je, kuna ruwaza zipi za matumizi lugha ambazo hujitokeza wakati ambapo Wamaragoli wanakutana wenyewe kwa wenyewe au Wamaragoli kwa Waluo?

12. Unaonaje hali ya Kimaragoli siku zinazokuja?

**KIAMBATISHO B**

MAHOJIANO YA KWANZA

(MZEE WA KIJIJI/KIONGOZI WA KANISA-TOLEO LA KIMARAGOLI)

Eneo: Nyumbani kwa Mzee M; Siku: Jumamosi; Saa: 11-11.30 asubuhi

Mtafiti: Yinzi ni Nixon Sangili, msomi wa University ya Rongo. Mbeye mu vohenzeritsi vwa vandu vitu Varogoori vang'anyira Migori yinu. Nyenya kumanya na korora niiva miima gya varogori, niiva ni yengo, niiva nu mwivugana, niiva nu muskuru gyikizizagila noho niva vagwa Vavo nu kuhamira mu mima gya vavo. Ma Kandi mbenza niiva vakitumikira Llogori noho vama vareka. Kandi mbenza ndore niiva Llogori tsana rwagirung'ana noho rukilla l'lara rwere.

Mzee M: ni llara rwere nitarii rutsitsa rugirung'ana. Rugirung'ana kigira eee kuri vaana mwakazugana na vatende vamoroma Rovoo, vandu vitu vanguha komoroma romovoo kuvita Llogori.

Mtafiti: Hahah Kigira ki gaveye ndi? Yaani vana vitu vanguha komoroma Rovoo vwangu kuvita Llogori?

Mzee M: Vavoraa ndi Llogori nu rudinyu kuvita Rovoo. Mang'ana malla gaveye mu gafwana madinyu kuvoo. Ni rahisi kwiga rovoo kuvita Llogori.

Mchungaji: Umanyi, nu kora comparison nu Rovo, Rovo ni rudoto kumanya no komoroma. Llogori vana vavora nu rudinyu. Ma kandi, vana vitu vaveye na varina Vavoo kutura vava vana kuduka mu rong'ele. Vamoroma tsinimi tsyosi kutura vatsya musukuru, vaveye mumikinu, vayitsa tsing'ombe. Bora tsa vaveye hala, varamoroma tsyosi.

Mtafiti: Sya ndakagenda mu tsisoma rugano na rugano indevelitsa, ndakavolwa ndi, chajira vandu va kare kutangiza mavugana ni tsisukuru mihiga gya 1940, yaari ndi vaduki kwirwadzira mu Llogori no kosominya vaana mu Llogori. Yaani venya vakori vindu vyoosi mu Llogori. Umanyi mang'ana gene yago kuvaa girigari?

Mzee M: Vakitangira hee, (yakiring'ana hakee). Umanyi hee, vakitangira venyaa ndio. Vandu venya vahiri vaana vavo mu tsisukuru zyavo. Vavoo vahira vaana mu tsyavo, na Varogoori valla ndi, kari kuyi kokore ndio. (Wakati huu tulikuwepo na mpangilio wa kuketi, viti vizuri vililetwa ili mtafiti aweze kukaa na kuandika vizuri.) Umanyi mkiri vageni, mbezanga na that unity, rwa mhamii yiraa. Rwa mutsidza mu vandu vandi, kuduka m'mba halla nohoo. Umanyi rwa varogoori vazira yinu, vavoo vari indangu yira,yinu yaariza varogoori veree. Rwa chifu yahana murimi, yakara ahimbi ikilomita ndara ndi kutura ku madzi, navoora ndi vatarimaa ku madzi dave, ku navoola Varogoori vavuguri mirimi gya iruhya na vareke indangu. Ku yaduka ing'inga nareta Vavoo navahaa mirimi indangu karibu ku madzi. Ku iruhya yaari varogoori veere, rwa vaduka kwari ku ni tsisukuru yinu da. Ku rwavatangiza isukuru, garoreka ndi, vaana vatsitsa mu tsisukuru yidzi vari, vana varogoori bere; kari avigidzi vukutanga vatura evorogori. Umanye ninii..riganisa rya Friends yiri yiryo ryari na vandu vanyingi, vandi vatangiza gavoo navutswa vatanguira mu Friends.Mavugana ga Salvation Army gororaa Kamsaki yira, gatangira yinu. Kari administration na supervisors wa masomo, vatura evorogori. Ku mihigya gyene yigyo, vavoo vatanga kuzaa mu tsisukuru zya varogori, na vivuli na vigidzi valaa ndi kunyara kuvakunga dave. Ku rigyiza Llogori mu tsiskuru zindala zyatanga kuroka kwigiza LLogori. Valaa ndi, Kulazimisha Vavoo kwiga Llogori, variruka vazyee mu tsiskull zindii.

Mtafiti: Koveye mu muno na mavugano gandi?

Mzee M: Hii, koveye muno na Friends, Salvation, na P.A.G na alafu kuvaa nu tuvugana tundi tudii kuri Pentekoste, African Israel, Vadivai. Mavugana yagaa nigakitangaa gaari varoogori veree navutswa vavoo vatanga kwingiramu.

Mchungaji: Mavugana manyingi Varogori ivo vatangiza yinu. Kutura ku Friends kuduka ku Salvation Army na gandi mu. Suvira kenene chaniga kutangizwa chari kurandiza ling'ana lya Nyasaye. Kigira vari varogori voosi, na gyari mihiga Ruswahiri rwari rukiri kumanyikana, haas, vandu vatumikira Llogori vutswa. Tsisukuru tsyari ndyo kandi.Umanyi kandi Varogori na vigitsi varahi kandi varuru. Ku madiku geneyago, yari rahisi konyora vigitsi Varogori kuvita Vavoo. Kandi mundu naveye mgeni, amayanzila kokora gege mwene kutanga nakiri kuranga vandi vandu.

Mtafiti: Na mirwadzo, matangazo, kwimba, na kindiki na kindiki, gaveza Mu llogori noho vazuganyia?

Mzee M: Uh, Mang'ana gave uniform dave, ni uniform dave, kigira, kuri hano (Bware Friends Church) unyara konyoora kuvugana na vaana (vasomi) na vigitsi vavo nivazii kutumikira Luswahili noho rusungu. Navustwa, kuri vakeere vahndira ku yava, nivatangaaza, vatumikiraza Llogori. Matangazo ga vakeree gavezaga rigari involviong na vandu vi ichova dave. Vang'ele yavo vaduka vatumikira Llogori, Luswahili nu Rusungu kigira na vaana kutura mu zimbega ni zimbega. Ku vangele vatumikira tsinimi yitsi kunangwa vavuri kufwana vitwiza ku vandi vandi dave. Ni kuranga harambee noho miyinzi gya rivugana varasura kutsa. Navutsaa koveye nu tuvugana tudii kuri Friends eveye Mu ngereka mura, Vallanga Kisangura friends church, vene yavo vatumikiraza Llogori kigira vavoo vaveye mu dave. Kuri Uriri Friends Church, venee yavo vatumikiraza Luswahili kigira vaveye ku mu town kabisa. Umanyi, embega wene yeyo, uranyora mundu yareta mukana Mmbo na yaivula vaana vasomera ichova. Vaana yava vamanyiku Llogori mba navutswa vamoromaza Rovoo. Kuri, Wamanya Prof. Sande? Mgogo wewe ni Principal wa Secondary, na amanyi Llogori dave, ku vaana veve vamoroma rovoo nu Ruswahiri. Sasa rwa vaveza mu vaguna, kuduka vatumikiri Ruswahili.

Mchungaji: Wange Bware umanyi riveye na vasomi na vigitsi ve Bware secondary. Vana na vagitsi yava vatura tsimbega ne tsimbega, varomora tsinimi rugano rugano. Ku kusangana navo vuri Jumapili kutura saa mbiri kuduka saa ine, makutumikiri Llogori dave. Llogori lunyala kutumika mu tsikamiti tsya vahindira, noho kuhana matangaso za vakuru. Lakini nutsya Uriri Friends mu town, yavo vatumikira Ruswahili nu Rusungu. Gandi gangovole gaveye mugati kabisa, gatumikira Llogori kigira si vaveye na Vavoo rigari mba. Na vaveye mu vamanya Llogori.

Mtafiti: Na ku mihiga gyu wakava yinu gyooosiii, koveye kun a vavoo vavunana na Varogori kigira mirimi noho kindiki?

Mzee M: Yivyo viveyeho. Kari mgamba gundi vandu vitana ku rigari. Koveye ho na vandu vagura mrimi ku vavo ma vafwana vachereva kuvugura Title deed. Ku rwavasukuru vagura mirimi vaduka havundu vakuzaa, vaana vaviruka va vavo, vatanga kotevana mundu uyu yanyoreka ndi hano. Ku rwa vateva title deed, ma vatamwa kuhana, mang'ana gatangira hene yaho.vaveye na title deeds, vamenyi ne mirembe sana na Vavoo.

Mtafiti: Niva msakuru Mmbo yadekiza mkana mrogori, ma akutsi, mariga no kosyominya, gekoreka mu Llogori noho rovo?

Mzee M: gekorechi ndyo, vamatumikira Rovoo nu Luswahili. Nina vamanyi vandu vi hiri yu mukana varaza, varatumikira Luswahili. Navutswa mariga gakizyaa, varogori vaveye vene ku vene, vamoromaza Llogori. Uranyora yavaa vamoroma Rovoo, na kunyi Komoroma Llogori. Nivaa kurava nu mkere noho msakuru kabisa, atamanyi Luswahili Vurahi mba, kari niiva nu mmariga gu mjaluo, aramoroma Llogori. Kindu keyehe ho ni yiki, kari vavoo vene vahula Llogori. Vala vama vavoora vagirung'anye, vandi vavora yikwo ni kwononyia vwiyangu.

Mchungaji: Mang'ana ga makumbusho nende vimila vya varogori vitumikira Llogori kutwura kare. Lakini vindu yivi vyatanga kogota. Vandu si vakora makumbusho rigari mba. Lakini kekevo, uranyora vasakuru vasarisa vana mu Llogori.

Mtafiti: eeeh sasa hee nohenza ku viika, yani, vaana, vang'ele na vasakuru, variha vadinyiritsa Llogori?

Mzee M: Vasakuru. Vang'ele dave. Vang'ele yivoo vadinyiritsa Ruswahili.

Mtafiti: Kwari nivi Mchungaji, Bware Friends nombola ndi, ridiku rya Christmas, novora ndi vandu varimba marago mu Llogori. Vasakuru na Vaana vavugiila navutswa vangele vavora ndi vanyara dave, kindiki kivaniga?

Mchungaji: Hii vang'ele vaveye nu vudinyu vonene komoroma Llogori, sanasana vavoleywe vimbi marago. Vatitsa sana. Vana vavura vudinyu kandi na vasakuru na vakere.Navutswa nutsya mu mavugana ga ngovole gaveye mu gatii, yavo kwimba Llogori ni vudinyu dave. Ku nohenza, garondekana. Nutsya mu conference ya vijana, uranyora vimba tsinyimbo tsyo Luhya sana kari kuvita Rusungu nu Ruswahili. Ku manyi kindiki kivatihitsa marago dave.

Mzee M: oh Influence. Ma kandi vadaka encouragement. Rwa vanara Ruswali, nuvavoola Llogori, rufwana ruvasumbura.

Mtafiti: Yaani varoraa Llogori ruvakonya dave noho yike?

Mzee M: awaaa, yani hee, richaya! Varora ndi ruvahira havundu da.

Mtafiti: Gaveye ndi vana yavo vavura vudinyu?

Mzee M: umanyi hee, ku vaana, rwu mwigizi yatsaza ma avavola ndi kurimba mu Llogori, rwa avigiza rwimbu, vatangaza kwimba. Unyara konyora ku vange'ele varazaa vaviri, vavagaa, na vandi vavura kuzaa mmarago, ku onyora voosi vakoreka. Lakini, nivavaa vandu vikaraza harara, varimbaa vitswa. Vakere na vasakuru yavo vaveza ni taabu mba igira ni kindu cha vakakora ku inginga indambi.

Mchungaji: Vwongo vwa vana vukiri kuhindira kutanga kurakavitsa dave. Ninavoleywe kindu, valla ndi ni muhimu kokora nu kwitihitsa.

Mtafiti:kindiki keromba vang'ele vatamwa komoroma llogori vurahi?

Mzee M: Orora vaana vitu vanyingi vamenyi ichova kigira masomo. Wa vaziza si vagana na varogori vavo mba, kari niva varava mu schools ziveyemu na varogori kuturaEvorogori,vatiza kuzya kuvoo kigira vamanyi Llogori vurah dave. Vivisaa. Kunarilla Ruswahili sana ruvarombaa vava nu vudinyu komoroma Llogori. Ku vaduka havundu vagadahara. Kuri vaana vamenyi mu town, rwavaza kumenya mmadara yinu, vaveza vamanyi Llogori dave, ku nave ni mihiga gyanga ndi, irwo rwahula Llogori kutanga. Ma naduki mihiga 10 kuzya imbiri, irwo rwatanga kwiga mang'ana gaviri gavage gu Llogori.

Mchungaji: Witu yira, ishida eveye ho ni ndara. Vaveye vatende na Vavo na Vamaasai.Vaveye vene ku vene, uranyora vamoroma Llogori. Navutswa vaveye na varina Vavoo na Vamasaai, Vamoroma Rovoo noho Ruswahili.

Mtafiti: Kuri msakuru , Mrindi, nogenda ku migizi nu muzinyumba zya vandu, mnyora vatumikira romoroma ki?

Mzee M:Kuzyii hango konyoraza vatumikira LLogori. Navutswa, Llogori rutumika sana kuvasakukuru na vivuri, ma na vandu vahindira ku. Lakini nonyora vana kindu 10, 12 kari 14, nivaa varazaa mmba ma vavatumii kindu, uranyora vivuri vavo vavatumira mu Ruswahili noho Rovo. Vana vitu ku mihiga yigyi, vahula Llogori, navutswa komoroma kuvaregelea. Ku mwivuri arora, havogono hu kumsumbura mwana, afadhali amoromee Ruswahili noho Rovo kumwanguhizira.

Mtafiti: Na vana zana yava vichaya kun di vamanyi Llogori dave?

Mzee M: Awaa, yavo valaa za vaveye vurahi.

Mtafiti: Na munyi muvavola ku ndi muyanza mutagotizi Llimi rwinyu dave?

Mzee M: Hii kuvavolaku navutswa time yu kudinyirizaa mwana mu Llimi yiru y'o itaveho dave. Niva kurava navo mwivugana, mu commitees, onyoraza kutumikirii Ruswahili. Kari niiva mwana mkana aravahira mu vavo, vavo varamrombaa amorome rovoo. Kari vana veve varigizwa rovoo. Ku rwa virana mu viiko vavo, vanyorandi, llogori ruvatamii, ku vamoroma ruswahiliza. Ingawa arenya mmorome Llogori mwivugana noho hayo, lakini nimmbola amoromee anyora vudinyu mno. Iho havaduka vatanga komoroma Ruswahili. Afadhali kari omorome rovoo kuvita Llogori.

Mtafiti: Vana vinyu vaveye mu viduma, kovore Varogori-Vavoo; Varogoori-Varogoori, vatumikira romoroma kii?

Mzee M: kindu chu kutanga, vaana vangele yava viga llogori kigira Mmbo wenya umanye mangana gege, wigi ma ummorominye mu Rovo. Kari anyala kokovola mangana gu mmwoyo gwige. Nomoroma naye Ruswahili, amatya, aganagana ndi amromoa na stranger. Ku vana vitu vigaa rovoo kuvita Llogori sana.

Mtafiti: Na veveye ku varogori vene ku vene?

Mzee M: vene ku vene uranyora vamoroma Llogori, kandi ru jaluo. Vala vamoromaa Llogori, na vandi kari onyora vamoromaza Rovoo. Uranyora Mrogori ku mrogori amoromaa rovoo.Unyara kari kuhula vamoroma rovoo vaveye hano, vaturaho visundi hambiri, uhula vagirunganyi vamoroma llogori. Nindyo sya vakoraa.

Mtafiti: Koveye ku na mang'ana go Rovo mu Llogori?

Mchungaji: Hii gaveyeku mu. Kuri Thim Jope, Varogori vavora Kitsimi. Mu Llogori ni kisaka. Ku makovore mu Rovo dave. Ku llomba riva ryu Llogori. Mang'ana kuri nyoyo, kuon, kandi gatumika sana.

Mtafiti: Ororandi mihiga gizyaa?

Mzee M: hambiri yaha hafwana haza have hadinyu. Umanyi mwana nasome romoroma muskuru vvezaku vwera kigira yiga kuhandika no kosoma. Viga kwimba ku mu llogori. Haas, karunu ndi, vaana vigaza ruswahili, vimbira mu ruswahili.

Mchungaji: Yinzi ndora Llogori rurazizagila kutumika. Fwana chatsa kigirung'ane ni mang'ana. Kari handi si sana. Kindu cha kwenyekana kokore, kwigitsi vana vitu kokonye Llogori kutsitsagila. Kuyanza kuri rwa utsi ndi kokora research.

Kumanya ndi vandu vatura embega ne embega kutsa kuvateveliza ku romoroma rwinyu ni kindu kenenene. Kwinye genyekana kwigitse vana vitu Llogori.

Mtafiti: orora ndi rwe serikali evora ndi venya viranye Mothertongue mu skulu?

Mzee M: ni vurahi sana. Navutswa orora yinu, vana vazunganika, fwana vavukanye vana mu virasi vya varogori, na vavoo.

Mtafiti: Haas gari gene yago vutswa. Ndanza ngende mgamba gundi.

## KIAMBATISHO C

## MWONGOZO WA MAHOJIANO YA PILI: WATU WA KWANZA KUHAMIA MIGORI

1. Mlikuja huku Migori lini na kwa njia gani?

2. Sababu gani iliwafanya kuhamia huku?

3. Unaweza kutuambia jinsi safari yenu ilivyokuwa?

4. Mlipofika huku je, mlielewana Kilugha? Mlifanyaje ndipo mkapatana na wenyeji?

5. Mlifanyaje masuala ya shule siku hizo za kitambo?

6. Ikizingatiwa kwamba mlikuwa wageni katika nchi mpya, Wenyeji Waluo waliwachukuliaje?

7. Huku inaonekana kwamba huwezi kutofautisha Mluo na Mmaragoli kwa sababu mnazungumza lugha zote. Je, mlianza kujifunza Kiluo mara moja baada ya kufika?

8. Je, ni Sababu zipi zimefanya Kimaragoli kuzungumzwa hadi sasa hapa?

9. Je, katika kuishi kwenu hapa, mshawahi kukosana na Waluo?

## KIAMBATISHO D

## (MAHOJIANO KATI YA MTAFITI NA WAZEE WATATU WALIOKUWA KATIKA KUNDI LA KWANZA KUWASILI MIGORI, ENEO LA EMUHANDA)

Mahojiano haya yalifanyika mwezi wa Mei 26 mwaka wa 2017 katika nyumba ya Mtafitiwa eneo la Emuhanda, eneobunge la Uriri. Mtafiti alielekezwa katika eneo hili na mjukuu wa mtafitiwa ambaye alikuwa pia mwanafunzi wa mtafiti mwaka wa nne, Chuo Kikuu cha Rongo.

Mtafiti: Vwira guuga? Na guuku?
Guuga 1: Harere mwana yivi? Yivi vwaha?
Mtafiti: Yinzi vananga Kenyani, ndura havundu havaranga Isavatia, Evorogoori wene.
Guuga 1: Ohooo Evorogoori, yinu okora kindiki?
Mtafiti: Mbeye mu vohenzeritsi hakeke ku vandu vitu varogoori, nyenya kibara chosi ndi koveye nindi ihiri ya Varogoori yinu ndi. Mundu angonyi kuduka hano nu mwisukuru wovo uyu, Indire.
Guuga 1: Yee ndyo okori vurahi mno. Kunyi ku koveye ho, karibu sana.
Mtafiti: Sande. Sasa hee, nyenya kumanya, mwadza yinu ri? Na mwaza ndi?
Guuga 1: Yinu kwadza kare, mihiga gya vakoroni. Gyari mihiga gya 1930 kutsia kutsia mu 1940. Kudza kwitu yinu chari kindu chatanga kare. Kwadza zinyumba zya Mmavi, Vamuku, Wasaniaga, Vavulugi ni zihiri zindi zingekekee.
Mtafiti: Yiki chavagema kung'anyira yinu?
Guuga 2: Chajira nikung'anyira yinu yaari mundu mula yalangwa Shadrack Amugo. Amugo yari nazitsa mu Vakurya ma navita havundu havayava Zifeza. Havundu hene yaho harangwa Macalda, Migori. Rwa yirana Evorogori mihiga gya 1930, yakovola vindu vya yarora,navutswa kenene, yakovola kivara kya yagana nacho. Chari kivara kirahi mno, na vandu sivarimu vanyingi dave. Yavora ni kirahi kurima nu kutaga. Ku y'e yajira kutsa yinu.
Mtafiti: Rwa mwadza yinu, rogendo rwari ndi?
Guuga1 : Mritanga, kwatanga rogendo rwitu kutura ivihiga ku virenge paga kuduka Kisumu. Kutura Kisumu, kwaziira ku madzi paga ikuduka havundu harangwanga Homa Bay. Kuduka homabay, kwari nu mudoga gwu msungu, kindu kuri karori, gwakuginga kuduka havundu havaranga Nyaribari. Kwidikira ha Nyaribari ku mihiga gya 1930, kwivurana kuva vanyingi rigaari. Vagisyii vaduka havundu vakutya, kigira kwari vanyingi na kufwana kuvugura mirimi gyavo. Vamihi vya Vagisyii varora ndi, kuvaa vanyingi, varatamwa kukwamiha. Ku vahenza inzira yu kokogehitsa mu kivara chavo. Chifu wa Vagisyii ing'inga yene iyo yarangwa Orema. Yamanya nahana vutumi vuziira Chofu Otieno wa Migori. Na chifu Otieno naye yaarii mrori. Yarota ndi avandu vaveye ku madzi vazaa. Vamoroma ullimi royovoyi. Ku navaranga vandu vene yava, Avayovoyi. Vamorooma Ullimi rugano ku Vavo. Has, Chifu Otieno yavola vandu veve ndi, Avayovoyi vaya, vaveye ku mato, mu nyanza, na mu mikono gyavo, vaginji tsimbatsi na magembe. Ku yamanya niduka ing'inga, Chifu Orema nakuha mkonyi, nikugenda kutsa Migori. Rwa kwaduka Migori, kwahirwa ku Chifu Otieno, naranga ibarasa vandu voosi vaari ku vwimilli bwibwe vatsaa.
Mtafiti: Ku mwamoroma ndi niiva munyi mwari mmnyi Rovo navo sivamanyi Llogori?

Guuga 1: Anza hee, rwa kwadza yinu, kwari zinyumba 15. Ku murumilla gwatsa yinu, kwari ku nu mundu mula, yatura ha Maseno. Mundu uyu yari musakuru na yarangwa Okango. Okango yamoroma Oronyore nindi Rovo. Ku Okango yahuliza makuva ga Vavo,agirung'anya Mu Ronyore, ma kumanya Vavo vavora ki. Ma kunyi vasakuruvitu vamoroma Llogori, Okango ahuliza, ma agirung'anya mu Rovo. Ku kwakora ndyo paga kumara baraza. Ku rwa kwamara, Chifu Otieno yamanya nakuha mundu yarangwa Okello akokonye kumanya hakwidikira. Ku rwakwatanga rogendo, Otieno yakovolla, niva kuragana nindi inyamanyama emboma, kurakamenye ni mirembe mu Vavo, na niiva kuragana ni inyamanyama imbarava, rimenya ryitu llava ryu vudinyumno. Ku Okello yamanya nakuhira havundu hatovolwa na Chifu Otieno. Havundu hene yaho hari muritu bere. Kwagenda korora tsisimba, tsimbogo, tsinzoka, vikondo navutswa si kwahenda mwoyo mba. Ku kwahirwa mu kiguru, nivakumanyia mrimi gwitu. Rwa kwaduka hene yahoo, kwari nu mundu museretse, yarangwa Igunza. Igunza yakovolla kwosi kumwaridzi tsimoni kusare. Yasara kuvee nindi mirembe mu kivaara kihya, komenye ma nu kwivurane. Hene yaho yiho ha kwatangiza Rivugana na Friends ryu kutanga embega yinu. Kuduka nunu ndi, rivugana yiryo, rikiraho ma rikitumika.

Mtafiti: Uhani history indahi sana, vindu villa kari kwari kumanyi mba. Na ku mwakora ndi mang'ana gi isukuru? Mwasoma ndi?

Guuga 1: Risoma ryar ridinyu mu ritanga. Navutswa rwa kumbaka tsingo nindi isukuru yukutanga, vandu vitu vatumana vigitsi vatura evorogoori kutsa kwigidza yinu Navutswa vigizi vatsa vatura Cheywe (currently known as Kakamega). Kunyi vene kwarombainzira yitu ya Oyani ma nikusaranaa mu Kanyamkago yoosi. Vandu vitu valla vaduka vasaranee kutsia paga Mu Vakurya, vakana vadeka yo ba vandi vingira mu Tanzania. Navutswa vanyingi vatsia mu Vakurya na Tanzania vamanya virana kigira vadambika muno. Vivirwaa tsingombe nende vindu vyu munyumba. Na vakana vadambizwa na vasatsa vakurya. Vaala kari vitwaa vayarivwa wene yeyo. Ku ni vakekee vikutsira vatigara.

Mtafiti: Rwa mwidikira sasa Migori, muromba hava hango hinyu, Vavo vavagulula ndi?

Guuga 1: Vavo ni vandu vadamanu daave. Vanyingi variku nu vudinyu nukunyi dave.Kwamenya ni mirembe. Nitarii hee, kwagaya vakana vitu kuvahira ku vavo kigira varonda mima gya murogori kokeva mwana muyayi dave. Ma kandi, rwa kwari mu baraza na Chifu Otieno,kwavugiridzana ndi: Mkana Murogori atavahira ku Mmbo dave na muyayi Murogori atadekidza ku Mmbo dave. Ku vakana vitu valla vari nu vidunyu kodeka. Kwatsia kuvahenzera vasatsa Evorogoori. Navutswa mihiga minyingi gyavita, vana vatanga kuzuganika na Vavo, ku rwa vahindira, uvurina vudinya. Lletana ryama rivaho, mukana murogori atsya ku Mmbo na Mukana Mmbo yatsa ku muyayi Murogori.

Mtafiti: Mwatanga ndi kwiga no komoroma rovoo?

Guuga 1: Ola hee mwanange, nutsiyi havundu, genyeka wiga romora rwa havundu hene yaho. Ni miima mirahi kigira wenya omenye nindi mirembe. Kari rwa kwari Kisii, kwiga Rugisyii kigira kukiri vaana, kwasanga isukuru navo. Kwakina navo. Wazya havundu udake isukuru yu kwigiza vana Llimi rwavo, ruma ruduka havundu rutanga kogota.

Mtafiti: Na kindiki charomba Llogori romoromwa kutura mihiga gya kare kuduka nunu ndi?

Guuga 2: Anze hee, murogori nu mundu agotitsa mima gigye dave. Hosi hakutsidza kuma komoroma lulimwi lwitu. Kwigiza vaana vitu Llimi rwavo koveye hango. Nohenza yinu, uranyora mita ge kerogori igo gatumika. Kunyi rwa kwatangiza tsisukuru, kwenye vana vitu vigitswe Llogori. Kandi yicho chagira kutsia

kuhenza vigitsi Evorogoori na Kakamega. Kwenya vaana vitu vatsitsangili komoroma Llimi rwavo. Kandi kindu chakokonya mihiga gya kare yigyo, kwavugiritsana ndi Murogori avahuri ku Murogori nu Mmbo ku Mmbo. Ku mutsinyumba zyitu, kwamoroma vutswa Llogori. Kari kwari kwamanya Ruswahiri vurahi mba.

(Baada ya kutushughulikia jikoni, alikuja na kujiunga nasi sebuleni ili kuchangia mjadala)

Mtafiti: Na Mwavunanaku na Vavo mu rikara ryinu hano?

Guuga 2: hii kwavunana ku rigari navutswa syikwavunana ku mang'ana gandi dave. Mirimi yigyo gyareta vurwani.

Guuku: Mugamba gundi, Vavo vakunga na kuhizilla varaogori kutura mu tsingo zyavo. Mang'ana yaga gatangira mu siasa muhiga gwa 2002. Varogori vanyingi vakungwa mu mirimi gyavo mu tsimbega tsindala nivaaza komenya mu varogoori vavo.

## KIAMBATISHO E

Mahojiano Na Mmoja Wa Watu Wa Kwanza Kuhamia Migori; Eneo La Mahojiano: Arambe, Nje Ya Nyumba Ya Mtafitiwa; Wakati: Disemba, 16 2017, Kuanzia Saa Tisa Alasiri Hadi Saa Tisa Na Nusu Alasiri

Mtafiti: Mwatsa Migori ri na mwatsa ndi?

Nyanya 2: Yinzi sinzitsuritsa lidiku lya ndatsa vulayi dave navitswa lwali mu Lwakane, muhiga gwa 1950. Ndavitira inzira ya Lake Victoria ma imbugura mudoga kuduka yinu. Inzira yali indayi mba

Mtafiti: Yiki chagira nung'anyira yinu?

Nyanya 2: Yinzi kutsa yinu chari kindu cha lazima. Yanomba kutsa yinu yari baba.Nzitsuritsa vulayi sana. Baba yakkora igasi Mu Ruguru. Ku, mama yakudza na ninuva vudinyu kutukidzira baba vutume kigira si kwari na nzira ya vwangu yu kutuma vutume dave. Ku mundu yatsia mu center kutuma Fax yo kovora ndi, mama yakutura ho. Baba yachereva konyola vutumi ma kandi kutanga logendo. Lwa yanyola, yatanga logendo vwangu. Madiku gene yago, kutura Nairobi kuduka yengo si yali safari ye lidiku lilala dave. Kuvandu yengo navo vali vakava nu mbiri gwa mama madiku gavage, valola ndi, rekakuyaviri kigira guloneka. Vayavira mama baba nakili kuduka. Ku vakuru vama vaamu kuyavira. Baba lwa yaduka, yalila sana. Yasioma mno. Yasinyika kandi. Yateva vakuru kigira ki vakuyavila mgogo weve vujira oyo kuvaho dave. Ku vasakuru vageritsa kumbola navutswa si ya vahulitsa mba kigira yu vutima. Yari nasikinyiki sana. Rwa madiku ganga ndi gafwa na vutima vukiri kososa, navola ndi atura hango na valimulola ku kandi mba. Ku yatula natsia kabisanagota. Ku vandu baada ya inginga, vatanga kumuhenza. Vatumwa vandu kutsya Nairobi wa yakola miyinzi vatevelitsa niva aduki ho. Navutswa vavavola ndi yavora atsiza mmariga ku akiri kwilana. Vatuma vandu mu viiko vitu voosi kuduka vandu valuha. Ni kindu chavugula mihiga minyingi. Ku kwari ho na kasakulu kandi katsa yengo kavola ndi, niiva kukiri konyola mundu wa kihenga, kunyara kugeritsa ku handi havundu. Yavolla vandu ndi, ku inyinga yakava hanyuma hano, Varogoli vakang'anya kutsya havundu halangangwa Migori. Havundu hano hali ku ihale na oyo mwene amanyi yo mba. Ku vandu vatanga kotevelitsa wene yeyo ni hayi. Ku rwa vamanya ni hayi, na kutsia yo ni ndi, vasakulu vatuma mwana myayi mula atsie wene yeyo kumuhenza. Ku yatanga logendo na yagenda sana ku vilenge. Lwa yaduka Migori, yagana na muritu munene. Na kandi yagana na vandu ma navateva wa vandu Fulani vang'anyira. Ku ingavi indayi, vandu veene yavo vari Varogori. Vamoloma mu vutambi ma ivammbola si vamanyi mundu Kikumba dave navutswa kigira Varogori vari vakeke, vwari vuve vudinyu kumnyora dave. Ku vamuha vogono,nagona madiku ma nivatanga kotevelidza. Vamnyola yang'anyila indangu yila amenyi wonyine. Ku mundu yatumwa oyo yamanya niyidzuritsa rigondo rirye. Vamoroma, namuhomba virane yengo navutswa nasura. Ku mtumwa yamanya niyirana yengo baada ya inyinga ingutsutsu. Lwa yaduka yengo, nahana lipoti, vandu vasangara mno nu kusanditsa kigira vari vamanya ndi uyu yakutsa varikamrore mba.

Mtafiti: Wakora ndi lwa wahulla mang'ana yago?

Nyanya 2: Ndari ingiri mwana navutswa ndamanya chekoreka. Ku yinsi na vambotso vange vari vahindira hake, kwari nu rusaa lwo kolola baba witu. Kandi umanyi kwali kukiri mu sukulu, ku vakotsa vitu vakuvugila dave. Kwikudzira kuduka kutwekitsa school.Ingavi yatulla yo, vayayi vitu vanyora miyinzi, na yinzi kindu chari ku mwoyo gwange, baba. Ku mgamba gundi, baba yatsa yengo, nambugura. Kwagendela kumatsi, mudoga na hatigara, kugenda ku virenge. Ha kwaduka

kwali nende mritu, vulimu vwatambiha havundu hoosi, Ndanyora baba yali yumbaka kanyumba kadi kuri kadisi. Ka madohi ma tsingedi, yasita nu vulimu. Tsinyumba madiku gene yago, tsyarange na madirisha noho miryango gyu kuhanaa mba. Viduku nu mmbasu. Ku tsinzoka tsingira mu kandi tsitura.

Kwarima yinzi na baba, nikutaga mbere no vooro. Ndatigara yengo wonyine baba natsiyi havundu kohenza chukulya.Vikondo vyanyangitsa sana. Uvirasila visala, vigimila, kandi vikulasila. Vyangola kehenyehenye. Vutii vwanditsa nzya kuvisa mmba. Baba niyatsi, vimuloli, vyene viluka vutswa. Rivaa lyali lidinyu…

Mtafiti: Ku wamenya na babovo wong'ine?

Nyanya 2: Hii indangu yinu yari yinzi na baba. Vandu vandi vatsa navutswa kare kare. Kari rwavatsa, vumbaka ihare ku kwinye. Umanyi inyinga yene yeyo, vandu vamhamba mirimi minenene bora utimuri mritu nu vurimu vwitsura zinzoka. Inzira indahi yarange kuhambitsa mullu. Gu nuwatumikira mullu, genyeka urimi mtaro kutanga, usame nyumba madzi kutanga. Mullu gwakunga tsinyamanyama kutsia Indangu ma nitsiduka havundu tsigota kabisa.

Mtafiti: Ku muriva ryrinyu yinu, mwagana ku na Vavo dave?

Nyanya 2: Hehehe! Vayayi Vavoo venya rigari kondekitsa. Ku varinda ninzitsa mu kidaho vamboritsa. Ku vatsa vanyingi nu tusababu tudi tudi navutswa ndavasura voosi. Kari ndavola ku baba, nyenyi kudekitsa ku Mmbo mba; yavo navandu vandamanyi miiima gyavo dave.

Mtafiti: Ku mwatumikira lomoloma ki?

Nyanya 2: Kutanga, vayoga vutswa Rovo ma nivamanya ndi yinzi manyi mba, nivatangaRuswahili. Madiku gene yago kari Ruswahili kwari kukiri kumanya vurahi mba.

Mtafiti: Rwu wamara masomo ga class 3, watsizagila?

Nyanya 2: Awaa. Maisha gari rugano madiku gene yago. Risoma ryange ryari rye ridari na kurimwanamukana, si kwasominywanga vurahi dave. Numanyi kosoma nu kuhandika, basi. Rwa ndatsa yinu, si kwari ku ne tsisukuru zyu komeda masomo ga intermediate mba. Ma kandi kwari vutswa na baba kwongine hango.

Mtafiti: Na wuwatura winu Vihiga, wayirana ku yo?

Nyanya 2: Hii. Kwatsiayo kogenda ku navutswa rigari mba. Yinzi mwene ndayirana ku yo hari kanyingi lakini kare ku ho. Ndatsia kuyavira vamwavo vange vasura kutsa yinu. Umanyi yinzi mwene ndamenya hano na baba ndatsia Evorogori ndakavahira.Ndahira vana vange vamanye wanga mama na guga wavo. Ku kandi baadaye, vandu vandamanya vakutsa vanyingi. Ku vaveye ho vamanyi mba. Ninziyi kuvagendela vaganaganyia nyenya mrimi. Umanyi kandi ndakera, kugenda hatambi haindegela.

Mtafiti: Na Visukuru wavahira ku yo? Noho vatsya yo na vivuri?

Nyanya 2: Oh! Awaa. Kari vamanyi yeyo ni hayi mba. Vahulatsa wanga guku ni Vihiga navutswa vamanyi yo mba. Kari umanyi visukuru yava valla vaveye na vana na vamanyi witu witu mba.

Mtafiti: Ndora yinu vandu vamoroma Rovo, kari yivi omoroma?

Nyanya 2: mmmmmm kutura inziza hano, ndayanzaku Rovoo mba. Mwoyo gwange gwasura kari kwiga Llimi yirwo. Kuduka nunu ndi, manyi Rovo mba. Valla madiku gitu viiga, yinzi nisura nimbora mbeye no romoroma rwange. Yicho kandi chagira nisura kuvahira kuvo. Mkana natsiyi kodeka ku musatsa na sivamoroma L'limi l'lara dave, mukana amanya yiga L'limi rwu musatsa. Ku uma onyora yenya avugulwi kuri mundu wa hango, anyara kukora vindu kuri vandu va hango hene yaho.

Mtafiti: Ku wavahira ndi?

Nyanya 2: Yaduka inyinga, vakana kuva vanyingi kuvita vayayi. Vakoretera vasatsa kutura evorogori, vamenye nu kunyi hano. Vandi vatamwa kurinda, vatsia ku Vavo. Valla kari vatsia ku Vakurya na kari vingira Tanzania. Navutswa vatsya Ivukurya vari nu vudinyu mno kigira vagana ne miima gyu kuhuga gyo kokeva. Nuwasura kokevwa, vakukubaga ne tsimbanga kari valla paga vitwaa. Vivuri valla kuduka nunu ndi, vakiri korora ku vana vavo mba. Valla vakutsa kare.

Mtafiti: Ndora Llogori romoromwa hano sana. Kuri sya orora kutura mihiga gyu watsira hano, kindiki keromba Llogori rudinyiritswa?

Nyanya 2: Kunyi kogotitsa Llimi lwitu mba. Kandi rwa kwatsa, kwiyahura ku Vavo. Kunyi kwamoroma Llogori, navo Roco. Madiku gene yago, ndatsa ninyora vatangiza isukuru ya varogori lakini si gari na intermediate mba. Niviti vurahi class 3, utsya western kosomerayo. Ku vigitsi vatura yengo vatsa ne vitabu, na vigitsanga vana yinu. Ku yinzi si ndenya kuvahura ku Mmbo kigira ndari ndeke Llogori morome Rovo.

Mtafiti: Na hee, mwakubana ku na Vavo?

Nyanya 2: Hii kwakubana navo kari vakukunga mu mirimi ne tsinyumba zyavo. Vavo vingira mu. Sasa, koveye ku ni kindu Vavo vakolwa paga vatya sana kigira valla vakuza.Kutura madiku gene yago, Vavo vatya Varogori.

Mtafiti: Vana vinyu hano vamoroma llimi ki?

Nyanya 2: Yinu Vamoroma Llogori, Ruswahili no Rovo. Vatsuganyia tsyosi. Navutswa garondekana kandi. Unyara kutsya hando hala, onyore vamoroma Llogori, handi Ruswahili no Rovo. Visukuru hano vamoroma Llogori kandi Rovo. Vana vitu vatsiyi kukina hango hu Mmbo, vamoroma Rovo, nivatsiyi wu Mrogori, vatumikira Llogori. Ku garondekana wavatsitsa kukina. Yinzi si manyanzila vana komoromela Rovo mba kigira vaveye nu rwavo. Manyanza dave dave.

Mtafiti: Noveye na visukuru na visukururwe, utumikira romoroma ki?

Nyanya 2: Nimbeye na visukuru hango hano, komoroma Llogori. Kari vakutsutsu yava. Umanyi nunaritsi vana koyoga, vayoga vutswa. Nivatsi wange yinu vamanya vitswa ndi, guku amanyi Rovo noho Ruswahiri dave, ku nivatsi, Komoroma Llogori. Yinzi ndasoma hatambi mba na kandi simanyi Rovo mba.

Mtafiti: Na orora ndi Llogori rwa Migori yinu madiku ga mgamba? Vana vamureka yava vatsa vadinyiritsi Llogori?

Nyanya 2: (Vulu hake) aaaaaaahhh! Vana vitu vononya Llogori lwitu sana. Madiku gatsa yaga,ndora kwatsa kove nu vudinyu vwu kudinyirirsa Llogori. Vana vitu venyekana kwiga nu kutumikira lomoloma lwavo havogono hu Rovo. Madiku gano, vana vange vandi vamoroma vutswa mu mugitsigwa Yise wavo. Vamoroma na vakari vavo.Vavoraku soni noho kutya mba. koveye na Varogori vala vamenyi Ombo wamoromaza Rovo. Kari vaveye yengo na Varagori vavo. Kindu kerombatsa umanya hano na hango hu Mrogori ni ryumbaka ryi tsinyumba tsyavo; kigira zifwanana na tsya Vavo dave. Nuwingiraho ma omorome Llogori, varakujiba mu Llogori. Kindu yiki kimakisalitsa sana korora vana vitu vareka Llogori kigira yo Rovo.

Mtafiti: Na mmbavola ku vamorome Llogori?

Nyanya 2: Kwahonga kuvavola. Kuvahomba varonde miima gyitu kutura kare navutswa venyi mba. Kunyi nikutsa hano, kware ne miima gyetu na si kwadzugana na vandi da.Vaana va

## KIAMBATISHO F

## MWONGOZO WA KUNDI LENGWA NA VIJANA WANAOZUNGUMZA KIMARAGOLI

1. Je, mnaongea lugha gani sana?

2. Je,unafikiria Kimaragoli chenu mnachoongea sasa ni kama cha zamani cha miaka ya 1940? Kama si sawa, je kimebadilika kwa namna gani?

3. Waluo wanachukuliaje Kimaragoli?

4. Mnajivunia Kimaragoli kama lugha yenu?

5. Kitu gani kinafanya Kimaragoli kuzungumzwa hapa Migori?

6. Mkiwa nyumbani mnapenda kuongea lugha gani? Ukicheza? Kanisani?

7. Unapenda kuongea gani sana kati ya Kimaragoli na Kiluo?

8. Je, wewe hujikuta umeingizia maneno ya Kiluo unapoongea? Mnayaingiza mkiwa wapi na wapi?

9. Mlijifunza wapi Kimaragoli?

10. Kama umeoa au ukioa, itakuwa lazima watoto wako waongee Kimaragoli?

## KIAMBATISHO G

Matokeo Ya Mjadala Na Vijana Wanaozungumza Kimaragoli; Mjadala Na Vijana Wanaozungumza Kimaragoli Yaliyofanyika Siku Ya Jumapili, Oktoba 22 Kuanzia Saa 11.00-11.45 Jioni Maeneo Ya Stella

Mahiojiano yaliyofanywa na Mtafiti Msaidizi (MS) na vijana watatu wanaozungumza Kimaragoli. Uteuzi wake ulifanywa kwa njia ya kinasibu na ilihusisha kijana anayefanya kazi na Acre Fund na pia mshiriki wa Kanisa la Friends; Kijana anayefanya kazi ya kuendesha bodaboda na binti mmoja analiyemaliza shule ya upili. Mtafiti ametumia misimbo K1, K2 na K3 kuficha usiri wa wahojiwa hawa.

MS: Mmoroma l'limi ki?
K1: Yinzi Moroma Llogori.
K2: Kari yinzi
K3: Llogori
MS: Kigira ki?
K2: Ni romoroma rwange rwa mbula vurahi. K1: Ni romoroma rwakivura.
K3: No romoroma rumanyia ndi yinzi ni Mmrogori. Ama?
MS: Yivi yo wenyekana ovore.
K3: Haas
MS: Llogori rwa mmoroma sai, ni same na rwari rwa kare mihiga gya 1940?
K1: Hahahah girigari, dave.
K2: Girigari ni kuri cha kare dave keveymu na mang'ana ge Kiluo.
MS: Mnyara kotova ku mang'ana gene yago?
K3: Nyoyo…Kidishi
K2: Kidish ni rusungu?
K3: Umanye shida Llogori roveye na mang'ana madinyu mala kari kumanyi mba (wakicheka)
MS: Koveye na mang'na zaidi?
K3: Yinzi fwana nzirake hasi ku nzizuritsi.
MS: Vavoo vavugulandi Llogori?
K1: Mmmm vayanzila rigari mba lakini garondekana na tsisehemu. hawapendi sana lakini inategemea mahali. Vakoveye navo hano, vidinyia kari komoroma lakini vandi kari venyi mba.
K2: Lakini yinzi ndora vakiyanza. Havundu hosi hosi hutsia, unyora Vavoo vamoromaku Llogori.
K3: Girigari, atleast hosi hutsitsa, onyora ku mmbo amoroma Llogori. Varusura ni kidogo sana.
MS: Na mwihula komoroma Llogori?
K1: Kandi sana
K2: Hii
MS: Voraku zaidi
K3: Nzihula Kigira isa ndara nimoroima na vasakuru vatamanyi Kiswahili dave anoho rusungu. Umanyi koveye na vasakuru va kare vatamanyi kosoma nu kuhandika mu ruswahili noho rusungu. Ku komoroma navo Llogori.
K1: Nomoroma navo Llogori ku vama vamanya kuhula
K2: Yinzi nzihula kigira nu romora rwange. Nduyanza sana. Na kari ni vasakuru vong'ine dave, kari vivuri na vikoo vala vamanya Llogori tsa. Ku ni vodoto komoroma Llogori.
MS: Kindiki keromba Llogori kutsitsagila yinu?

K1: Girigari hee, eredio ekonya kusambaza Llogori. Lakini yinu iduka mba. Nutsia engereka yira, vahulitsa tsa.
K2: eredio yaromba Llogori kusambazika sana .
MS: Na yive K3?
K3: Mikutano gya utamaduni kuri kekevo chakavita, mikutano gye ibaraza kandi. Ma kandi koveye ku nu mkutano gwa vasukuru vatsitsamu ingereka Bware. Wa Baba Cynthia ma atsitsa.
K1: Kari mikutano gya machifu.
K2: Machifu madiku gano vatumirika ruswahili sana. Ndatsyaumu. Fwana madiku gakavitayago.
K3: Yinzi, mware wa munane kwatsiyi Kakamega mu rivugana rya Friends. Ryavugura Warogori kutura mu tsimbega tsimbega. Kari Main Pastor yamoroma Llogori.
K1: Hata nyanya yangu wa Jeshi la Wokovu walikuwa na wageni kutoka Mbale. Ingawa mimi sijawahi kuenda kule na sijui ni wapi lakini inasaidia kwa sababu watu wanongea kwa Kimaragoli kutoka maeneo mbalimbali.
K3: Kari kusara mwivugana
MS: Na kwigitsa Llogori?
K2: Hii navutswa si sana kigira vana viruka vatsya kukina.
MS: Yivi uvigitsa dave?
K2: Yinzi manzigitsa Cynthia lakini niyatsi kwinze, amoroma ruswahili. Ngotwa yigira hai ruswahili
K1: Yinzi mandora babitu niyigitsa vana vitu Llogori. Vanga Joy baba avitsa.
MS: Koveye ku ni tsinzira tsindi?
K2: Eeeee Disemba, kovetsa na mashindano ga marago mu Llogori. Sasa garomba vandu vidinya mu Llogori.
MS: Ni mmbeye yengo, myanzila komoroma l'limi ki? Na nu mkina? Mwivugana?
K2: Gatemea. Yengo komoroma Llogori. Koveye mwivugana, komoroma Llogori nu Ruswahiri.Yinzi ningina mpira, paga njanganye na Rovoo.
MS: Rivugana ryinyu riveye na Vavoo?
K1: Kuri kunyi, koveye na Pastor Ochieng atura indangu yira. Kandi koveye mu na Vamasaai kiasi. Ochieng amoroma Llogori.
K2: Kunyi koveye nu Mluo arangwa Doreen Achieng. Amoromaa Llogori vurahi sana so Friends church yitu komoromaa Llogori sana.
MS: Na nimbeye yengo na vivuri? Vaguga na vandi?
K2: Vivuri garondekana. Uranyora kari mama Mluo, vamoromaa Llogori no Rovoo. Voosi vaveye Varogori, Llogori tsa.
MS: Na myanzila komoroma l'liha?
K3: Kunyi rwakwatsia Kakamega, kwamoroma Llogori lakini sasa kwavikamu Rovoo nikwenya vavuri kumanya chakovora. Manyingi kwamoroma Llogori.
MS: Mwigira hayi Llogori?
K1: Yengo na vivuri.
K2: kari yinzi yengo
K3: Yengo
MS: Mnyara kwimba, kusara na kokora mang'ana gandi mu Llogori?
K2: Nyara yinzi.
K3: Kari yinzi. Rivugana ryanzigitsa.
MS: Ku vasakuru na vijana, variha vamoroma kuu Llogori sana kandi vurahi?
K2: Vasakuru.
MS; Kigira ki?
K3: Kunyi vijana, varina vitu vanyingi ni Valuo. Komora kwingiritsa mu Rovo.

K2: Halafu umanye kuri kunyi vandu va bodaboda… Umanyi wenya unyare mmbo, wigi romora rwirwe. Ndio aravugila umgingi ku kibigibigi chichyo.

K1 : Kari vutswa, yenya akutume, arakuranga mu Rovo. So ni lazima wigi ku onyore churya.Ni rahisi onyore ku vasakuru vakora ndyo mba.

K2: Vasakuru kigira vamenyi mihiga minyingi.

K1: Kunyi kuchanganya Llogori no Rovoo.

MS; Kuri kijana, kiwango chichyo chyu Llogori keveye ndi?

K1: mmmmm, waaaaaa…umanyi kirahi dave.

K3: Kwa mfano, rwa kwari Evorogori madiku ga rivugana, kanisa, kwavoraa, "sasa hii enyoyo haikuiva." Yavo varamoromaa mang'ana gu Llogori tsa. Nutsia Western, uramnaya kumbe vandu vamoromaa Llogori.

MS: Uma wenyoraku wakwingiritsa mang'ana gu Rovo nomoroma Llogori?

K1: Hii

K2: Hii

MS: Mwingiritsa mbeye hayi?

K3: Kari yengo, msogoni, ku nzira. Yaani witsukana vutswa wakwingiritsa mu.

K2: Kwanza msogoni ndio mbaya sana. Umoromatsa korondekana na vandu wu wagana navo.Kari varogori venee vamoroma Rovo.

K1: Noveye ku inzira, mundu nakoteva, "Omera yuoni di Kanye" yaani bwana hii njia inaendaje? Paga omorome.

K3: Umanyi kari koveye na varina vitu. Tunachanganya tu. Witsuritsa koveye mu Ryaruka Makuyu? Llogori rwatumika sana na chifu yakola translation mu rovo ku vandu vatahula Llogori mba. Kari havundu kuri ha mariga, uranyora kutumikira tsyosi kokora translation.

MS: Na kugasi nu mmurimi?

K3: Ah, ninyoye kagasi ku mu Acre Fund, kutumikira tsyosi kwagani na Vavoo, komoroma Rovo, kwagani nu Murogori, komoroma Llogori.

K1: Yinsi ninginji vandu ku boda boda, namix zote. Manyatsa uyu ni Mluo, uyu ni Mmrogori.

K2: Nimbeye mu mikinu, kuri ningina mpira, paga morome ku Rovo isaa yindi. Paga mboleku defender, "Omera, momiting'o, nanikichung'o mpira"

MS: Koveye na havundu handi hamtsuganya?

K2: Kari msivitari vachanganya.

K1: Kari nutsya mu tsiofisi zyetu, nutamanyi Rovo, paga vakusumbure sana. Sasa numanyi omoromatsa Rovo kandi.

MS: Niva wareta noho watsa orete, vana vovo vatsa vamorome Llogori?

K2: Hii lazima.

K1: Yinzi wange paga amoromee.

K3: Yaho lazima.

MS: Haya, sande sana, ndora isaa yakutsia rigari. Korekere hene yaho.

# KIAMBATISHO H

## MWONGOZO WA MJADALA NA WAZAWA WA KILUO WANAOZUNGUMZA KIMARAGOLI

**1.** Mlijifundishia wapi Kimaragoli?

**2.** Kwa nini mliamua kujifunza?

**3.** Je, mnachukuliaje lugha hii?

**4.** Je, huwa mnaitumia sana au nadra?

**5.** Je, kuna maneno ambayo mliunda kufafanua Wamaragoli na lugha yao?

**6.** Kwa maoni yenu, ni sababu gani ambazo zimefanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa hapa Uriri kwa miaka mingi?

**7.** Wamaragoli wanawachukuliaje nyinyi Waluo? Kuna heshima kutoka kwao hadi kwenu?

## KIAMBATISHO I

## MATOKEO YA MJADALA WA KUNDI LENGWA

Mjadala wa Kikundi lengwa cha wazawa wa Kiluo wanaozungumza Kimaragoli uliofanyika Stella, nyumbani kwa Mama Mercy siku ya Jumamosi kuanzia saa 4-4.30 asubuhi. Jumla ya washiriki ni 10: sita wa kike na wanne wa kiume. Wawili wa kike wanatoka Thim Jope, mmoja anatoka Ombo, wawili wanatoka Bware, mmoja anatoka Emuhanda na mmoja anatoka Kajulu II. Kwa upande wa wanaume, mmoja anatoka Arambe, mmoja ni wa eneo la Lwala, mmoja ni wa kutoka Kajulu I na mwingine Kajulu II. Baada ya kunywa chai, mtafiti alianzisha mazungumzo.

**Mtafiti:** Mmmm...Hamjambo wote. Mimi ni Sangili Kenyani Nixon, nafanya utafiti kuhusu udumishaji wa Kimaragoli katika eneo la Migori, na hasa Eneobunge la Uriri. Miminatoka maeneo ya Magharibi mwa Kenya na ninazungumza Kimaragoli kama lugha yangu ya kwanza. Ninaamini kwamba mchango wenu kuhusu maswali nitakayouliza utanisaidia kutimiza lengo hili. Kwanza nawashukuru kujitolea kuchukua muda mchache kutoka kwa shughuli zenu mbalimbali kuja kwa Mama Mercy, ambaye wengi mnasema mmewahi kufudisha naye katika shule mbalimbali.

**Mama A:** Na hata wanne hapa tuko chama Kimoja cha kina mama…

**Mtafiti:** Hahah. Asante sana kwa hilo. Hivyo naamini eh nyinyi ni marafiki kwa njia moja au nyingine. Sasa naomba kujua mlijifunzia wapi Kimaragoli na kwa nini?

**Mama Mercy:** Mimi nimejifunza Kimaragoli wakati nimeolewa hapa kwa boma langu. Bwanangu wakati huo alikuwa kijana tumejuana tukiwa shule moja ya TTC kusomea Ualimu. Tulipendana sana. Mimi kwetu ni upande wa Rusinga, Brian Weke, si unamjua? Ni mtu mkubwa sana katika siasa za Nairobi ni kama cousin wangu. Sasa kwetu tulikuwa tunaongea Kiluo tu. Nilipoolewa hapa, ilikuwa karibu miaka ya 1980, nilikaa kwanza na bwanangu kisha akasema tuhame turudi nyumbani. Eh, tukifika huku, nilijikuta katika hali ngumu kwa sababu wazazi wake walikuwa wanaongea Kimaragoli na Kiswahili kidogo. Sasa nilianza kujifunza tu polepole. Ukimuuliza atakwambia nilisumbuka kwanza lakini baadaye nikawa naendelea vizuri. Sasa hivi huwezi kujua kama mimi ni Mluo kwa sababu naongea Kimaragoli hata kushinda Wamaragoli wengine huku wale nimekutana nao.

**Mtafiti:** Nawe mama B?

**Mama B:** Mimi kusema kweli sijui Kimaragoli kama Mama Mercy lakini naweza kusikia maneno yote ya Kimaragoli. Ahhhhh Kuongea ndio shida yangu tu. Lakini siku nyingi huwa najikaza mpaka nizungumze. Sasa mimi nimeishi mjini Migori sana na bwanangu. Ni Mmaragoli pia. Alinifunza Kimaragoli lakini sikuwa na hamu sana. Vile nimekuja nyimbani baada ya kustaafu, nimeanza kuongeza maneno mawili au matatu lakini sijui vizuri

**Mtafiti:** Nawe Mama C?

**Mama C:** Mimi nasikia kidogo tu lakini siwezi kuongea. Nimeishi Nairobi muda mrefu nikifanya kazi. Sasa shida bwanangu ni Mkisii.(watu wanacheka)

**Mama Mercy:** Mama C si ukienda ulikuwa unajua Kimaragoli kidogo. Nakumbuka siku ulikuja kuniambia umepata kazi Nairobi.

**Mama C:** Sasa sikutumia Kimaragoli. Kama ni wewe utakumbuka jaber? (Vicheko)

**Bwana A:** Wamama wameongea sana. Sisi pia tuongee. Mimi ni mwalimu nafunza shule ya msingi huko Awendo lakini kwangu ni hapo juu ukipita fishpond. Kimaragoli nimejua nikiwa tangu mdogo sana. Tulisoma kwa shule ya Wamaragoli hizo siku,

Emuhanda Primary, mimi na huyu rafiki yangu Kijana A. Nilikuwa mbele yake darasa mbili. Sasa sisi tulicheza na watoto wa Kimaragoli sana. Unajua ukiwa mtoto, unajikuta unacheza halafu unaongea. Sijui huwa inafanyikaje watoto wanashika maneno haraka. Sasa tukirudi nyumbani hata tungesema tumejua kuongea lugha ya kina John shule. Sasa wazazi hawakuwa na shida hata kidogo.

**Baba M:** Unajua ndugu yangu, sisi wengi hapa wanaume tumekua na hawa Wamaragoli wetu.Tangu tukiwa watoto. Shule moja. Kucheza mahali pamoja. Tumekula mahali pamoja na tumefanya mambo mengi sana. Sasa Kimaragoli na Kiluo ndizo zilikuwa lugha zetu sote. Tunacheza na kuongeleshana lugha zote kwa wakati mmoja.

**Kijana A:** Nakubaliana na Baba M kabisa. Tumekuwa na marafiki wengi sana wa Kimaragoli shuleni, michezoni, kila mahali. Mpaka sasa bado ni marafiki ingawa wengine walienda mijini after kumaliza masomo. Lakini mimi naongea Kimaragoli vizuri kabisa.

**Mama C**: Na huyu mama hajasema. Pia huyu.

**Mtafiti**: Wataongea tu.

**Mama F**: Mimi nimeishi hapa Kakrao siku zangu tangu kuzaliwa. Ilikuwa bahati nzuri nikawa kanisa moja na Mama Mercy. Sasa nimekuwa nikiongea Kimaragoli kuanzia nikiwa mtoto tu.

**Bwana L**: Watu wengi hapa tunaongea Kimaragoli kwa sababu tumeishi na Wamaragoli. Mimi nimezaliwa Lwala na huko ndiko nimeishi siku zote isipokuwa wakati nilienda shule ya Sekondari.

**Mtafiti**: Nawe Mama T?

**Mama T**: Haaaaiyaa. Mama Mercy ni rafiki yangu na tulikutana sote huku wakati wa ndoa. Kwa kweli ni jirani yangu upande huu mlitokea na Ajema. Sasa mimi na bwanangu tunaongea Kimaragoli kwa sababu tumejifunza kutoka kwa kina Mama Mercy na watoto wake hawa wakubwa kina Mark na wengine. Bwanangu hakunifunza mimi. Halafu tukiwa na Mama Mercy, Mama F na Mama A kwa chama kimoja, tulikua tunahimizana sana. Kusema ukweli, mama mwanamke mgeni katika boma, unakuwana uoga kidogo ukisikia watu wanaongea lugha nyingine na wewe hujui. Unaweza kufikiri wanakusengenya au wanakusema kwa mabaya. Pengine hukupika vizuri (wote wanacheka).Sasa tulijihimiza kujua Kimaragoli kutoka kwa watu wa boma au majirani. Wakati mwingine, kama Mama Mercy amejifunza neno jipya, tukikutana kwa chama, tunafunzana tu wenyewe kwa wenyewe. Hatukujua utamkaji vizuri lakini kujua maneno yote ndio tujue kama wanatusengenya au wanatusifu. Sasa uoga kulinda nyumba zetu ulitufanya kujua Kimaragoli.

**Mtafiti:** Asante sana. Kweli mna mambo ya kufurahisha sana. Sasa, mnachukuliaje lugha hii?

**Mama Mercy**: Kuchukulia aje yaani?

**Mtafiti:** Uuh, yaani, mnaipenda, mnaidharau? Ni nzuri au ni mbaya? Ni ngumu au rahisi?

**Mama Mercy:** Oh! Kimaragoli si rahisi lakini pia si kigumu. Shida tu ni vile unafaa kuzungumza. Kuweka weka maneno mengi kwa pamoja. Si kama Kiluo.

**Bwana L:** Mimi nitasema Kimaragoli tunakipenda. Eeeh pia tunakiheshimu kwa sababu si chawatu wabaya. Ni wangwana sana.

**Kijana A:** Mimi kwa upande wangu nitasema Kimaragoli kujifunza kama mtoto ni rahisi sana kwa sababu unaongea na watoto wengine. lakini kuongea kama mtu mkubwa (mzima) ni vigumu sana.

**Mama F**: Kimaragoli ni moja ya lugha rahisi. Ni kama tu Kikisii. Halafu marafiki wangu wengi ni watu wazuri sana.

**Mama C:** Mimi siwezi kusema ni rahisi kwa sababu siongei lakini nasikia. Lakini kama ningeishi huku siku zote ningekuwa naongea sasa. Ni lugha ngumu mtu kujifunza sasa hivi kama mzee.

**Bwana M:** Mama C unajua ni kitu rahisi sana kujua Kimaragoli. Unakaa karibu nao tu unasikia.

**Mama C:** Sasa hivi mimi ni mzee jameni Japuonj.

**Bwana A**: Kweli kujifunza kama mtoto, ni rahisi. Lakini kwa mtu mkubwa ni vigumu. Akili inamambo mengi ya kufikiria. Lakini mimi nitasema Kimaragoli ni lugha ya heshima. Tena watu wake hatujapigana nao hapa kwetu.

**Mtafiti:** Lakini nasikia kulikuwa na vita hata Wamaragoli wakafukuzwa…

**Bwana A:** Ndio. 2002. Tena 2013 lakini ukiangalia vizuri, shida ilikuwa ya siasa tu. Mambo ya lugha hayakuwa ndani.

**Mtafiti:** Sawa, asanteni sana kwa majibu. Eh je, mnatumia Kimaragoli sana au si sana?

**Bwana A:** Kimaragoli kinategemea. Kama nyumbani kwangu, bibi yangu ni Mluo, mimi pia na watoto. Sasa tunaongea na marafiki kama tumeenda kunywa busaa. (vicheko kwa wote)

**Kijana A:** Kimaragoli hatutumii sana kwa sababu watu wengi tuliosoma nao sasa wako mbali.Pengine kama tu ni salamu kidogo na maongezi kidogo tukikutana au kwa simu kama tunaongea nao. Watoto wa sasa kama wamekuja nyumbani wanisalimu kwa Kimaragoli. Lakini wakija kwangu wanajua mimi ni Mluo, sasa wanaongea tu Kiluo. Na ni watoto wa Kimaragoli.

**Mama Mercy:** Mimi natumia siku zote. Bwanangu ni Mmragoli. Watoto wangu wanaongea Kimaragoli na Kiluo. Lakini siku zingine tunaongea Kiluo tu hapa kwa nyumba Nikienda kwa mama, hiyo nyumba unaona hapo chini, mama anaongea Kimaragoli na hajui Kiluo kabisa. Sasa ni lazima niongee naye Kimaragoli. Hata si Kiswahili.

**Mama C:** Mimi siongei Kimaragoli

**Mama F:** Mimi bado naongea Kimaragoli kila siku. Marafiki wangu wengi wa kanisa, wa kazi, na majirani wote Kakrao wanaongea Kimaragoli tu. Sasa nakitumia kila mahali.

**Baba M:** Mimi nakitumia pia lakini mahali maalumu. Kwangu sikitumiii sana pengine kama rafiki wangu wa kitambo amekuja kuniona tuanze kuongea mambo ya kitambo. Kama tunapiga siasa na Wamaragoli kama sasa hivi mambo ya NASA, tunaongea Kimaragoli, Kiluo, Kiingereza na Kiswahili. Hapo hatujifungi ati oh Kimaragoli au Kiluo.

**Mama T:** Mimi nakitumia karibu kila siku ingawa si kila wakati. Lakini kitambo tulikiongea sana. Tukiwa kanisani, tunasalimiana na Wamaragoli kwa Kimaragoli na pia kwa Kiluo.

**Bwana L:** Mimi naongea Kimaragoli siku zote. Lwala ni kama kitovu cha Wamaragoli. Kwanza sisi Waluo hapo tuko wachache sana. Sasa ni kama lugha yangu kwa sababu najikuta naongea hata kushinda Kiluo siku zingine. Majirani wote ni Wamaragoli.

**Mtafiti:** Haya hapo sawa kabisa. Sasa nataka kuuliza, kuna maneno ambayo nyinyi huwa mnatumia Kuita Wamaragoli. Yanaweza kuwa maneno mazuri au mabaya.

**Mama Mercy:** Sijasikia neno lolote baya kwa Wamaragoli mimi tangu niolewe hapa.

**Mama T:** Hata mimi.

**Bwana L**: Pengine utueleze zaidi naniii Sangili.

**Mtafiti:** Yaani kuna jamii ambazo huita zingine majina ya kuonyesha ukosefu wa heshima au wakati mwingine, yanaweza kuwa majina ya sifa.

**Bwana L**: Hapo ni ngumu sijasikia neno baya.

**Mama C:** Mimi nimeishi mbali kwa muda mrefu sasa sijui kabisa.

**Kijana A:** Kuna watu huita Jomwa.

**Bwana L:** Hilo si neno baya. Wanataka neno baya. Ni kama unasema JaMaragoli. Jamaragoli si neno baya.

**Mtafiti:** Kwa hivyo mnasema kwamba hakuna neno linaloonyesha madharau, hasira au chuki kwa Wamaragoli?

**Bwana L**: Lingekuwa ungejua kwa sababu hata tunaishi nao kwa Amani na kupendana kwa muda mrefu. Hatujapigana kwa sababu ya chuki ya ndani kwa ndani. Siasa ndio nadhai kilikuwa kitu kilitufanya tukapigana. Eeh nadhani pia mashamba.

**Mtafiti:** Asanteni sana. Sasa tuendelee. Kwa maoni yenu, ni sababu gani ambazo zimefanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa hapa Migori kwa miaka mingi?

**Mama Mercy:** Wamaragoli ni watu wanapenda utamaduni wao. Hata wewe mwenyewe ulijionea wakati Mercy na vijana walikupeleka huko Mukuyu kujionea. Na unajua wanafanya hivi kila mwaka bila kuchoka.

**Baba M**: Kweli kabisa, Naunga mkono mama Mercy. Wamaragoli wanapenda utamaduni na mila zao. Wao wanatahiri huku, wanasherehekea na hata ukienda matanga yao, wanaongea Kimaragoli tu.

**Mama F:** Sisi tunaongea Kimaragoli mahali tofautitofauti. Wao pia wanaongea nyumbani,wakiwa kazi za mashambani, utasikia vijana wa boda boda hapo Stella wanaongea. Sasa kitu kimewasaidia naona ni kuongea sana. Halafu sisi tunawasaidia wakati tunaongea nao. Nao pia wanasaidia sisi Waluo kwa sababu tunaongea Kiluo nao siku zote. Sasa tuna heshima pande zote huku tena huku.

**Mama C:** Mimi naona siku walikuwa wanafundishwa shuleni. Unajua hizo siku watu wa kitambo sasa ni wazee walikuwa wanaongea Kimaragoli hata shuleni.

**Kijana A:** Sisi tulicheza shuleni na Wamaragoli wakati huo na sasa tunaweza kuongea Kimaragoli tu. Nafikiri wakati wa kuenda nyumbani, tunatembea tukicheza kwa Kimaragoli na Kiluo. Lakini naona kitu kimesaidia sana ni mila.

**Mtafiti:** Naambiwa kwamba Wamaragoli walipokuja huku walikubaliana na Waluo kwamba hakuna kuoana kati ya Mluo na Mmaragoli. Je, mshasikia maneno kama hayo? Je, inaweza kuwa ilisaidia Kimaragoli kuendelea?

**MamaA**: Miaka gani hiyo?

**Mtafiti:** Miaka ya 1939 ama 1940. Yaani wakati Wamaragoli waliingia hapa Migori kutoka Kisii.

**Mama A**: Sitajua historia hiyo sasa.

**Mama Mercy**: Nyanyake Mercy aliwahi kutuambia mambo kama hayo lakini sasa siwezi kujua kama yalikuwa kweli. Lakini yaweza kuwa kweli kwa sababu yeye mwenyewe alisema alitongozwa na wanaume wa Kiluo lakini hakukubali yeyote. Aliambiwa na babake kwamba avumilie wataenda kumtafutia bwana huko Umaragoli.

**Bwana L:** Mimi sijasikia hiyo historia. Wazee wetu ubaya hawakutusimulia chochote cha Wamaragoli. Lakini naamini Wamaragoli wenyewe walikuwa na historia yao.

**Mtafiti:** Je, kuna mtu anajua historia hiyo? (Hakuna aliyekubali anajua)

**Mtafiti:** Sawa, naomba tuende kwa swali jingine. Wamaragoli wanawachukuliaje nyinyi Waluo? Kuna heshima kutoka kwao hadi kwenu?

**Mama A:** Tangu kitambo hakujakuwa na shida kati yetu na Wamaragoli. Kila mtu anatunza heshima yake pengine kama kuna kosa hapa na pale kwa watu binafsi. Lakini ni watu hawana mambo mengi.

**Kijana A**: Mimi kwa upande wangu, tumesoma na kukaa na Wamaragoli kwa muda mrefu tangu nikiwa mtoto. Tumecheza nao pia hivyo hakujakuwa na shida kati yetu na wao. Wanatuheshimu na tunawaheshimu. Tukiwa watoto ndio tulikuwa tunapigana. Ilikuwa ya upimana nguvu tu kuhusu wasichana lakini. (Watu wote wanacheka)

**Mama Mercy:** Mimi tangu niingie kwa ndoa na baba Mercy, hatujawahi kugombana. Hata tulipokubaliana kurudi shule kuongeza masomo, tulikubaliana. Mimi nilienda kwanza nikamwachia watoto. Aliwalea tu. Na yeye aliporudi shuleni baadaye, nikabaki na watoto. Kila mtu alielewa umuhimu wa masomo kwa maisha yake na hata ikafika mahali yeye akaamua hataendelea na masomo ili karo ipatikane ya kusomesha watoto waliokuwa wameanza shule wakati huo. Sasa yeye ni mtu muungwana sana lakini sasa amestaafu kama mwalimu.

**Mtafiti**: Sawasawa kabisa. Je, hali yako je vipi Bwana L?

**Bwana L**: Ahh heshima iko pande zote mbili. Unajua kama haingekuwa tuna heshima kati ya kabila hizi mbili, tungekuwa tunagombana sana siku zote. Lakini kuweko kwa heshima kati yetu na hao ni kitu kilianza kitambo sana. Tangu utotoni.

**Mama C:** Mimi naona kwamba hapa Migori kuna makabila mengi. Kuna Wakuria, Wakisii, Wakamba, Wakikuyu, Wasomali huko Suna. Sasa unajua sehemu hii si kama zingine. Umewahi kusikia kumekuwa na vita? Au watu wanazozana mpaka wanapigana na kuuana? Kitu najaribu kusema ni kuwa huku kuwepo kwa lugha nyingi kumefanya watu kuwa na heshima. Hivyo ndivyo Kenya tunastahili kuishi. Mambo ya kupigana tuwache kabisa.

**Mama F**: Kweli kabisa.

**Mtafiti**: Mama F wewe unaona? Umewahi kusikia Mmragoli amekosana na Mluo?

**Mama F:** Kukosana ni kitu cha kawaida sana. Wazazi watakosana kwa sababu mtoto wao amefanya kosa au mambo ya ng'ombe kuenda kwa shamba la mwingine. Si mambo makubwa sana ya kikabila. Hapa Migori ukabila haujulikani sana.

**Bwana A:** Wamaragoli ni watu wangwana sana. Tangu tusome nao shule ya msingi, wengine urafiki uliendelea kwa muda mrefu mpaka walipokufa.

**Mama A:** Sisi kweli hapa Uriri tuna heshima kwa wengine na wengine wanatuheshimu.

**Mtafiti:** Ah asanteni sana wote. Nadhani ni hayo tu kwa sasa ikiwa nitakuwa na jambo zaidi, nitawajuza tena tukutane.

**Mama Mercy**: Asante pia kuja kutusalimia. Utakapofuzu utuite tukuvishe maua. Sasa wewe ni kama mtoto wetu hapa.

**Mtafiti**: Sawasawa mama.

Mtafiti alimaliza mjadala mwendo wa saa nne na dakika 37 na baada ya chakula, watu wakawa huru kuondoka.

# KIAMBATISHO J

## MWONGOZO WA UCHUNZAJI

### 1. Uzungumzaji wa Kimaragoli miongoni mwa makundi mbalimbali

Viwango vya uzungumzaji:

| **Eneo/Muktadha** | **Sana** | **Kidogo** | **Wanachanganya ndimi** | **Wanahamisha ndimi** |
|---|---|---|---|---|
| Kanisani | | | | |
| Michezo | | | | |
| Nyumbani | | | | |
| Sokoni/Madukani | | | | |
| Shambani | | | | |
| Sherehe/matanga | | | | |

## KIAMBATISHO K : HOJAJI YA WATOTO WA MIAKA 12-17

**SEHEMU YA KWANZA**

Lengo la maswali haya ni kukusanya habari kuhusu mielekeo ya Wamaragoli kuhusu kuendeleza lugha yao katika Kaunti ya Migori na hasa eneo la Uriri. Majibu yako yote yatawekwa siri. Tafadhali jibu maswali kwa uaminifu. Huu si mtihani, kwa hivyo kila jibu utakalotoa litakubaliwa.

**SEHEMU YA PILI**

Jinsia yako Kiume ☐ Kike ☐ Miaka ☐

**SEHEMU YA TATU**

1. Unaongea Kimaragoli au Kiluo au zote ? …………………….…………….
2. Ni lugha gani ambayo unaongea vizuri ? ………………………….…………………..
3. Kiluo kimeathiri matumizi ya Kimaragoli chako ? Ndio ☐ La ☐
4. Ni muhimu wewe kuongea Kimaragoli ? Ndio ☐ Hapana ☐
   (Eleza zaidi hapa chini)
   ……………………………………………………………………………..…
5. Je, unafikiria Kimaragoli mnachozungumza sasa hivi ni kama cha zamani wakati ambapo Wamaragoli walihamia hapa miaka ya 1940 ama wameingiza maneno ya Kiluo ? (Tick Moja tu)
   Ni kama cha zamani ☐
   Kiko na maneno ya Kiluo siku hizi ☐
   Kama kina maneno ya Kiluo, hebu yataje hapa chini
   ………………………………………………………………………………………
6. Je, Waluo wanachukuliaje lugha ya Kimaragoli ? (Weka sahihi kwa sanduku moja)
   Wanaipenda sana ☐ Wanaichukia ☐
   Wanaipenda ☐ Wanaichukia sana ☐
7. Kitu gani ambacho kinafanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa mpaka leo hapa Uriri? (Unaweza kuweka sahihi kwa sanduku zaidi ya moja)
   a. Redio ya *Vuka FM* na *Mulembe* ☐
   b. Mikutano ya Kitamaduni kama vile baraza nk ☐
   c. Kutembeleana na watu wa Vihiga ☐
   d. Kuabudu kanisani kwa Lullogoli ☐
   e. Wazee kufundisha vijana na watoto Lullogoli ☐
   f. Kuongea Lullogoli tukiwa nyumbani ☐
   g. Mikutano ya chama cha kina mama au wazee (Lisanga) ☐
   h. Kufanya sherehe za tohara na mila za Wamaragoli ☐
   i. Watoto wanafundishwa Lullogoli shuleni ☐
      Elezea njia zingine ambazo huwa mnatumia kuendeleza Kimaragoli…………………………………………………………………………
8. Wewe unajivunia kuongea Kimaragoli hapa Uriri? Ndio ☐ Hapana ☐
   Elezea jibu lako hapa chini
   ………………………………………………………………………………………
9. Unapenda kuongea sana lugha gani ukiwa :
   a. Nyumbani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
   b. Ukicheza Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
   c. Ukiwa kanisani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

d. Na marafiki Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

e. Sokoni/Madukani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

f. Shambani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

10. Unaongea lugha gani sana ukiwa na

a. Nyanya na Babu Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

b. Wazazi Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

c. Watu wa ukoo (wajomba/shangazi ; mashemeji)Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

d. Ndugu zako Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

e. Majirani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

f. Watoto wengine Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

11. Kati ya Kiluo na Kimaragoli, lugha gani unapenda kuongea sana ? Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Kwa nini ?
------------------------------------------------------------------------------------------------

12. Ulijifundishia wapi Kimaragoli ?
------------------------------------------------------------------------------------------------

13. Unaweza kuimba, kuomba, kuongea, kusimulia hadithi kwa Kimaragoli? ☐ Ndio ☐ La
Kama la, kwa nini ?
..............................................................................................................................

14. Kama mtoto ukiulizwa useme kiwango chako cha Kimaragoli, utajibu nini ? (Chagua moja)
Kizuri sana ☐ Kizuri ☐ Kizuri Kidogo ☐ Kibaya ☐

15. Je, kuna mambo ambayo wewe hupata shida kuelezea kwa Kimaragoli ? Ndio ☐ La ☐

Kama ni ndio, unaweza kutaja mambo hayo ?
..............................................................................................................................

16. Wewe huchanganya Kiluo na Kimaragoli wapi ? (unaweza kuweka alama kwa zaidi ya sanduku moja)

Nyumbani ☐
Sokoni ☐
Barabarani ☐
Na marafiki ☐
Shuleni ☐
Katika mikutano ☐
Shambani/kazini ☐
Michezoni ☐
Kanisani ☐

Taja mahali pengine ambapo wewe huchanganya Kimaragoli na Kiluo……………………………………………………………………………………………………

**SEHEMU YA NNE : MIELEKEO YA WATOTO WANAOSEMA LULLOGOLI**
**Nakubali Kabisa [NK], Nakubali [N], Sina Hakika [SH], Sikubali [S], Sikubali Kabisa [SK]**
**Muhimu**: Weka alama ya sahihi **moja tu** [ √ ] kwa kila kauli katika hojaji hii.

| Na. | Kauli | NK | N | SH | S | SK |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hakuna haja ya mimi Kuongea Kimaragoli hapa kwa Waluo. | | | | | |
| 2. | Najivunia kuongea Kimaragoli hata kama sisi tuko wachache Uriri. | | | | | |
| 3. | Naongea Kimaragoli ili kukidumisha. | | | | | |
| 4. | Mimi hufundishwa watoto wetu na marafiki Waluo Kimaragoli. | | | | | |
| 5. | Mimi na watoto wetu tunajua Kuongea Kimaragoli zaidi kushinda Kiluo. | | | | | |
| 6. | Tukiwa nyumbani, tunachanganya Kimaragoli na Kiluo. | | | | | |
| 7. | Kiluo kinatupatia heshima kubwa kuliko Kimaragoli. | | | | | |
| 8 | Watoto wetu hawajui Kimaragoli vizuri. | | | | | |
| 9 | Tukiwa nyumbani tunapenda kusikiliza idhaa za redio ya Kimaragoli ili kujifundisha, kujikumbusha na kuendeleza Kimaragoli. | | | | | |
| 10 | Tukiwa Kanisani, tunatumia Kimaragoli. | | | | | |
| 11 | Sisi huongea Kimaragoli kwa simu na watu wetu wa ukoo | | | | | |
| 12 | Wamaragoli tunaheshimiwa na kabila zingine hapa Uriri. | | | | | |
| 13 | Wamaragoli tunapenda kuheshimu lugha zingine hapa Uriri. | | | | | |
| 14 | Mimi kama mtoto sina muda wa kujifunza Kimaragoli. | | | | | |
| 15 | Kimaragoli kinafaa kuendelea kufundishwa na kurithishwa kwa watoto, wajukuu na vitukuu wetu ili kisipotee. | | | | | |
| 16 | Mimi huona aibu kuona watoto Waluo wanajua kuongea lugha yao na mimi sijui Kimaragoli. | | | | | |
| 17 | Mimi huongea vizuri kwa Kiluo kuliko kwa Kimaragoli. | | | | | |
| 18 | Nitahisi vibaya sana ikiwa sisi watoto tutawacha kuongea Kimaragoli kabisa na kuongea Kiluo. | | | | | |

**Asante kwa kutenga muda wako ili kuchangia majibu yako**

**KIAMBATISHO L : HOJAJI YA VIJANA KATI YA MIAKA 18-35**

**SEHEMU YA KWANZA**

Lengo la maswali haya ni kukusanya habari kuhusu mielekeo ya Wamaragoli kuhusu kuendeleza lugha yao katika Kaunti ya Migori, hasa Uriri. Majibu yako yote yatawekwa siri. Tafadhali jibu maswali kwa uaminifu. Huu si mtihani, kwa hivyo kila jibu utakalotoa litakubaliwa.

**SEHEMU YA PILI**

Jinsia yako Kiume ☐ Kike ☐ Miaka ☐

**SEHEMU YA TATU**

17. Unaongea Kimaragoli au Kiluo au zote ? …………………….…………….
18. Ni lugha gani ambayo unaongea vizuri ? ………………………………………..
19. Ulijifundishia wapi Kiluo ? Nyumbani ☐ Shuleni ☐ Kwa marafiki ☐
    Elezea mahali pengine ambapo ulijifundishia Kiluo………………………………………………………………………………
20. Marafiki zako wa Kiluo wanajua Kuongea Kimaragoli ? Ndio ☐ Hapana ☐
21. Unafikiria walijifundishia wapi ? ………………………………………………………………………………………
22. Kiluo kimeathiri matumizi ya Kimaragoli chako ? Ndio ☐ La ☐
23. Wewe kama kijana unaongea lugha gani ukiwa nyumbani na familia yako ? (Weka alama kwa kisanduku ya lugha mnayoongea)
    Kimaragoli ☐ Dholuo ☐ Zote ☐
24. Ni muhimu wewe kuongea Kimaragoli ? Ndio ☐ Hapana ☐
    (Eleza zaidi hapa chini)
    ………………………………………………………………………………
25. Je, unafikiria Kimaragoli mnachozungumza sasa hivi ni kama cha zamani wakati ambapo Wamaragoli walihamia hapa miaka ya 1940 ama wameingiza maneno ya Kiluo ? (Alam aya sahihi Moja tu)
    Ni kama cha zamani ☐
    Kiko na maneno ya Kiluo siku hizi ☐
    Kama kina maneno ya Kiluo, hebu yataje hapa chini
    ………………………………………………………………………………
26. Je, Waluo wanachukuliaje lugha ya Kimaragoli ? (Weka alama ya sahihi kwa sanduku moja)
    Wanaipenda sana ☐ Wanaichukia ☐
    Wanaipenda ☐ Wanaichukia sana ☐
27. Je, unajivunia Kimaragoli kama lugha yako ? Ndio ☐ Hapana ☐
    (Eleza jibu lako)
    ………………………………………………………………………………
28. Utakuwa na hisia gani ikiwa vijana Wamaragoli watawacha kuongea Kimaragoli kabisa na badala yake kuongea Kiluo?
    Nitasikia vibaya ☐ Nitasikia vizuri ☐
    Sitasikia kitu chochote ☐ Sijui ☐
    (Elezea jibu lako zaidi hapa chini)
    ………………………………………………………………………………
29. Kitu gani ambacho kinafanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa mpaka leo hapa Uriri? (Unaweza kuweka alama ya sahihi kwa sanduku zaidi ya moja)
    a. Redio ya *Vuka FM* na *Mulembe* ☐
    b. Mikutano ya Kitamaduni kama vile baraza nk ☐
    c. Baraza za Machifu ☐ ☐

d. Kutembeleana na watu wa Vihiga
e. Kuabudu kanisani kwa Lullogoli
f. Wazee kufundisha vijana na watoto Lullogoli
g. Kuongea Lullogoli tukiwa nyumbani
h. Mikutano ya chama cha wamama au wazee (Lisanga)
i. Kufanya sherehe za tohara na mila za Wamaragoli
j. Watoto wanafundishwa Lullogoli shuleni

Elezea njia zingine ambazo huwa mnatumia kuendeleza Kimaragoli…………………………………………………………………

30. Wewe unajivunia kuongea Kimaragoli hapa Uriri? Ndio Hapana
Elezea jibu lako hapa chini
………………………………………………………………………………

31. Unapenda kuongea sana lugha gani ukiwa :

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. Nyumbani | Kimaragoli | Kiluo | Zote |
| b. Ukicheza | Kimaragoli | Kiluo | Zote |
| c. Ukiwa kanisani | Kimaragoli | Kiluo | Zote |
| d. Na marafiki | Kimaragoli | Kiluo | Zote |
| e. Sokoni/Madukani | Kimaragoli | Kiluo | Zote |
| f. Shambani | Kimaragoli | Kiluo | Zote |

32. Unaongea lugha gani sana ukiwa na

a. Nyanya na Babu Kimaragoli Kiluo Zote
b. Wazazi Kimaragoli Kiluo Zote
c. Watu wa ukoo (wajomba/shangazi ; mashemeji)Kimaragoli Kiluo Zote
d. Ndugu zako Kimaragoli Kiluo Zote
e. Watoto wako Kimaragoli Kiluo Zote
f. Majirani Kimaragoli Kiluo Zote

33. Kati ya Kiluo na Kimaragoli, lugha gani unapenda kuongea sana ? Kimaragoli
Kiluo Kwa nini ?---------------------------------------------------

34. Ulijifundishia wapi Kimaragoli ?-------------------------------------------------------------

35. Unaweza kuimba, kuomba, kuongea, kusimulia hadithi kwa Kimaragoli?
La
Kama la, kwa nini ?.............................................................

36. Ukilinganisha vijana na wazee, nani wanaongea Kimaragoli sana na pia vizuri ?
Wazee Vijana Sote
Kwa nini ? ...................................................................

37. Kama kijana ukiulizwa useme kiwango chako cha Kimaragoli, utajibu nini ? (Chagua moja)
Kizuri sana Kizuri Kizuri Kidogo Kibaya

38. Je, kuna mambo ambayo wewe hupata shida kuelezea/kufanya kwa Kimaragoli ?
Ndio La

Kama ni ndio, unaweza kutaja mambo hayo ?
………………………………………………………………………………………

**SEHEMU YA NNE : MIELEKEO YA WASEMAJI WA LULLOGOLI**

**Nakubali Kabisa [NK], Nakubali [N], Sina Hakika [SH], Sikubali [S], Sikubali Kabisa [SK]**

**Muhimu**: Weka alama ya sahihi **moja tu** [ √ ] kwa kila kauli katika hojaji hii.

| Na. | Kauli | NK | N | SH | S | SK |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hakuna haja ya mimi Kuongea Kimaragoli hapa kwa Waluo. | | | | | |
| 2. | Najivunia kuongea Kimaragoli hata kama sisi tuko wachache Uriri. | | | | | |
| 3. | Naongea Kimaragoli ili kukidumisha. | | | | | |
| 4. | Mimi hufundisha watoto wetu na marafiki Waluo Kimaragoli. | | | | | |
| 5. | Mimi na watoto wetu tunajua Kuongea Kimaragoli zaidi kushinda Kiluo. | | | | | |
| 6. | Tukiwa nyumbani, tunachanganya Kimaragoli na Kiluo. | | | | | |
| 7. | Kiluo kinatupatia heshima kubwa kuliko Kimaragoli. | | | | | |
| 8. | Tunajua Kiluo kwa sababu ya uchumi na kazi hapa Uriri. | | | | | |
| 9. | Mimi husisitiza watoto wetu kuongea Kimaragoli. | | | | | |
| 10. | Watoto wetu hawajui Kimaragoli vizuri. | | | | | |
| 11. | Tukiwa nyumbani tunapenda kusikiliza idhaa za redio ya Kimaragoli ili kujifundisha, kujikumbusha na kuendeleza Kimaragoli. | | | | | |
| 12. | Tukiwa Kanisani, tunatumia Kimaragoli. | | | | | |
| 13 | Sisi huongea Kimaragoli kwa simu na watu wetu wa ukoo huko Vihiga. | | | | | |
| 14. | Mimi hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli. | | | | | |
| 15. | Wamaragoli tunaheshimiwa na kabila zingine hapaUriri. | | | | | |
| 16. | Wamaragoli tunapenda kuheshimu lugha zingine hapa Uriri. | | | | | |
| 17. | Nikioa haitakuwa lazima watoto wangu wajue Kimaragoli. | | | | | |
| 18. | Mimi kama kijana sina muda wa kujifunza Kimaragoli. | | | | | |
| 19. | Lullogoli inafaa kuendelea kufundishwa na kurithishwa kwa watoto, wajukuu na vitukuu wetu ili isipotee. | | | | | |
| 20. | Mimi huona aibu kuona vijana Waluo wanajua kuongea lugha yao na mimi sijui Kimaragoli. | | | | | |
| 21. | Mimi hujiwasilisha vizuri kwa Kiluo kuliko kwa Kimaragoli. | | | | | |

## KIAMBATISHO M : HOJAJI YA MAKAMO NA WAZEE

**SEHEMU YA KWANZA**

Lengo la maswali haya ni kukusanya habari kuhusu mielekeo ya Wamaragoli kuhusu kuendeleza lugha yao katika Kaunti ya Migori, hasa Uriri. Majibu yako yote yatawekwa siri. Tafadhali jibu maswali kwa uaminifu. Huu si mtihani, kwa hivyo kila jibu utakalotoa litakubaliwa.

**SEHEMU YA PILI**

Jinsia yako Kiume ☐ Kike ☐ Miaka ☐

Umeoa/Kuolewa? Ndio ☐ La ☐

**SEHEMU YA TATU**

Unaongea Kimaragoli au Kiluo au zote ? …………………….…………….

Ni lugha gani ambayo unaongea vizuri ? ………………………………….……..

Marafiki zako wa Kiluo wanajua Kuongea Kimaragoli ? Ndio ☐ Hapana ☐

Unafikiria walijifundishia wapi ?

………………………………………………………

Kiluo kimeathiri matumizi ya Kimaragoli chako ? Ndio ☐ La ☐

Wewe kama mzee unaongea lugha gani ukiwa nyumbani na familia yako ? (Weka alama kwa sanduku ya lugha mnayoongea)

Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

Ni muhimu wewe kuongea Kimaragoli ? Ndio ☐ Hapana ☐

(Eleza sababu za wewe kuongea Kimaragoli hapa chini)

………………………………………………………………………………

Je, unafikiria Kimaragoli mnachozungumza sasa hivi ni kama cha zamani wakati ambapo Wamaragoli walihamia hapa miaka ya 1940 ama wameingiza maneno ya Kiluo ? (Weka alama moja tu)

Ni kama cha zamani ☐

Kiko na maneno ya Kiluo siku hizi ☐

Kama kina maneno ya Kiluo, hebu yataje hapa chini

………………………………………………………………………………

Kitu gani ambacho kinafanya Kimaragoli kuendelea kuzungumzwa mpaka leo hapa Uriri? (Unaweza kuweka Tick kwa sanduku zaidi ya moja)

a. Redio ya *Vuka FM* na *Mulembe* ☐
b. Mikutano ya Kitamaduni kama vile baraza nk ☐
c. Baraza za Machifu ☐
d. Kutembeleana na watu wa Vihiga ☐
e. Kuabudu kanisani kwa Lullogoli ☐
f. Wazee kufundisha vijana na watoto Lullogoli ☐
g. Kuongea Lullogoli tukiwa nyumbani ☐
h. Mikutano ya chama cha wamama au wazee (Lisanga) ☐
i. Kufanya sherehe za tohara na mila za Wamaragoli ☐
j. Watoto wanafundishwa Lullogoli shuleni ☐

Elezea njia zingine ambazo huwa mnatumia kuendeleza Kimaragoli………………………………………………………………

Wewe unajivunia kuongea Kimaragoli hapa Uriri? Ndio ☐ Hapana ☐

Elezea jibu lako hapa chini

Unapenda kuongea sana lugha gani ukiwa :………………………………..

| | | | |
|---|---|---|---|
| Nyumbani | Kimaragoli ☐ | Kiluo ☐ | Zote ☐ |
| Kanisani | Kimaragoli ☐ | Kiluo ☐ | Zote ☐ |
| Na marafiki | Kimaragoli ☐ | Kiluo ☐ | Zote ☐ |

Sokoni/Madukani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Shambani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

Unaongea lugha gani sana ukiwa na

Wajukuu Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Wazazi Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Watu wa ukoo (wajomba/shangazi ; mashemeji)Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Ndugu zako Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Watoto wako Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Majirani Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐
Wazee wenzako Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Zote ☐

Kati ya Kiluo na Kimaragoli, lugha gani unapenda kuongea sana ? Kimaragoli ☐ Kiluo ☐ Kwa nini ?.......................................................................................

Ulijifundishia wapi Kimaragoli ?.....................................................................

Unaweza kuimba, kuongea, kusimulia hadithi kwa Kimaragoli? Ndio ☐ La ☐
Kama la, kwa nini ?...........................................................................................

Ukilinganisha vijana na wazee, nani wanaongea Kimaragoli sana na pia vizuri?
Wazee ☐ Vijana ☐ Sote ☐
Kwa nini ? ……………………………………………………………

Kama mzee ukiulizwa useme kiwango chako cha Kimaragoli, utajibu nini ? (Chagua moja)
Kizuri sana ☐ Kizuri ☐ Kizuri Kidogo ☐ Kibaya ☐

Je, kuna mambo ambayo wewe hupata shida kuelezea kwa Kimaragoli ? Ndio ☐ La ☐
Kama ni ndio, unaweza kutaja mambo hayo ?......................................................................

Je, wewe hujikuta umeingiza maneno ya Kiluo wakati unaongea Kimaragoli ?
Ndio ☐ La ☐

Wewe huchanganya Kiluo na Kimaragoli wapi ? (unaweza kuweka alama kwa zaidi ya sanduku moja)

Nyumbani ☐
Sokoni ☐
Barabarani ☐
Na marafiki ☐
Shuleni ☐
Katika mikutano ☐
Shambani/kazini ☐
Nikitazama michezoni ☐
Kanisani ☐
Hakuna ☐

Taja mahali pengine wakati wewe huchanganya Kimaragoli na Kiluo……………………………………………………………………………

**SEHEMU YA NNE : MIELEKEO YA WASEMAJI WA LULLOGOLI**

**Nakubali Kabisa [NK], Nakubali [N], Sina Hakika [SH], Sikubali [S], Sikubali Kabisa [SK]**
**Muhimu**: Weka alama ya sahihi **moja tu** [ √ ] kwa kila kauli katika hojaji hii.

| **Na.** | **Kauli** | **NK** | **N** | **SH** | **S** | **SK** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hakuna haja ya mimi Kuongea Kimaragoli hapa kwa Waluo. | | | | | |
| 2. | Najivunia kuongea Kimaragoli hata kama sisi tuko wachache Uriri. | | | | | |
| 3. | Naongea Kimaragoli ili kukidumisha. | | | | | |
| 4. | Mimi hufundisha watoto wangu, wajukuu na marafiki Waluo Kimaragoli. | | | | | |
| 5. | Mimi na ndugu zetu tunajua Kuongea Kimaragoli zaidi kushinda Kiluo. | | | | | |
| 6. | Tukiwa nyumbani, tunachanganya Kimaragoli na Kiluo. | | | | | |
| 7. | Kiluo kinatupatia heshima kubwa kuliko Kimaragoli. | | | | | |
| 8. | Tunajua Kiluo kwa sababu ya uchumi na kazi hapa Uriri. | | | | | |
| 9. | Mimi husisitiza ndugu zangu kuongea Kimaragoli. | | | | | |
| 10. | Ndugu zangu hawajui Kimaragoli vizuri. | | | | | |
| 11. | Tukiwa nyumbani tunapenda kusikiliza idhaa za redio ya Kimaragoli ili kujifundisha, kujikumbusha na kuendeleza Kimaragoli. | | | | | |
| 12. | Tukiwa Kanisani, tunatumia Kimaragoli. | | | | | |
| 13 | Sisi huongea Kimaragoli kwa simu na watu wetu wa ukoo | | | | | |
| 14. | Mimi hupenda kujitambulisha kama Mmaragoli. | | | | | |
| 15. | Wamaragoli tunaheshimiwa na kabila zingine hapa Uriri. | | | | | |
| 16. | Wamaragoli tunapenda kuheshimu lugha zingine hapa Uriri. | | | | | |
| 17. | Lullogoli inafaa kuendelea kufundishwa na kurithishwa kwa watoto, wajukuu na vitukuu wetu ili isipotee. | | | | | |
| 18. | Mimi huona aibu kuona vijana Waluo wanajua kuongea lugha yao na watoto na vijana wetu hawajui Kimaragoli. | | | | | |
| 19. | Mimi hujiwasilisha vizuri kwa Kiluo kuliko kwa Kimaragoli. | | | | | |
| 20. | Waluo wanapenda Wamaragoli na lugha ya Kimaragoli | | | | | |
| 21 | Nitahisi vibaya sana ikiwa watoto, vijana na wazee watawacha kuongea Kimaragoli kabisa na badala yake kuongea Kiluo | | | | | |

## KIAMBATISHO N: IDHINI YA UTAFITI YA CHUO KIKUU CHA RONGO

RONGO UNIVERSITY

Goldmine of Knowledge and Innovation

OFFICE OF THE DEAN

SCHOOL OF GRADUATE STUDIES

Tel. 0771349741

P.O. Box 103 - 40404
**RONGO**

Our Ref: **PKIS/9305/2014**

**Date:** Wednesday, January 4, 2017

The Chief Executive Officer,
National Commission for Science, Technology & Innovation,
Utalii House,
Off Uhuru Highway, Nairobi,
P.O Box 30623-00100,
**Nairobi-KENYA**.

Dear Sir,

**RE: RESEARCH PERMIT FOR MR. NABETA KENYANI NIXON SANGILI - PKIS/9305/2014**

We wish to inform you that the above person is a bona fide graduate student of Rongo University in the School of Arts & Social Sciences pursuing a PhD degree in Kiswahili. He has been authorized by the University to undertake research titled; ***"Udumishaji wa Lugha ya Lullogoli Katika Kaunti ya Migori, Kenya."***

This is, therefore, to request the commission to issue him with a research permit to enable him proceed for field work.

Your assistance to him shall be highly appreciated.


Thank you.

Prof. Zachary O. Ngalo
**Ag. DEAN, SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

RONGO UNIVERSITY
THE DEAN
04 JAN 2017
SCHOOL OF GRADUATE STUDIES
P. O. BOX 103 - 40404, RONGO

Copy to: Ag. Vice Chancellor
Ag. Deputy Vice Chancellor (Academic and Student Affairs).
Dean, School of Arts & Social Sciences.
HoD, Languages, Linguistics & Literature.

## KIAMBATISHO O: BARUA YA NACOSTI



NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION

Telephone:+254-20-2213471, 2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email:dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
when replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No.

**NACOSTI/P/17/83114/15423**

Date:

**13th February, 2017**

Nixion Nabeta Sangili
Rongo University College
P.O.Box 103-40404
**RONGO.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Udumishaji wa lugha ya lullogoli katika Kaunti ya Migori, Kenya,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Migori County** for the period ending **11th February, 2018.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Migori County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are expected to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**BONIFACE WANYAMA**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Migori County.

The County Director of Education
Migori County.

*National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO 9001: 2008 Certified*

## KIAMBATISHO P: KIBALI CHA NACOSTI



THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MR. NIXION NABETA SANGILI*
of RONGO UNIVERSITY COLLEGE,
0-50311 wodanga,has been permitted
to conduct research in *Migori* County

on the topic: *UDUMISHAJI WA LUGHA YA LULLOGOLI KATIKA KAUNTI YA MIGORI, KENYA*

for the period ending:
11th February,2018

Applicant's
Signature

Permit No : NACOSTI/P/17/83114/15423
Date Of Issue : 13th February,2017
Fee Recieved :Ksh 2000

Director General
*National Commission for Science, Technology & Innovation*

# KIAMBATISHO Q: BARUA YA WIZARA YA ELIMU, KAUNTU YA MIGORI

HARAMBEE

**MINISTRY OF EDUCATION**

**State Department of Education**

Telephone: (059) 20420
Fax: 05920420
When replying please quote

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
MIGORI COUNTY
P.O. Box 466-40400
SUNA – MIGORI

*REF: MIG/CDE/ADMN./1/VOL.III/* 155

DATE: 25th July, 2017

**Nixion Nabeta Sangili**
Rongo University
P.O. Box 103-40404
**RONGO**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on *"**Udhumishaji wa lugha ya lullogoli katika kaunti ya Migori, Kenya**".* I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Migori County** for a period ending **11th February, 2018.**


On completion of the research, you are expected to submit one hard copy and a soft copy of the research report/Thesis to this office.

Thank you.

**Luka Chebet**
County Director of Education
**MIGORI COUNTY**

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
MIGORI
P. O. Box 466,
SUNA - MIGORI.

**KIAMBATISHO R: BARUA YA KAMISHNA WA KAUNTI**



**OFFICE OF THE PRESIDENT**

**MINISTRY OF INTERIOR AND COORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT**

**Tel No.**:(059) 20511
**Fax:** 059-20361
**Email**: countycommissionermigori@yahoo.com

OFFICE OF THE COUNTY COMMISSIONER
MIGORI COUNTY
P.O. BOX 2-40400,
**SUNA MIGORI.**

***When replying please quote***

**Date**: 25TH July, 2017

**Ref. No.:** ED.12/19AVOL.II/7

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Nixion Nabeta Sangili NACOSTI/P/17/83114/15423 a student at Rongo University has been authorized to carry out research on ***"Udumishaji wa lugha ya lullogoli katika Kaunti ya Migoori, Kenya"*** for the period ending 11th February, 2018.

Accord him the necessary assistance.

COUNTY COMMISSIONER
P.O BOX 2 – 40400
SUNA — MIGORI
MIGORI COUNTY

PETER G. MUTU
FOR: COUNTY COMMISSIONER
**MIGORI COUNTY**

**CC**

The County Director of Education
**MIGORI**

## KIAMBATISHO S
## RAMANI YA WADI KATIKA ENEOBUNGE LA URIRI

